Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 5 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2013.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati

Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. PAULINA P.GEKUL (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ujenzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi na tutakuwa na maswali ya aina mbili, Maswali kwa Waziri Mkuu na Maswali ya Kawaida. Sasa tutaanza na maswali kwa Waziri Mkuu halafu maswali ya kawaida. Kwa hiyo, kama kawaida yetu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ndiye atauliza swali la kwanza, Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la kwanza.

(a) Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika nchi yetu kwa muda mrefu sasa yamekuwepo mauaji mengi na baadhi ya vifo hivi vimekuwa ni vya utata mkubwa. Baadhi ya vifo hivi vimekuwa vikihisiwa kuhusisha vyombo vya dola kama vile Jeshi la Polisi na katika hotuba yako ya Bajeti ya mwaka jana ulikiri kuwepo kwa tatizo hilo na ukakiri kwamba Sheria ya Uchunguzi ya Vifo Vyenye Utata itafanyiwa kazi na Serikali na vifo

vyote vilivyokuwa na utata huo vitafanyiwa uchunguzi wa kina. Ni kwanini hadi sasa ahadi yako hiyo ambayo ni muhimu sana kwa Taifa haijafanyika?

(b) Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutofanyika kwa hatua hiyo huoni kwamba unakuza hisia kwamba Serikali na Viongozi pengine wanahusika katika kuagiza mauaji hayo?

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mwaka jana nilitoa maelezo hayo na ninataka nimwarifu Mheshimiwa Mbowe kwamba baada ya pale tulitoa maelekezo kwa vyombo vyote. Maeneo yote ambayo yanahusika na jambo hili ili Sheria hiyo ianze kuzingatiwa kikamilifu.

Ni jambo ambalo tumeishaanza kulifanya lakini kusema kwamba pengine tunapuuza na kujenga hisia inategemea mtu na mtu anaweza akawa na hisia za namna hiyo lakini kubwa ni hili tulilolisema la kwamba Sheria ile ifuatwe. Kwa hiyo, mimi ninadhani tukiifuata ile itatusaidia kututoa hapa tulipo. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini ni kweli kwamba hisia za dola kuhusika katika mateso na mauaji ya raia zimeendelea kuwepo. Jinsi ninavyouliza swali hili wakati huu sifa ya Taifa letu iko mashakani katika anga za kimataifa kutokana na mateso ambayo yanaonekana yalikuwa na kusudio la mauaji ambayo alifanyiwa Mwenyekiti wa Madaktari, Dkt. Stephen Ulimboka na vilevile yamekuwepo

mashambulizi mengine ya viongozi kama walivyofanyiwa Wabunge wa CHADEMA kule Mwanza.

Je, Serikali haioni ili kuiondoa nchi yetu kwenye sifa hii mbaya ambayo inajengeka ingekuwa wakati muafaka ikubali kuunda Tume huru ya Uchaguzi kwa sababu Serikali ni sehemu ya washutumiwa katika hili?

**SPIKA:** Tume nzima ya Uchaguzi au ya Uchunguzi?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Serikali iunde Tume Huru ya Uchunguzi.

**SPIKA:** Okay!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Kuweza kubaini chanzo halali badala ya kuliachia jeshi la polisi ambalo ni sehemu ya tatizo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani sana na Mheshimiwa Mbowe kwamba jina la nchi yetu limechafuka sana. Siyo kweli hata kidogo, kuchafuka sana kwa lipi? Kwa sababu ukisema hivyo ni lazima vilevile uwepo ushahidi wa dhati unaoonyesha kwamba ni kweli Serikali inahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe ametumia mfano wa Dkt. Ulimboka, siyo mfano mzuri. Wewe huna ushahidi kama ni Serikali imefanya hivyo na hakuna mpaka sasa ambaye anaweza kusema ana ushahidi huo ndiyo maana tulisema mara ya mwisho kwamba ni vizuri jambo hili likafanyiwa

uchunguzi wa kina ili tujue kilichotokea hasa ni kitu gani. Kwa sababu mimi kama nilivyosema mara ya mwisho hainiingii kichwani hata kidogo kwa Serikali kumdhuru mtu ambaye tumekuwa tunafanya kazi naye muda wote. Tulijua kabisa kuwa kuna amri ya Mahakama tena nzuri ambayo ilikuwa inatusaidia sisi upande wa Serikali. Sisi haohao tuchukue tena hatua ya kutaka kwenda kumwadhibu kama namna ilivyotokea.

Mheshimiwa Spika, haiingii kichwani ndiyo maana nikasema ni vizuri jambo hili tupate ukweli hasa ukoje ndiyo maana niliishia pale siku ile.

**SPIKA:** Tunaendelea kwa Waheshimiwa Wabunge wengine nawaombeni maswali yenu yawe mafupi kusudi tuweze kuwa–*cover* wale wote watakaohusika. Nitamwita Mheshimwa Murtaza Ally Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika awamu ya tatu na awamu ya nne Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imefanya jitihada kubwa sana kuwekeza katika sekta ya Afya hasa katika maeneo ya Hosptali za Rufaa ikiwemo Muhimbili. Je, nini tathmini ya Serikali baada ya uwekezaji huu kiutendaji na kiufanisi?

**SPIKA:** Haya sina hakika.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mangungu kwamba jitihada zimefanyika kubwa kuwekeza katika sekta ya Afya na

hasa katika maeneo yale ambayo yanahitaji taaluma mahususi. Kama alivyosema kwa Mhimbili kwa kweli jitihada iliyowekwa pale ni kubwa ndiyo maana sasa hivi unaona muda si mrefu tutafungua jengo lile la Taasisi ambalo litakuwa linashughulika na magonjwa ya moyo ambalo ni eneo moja limekuwa linatumia sana fedha zetu kwenda nje, lakini vilevile ukienda kwenye Idara ya meno tumejitahidi sana kuboresha huduma na Mheshimiwa Rais alijitahidi tumepata vifaa vya kisasa kabisa na ni moja kati ya kituo ambacho kinatoa huduma ya meno kwa kiwango cha hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini mkipita pale *Ocean Road Hospital* mtaona kuwa tunaendelea kujenga tunataka Taasisi ile iweze kutoa huduma kwa kiwango cha hali ya juu. Kwa hiyo, tutakuwa na nafasi ya kutosha ya malazi lakini pia tumejiimarisha katika kuhakikisha vifaa vinaendelea kupatikana.

Kwa hiyo, ni kweli zipo jitihada kubwa lakini lazima nikiri vilevile kama mmoja wa viongozi ndani ya Serikali kwamba changamoto bado ni nyingi lakini bado tunaendelea kuzikabili kwa kadri itakavyowezekana lengo ni kujitahidi kutoa huduma iliyo bora na ndiyo maana baada ya mchakato mrefu hatimaye tumefikia uamuzi ule kwamba hata Lugalo sasa tuipandishe kuwa ni Hospitali ya Rufaa ili na yenyewe tuweze kui-*equip* vizuri kwa lengo la kutoa huduma zaidi kwa Watanzania. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninashukuru kwa majibu hayo

yanayowiana na swali lakini ningependa kujua nini wito wa Serikali kwa Watumishi wa Afya ambao kimsingi inaonekana wamekuwa wakipata upendeleo maalum katika kusomeshwa. Kwa maana ya kupewa 100% ya udhamini na hawalipi deni kama watu wengine wanavyokopeshwa katika sekta nyingine?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Serikali tumekuwa muda wote tunajitahidi sana kulieleza jambo hili kuwasihi madaktari, wauguzi, wafamasia na watumishi wengine katika sekta ya Afya kutambua tu kwanza kwamba wao ndiyo Serikali imewapa dhamana wa kulea uhai wa Watanzania hasa tunapokwenda katika vituo vyao vya kutolea huduma. Kwa sababu wakilijua hili utaona ni nini hasa ambacho Serikali inalenga.

Lakini pili, tumekuwa vilevile tunasema kwamba inawezekana kabisa wengine bila kujua wakawa wanafanya mambo ambayo Mtanzania wa kawaida akimtazama anashangaa kwa nini hili linafanyika. Ndiyo maana tukasema ni vizuri tuendelee kutoa elimu kwamba sekta ya Afya ni moja kati ya sekta chache ambazo zimewekewa utaratibu mahususi wa kutojiingiza katika migomo kwa sababu ya hali ya unyeti wake ilivyo kwa maisha ya binadamu, sasa lengo ni elimu kwa wale ambao wasiolijua ili tuweze kufika mahali na kuendelea vizuri.

Tatu, tunatambua vilevile kuwa yapo bado matatizo, bado zipo changamoto nyingi na ndiyo maana muda wote Serikali imekuwa tayari kuzungumza. Katika maeneo ambayo tunaweza

kukubaliana tukubaliane, lakini pia katika maeneo tusiyokubaliana tukubaliane. Vilevile namna nyingine ya kuweza kufikia muafaka wa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya mambo ambayo tunakiwa tuyafanye sana kwa lengo la kuhakikisha kwamba hatuwaingizi Watanzania katika matatizo makubwa.

**MHE. RAJABU M. MOHAMED:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, siku chache zijazo kwa uwezo wa Mwenyenzi Mungu Watanzania na Duniani kwa ujumla tutaingia katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Uzoefu unaonyesha kwamba wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kunakuwa na mfumuko mkubwa wa bei hususani katika vyakula. Je, Serikali yako imejipangaje ili kuwasaidia wananchi hawa wasipambane na adha hii ya wafanyabiashara ambao wanapandisha bei vitu, wakati huohuo ukizingatia kwamba wananchi hawa ndiyo ambao tunawategemea katika kutoa maoni yao kwa ajili utengenezaji wa Katiba mpya na vilevile katika suala zima la Sensa wakati wao watakuwa katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

**SPIKA:** Bei, sensa, nini vyote hivyo. Nadhani ubaki kwenye bei tu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kubwa labda nianze kwa kutoa wito tu kwa Watanzania wote kuwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni fursa kwa wenzetu Waislamu wanaoitumia katika kutimiza eneo moja muhimu sana katika ibada. Kwa hiyo, ni vema watu tusitumie mwanya huo kutaka kupata utajiri kwa njia

ambazo siyo halali; tusipandishe bei ya vyakula bila sababu za msingi. Wote tutambue kwamba tunayo dhamana ya kuhakikisha hatutumii mwanya huo kujinufaisha wakati hakuna sababu ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali, sisi tutachukua hatua stahiki tutakazoona ziko ndani ya uwezo wetu ili kuhakikisha kwamba mwezi Mtukufu wa Ramadhani unapita vizuri bila mikwaruzo mikubwa. Lakini kubwa ni kwa wafanyabiashara ambao kwa miaka yote ndiyo wamekuwa wakitupatia tatizo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk naomba maswali yenu yawe mafupi kwa sababu wenzenu wengi pia wameomba nafasi. *(Makofi)*

**MHE. RAJABU M. MOHAMED:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na majibu yako mazuri ni dhahiri kwamba elimu kwa umma inahitajika. Je, umejipangaje kuweza kutumia mhimili wa nne ambao siyo rasmi yaani vyombo vya habari kuweza kulieneza hili ambalo unalizungumza sasa hivi?

**SPIKA:** Wanaposema mhimili ni zile *checks and balances*_hii ya safari hii ni kutoa habari kutumia vyombo vya habari tu siyo kuhimili mtu yoyote.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tutajihidi na tutatumia vyombo vya habari na tutajitahidi vilevile kutoa elimu kwa Umma kwa ujumla tu kwa njia mbalimbali ili tuweze kuhakikisha kwamba hakutokei mtikisiko mkubwa utakaowafanya wenzetu mnao

husika kupata athari wakati wa kutimiza nguzo hiyo muhimu ya Ibada.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru ninaomba wnimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hapa Tanzania kuna zao moja la biashara ambalo ni alizeti limeshamiri sana na kuongeza kipato kwa Watanzania. Lakini hivi karibuni Serikali katika Mkoa wa Singida ilitoa amri ya kuzuia wafanyabiashara wa zao lile wasiende kununua alizeti kwa wakulima moja kwa moja bali wakulima wapeleke kwenye Vyama vya Ushirika lakini amri ile ilikuja bila kutoa elimu kwa wananchi na Vyama vya Ushirika ambavyo vilitajwa havitoshelezi hivyo kupunguza na kuzuia ajira kwa Watanzania waishio Mkoa wa Singida, ambao siyo chini ya 60,000.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba uwaeleze wananchi wa Singida. Je, Serikali inakusudia kuwaweka katika mikono ipi kwa sababu zao lile limekuwa ndiyo mkombozi. Kwanza, kwa amri ya kufungwa miaka miwili lakini kwa wananchi zaidi ya 60,000 kukosa ajira. Asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijui kama umeelewa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkuu wa Mkoa wa Singida ametoa amri, au maagizo au maelekezo kuhusiana na namna zao hilo la alizeti litakavyonunuliwa mwaka huu. Mimi nilipata nafasi ya kuzungumza naye alipokuwa hapa kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alichoniambia ambapo mimi nilifikiri lilikuwa ni jambo jema alisema kwamba nia yake ni kuona kwamba mkulima huyu mdogo aweze kupata faida au manufaa makubwa zaidi hata kuliko ilivyo sasa kwa maana kwamba watu wanaohusika na zao hili wanaonunua alizeti waende wakanunue katika maeneo mahususi, kwa namna ambayo itawapa nafasi ya kushindana katika kutoa bei nzuri kwa mkulima. Sasa hiyo kwa imani yake aliona ingeweza kupandisha bei zaidi kuliko kiwango kilichopo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilimwuliza kama wanavyo Vyama vya Msingi vya kutosha akaniambia wanavyo karibu themanini (80). Nikamwuliza kama wanazo *SACCOS* akaniambia zipo, nikamwuliza kama kuna vikundi ambavyo ni *organised* ambavyo vinaweza vikatumika akaniambia vipo. Kwa hiyo, akasema siyo kweli kwamba wamekataza isipokuwa wanataka wote wanaonunua wakanunue katika vituo hivyo. Nadhani lengo lake lilikuwa ni kutekeleza Sheria ile ya Stakabadhi Ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli suala hili limeleta mtikisiko kidogo kwa jamii na hasa wale wafanyabiashara. Lakini lengo lake lilikuwa ni zuri sana. Rai ya Mheshimiwa Martha Mlata ni nzuri kwamba inawezekana tu kwa sababu limekuja ghafla, labda watu walikuwa hawajaelezwa vya kutosha, hawajapewa elimu ya kutosha.

Kwa hiyo, nimezungumza naye tena jana ili kuona anaendeleaje na zoezi hili. Bahati nzuri ameniambia

kwamba leo watakutana viongozi pale Mkoani kuzungumzia jambo hili, nami nimeahidi kwamba nitamtuma Waziri mmoja aende pale ili kupata hali halisi ikoje. Kwa sababu kwangu mimi kulisogeza zoezi hili mbele sioni tatizo hata kidogo kama nia ni njema.

Kwa hiyo, mimi nadhani viongozi watakapokuwa wamekutana na wenyewe walione, kama wanaona kwa sasa halikupata maandalizi ya kutosha lakini dhamira ni ya kumsaidia mkulima, halina tatizo waone kwa dhamira hiyo ya kwenda mbele badala ya kuleta tatizo ambalo baadaye linaweza likaleta mtafaruku mkubwa. Lakini naamini viongozi wakikutana na Waziri atakayekuwa amekwenda, tunaweza tukafikia hatua nzuri ya kuelewana tufanye nini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlata nilidhani na wewe unakwenda?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nashukuru. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri yenye matumaini kwa wananchi wa Singida. Kwa kuwa zao hili linazidi kukua na kushamiri lakini hakuna Bodi inayolisimamia zao hili.

Je, unatuambia nini wakulima wa zao hili la alizeti?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba wakulima wanaolima zao hili wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka na mimi nataka niamini vile vile kwamba baada ya uamuzi wa juzi wa kuona uwezekano wa kupandisha ushuru kwa mafuta

yanayotoka nje utaongeza zaidi uzalishaji wa zao hili kwa upande wetu hapa ndani jambo ambalo litakuwa ni zuri sana. Ni lazima Serikali sasa ione namna tutakavyotumia chombo ambacho kimsingi kilikwishaanza. Bodi ya Mazao Mchanganyiko, maana hii ndiyo tulilenga ifanye kazi ya kununua mazao kama alizeti na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tutakuwa waangalifu vile vile kwamba lengo si kutaka chombo hiki, sasa kiweze kuwa na ukiritimba wa bei ambazo tunadhani wakati mwingine nazo si kwa maslahi ya wakulima wadogo. Kwa hiyo, ni lazima kiwe ni chombo kitakachosaidia kuongeza bei ya zao hilo badala ya kuteremsha bei hiyo. Kwa hiyo, chombo hicho kipo, tumekitengenezea Bajeti kidogo mwaka huu tutaanza ili waweze kujipanga vizuri kwa lengo la kuona namna tutakavyosimamia zao hili pamoja na mazao mengine ambayo hayana mifumo mahsusi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, niliwahi kukuuliza swali hapa kuhusu kampuni ya *Bayport* na *DECI* ambazo zimekuwa zinatoa mikopo kwa wafanyakazi na kampuni ya *Bayport* inaendelea kutoa mikopo hii kwa riba kubwa sana na kusababisha wafanyakazi wengine kubaki wanapokea shilingi elfu mbili au shilingi elfu tatu. Ulisema suala hili litafanyiwa kazi, lakini watu hawa wanaendelea. Nataka kujua tamko la Serikali kuhusu kuwazuia watu hawa wasiendelee kufanya mchezo huu kwa wananchi. Lakini pia hatma ya watu waliokopa *DECI* ni ipi hasa wale watu watano ambao kesi yao iko mahakamani.

**SPIKA:** Ile *DECI* kwa mujibu wa kanuni zetu, swali likiamuliwa katika mkutano huo haliulizwi tena, naomba Waziri Mkuu uzingatie *Bayport*.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunisaidia kwenye eneo lile la pili. Labda nizungumzie tu hili la *Bayport*. Ni kweli kipo chombo hiki ambacho kinatoa hiyo mikopo na mara ya mwisho ulikuwa umeligusia. Kwa kweli unajua mambo mengine haya ni mambo ambayo mnayafanya jamii huko huko kwa ridhaa yenu ninyi wenyewe.

Sisi tulichofanya ni kuwaandikia Wizara maana walio wengi katika *Bayport* hasa ni walimu. Kwa hiyo tulijaribu kuitahadharisha Wizara ya Elimu wachukue hatua stahiki kuwaelimisha watumishi wao kwamba vyombo vingine hivi ni vizuri kama havina manufaa kwao wao wasivitumie. Sasa kama mtu anaendelea kukitumia kwa hiari yake maana yake karidhika.

Kwa hiyo, siwezi nikasema zaidi ya hapo wala siwezi kusema kwamba labda kama kumetokea makosa ya kisheria hapo tunaweza kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunasimamisha shughuli zinazofanywa na chombo hicho.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Waziri Mkuu, lakini ili mtumishi akatwe mshahara wanaoidhinisha ni Wakurugenzi wa Halmashauri. Sasa, mnawaagiza nini kwa sababu wanaona kabisa sheria zinakiukwa na riba ile ni kubwa

kinyume cha sheria mnawaagiza nini ili wazingatie haya mambo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tulikwisha kutoa maelekezo lakini kwa maana ya kutoa elimu. Riba kubwa hata mabenki yanatoza riba kubwa lakini bado tunakopa. Kwa hiyo isiwe kwamba hilo ndilo eneo ambalo ni juu ya kila mtu. Maana ukiamua kwenda kukopa *CRDB* inakuambia ni asilimia 16 au asilimia 20, wanakopa hata kwenye baadhi ya vyombo, *PRIDE* na maeneo mengine riba ni kubwa vile vile, ni juu ya kila mmoja kuona kipi kwake anaona kina manufaa.

Mimi nakubaliana na wewe tutatoa tena maelekezo kwa Halmashauri, watoe elimu kwa walimu na watumishi wengine, ili kwa mtindo huo waweze kuachana nayo. Lakini upande wa pili Mheshimiwa Mkosamali tumekuwa tunajaribu sana tunawaambia jamani hebu undeni vyombo vyenu wenyewe. Baadhi ya maeneo wamefanya vizuri sana kwa kuwa na *SACCOS* za Walimu, *SACCOS* za Watumishi, wao wanakopeshana kwa riba ndogo katika misingi ambayo ina nafuu zaidi. Kwa hiyo, bado niendelee kutoa wito kwamba pengine katika mazingira haya ni vizuri tukaona uwezekano wa vyombo kama hivyo badala ya kutegemea vyombo binafsi ambavyo wakati mwingine havina maslahi sana kwao.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Kumekuwa na wimbi kubwa hivi sasa la vijana kukimbia maeneo ya vijiji na kuhamia mijini jambo ambalo linaweza kusababisha matatizo

makubwa na uvunjifu wa amani katika maeneo ya miji. Je, Serikali imepangaje kukabiliana na jambo hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kutoa maelezo kidogo kwa Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, kuhusiana na jambo hili. Ni kweli anachosema kwamba hii changamoto ya watu kutoka vijijini kuja mijini kwa matumaini kwamba mijini kuna fursa nzuri ambayo ni kweli ziko fursa nyingi, lakini ni kweli vile vile kwamba haziwezi kuwatosheleza wote wanaokimbilia mijini. Sasa mmejipangaje au mnafanya nini kukabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, muda wote mtakuwa mmeona mwelekeo wetu wote ni kuona ni maeneo gani ambayo kule vijijini yakisaidiwa yanaweza kupunguza kasi ya watu kuja mijini. Moja ni kuboresha hali ya maisha kule vijijini na kuboresha maisha maana yake kwa sisi Watanzania ni lazima tujikite katika maeneo ambayo ndiyo hasa yanatugusa mfano Kilimo. Ni lazima tuendelee kuzungumza kwa lugha moja namna ya kuboresha kilimo, tukifanye kiwe chepesi, kiweze kuwa cha manufaa kwao kwa sababu ndicho kinachowaleta mijini, kuona kwamba pengine akija mjini atapata pesa.

Lakini mimi nimebahatika katika zungukazunguka katika nchi hii, kilimo ni eneo moja ambalo linaweza likasaidia sana. Ukienda Mbarali pale unakutana na vijana ambao wanalima mpunga wapo katika hali nzuri sana. Nimetembea na maeneo mengine ambako unakuta kwa sehemu kubwa kabisa jitihada za kilimo

zimeanza kuzaa matunda mazuri pamoja na Mkoa wa Singida ambao nilikwenda kuutembelea juzi juzi.

Kwa hiyo, kilimo ni lazima tukipe nafasi kubwa, tuhakikishe maeneo kama mifugo ambako ndiyo watu wengi tu, maeneo kama ufugaji wa nyuki, uvuvi wa samaki, haya maeneo tukiyaimarisha tukayafanyia vizuri, nina hakika tutaweza kuwasaidia sana vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili ni lile jambo ambalo mmekuwa mkilisema muda wote, mambo mengine ni madogo madogo lakini yanaweza kuwa na *impact* kubwa. Ni lazima tujitahidi sana kuhakikisha kwamba vijijini nako maisha yanakuwa ni mepesi. Moja ya eneo ni kuhakikisha kunakuwepo msukumo wa kutosha katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na umeme vijijini, jambo ambalo limepewa nafasi na tunaendelea kulisukuma kwa nguvu sana. Vijana wakiweza kupata umeme watazalisha wenyewe katika baadhi ya maeneo bila kulazimika kukimbilia mijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni wito wa jumla tu, lakini upande wa Serikali na sisi tunalijua na tunaendelea kulifanyia kazi kwa nguvu zetu zote.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Nilitaka kufahamu kama Serikali itakuwa tayari kuja na mpango wa vijiji vya vijana ambapo Serikali inaweza kuwa-*guarantee* vijana hawa katika maeneo ya vijiji hivyo kwa kuwapa matrekta kuwawezesha ili wafanye kazi ya uzalishaji katika maeneo hayo ya vijijini badala ya kukimbilia mijini.

**WAZIRI MKUU:** Ni wazo zuri kuwa na kitu wanakiita Vijiji vya Vijana, kwa sababu tumejaribu pale Kigoma nadhani eneo moja wanaliita Lugufu sikumbuki vizuri jina. Lakini tumejaribu Mkoa wa Kigoma ambako tulichukua vijana tukawapeleka pale, tukajaribu kuwasaidia tukaenda kuwatembelea, unaona ari ni nzuri na ni kubwa, lakini lina changamoto zake vile vile. Maana kuwaweka vijana katika eneo moja unawapa matumaini makubwa, lakini matumaini kwa kupitia kilimo hayaji siku moja, ni vitu vinachukua miaka mitatu minne mitano kabla hujaona matokeo yake. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe ni rai nzuri lakini ina changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaloliona zuri ni vijana katika maeneo haya walipo vijijini, tuwapange tuwasaidie na tuwalenge kama ndiyo walengwa wakubwa wa kilimo ambacho ni chepesi cha matumizi ya trekta.  Mimi naamini hili linawezekana kabisa. Tumejaribu hapa Chinangali ukienda pale utakuta watu waliopo pale wengi ni vijana. Lile shamba kwa sehemu kubwa washiriki wakubwa ni vijana lakini wote wameshaanza kuona matunda yake yalivyo mazuri.

Mheshimiwa Spika, haya matrekta ambayo sasa tunajaribu kuyauza kwa kasi kubwa, tumeziambia Halmashauri chukueni matrekta haya, lengeni vijana katika makundi yao mbalimbali vijijini ili wao wawe ndiyo ndiyo vitovu vha umiliki wa haya matrekta, walimie lakini wasaidie vile vile kutoa huduma kwa wakulima wengine. Kwa hiyo, ni jambo

linalowezekana na mimi naamini tukijipanga vizuri tutafanya vizuri zaidi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kitengo cha Mpigachapa wa Serikali ni moja ya nyenzo za habari. Kwa kuwa hapo awali kitengo hicho kilikuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na baadaye kuhamishiwa chini ya Wizara yako. Je, ni sababu gani zilizofanya kitengo hicho kuhamishiwa chini ya Wizara yako?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vinavyosimamiwa na Serikali ni vyombo ambavyo Serikali wakati wowote inaweza ikaamua kuvibadilisha kutegemea na tunataka kuvisaidia kiasi gani. Idara hii ya Mpiga Chapa wa Serikali ni Idara kubwa, ni Idara ambayo inachapisha wakati mwingine nyaraka nyeti ambazo zinataka usiri mkubwa.

Kwa hiyo, Serikali iliona ni lazima tukitafutie namna ya kukiimarisha, lakini kitaimarika vizuri zaidi kikiwa karibu na ofisi ambayo ina uwezo wa kukisaidia kwa nguvu.

Lakini vile vile tuliona ni vizuri chombo hiki kiwe karibu na ofisi hii kwa sababu nyingine ya msingi. Kwamba tungelipenda vile vile kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa, zinatolewa kwa ufanisi mkubwa, lakini kwa yale maeneo ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa maana ya *documents* ambazo ni Serikali zenye

usiri basi tuwe karibu nao ili kuhakikisha wanasimamia vizuri maeneo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Mnyaa swali la mwisho, naomba liwe fupi muda umeisha, tunatumia zile dakika ambazo walifanya mawasilisho ya Hati hapa mbele mezani.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Usingizi wangu wa saa kumi utalipwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kufuatilia sera za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazoshirikisha Umma ili kufanikisha malengo ya Jumuiya, maoni ya wananchi ni muhimu kusikilizwa na kujadiliwa katika mabunge yao. Hii iko katika *Article* ya 65 ya *Treaty* iliyoanzisha Jumuiya hii, ambayo katika Kifungu (B) inatakiwa Katibu wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki alete vivuli vya miswada na maazimio kwa Mabunge ya nchi wanachama; na Katibu wa Bunge wa hiyo nchi mwanachama anatakiwa a-*table* muswada huo kujadiliwa katika Bunge lake. Inaonekana hali hii haijatekelezwa huu ni mwaka wa kumi hatujaona vitu kama hivyo.

Je, Waziri Mkuu ni nini tufanye ili kurekebisha hali hiyo na kwa nini haitekelezwi ili kwamba miswada au maazimio yake *cross boundary ecosystem* ambayo ina matatizo kwa baadhi ya nchi isije ikatuletea athari.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nafikiri swali hili ni *highly technical* wala halihusiki naomba

kabisa Waziri wa Afrika Mashariki akifika wewe mwulize swali hili atalijibu, lakini Waziri Mkuu hili hapana.

Naomba nitumie muda huu kukushukuru Waziri Mkuu kwa majibu. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa na maswali mafupi tumeweza kumaliza kazi hiyo.

Hili swali aliloliuliza Mheshimiwa Mnyaa hata Ofisi yangu na Wizara ya Afrika Mashariki tunajaribu kusoma kwamba hii miswada inayosomwa kule ije vipi hapa, halafu tunajaribu kuangalia utaratibu *technically* wale wamepitisha miswada yao kule halafu tunaleta hapa Bungeni tunafumua haiwezekani! Kwa hiyo tunajaribu kuona tunafanyaje, wale Wabunge wetu kama tunavyokuwa na *public hearing* tutumie Bunge letu ama Kamati zetu hapa ziwe na *Public hearing* kabla wenyewe hawajaenda huko, ili kusudi kama maoni yetu wapokee kabla, siyo miswada imepita halafu inakuja huku ndani haiwezekani. Kwa hiyo pia tunakusudia kuunda Kamati humu ndani ya Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, ndiyo maana nilikuambia Waziri Mkuu hawezi kujibu hayo kwa sababu hayo tunafanya sisi huku.
Haya ni *technical* lakini Waziri wa Afrika Mashariki ungemwuuliza angekujibu. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 138

## Matumizi Mabaya ya Bahari Zetu.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aiuliza:-

Rasilimali zilizopo kwenye Bahari yetu zinatumika kinyume na sheria na taratibu za Nchi kama vile uvuvi haramu unaofanywa na meli kubwa za nje na pia kuchukuliwa kwa matumbawe ya baharini.

Je, Serikali inachukua hatua gani ili hali hii isiendelee kutokea?

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa uvuvi katika maeneo ya maji ya kitaifa ya bahari yetu husimamiwa na sheria ya uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009 kwa upande wa Tanzania Bara na sheria ya Uvuvi Na. 7 ya mwaka 2010 ka upande wa Tanzania, Zanzibar. Aidha, uvuvi katika Bahari Kuu *(EEZ)* husimaiwa na Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu sura ya 388 iliyofanywa marekebisho mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la uvuvi haramu unaofanywa na baadhi ya wavuvi wenye meli kubwa za kigeni na wavuvi wadogo Serikali imeendelea kufanya doria za majini na nchi kavu katika maji ya kitaifa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, vikundi vya ulinzi shirikishi ama *Beach Management Unit* na wadau wengine.

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 jumla ya doria zenye jumla ya siku kazi 5792 zilifanyikakatika maeneo yote ya uvuvi nchini. Serikali kupitia Mamlaka ya kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu, imefanya doria za anga 28 katika eneo la Bahari Kuu ambapo hakuna meli iliyoonekana ikivunja sheria.

Vilevile Serikali inatumia mfumo wa kufuatilia mienendo ya meli *Vessel Monitoring System (VMS)* katika kuhakikisha kuwa meli hizo zinafanya shughuli za uvuvi kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo. Aidha, Serikali imeendelea kutoa hamasa kwa wadau wa uvuvi na wananchi kuhusu uharibifu wa mazingira ambapo hadi sasa jumla ya vikundi 703 vimeanzishwa na kati ya hivyo 179 vipo ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, Matumbawe ni sehemu muhimu ya mfumkoikolojia katika Bahari ambao ndio eneo la mazalia na makulia ya viumbe hai/samaki majini. Aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo raia wasio wema wanaovua kinyume cha Sheria. Raia hao wasio wema wanaofanya uhalifu wa kuchukua matumbawe na kuyatumia kwa kujengea nyumba na kutengeneza chokaa.

Uhalifu huu pia hususisha uvuvi haramu wa kutumia baruti vyote vikiwa ni kinyume cha Sera ya Taifa ya Uvuvi na mikakati yake ya mwaka 1997 hasa tamko Na. 8 la Sera na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo ya Tengefu ya mwaka 1994 sehemu ya 10 na kanuni zake sehemu ya 22 (i) (b).

Pia Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na mikakati ya kupambana na uvuvi haramu, uharibifu wa mazingira na utumiaji wa matumbawe. Uhamasishaji wa jamii, wavuvi na wadau, kuhusu uanzishaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi na utoaji elimu kuhusu athari za uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira ni sehemu ya hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha kuwa hali hiyo haindelei.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kumpa nafasi ya swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri pia nina maswali ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, meli zinazofanya utafiti wa mafuta na gesi baharini zinachafua mazingira pamoja na kutorosha samaki. Hali hii inawafanya wavuvi wazalendo kutokupata samaki wa kutosha.

Je, Serikali ina mkakati gani kwa uchafuzi huu na pia itawafidiaje hawa wavuvi wazalendo kwa kadhia hii iliyowakumba?

(b) Kwa kuwa vijana wetu wengi hawana ajira…

**SPIKA:** Mbona umeuliza mawili, utafanyaje na atafidia vipi basi inatosha.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Rukia Kassdim Ahmed, lenye sehemu mbili kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ni kweli kumekuwepo na *concern* kwamba meli zinazofanya utafiti huko zinachafua mazingira. Lakini naomba niseme kwamba tayari katika ngazi ya sera tuna miongozo na kwamba kila mradi mkubwa kabla haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa *environmental impact assessment*. Niseme tu katika sehemu hii kwamba natoa maagizo kupitia Bunge hili kwamba meli zote zinazohusika kwamba zifuate taratibu tulizojiwekea kinchi.

Kwa upande wa fidia kwa watu wetu tayari tumekuwa na mfano ambao tutapaswa kuufuata kwenye meli ya Tawafiq iliyoshikwa ikapelekwa mahakamani moja kati ya adhabu tatu zilizotolewa baada ya kuonekana kwamba wana makosa ni kutozwa faini ya shilingi bilioni 20 kwa sababu ya uchafuzi wa mazingira.

Kwa hiyo, mimi nadhani kama Serikali tumeshaweka mfano na mfano huo utafuatwa pale ambapo utathibitika kwamba kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira. Sheria kama hizi zitatumika kuhakikisha kwamba fidia itatolea na itatolewa vya kutosha.

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Baada ya kukaa na kutathimini kuona kwamba idara ya uvuvi katika Wizara yetu ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeshindwa kabisa katika kuleta tija kwa taifa hili kwa maana ya kufikiria ni jinsi gani bahari, maziwa yetu, mito yetu na mabwawa tuliyokuwa nayo yanaweza yakachangia pato kubwa la taifa katika nchi hii.

Sasa je, Serikali iko tayari kuanzisha timu maalum ya kitalaam ikijumuisha wanasayansi waliobobea wa bahari kutoka hapa nchini pamoja na wachumi ambao wanaweza wakasaidia ni jinsi gani ya kuweza kuondoa umaskini kwa maana wananchi wanaotumia rasilimali ya uvuvi ukichanganya na wadau waliozoea uvuvi kama mimi ili kuweza kuondoa tatizo hili ambalo idara ya uvuvi sasa kazi yake imekuwa ni kuchonganisha kati ya jamii na Serikali yao. Maana sasa wananchi wanaojishughulisha wanagombana na Serikali yao kwa kisingizio cha kulinda mazingira ambao wao pia wanahusika na ulinzi wa mazingira?

**SPIKA:** Kwanza swali lenyewe huyu aliyeuliza swali Meli kubwa zinazoleta uchafuzi. Sasa hili swali lako ndio litafuta uchafuzi labda.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shah, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Kuhusu uundaji wa timu maalum yenye wana sayansi naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Shah

kwamba tayari ndani ya Wizara yetu tuna taaluma kubwa ndani ya *TAFIRI* Chuo cha Utafiti Tanzania. Ningeomba nimkaribishe Mbunge awatembelee hawa. Hawa wameshachangia kiasi kikubwa kuhusu jinsi ya kujipanga na kutumia uvuvi na rasilimali zake kujinufaisha kitaifa zaidi. Kama nilivyosema mara nyingi hapa pia, kama Serikali tumeshaandaa mpango mkakati wa kuweza kuendeleza sekta ya uvuvi na rasilimali zake.

Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira na kwa kuwa yeye ni mdau mkubwa ashiriki katika kuchangia mawazo jinsi ya kuboresha program hiyo na kupata rasilimali ili hayo anayoyasema yaweze kwa kweli kutendeka kiukamilifu. (*Makofi*)

Na. 139

## Ukamilishaji wa Nyumba Mbili Zilizochomwa Moto – Kiraracha

**MHE. DKT. AUGUSTINE LYATONGA MREMA** aliuliza:-

Mwaka 2011 Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiraracha Ndugu Lekule pamoja na ndugu yake walichomewa nyumba zao wakati wakiwa kwenye kazi zao za sungusungu na kusababisha Mwenyekiti huyo kupoteza mke na mtoto wake, kutokana na hali hiyo wananchi walichanga shilingi 26,000,000.00 kujenga nyumba mbili lakini bado zinatakiwa shilingi 16,000,000 kujenga nyumba mbili lakini bado zinatakiwa shilingi milioni 16,000,000 kukamilisha ujenzi wa nyumba hizo:-

(a) Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Vuai Nahodha aliahidi kuwa Serikali itakamilisha ujenzi ujenzi. Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia hatua gani?

(b) Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kusaidia wahanga hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nne wa Kikao cha thelathini na sita siku ya tarehe 29 Julai, 2011 wakati wa hitimisho la Bajeti ya Wizara yangu Mheshimiwa Dkt. Mrema aliwasilisha ombi la kutaka Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiraracha asaidiwe kutokana na madhara aliyopata ya kuchomewa nyumba. Mheshimiwa Waziri alilichukua jambo hilo ili kulifanyia kazi. Suala hili bado linaendelea kufanyiwa kazi na tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge pale itakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijatenga fedha kwa sababu uamuzi haujakamilika.

**MHE. DKT. AUGUSTINE LYATONGA MREMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru Waziri wa Mambo ya Ndani aliyetangulia Mheshimiwa Vuai Nahodha kwa upendo, kwa utu, kwa ukarimu katika msiba huo akachangia fedha za mfukoni shilingi milioni tatu. Wananchi wa Kiraracha wanashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mlheshimiwa Mrema, nenda kwenye swali.

**MHE. DKT. AUGUSTINE LYATONGA MREMA:** Sasa swali, kwa nini Naibu Waziri akishirikiana na Waziri wa Mambo ya Ndani usimwendee hata Waziri Mkuu ana upendo, ana utu, ana mfuko wa majanga akatoa hela kidogo ikakamilisha ile kazi.

Je, kwa kuwa inavyoonekana hili ni suala la siku nyingi, sijui kama mmeandaa utaratibu au sheria za kuweza kusaidia hawa watu wanaofanya kazi nzuri, wanaosaidia Polisi Jamii, wanaosaidia ulinzi wa Umma hawa Sungusungu ili wawe na hakika kwamba wakipata majeruhi, wakipata hasara wanapokuwa wanafanya ulinzi, Serikali inaweza ikawasaidia mara moja badala ya suala hili kuchukua karibu miaka miwili? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, kama ifuatavyo:-

Kuhusu haya maombi kuingizwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya Mfuko wa Maafa, kama nilivyosema kwamba hili suala bado tunalizingatia na

kutazama njia ya kuweza kusaidia zaidi kibinadamu kutokana na mazingira yalivyokuwa. Kwa hiyo, tunaendelea halafu ikiwa ni lazima tunaweza tukafika huko. Lakini siwezi nikasema moja kwa moja kwamba mazingira yale yanaruhusu hilo.

Kuhusu sheria ni kwamba kuna sheria ambazo zinakubali kutoa fidia kwa sungusungu, mgambo au polisi jamii ambao wanashiriki kwenye tukio au kuna ukamataji, au kusaidia polisi hasa Afisa wa Mahakama katika hatua za kazi.

Lakini kinachohitajika ni ile kwamba ameshiriki *physically* na kuna sheria nafikiri hata sheria ya makosa ya jinai kifungu 37 kinatoa maelekezo ya fidia ambayo pengine yanafanana na polisi *constable* ambaye atapata maafa kama hayo wakati wa kazi.

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru hakuna swali linalofanana na hilo na ningeshangaa kweli mngesimama mkasema linafanana na hili.

Na. 140

**Kukosekana kwa Askari wa Kike Kituo cha Polisi Kata ya Mbuguni**

**MHE. REBECCA M. MNGODO** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kabla ya swali langu namba 140 kujibiwa na Mheshimiwa Waziri niombe kwamba ajibu namba (a) tu.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anavyosema ujibu swali la (a) sasa wewe unajipangaje utajua wewe mwenyewe.

Kituo cha Polisi Kata ya Mbunguni Wilaya Arumeru Mashariki, hakina askari wa kike kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo hicho askari wa kike ili kuondoa udhalilishaji wa mahabusu wa kike unaendelea kituoni hapo?

(b) Je, ni lini sasa Serikali itajenga chumba cha mahabusu wa kike ili kuondoa hali hiyo ambayo sio sahihi kuweka mahabusu wa jinsia zote mahali pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, lenye sehemu moja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kituo cha Kata ya Mbuguni hakina askari wa kike. Hii inatokana na upungufu wa askari wa jinsia hiyo na mazingira yanayozingatiwa wakati wa kuwapangia kazi. Pamoja na ukosefu huo kazi zinazohitaji mazingara ya jinsia hufanywa kwa kutumia wanawake wengine katika eneo hilo kwa mujibu wa sheria na kazi inaendelea vizuri kiasi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimekuwa nikiwaomba Waheshimiwa Wabunge narudia kusema kwamba tushirikiane kuwahamasisha wananchi na wadau wengine kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba miundombinu inayohitajika ili vituo hivi vifanye kazi zake kikamilifu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa nasikitika kwamba majibu ya Mheshimiwa Waziri hayajaniridhisha kwa kuwa ni zaidi ya miaka 10 sasa katika Kituo hiki cha Mbuguni wanawake wamekuwa wakiwekwa katika mahabusu chini ya ulinzi wa askari wa kiume na hatujui ni kwa kiwango gani wanawake hawa wameathirika kisaikolojia na kimaumbele.

(a)Je, Serikali iko tayari kujenga nyumba ya maaskari wa kike na kuajiri maaskari wa kike ili kukomesha mara moja udhalilishaji huu wa kijinsia? (*Makofi*)

(b)Hali ya vyumba vya mahabusu hairidhishi pale Mbuguni sakafu, ukuta vimebomoka viko katika hali mbaya. Je, ni lini Serikali itajenga vyumba vya mahabusu na nyumba za askari pale Mbuguni? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Rebecca Mngodo, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na ukosefu wa askari wa kike ambaye amepangiwa kazi pale, pale kuna mahabusu ya wanawake ambayo imetengwa na mahabusu ya wanaume. Kwa hiyo, siyo sahihi kusema kwamba wanawake pengine wanashughulikiwa na wanaume. (*Makofi*)

Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu msingi ni kwamba kwenye taratibu za kipolisi pale ambapo imetokea haiwezekani askari mwanamke kusaidiwa au kupekuliwa na mwanaume huwa tunatumia wanawake ambao wako katika maeneo yale. Jambo hili ndio linalofanyika na hakujatokea tatizo la kuwa mwanaume atampekua mwanamke pale kituoni. Pamoja na yote nakiri kwamba kasoro ya kukosekana askari wa kike ni kubwa na tunahitaji tujizatiti tuongeze ili tatizo hili liondoke. Tatizo la pale kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba miundombinu kwa maana ya chini ya *PGO* au kanuni za kudumu za polisi kwenye 353 zinasema kwamba askari wa kike wapelekwa popote ambapo hakuna nyumba ya uhakika. Kwa hiyo, hili linazuia utekelezaji na uwekaji sawa wa hili tatizo. Lakini kama nilivyosema Wizara/Serikali tulifanyia kazi na naomba nitoe wito tena kwa wadau ili tusaidiane kuhakikisha kwamba miundombinu inayotakiwa iwekwe ili hili tatizo liwe historia.

**SPIKA:** Sehemu ya pili ya swali lake hujajibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Sehemu ya pili alitaka lini tutajenga kituo hicho hii

nimesema itategemea na upatikanaji wa Bajeti na ushiriki wa wadau mbalimbali.

Na. 141

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Nyakahura Hadi Murugarama**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Mwaka 2010 wakati wa kampeni, Mheshimiwa Rais akiwa Wilaya Ngara alitoa ahadi mbalimbali ikiwemo ya ujenzi wa barabara ya lami ya kutoka Mzani (Nyakahura) Wilayani Biharamulo kupitia Buseke, Keza, Rulenge, Mbuba hadi Murugarama.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo muhimu utaanza ili kutoa matumizi kwa wananchi wa Ngara ambao wana hamu ya kusikia kauli ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kupenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazima, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati wa kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2010 barabara ya Nyakahura hadi Murugarama ambayo ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilomita 85 iliahidiwa na Mheshimiwa Rais kujengwa kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 150 zimeombwa kwa ajili ya kuanza kuifanyia upembezi

yakinifu na usanifu kwa lengo la kujenga barabara hio kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa usanifu, Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yameanza kuleta matumaini kwa wananchi wa Ngara nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, huu upembuzi yakinifu na usanifu utaanza lini na utakamilika lini?

(b) Kwa kuwa barabara hii ni muhimu na inasubiriwa kwa hamu sana na Serikali ya Burundi kwa ajili ya kupitisha malori yao ya mizigo na kwa kuwa pia barabara hii ni muhimu sana kwa mgodi mkubwa wa *Kabanga Nikel* ambao ni mgodi wa pili duniani na kwa kuwa Serikali hivi karibuni itaanza ukarabati wa Barabara Rusahunga hadi Rusumo.

Je, usanifu huu ukikamilika Serikali inaweza kuanza kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami, sambamba na ukarabati wa Barabara ya Rusahunga mpaka Rusumo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ntukumazima kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kwenye jibu la msingi, nimesema tumeshaweka fedha za kuanza upembuzi yakinifu ina maana kwamba ukishapitisha bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ataisoma leo, tutaanza mchakato wa kufanya kazi hiyo ya upembuzi yakinifu. Hatuwezi kusema lini itakamilika kwa sababu itategemeana na hali ya barabara yenyewe ilivyo.

Naomba nikuhakikishie kwa sababu Rais ameshaagiza nah ii ni Serikali ya kwake, barabara hii itajengwa kulingana na matakwa ambayo wananchi wa Ngara wanayategemea.

Na. 142

**Ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Kidatu Hadi Ifakara**

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga barabara ya kidatu hadi Ifakara kwa kiwango cha lami kwa kuanzia Ziginali hadi Ifakara:-

(a) Je, ni kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa mpaka sasa?

(b) Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa kwa lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdull Rajab Mteketa Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu-Ifakara ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi-Ifakara-Mahenge yenye urefu wa jumla ya Km 178. Sehemu ya barabra kutoka Kidatu hadi Ifakara ina urefu wa Km. 73.26 kati ya hizo Km. 57.09 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na Km. 16.17 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Azma ya Seriklai ni kujenga sehemu hii yote ya barabara kwa kiwango cha lami.

Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali imekuwa ikitekeleza kazi hiyo kwa awamu. Katika awamu ya kwanza, Serikali iliweka lami Km. 10 kutoka Kiberege (Magereza) hadi Ziginali, awamu ya pili iliweka lami Km. 16.17 kutoka Kibaoni (Ifakara) hadi Ifakara Mjini, awamu ya tatu Serikali imepanga kuweka lami Km. 16.8 kutoka Ziginali hadi Kibaoni (Ifakara Mjini).

Katika awamu ya nne Serikali imepanga kuweka lami sehemu yote ya barabara iliyobaki ya kutoka Kidatu hadi Kiberege (Magereza) yenye jumla ya Km. 57.09. Sehemu hii ya barabara ipo kwenye mpango wa ujenzi a barabara ya lami kutoka Kidatu-Ifakara-Lupiro-Malinyi-Londo-Lumecha (Km. 512), ambayo utekelezaji wake upo kwenye hatua ya kuwapata Wahandisi washauri watakaoshindanishwa kwenye zabuni ili kumpata Mhandisi mshauri atakayefanya kazi ya

upembuzi yakinifu, usanifu wa kina pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

**MHE. ABDULL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. nashukuru kwa majibiu mazuri aliyotoa Naibu Waziri lakini ahadi hiyo inakuwa mwaka kila mwaka.Kwa kuwa Jimbo la Kilombero limechaguliwa kuwa ya kwanza katika kilimo cha SAGCOT na wawekezaji wengi watakuwa wanaenda kufanya kazi ya kilimo katika Jimbo la Kilombero:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza hii barabara kwa haraka?

(b) Wananchi wa Kilombero wanataka kujua kiasi gani kimetengwa katika barabara hiyo kwatika mwaka 2012/2013 na lini hasa ujenzi huu utaanza? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mteketa kama ifuatayo:-

Kwanza kabisa nakupongeza kwa kufuatilia ujenzi wa barabara hii. Lakini ni kwamba katika jibu langu la msingi, kwanza kule kuanza upembuzi yakinifu maana yake Serikali tayari imeshakubali na imeona umuhimu wa barabara hii na swali la pili kwamba kiasi ganbi kimetengwa, nakuomba Mheshimiwa Mteketa usubiri bajeti Waziri wetu atakaposoma utaona ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya barabara hii.

**SPIKA**: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda pia umeisha lakini nasikitika kwamba sina orodha ya wageni kwa hiyo itabidi twende hatua zingine. Kwa hiyo, wageni wote mlioko humu ndani mnakaribishwa, tunaingia Wizara ya Ujenzi. Waheshimiwa Wabunge mmeona siku mbili, tatu sikuwepo, tulikuwa na msiba ambae ni Dada yangu ambae alikuwa amenisaidia sana kumtunza marehemu Mama yangu kipindi chote.

Kwa hiyo, aliugua na yeye, nikawa nae kule Dar es Salaam bahati mbaya akawa ameondoka na tumemzika salama, tunashukuru kwa maombi na Dua mlizotupa. Ahsante sana. Katibu. Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Ujenzi. Hakuna wageni leo, wapo lakini hawapo. Mazoea, leo wageni hawapo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumzi Kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Wizara ya Ujenzi

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yotenakupa pole sana kwa msibauliokupata na roho ya marehemu ipumzike kwa amani.

Mheshimiwa Spika, utangulizi.Baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya

Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu tangu achaguliwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili. Amesimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na kuendelea kutekeleza yale ambayo ameahidi kwa wananchi. Aidha, nampongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa hekima katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kwa kuendelea kuongoza vema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa hekima, umahiri na busara unazotumia katika kuliongoza Bunge hili Tukufu ambalo

limefanya maamuzi mazito katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Aidha, nampongeza Naibu Spika Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa, na Wenyeviti wote wanaokusaidia katika kuongoza shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi kutoa salamu za pole nyingi kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo vya Waheshimiwa Wabunge vilivyotokea katika nyakati tofauti tangu kikao cha Bunge la Bajeti la mwaka 2011/2012. Tutawakumbuka marehemu kwa michango waliyoitoa katika vikao mbalimbali ndani na nje ya Bunge kwa lengo la kuleta maendeleo ya nchi yetu. Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi – Amina. Aidha, nawapa pole wabunge wote waliopatwa na matatizo katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, niruhusu, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzagu, nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wa viti maalum walioteuliwa na vyama vyao na waliochaguliwa hivi karibuni kutoka kwenye majimbo ya uchaguzi. Ni matarajio yetu kwamba michango yao katika Bunge hili itasaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kuwa Wabunge wa Kuteuliwa. Wabunge hao ni Mheshimiwa Profesa Dkt. Sospeter Mwijarubi Muhongo (Mb) (CCM), Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb) (CCM), Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (Mb) (CCM) na Mheshimiwa James Francis Mbatia (Mb) (NCCR-Mageuzi). Aidha, napenda kuwapongeza Watanzania waliochaguliwa na Bunge hili kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Abdallah Ali Hassan Mwinyi; Mheshimiwa Adam Omar Kimbisa; Mheshimiwa Angela Charles Kizigha; Mheshimiwa Bernard Musomi Murunya, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Maryam Yahaya Ussi, Mheshimiwa Nderakindo Perpetua Kessy, Mheshimiwa Shy-Rose Sadruddin Bhanji na Mheshimiwa Twaha Issa Taslima.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa au kuhamishwa Wizara kutokana na mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa hivi karibuni na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hali ya kiutendaji ilivyokuwa kwenye sekta ya ujenzi kwa kipindi cha 2011/2012 naomba kuishukuru Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini, kwa kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza sekta hii. Ushauri na maelekezo yao yaliiwezesha Wizara kutekeleza mipango ya utendaji kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma zitolewazo na sekta. Ushauri wa Kamati na

Wabunge wote kwa ujumla utaendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kuwapongeza na kuwashukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mbunge wa Jimbo la Bunda, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013.

Naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Waziri Mkuu, hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Waziri anayesimamia Mipango. Ni matumaini yangu kuwa maoni yao yatasaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Dira Na Dhima Ya Wizara. Dira ya Wizara ni kuwa na Barabara, Madaraja, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi zenye ubora wa kiwango cha juu, zenye gharama nafuu, zinazozingatia usalama na utunzaji wa mazingira. Aidha, dhima ya Wizara ni kuwa na Barabara, Vivuko, Nyumba za Serikali na Huduma za Ujenzi; ambazo ni salama; zinazotegemewa; zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji katika kiwango bora na kwa bei nafuu zinazoendana na mikakati ya Serikali ya

maendeleo ya kiuchumi na kijamii na wakati huo huo zikiwa endelevu kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Majukumu Ya Wizara.Wizara ya Ujenzi imekabidhiwa majukumu ya kusimamia ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko pamoja na ukarabati wa majengo ya Serikali na masuala ya ufundi. Aidha, Wizara inahusika na shughuli za uhandisi na usanifu wa ujenzi, masuala ya usalama na mazingira pamoja na uboreshaji wa utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Wizara. Pia, Wizara husimamia majukumu ya taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Malengo Ya Wizara.Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imejiwekea malengo yafuatayo: Kuunganisha miji yote Mikuu ya Mikoa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2017/18 na kuendelea kusimamia na kudhibiti wataalamu wa sekta, kwa mfano, Makandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa kutumia Sheria husika.

Aidha, Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya ujenzi. Wizara pia itaendelea kushirikiana na taasisi husika katika kushughulikia masuala mtambuka kama vile kampeni za kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, uhifadhi wa mazingira, masuala ya jinsia pamoja na uendelezaji wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano *(TEKNOHAMA)* katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Ili malengo haya yatimie Wizara itaweka mazingira mazuri ya makazi kwa watumishi wa Umma kwa kuiwezesha miradi ya ujenzi wa nyumba za kuishi pamoja na majengo ya Serikali. Wizara pia itaendelea kusimamia Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 hususan kifungu cha 29 (1) kinachohusu matumizi ya hifadhi ya barabara (Road Reserve) pamoja na Sheria nyingine zinazohusu utunzaji na utumiaji wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Mikakati Ya Wizara Katika Kufikia Malengo.Ili kuweza kutekeleza malengo yake, Wizara imeweka mikakati ya kuendelea kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha, hususan fedha za Mfuko wa Barabara zinazopelekwa Mikoani na Wilayani ikiwa ni pamoja na kuwasimamia wadau wote wanaohusika na shughuli za ujenzi ili kazi zilingane na thamani ya fedha *(value for money).*

Aidha, Wizara itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria za kisekta ili ziweze kuendana na mazingira ya mifumo ya kiutendaji na kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa na kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Community-EAC)* na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Kusini mwa Africa *(SADC)* katika kutekeleza sera za ujenzi na sera ya usalama barabarani. Wizara pia itasimamia utoaji elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 pamoja na Sheria nyingine ili miundombinu ya barabara iweze kutunzwa na kudumu kwa muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuendelea kutekeleza programu ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi *(Transport Sector Investment Programme – TSIP)* kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia stahiki *(Appropriate Technology)* katika sekta ya ujenzi na kujenga mazingira mazuri yatakayowezesha ushiriki wa sekta binafsi chini ya utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP).*

Aidha, Wizara itahakikisha Makandarasi, Wahandisi Washauri na Wasanifu Majenzi wa kizalendo wanahusishwa kikamilifu katika ujenzi wa miradi mikubwa hususan ya barabara, madaraja, nyumba na vivuko inayogharamiwa na Serikali badala ya kutegemea kampuni za nje ili kuwajengea wananchi uzoefu stahili katika sekta ya ujenzi na kupunguza kasi na wingi wa fedha zinazotokana na vyanzo vyetu kuhamishiwa nje ya nchi kwa kulipia kazi za kampuni za nje.

Mheshimiwa Spika, Mtandao Wa Barabara Nchini.Nchi ya Tanzania ina ukubwa wa eneo linalofikia kilometa za mraba 949,000 na mtandao wa barabara wenye jumla ya km 87,581. Mchanganuo wake ni kwamba, km 12,786 ni za Barabara Kuu, km. 22,214 ni za Barabara za Mikoa na Barabara za Wilaya ni kilometa 52,581. Aidha, kuna jumla ya Madaraja 4,880 katika Barabara Kuu na za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mapitio Ya Utekelezaji Wa Mpango Na Bajeti Ya Mwaka 2011/2012 Wizara ya Ujenzi ina jukumu la kusimamia sekta ya ujenzi ambayo ni kichocheo kikubwa katika ukuaji na maendeleo ya

sekta za kiuchumi na kijamii nchini. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2011/2012 ulizingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; ahadi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 (National Development Vision 2025); Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2012/2013; Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Miundombinu ya Uchukuzi *(Transport Sector Investment Program (TSIP)* ambayo ni programu ya miaka kumi (2007-2017) inayolenga kuimarisha na kuboresha miundombinu ya uchukuzi; Sera na Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira na malengo ya kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(Millennium Development Goals- MDGs).*

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji Wa Mapato Na Matumizi Ya Kawaida. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 41,873,788.00 kupitia Idara ya Utawala; Idara ya Huduma za Kiufundi na Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi. Hadi Juni, 2012, jumla ya shilingi 16,606,114.09 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 39.66 ya malengo. Sababu za kukusanya fedha pungufu ni kutokana na kuwa na zabuni chache zilizouzwa katika kipindi husika, zabuni nyingi kushughulikiwa na Wakala wa Serikali wa Huduma za Ununuzi pamoja na kupungua kwa idadi ya magari yaliyosajiliwa kutokana na uamuzi wa Serikali wa kupunguza ununuzi wa magari mapya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitengewa shilingi 245,440,294,000.00 kwa ajili ya

matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,974,670,219.00 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na mishahara shilingi 15,829,643,781.00. *(Makofi)*

Hadi kufikia Juni, 2012, Shilingi 242,004,520,900.00 sawa na asilimia 98.60 ya bajeti zilitolewa na HAZINA kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 16,763,849,878.00 ni mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi, shilingi 221,585,980,000.00 ni fedha za Mfuko wa Barabara sawa na asilimia 100.00 ya Bajeti na shilingi 3,654,691,071.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Miradi Ya Maendeleo Kwa Mwaka 2011/2012.Katika mwaka wa 2011/2012 Wizara ilitengewa shilingi 1,155,976,936,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 526,106,746,000.00 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 629,870,193,000.00 zilikuwa ni fedha za nje. Fedha zilizotolewa hadi Juni, 2012 ni shilingi 565, 037, 320,000.00 (shilingi 367, 829, 870,000.00 fedha za ndani na shilingi 197, 207, 460,000.00 fedha za nje).

Mheshimiwa Spika, Miradi Ya Barabara. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ilipanga kuendelea kukamilisha ujenzi wa km 866 za Barabara Kuu kwa kiwango cha lami, kukarabati km 250.10 kwa kiwango cha lami na madaraja 11. Hadi kufikia Juni, 2012, km 305 za barabara Kuu zilikamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, ukarabati wa km 78.4 za Barabara Kuu ulikamilika kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa madaraja ya Malagarasi

(Daraja la Kikwete) Mkoani Kigoma na Nangoo Mkoani Mtwara uliendelea. Kuhusu matengenezo ya Barabara Kuu, lengo lilikuwa ni kuzifanyia matengenezo km 9,931.7 na madaraja 1,124. Hadi kufikia Juni, 2012 km 7,721.7 za Barabara Kuu na madaraja 726 yalifanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Barabara za Mikoa, Wizara ilipanga kujenga km 981 kwa kiwango cha changarawe, km 29.5 kwa kiwango cha lami na kukamilisha ujenzi wa madaraja 24. Kati ya hizo km 327.8 za changarawe, km 10 za lami na madaraja manane (8) yalipangwa kutumia fedha za mfuko wa barabara. Hadi kufikia Juni 2012, jumla ya km 463.17 zimefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe, km 17.15 zilijengwa kwa kiwango cha lami na ujenzi wa daraja la Lubiga Mkoani Simiyu na Kalulu Mkoani Ruvuma ulikamilika. Aidha, Wizara ilipanga kuzifanyia matengenezo barabara za Mikoa zenye urefu wa km 20,703.6 na madaraja 1,200. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 12,050.6 zilikuwa zimekamilika na madaraja 703 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kudhibiti uzito wa magari iliendelea katika mwaka wa fedha 2011/12 kwa kutumia mizani 26 za kudumu na mizani 17 zinazohamishika katika barabara Kuu za lami. Hadi Juni, 2012, magari yapatayo 2, 078,260 yalipimwa na kati ya hayo magari 482,638 (sawa na asilimia 23.22 ya magari yaliyopimwa) yalikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya fedha iliyokusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida ilikuwa ni shilingi milioni 3,260.53.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya barabara kama nitakavyoeleza hapa chini.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bagamoyo-Makofia-Msata (km 64), kazi ilianza tarehe 11 Agosti 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 89.61. Mkandarasi ni *ESTIM* na Msimamizi ni *Gauff.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 29 za tuta la barabara, *km 28* za tabaka la chini la msingi, km 28 za tabaka la juu la msingi na km 27 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Usagara – Geita – Bwanga – Buzirayombo – Kyamyorwa (*km 422)* unahusisha ujenzi wa barabara hii katika sehemu tatu zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo – Geita (km 220) ambao ulikamilika Februari, 2008;

Sehemu ya pili ilihusu ujenzi wa barabara ya Geita – Sengerema (km 50) na Sengerema – Usagara (km 40) ambayo ujenzi wake ulianza Februari, 2008 na umekamilika; na

Sehemu ya tatu inahusu ujenzi wa barabara ya Uyovu – Bwanga – Biharamulo *(km 112).* Utekelezaji wa ujenzi kwa sehemu hii upo katika maandalizi ambapo

zabuni zimetangazwa na kazi za ujenzi zinategemewa kuanza mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Tabora – Urambo *(km 94)* umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

Tabora-Ndono *(km 42):*Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 51.35 na Mkandarasi ni *China Henan International Cooperation Group Co. Limited* na Msimamizi ni Kampuni ya *SAI Consultant.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya *km 12* za kusafisha barabara na km 10 za tuta la barabara zimekamilika.

Ndono-Urambo (km 52):Mkataba ulisainiwa tarehe 30 Julai 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 59.77 na Mkandarasi ni *China Civil Engineering* na Msimamizi ni *Crown Tech Consult.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 9 za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Uvinza – Kidahwe (km 76.6) ulikwishaanza na kazi inatarajiwa kukamilika tarehe 23 Juni, 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 78.24 na Mkandarasi ni *China Henan International Cooperation Group Co. Limited* na Msimamizi ni *Intercontinental Technocra*ts.

Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 52 za tuta la barabara, km 21 za tabaka la chini, km 15 za tabaka la juu na km 15 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 54.00. Aidha, ujenzi wa Daraja la Malagarasi (Daraja la Kikwete) na barabara

zake (km 48) unaendelea na kazi inatarajiwa kukamilika Desemba, 2013. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 78.91 na Mkandarasi ni Hanil *Engineering* na Msimamizi ni Cheil Engineering wa Korea. Hadi kufikia Juni, 2012 kazi za usanifu wa daraja zimekamilika, ujenzi wa msingi wa daraja na mihimili yake umekamilika, ujenzi wa *"deck"* umeanza na km 3 za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Marangu-Rombo Mkuu na Mwika-Kilacha (km 34), kazi ilianza tarehe 17 Juni, 2008. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 25.1, Mkandarasi ni General Nile na Msimamizi ni *UNETEC.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 32 za tuta la barabara, km 30 za tabaka la chini, km 26 za tabaka la juu la msingi na km 26 za lami zimekamilika.

Kwa upande wa barabara ya Kwa Sadala-Masama (km 12.5), kazi ilianza tarehe 10 Machi 2010 na gharama ni shilingi bilioni 5.34. Mkandarasi ni Atlantic na Msimamizi ni *Crown Tech.* Jumla ya km 9.5 za tuta la barabara, km 7 tabaka la chini, km 5.5 tabaka la juu na km 1.6 za lami zimekamilika. Aidha, barabara ya Kibosho Shine – International School (km 12.5), kazi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2012. Gharama ni shilingi bilioni 8.93 na Mkandarasi ni *DOTT Services* na Msimamizi ni *Crown Tech.* Jumla ya *km 15* za tuta la barabara, *km 11* za tabaka la chini na km 3 za tabaka la juu zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Rau Madukani-Uru Njari (km 2.5), kazi za ujenzi zinaendelea. Gharama ni shilingi bilioni 4.88 na Mkandarasi ni *DOTT Services* na

Msimamizi ni *Inter-Consult.* Hadi Juni,2012 jumla ya km 10 za tuta la barabara na km 9.5 za tabaka la chini na la juu zimekemilika. Kwa upande wa barabara ya Kawawa – Nduoni – Marangu Mtoni *(km 31.5)* kazi za ujenzi zinaendelea. Gharama ni shilingi bilioni 9.10 na Mkandarasi ni *DOTT Services* na Msimamizi ni kampuni ya *Inter-Consult.* Hadi Juni 2012 jumla ya km 10 za tuta la barabara, km 4 za tabaka la chini na km 2 za tabaka la juu zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Mbwemkulu (km 95) ulikwishakamilika. Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi ilikataa kuipokea barabara hii kwa kuwa haikukamilika kwa kiwango kilichokusudiwa na hivyo kuwepo kwa marekebisho yanayohitaji kufanywa. Mkandarasi anaendelea na marekebisho ya kasoro zilizojitokeza ili barabara hiyo iweze kukabidhiwa rasmi kulingana na mahitaji ya Mkataba. Hadi kufikia Juni, 2012 kazi ya kufanya marekebisho imekamilika kwa asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami cha barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) uligharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa utaratibu wa usanifu na ujenzi *(Design and Build).* Mradi huu ulikamilika tarehe 22 Novemba, 2009 na bado upo kwenye kipindi cha uangalizi hadi Novemba, 2012. Kwa mwaka 2011/2012 fedha zilitengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Manyoni – Isuna (km 54) kwa kiwango cha lami ulikamilika tarehe 7 Januari, 2011 na kipindi cha

uangalizi cha miaka mitatu kitamalizika tarehe 7 Januari, 2014. Fedha zilizotengwa mwaka 2011/2012 zilikuwa kwa ajili ya sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi. Kwa upande wa barabara ya Isuna – Singida (km 63) ujenzi ulikamilika tarehe 30 Juni, 2008 na kipindi cha uangalizi wa mradi cha miaka mitatu kilimalizika tarehe 30 Juni, 2011. Fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka 2011/2012 zilikuwa ni za malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Mandela (km 16.8) ulianza tarehe 1 Oktoba 2007 na ulikamilika tarehe 30 Juni 2011. Kipindi cha uangalizi kiliisha mwezi Juni, 2012. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 41.22, Mkandarasi ni Maltauro/Spencon na Msimamizi ni *B CEOM.*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa barabara ya Dumila – Kilosa (km 63) umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

*Dumila-Rudewa (km45):* Kazi ilianza tarehe 1 Februari 2009 na inatarajiwa kukamilika tarehe 10 Februari 2013. Gharama ni shilingi bilioni 41.93 na Mkandarasi ni *China Civil Engineering* na Msimamizi ni SMEC. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 32 za tuta la barabara na km 20 za tabaka la chini la msingi zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 62.

*Rudewa-Kilosa (km 18):* Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Sumbawanga-Matai-Kasanga *Port (km 112),* ulianza tarehe 13 Januari, 2010 na gharama ni shilingi bilioni 133.29. Mkandarasi ni *China Railway 15 Bureau Group Corporation (CR15G) na Henan Pronvincial Newcentury Road and Bridge Consultants Ltd.* kutoka China. Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited* ikishirikiana na kampuni ya *Apex Engineering.* Kazi inafanyika kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga *(Design & Build).* Hadi Juni 2012 kazi ya usanifu wa kina imefikia asilimia 85, kilometa 12 za kusafisha barabara na kilomita 10 za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Kawawa Junction-Mwenge-Tegeta *(km 17),* sehemu ya Mwenge – Tegeta kazi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika tarehe 15 Agosti, 2013. Gharama ni shilingi billioni 88.403 kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan na Mkandarasi ni Konoike na Msimamizi ni *Ingerosec.* Aidha, sehemu ya Mwenge – *Kawawa Junction (km 4.3)* itafadhiliwa pia na Serikali ya Japan. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 12.3 za tuta la barabara, km 11.3 za tabaka la chini na km 5 za tabaka la juu zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Kyaka-Bugene (km 59.1). Kazi za ujenzi zimekwishaanza. Gharama ya ujenzi wa mradi huo ni shilingi bilioni 64.96. Mkandarasi ni kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Company Limited* na

Msimamizi ni kampuni ya *SAI Consultant.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 9 za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Isaka – Lusahunga yenye urefu wa km 242 umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

*Isaka-Ushirombo (km 132):* Kazi ilianza tarehe 18 Februari 2010 na inatarajiwa kukamilika tarehe 17 Mei, 2013. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 145.34. Mkandarasi ni kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Company Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 72.2 za tuta la barabara, km 72.2 za tabaka la chini na km 72.2 za tabaka la lami zimekamilika. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla ni asilimia 54.

*Ushirombo-Lusahunga (km 110):* Kazi ilianza tarehe 18 Februari 2010 na gharama ya shilingi bilioni 114.56. Mkandarasi ni kampuni ya Strabag na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 53.3 za tuta la barabara, km 53.4 za tabaka la chini na km 53.3 za tabaka la lami zimekamilika. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla ni asilimia 46.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Manyoni-Itigi-Tabora (km 264) umegawanywa katika sehemu tatu zifuatazo:-

*Tabora-Nyahua (km 85):* Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na gharama ni shilingi bilioni 93.41. Mkandarasi ni kampuni ya *Chongqing Foreign Trade* na Msimamizi ni kampuni ya *Consulting*

*Engineering.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 6 za tuta la barabara zimekamilika na kazi inaendelea.

*Manyoni-Itigi-Chaya (km 89.4):* Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na gharama ni shilingi bilioni 109.64. Mkandarasi ni *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 13 za tuta la barabara zimekamilika na kazi inaendelea.

*Chaya – Nyahua (km 90):* Usanifu wake umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi. Kwa barabara ya Korogwe – Handeni (km 65) kazi inaendelea na inatarajiwa kukamilika tarehe 14 Mei, 2013. Gharama ni shilingi bilioni 63.2. Mkandarasi ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *SMEC Internacional (Pty) Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 18 za tuta la barabara, km 18 za tabaka la chini, km 7.2 za tabaka la juu na km 7.2 za lami zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Handeni – Mkata (km 54) kazi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Mei, 2013. Gharama ni shilingi bilioni 57.34. Mkandarasi ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *SMEC Internacional (Pty) Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012, jumla ya km 49 za tuta la barabara, km 22 za tabaka la chini, km 15 za tabaka la juu na km 15 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa jumla ni asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, kwa barabara ya Mwandiga – Manyovu (km 60) ambayo inaunganisha Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi kwa kiwango cha lami ujenzi wake ulikwishakamilika na kwa sasa uko katika kipindi cha uangalizi hadi tarehe 31 Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Ndundu-Somanga (km 60) ulianza tarehe 15 Julai, 2008 na unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 58.82. Mkandarasi ni kampuni ya *M. A. Kharafi & Sons Limited* ya Kuwait na Msimamizi ni kampuni ya *Engineering Systems Group (ESG)* ya Kuwait ikishirikiana na kampuni ya *Mouchel Parkman* ya Uingereza na kampuni ya *M-Konsult Limited* ya Tanzania. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 41 za tuta la barabara, km 42 za tabaka la chini la msingi, km 21 za tabaka la juu la msingi na km 20 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 76.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Kidatu – Ifakara (km 30), lengo ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami nyepesi yaani, *Otta Seal*. Hadi kufikia Juni, 2012 kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012, Wizara ilipanga kufanya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina wa barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359) kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Mkataba wa kazi hii ulisainiwa tarehe 8 Juni, 2009 kwa muda wa miezi 20. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika na maandalizi ya

kutangaza zabuni za kazi za ujenzi kwa sehemu ya Tabora – Sikonge (km 70) yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, lengo la mradi wa barabara ya Makutano – Natta – Mugumu / Loliondo – Mto wa Mbu (km 328) ni kujengwa kwa kiwango cha lami. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kufanya usanifu wa kina. Mikataba kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa sehemu ya Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo (km 239) na Mto wa Mbu – Loliondo (km 213) ilisainiwa tarehe 26 Agosti, 2009. Kazi ya usanifu wa kina ilishakamilika na maandalizi ya kutangaza zabuni za kazi za ujenzi kwa sehemu ya Makutano – Natta (km 50) yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Ibanda – *Itungi Port (km 26)* unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa sehemu ya Ibanda – Uyole kwa kiwango cha lami na kufanya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Kyela – *Itungi Port.* Hadi kufikia Juni, 2012 mradi ulikuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Tanga – Horohoro (km 65), kazi ilianza tarehe 22 Desemba, 2009 na ujenzi umekamilika Mei, 2012 kwa kutumia fedha za MCC. Gharama ni shilingi bilioni 69.894. Mkandarasi ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Intercontinental Consultants and Technocrats (ICT).*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nzega-Tabora (km 115) imegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

*Nzega-Puge (km 56.1):* Mkandarasi ni Kampuni ya *China Communications Construction Company Limited* na Msimamizi ni Kampuni ya *SMEC International (Pty) Limited*. Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 66.36. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 12 za barabara zimesafishwa, makalvati 6 na km 6 za tuta la barabara zimekamilika. Ujenzi unaendelea.

*Puge-Tabora (km 58.8):* Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 62.74. Mkandarasi ni Kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International (Pty) Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 20 za barabara zimesafishwa, makalvati 8 na km 15 za tuta la barabara zimekamilika. Ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga-Mpanda-Nyakanazi (km 829) imegawanywa katika sehemu nne zifuatazo:-

*Sumbawanga-Kanazi (km 75):* Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 78.84. Mkandarasi ni kampuni ya *Jiangxi Geo-Engineering (Group) Corporation.* Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited* ikishirikiana na kampuni ya *Apex Engineering Company Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 19 za tuta la barabara na km 1.1 za tabaka la chini zimekamilika.

*Kanazi- Kizi- Kibaoni (km 76.6):* Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2009 kwa kipindi cha miezi 36. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 82.84. Mkandarasi ni kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Company Limited.* Msimamizi ni

kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 8.3 za tuta la barabara zimekamilika.

Kizi-Sitalike-Mpanda (km 95): Usanifu umekamilika na zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sitalike-Mpanda (km 35) zimetangazwa. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2012/2013.

*Mpanda-Uvinza-Kidahwe – Kasulu-Nyakanazi (km 575.17):* Ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea kwa sehemu ya Uvinza-Kidahwe (km 76.6). Kwa sehemu ya Mpanda-Uvinza (km 188.57) na Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi (km 310) Usanifu umekamilika na maandalizi ya kutangaza Zabuni za kazi ya ujenzi kwa sehemu ya Kidahwe–Kasulu-Nyakanazi yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Musoma-Mwanza/*Mara Border (km 85.5)* mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 85.368 na Mkandarasi ni *China Henan International Cooperation Group Company Limited.* Hadi Juni, 2012 jumla ya kilometa 51 za tuta la barabara na kilometa 8 za tabaka la chini zimekamilika. Kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa barabara ya Mziha – Turiani – Magole (km 84.6) umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:

Magole – Turiani (km 48): Kazi ilianza tarehe 3 Machi, 2010. Gharama ni shilingi bilioni 48.2 na

Mkandarasi ni *China Civil Engineering.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 23 za tuta la barabara na makalvati 12 yamekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 51.

Turiani – Mziha (km 36.6): Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Bariadi-Lamadi (km 71.8), kazi za ujenzi zinaendelea. Gharama ni shilingi bilioni 67.41 na Mkandarasi ni *China Communication* na Msimamizi ni *Intercontinental Technocrats.* Hadi kufikia Juni, 2012, km 3.3 za tuta la barabara na km 1 ya tabaka la chini zimekamilika na kazi zinaendelea.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilipanga kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Ipole – Rungwa (km 95) kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina haukuweza kuanza kuokana na upungufu wa fedha. Mradi huu sasa umepangwa kufanyiwa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali ilipanga kuanza kutekeleza mradi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310) kwa kujenga kwa awamu kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, mradi huu haukuweza kuanza kutokana na upungufu wa fedha. Mradi huu sasa umepangwa kuanza kutekelezwa mwaka wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ilipanga kufanya Upembuzi Yakinifu pamoja na Usanifu wa Kina wa barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia *Airport Access Road) (km 14).* Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha, mradi haukuweza kuanza na sasa umepangwa kuanza mwaka wa fedha 2012/2013. Barabara ya Dodoma – Chuo Kikuu cha Dodoma *(Dodoma University Road) (km 12)* itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani. Maandalizi ya kutangaza zabuni yanaendelea. Ujenzi utaanza mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Tunduma-Sumbawanga (km 231), unagharamiwa kwa fedha za *Millennium Challenge Corporation (MCC)* ya Marekani na umegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

*Tunduma-Ikana (km 63.7):* Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 82.52. Mkandarasi ni *Consolidated Contractors Group S.A.L. (CCC) (Offshore)* na Msimamizi ni kampuni ya *Egis BCEOM.* Hadi kufikia Juni, 2012, jumla ya km 28 za barabara zimesafishwa. Km 1 ya tuta la barabara na makalavati 23 yamekamilika. Kazi zinaendelea.

Ikana-Laela (km 64.2): Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 76.1. Mkandarasi ni kampuni ya *China New Era Internacional Engineering Corporation* na Msimamizi ni kampuni ya *Egis BCEOM.* Hadi kufikia Juni,

2012, km 10 za tuta la barabara na km 1 ya tabaka la chini zimekamilika. Kazi zinaendelea.

Laela-Sumbawanga (km 95.1): Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 76.1. Mkandarasi ni kampuni ya *Aarsleef – BAM Internacional Joint Venture V.O.F* na Msimamizi ni kampuni ya *Egis BCEOM.* Hadi kufikia Juni, 2012, jumla ya km 24 za tuta la barabara, km 22 za tabaka la chini na km 19 za tabaka la juu zimekamilika. Kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa barabara ya Kagoma – Biharamulo - Lusahunga (km 154), kazi ilianza tarehe 16 Septemba, 2009. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 191.46. Mkandarasi ni kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Co. Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Intercontinental Consultants and Technocrats (ICT).* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 136 za tuta la barabara, km 123 za tabaka la chini la msingi, km 98 tabaka la juu la msingi na km 98 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa jumla ni asilimia 65.60.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Arusha-Namanga (km 105), kazi ilianza tarehe 14 Julai, 2008 na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 81.77. Mkandarasi ni kampuni ya *China Geo Engineering* na Msimamizi ni kampuni ya John Burrow. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 103 za tuta la barabara, km 103 za tabaka la chini, km 103 tabaka la juu na km 103 za lami zimekamilika. Aidha, ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha *(One Stop Border Post -*

*OSBP)* unaendelea. Maendeleo ya mradi kwa jumla ni asilimia 82.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa barabara ya Minjingu – Babati – Singida yenye urefu wa km 223.5, utekelezaji wake umegawanywa katika sehemu tatu zifuatazo:

*Singida-Kateshi (km 65.1):* Kazi ilianza tarehe 11 Machi, 2009 na imekamilika kwa asilimia 100. Gharama ni shilingi bilioni 51.63. Mkandarasi ni kampuni ya Sinohydro *Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *AFRICON.*

*Kateshi-Dareda (km 73.8):* Kazi ilianza tarehe 11 Machi, 2009. Gharama ni shilingi bilioni 64.14. Mkandarasi ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *COWI.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 74 ya tuta la barabara, km 70 tabaka la chini, km 61 za tabaka la juu na km 56 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa jumla ni asilimia 95.

*Dareda-Babati-Minjingu (km 84.6):* Kazi ilianza tarehe 11 Machi, 2009. Gharama ni shilingi bilioni 84.92. Mkandarasi ni kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Company Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Crown Tech.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 84 ya tuta la barabara, km 79 tabaka la chini na km 75 tabaka la juu na km 72 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa jumla ni asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Arusha-Minjingu (km 104) mkataba wa ukarabati kwa gharama ya shilingi bilioni 75.51 ulisainiwa tarehe 12 Mei, 2011. Ukarabati unagharamiwa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mkandarasi ni Kampuni ya Sogea Satom na Msimamizi ni Kampuni ya *LEA Associates.* Hadi kufikia Juni, 2012 Mkandarasi ameanza kusaga kokoto na kujenga barabara za mchepuo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilwa/Dar es Salaam - Mbagala (km 12), Bendera Rangi Tatu – Mtoni Mtongani (km 5) kazi ilianza Novemba 2006 na kukamilika Machi 2008. Sehemu ya Mbagala Zakhem mpaka Mbagala Rangi Tatu yenye urefu wa km 1.5 kazi ilianza Aprili, 2011 na kukamilika Aprili, 2012. Hata hivyo, sehemu ya Mtoni Mtongani hadi Mbagala Zakhem yenye urefu wa km 5.1 ujenzi wake ulioanza Aprili, 2008 na kukamilika haikupokelewa kutokana na mapungufu yaliyojitokeza. Mkandarasi kampuni ya KAJIMA amekubali kurudia kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe na kazi ya kurudia imeanza Juni, 2012.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa barabara ya Msimba – Ikokoto – Mafinga (km 219) umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

Iyovi-Kitonga Gorge (km 86.30) na Ikokoto – Iringa (km 60.90): *na mchepuo wa kuingia Iringa Mjini (km 2.1)* Kazi ya ukarabati imefikia asilimia 100 kwa fedha za *DANIDA.* Gharama ni shilingi bilioni 127.7. Mkandarasi ni kampuni ya *Aarslef-Interbeton* na Msimamizi ni kampuni ya *COWI.*

Iringa-Mafinga (km 69.4): Kazi ilianza tarehe 9 Septemba, 2011 kwa fedha za *DANIDA.* Gharama ni *Euro 38,500,000.* Mkandarasi ni kampuni ya Aarslef na Msimamizi ni kampuni ya *COWI.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 14.5 za tuta la barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Korogwe – Mkumbara - Same *(km. 172)* umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

Korogwe – Mkumbara (km 76): Mkataba ulisainiwa Januari 2012 na inatarajiwa kukamilika Julai 2014. Mkandarasi ni kampuni ya Strabag kwa gharama ya shilingi bilioni 62.87 na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Partner.* Hivi sasa Mkandarasi yupo kwenye kipindi cha maandalizi *(mobilization period).*

Mkumbara – Same section (96 km)*:*Mkataba ulisainiwa Januari 2012 na inatarajiwa kukamilika Julai 2014. Mkandarasi ni kampuni ya *DOTT Services* kwa gharama ya shilingi bilioni 65.13. Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Partner.* Hivi sasa Mkandarasi yupo kwenye kipindi cha maandalizi *(mobilization period).*

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi *(km. 115)* umegawanywa katika sehemu tatu zifuatazo:-

Mbeya-Lwanjilo (km 36): Baada ya Mkandarasi wa awali (Kundan Singh) kushindwa kazi na kufukuzwa,

Mkataba mpya ulisainiwa Desemba, 2010. Gharama ni shilingi bilioni 55.38. Mkandarasi ni kampuni ya *China Communications Construction Company Ltd.* na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 10 za tuta la barabara zimekamilika.

Lwanjilo-Chunya (km 36): Kazi ilianza tarehe 5 Agosti, 2009 kwa gharama ya shilingi bilioni 40.28. Mkandarasi ni kampuni ya China Communications Construction Company Limited na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited* ikishirikiana na kampuni ya *Data Consult Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 15 za tuta la barabara na makalvati zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 43.

*Chunya-Makongorosi (km 43):* Usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Chalinze-Segera-Tanga (km 245), ukarabati umekamilika Oktoba, 2011 katika sehemu ya Chalinze - Kitumbi (km 125) upo katika kipindi cha uangalizi wa ufanisi wa mradi kwa miaka miwili. Kwa sehemu ya Kitumbi – Segera – Tanga (km 120) kazi inaendelea na hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 17 za tuta la barabara, km 16 za tabaka la chini na km 15 za tabaka la juu na km 2 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 24. Mradi huu unagharamiwa na fedha za *DANIDA.*

Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya Dodoma – Iringa (km 260) unagharamiwa na fedha za mkopo toka ADB na JICA Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 13 Januari, 2011 na kazi inatarajiwa kukamilika mwezi Januari 2014. Mradi umegawanyika katika sehemu tatu kama ifuatavyo:-

*Sehemu ya Iringa – Migori (km 95.10):* Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 84.22. Mkandarasi ni Kampuni ya *China Sichuan International Corporation Company Ltd* na Msimamizi ni *Egis International*. Hadi kufikia Juni, 2012, jumla ya km 20 za tuta la barabara na km 13 za tabaka la chini zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 11.

*Migori – Fufu Escarpment (km 93.80)*: Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 73.61. Mkandarasi ni Kampuni ya *China Sichuan International Corporation Company Ltd.* na Msimamizi ni Bonfica S.p.A . Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 15 za tuta la barabara na km 14 za tabaka la chini zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa jumla ni asilimia 12.00.

*Fufu Escarpment – Dodoma (km 70.90):* Gharama ya ujenzi ni shilingi bilioni 64.33. Mkandarasi ni Kampuni ya China *Communication Construction Company Ltd.* na Msimamizi ni *LEA International.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 6 za tuta la barabara na km 2 za tabaka la chini zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 9.50.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma – Babati (km 261) umegawanywa katika sehemu zifuatazo:-

*Dodoma – Mayamaya (km 43.60):* Kazi ilikwishaanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2012. Gharama ni shilingi bilioni 40.61. Mkandarasi ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Consulting Engineering Services.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 19.2 za tuta la barabara zimekamilika.

*Mayamaya - Mela – Bonga (km 188.15).* Maandalizi ya ujenzi katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 yanafanyika kwa kutumia fedha za mkopo wa *ADB* na *JICA.*

*Bonga – Babati (km 19.2)* Ujenzi wa barabara hii ulikwishaanza. Gharama ni shilingi bilioni 19.69. Mkandarasi ni kampuni ya *China Henan International Cooperation Group Company Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Crown Tech Consult Ltd.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 19.2 za tuta la barabara, km 13.2 za tabaka la chini, km 11 za tabaka la juu na km 11 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 60.3.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Masasi – Songea – *Mbamba Bay (km 649)* utekelezaji wake umegawanywa katika sehemu nane zifuatazo:-

*Masasi – Mangaka (km 54):* Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 21.62. Mkandarasi ni Kampuni ya TOKURA wa Japan na Msimamizi alikuwa ni kampuni ya *Ingerosec Corporation ya Japan.* Kazi za ujenzi

zimekamilika. Mradi uligharamiwa na Serikali ya Japan na Serikali ya Tanzania.

*Mangaka – Tunduru (km 137):* Upembuzi yakinifu na usanifu umekamilika. Kazi za ujenzi zitaanza katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 kwa fedha za mkopo kutoka *ADB na JICA.*

*Tunduru – Matemanga (km 58.70).* Kazi za ujenzi zinaendelea. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 63.41. Mkandarasi ni kampuni ya *Progressive Construction Limited-Higleig Joint Venture* na Msimamizi ni kampuni ya Wanjohi *Consulting Engineers* ikishirikiana na kampuni ya *ACE Consultants Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 4 za tuta la barabara zimekamilika.

*Matemanga – Kilimasera (km 68.20):* Kazi za ujenzi zinaendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 64.02. Mkandarasi ni kampuni ya *Progressive Constructions Limited-Higleig Joint Venture* na Msimamizi ni kampuni ya *Sheladia Associates Inc.* ya Marekani ikishirikiana na kampuni ya *Ambicon Engineering Limited.* Hadi kufikia Mei, 2012 jumla ya km 5 za tuta la barabara zimekamilika.

*Kilimasera - Namtumbo (60.70 km).* Kazi za ujenzi zinaendelea kwa gharama ya shilingi bilioni 53.23. Mkandarasi ni kampuni ya *Progressive Constructions Limited – Higleig Joint Venture* na Msimamizi ni kampuni ya SGI – *Studio Galli Ingegneria S.p.A* ikishirikiana na kampuni ya *Sari Consulting S.r.l.* na kampuni ya KAPSEL. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 10.5 za tuta la barabara zimekamilika na kazi zinaendelea.

*Namtumbo – Songea (km 67.00):* Kazi za ujenzi zinaendelea kwa gharama ya ujenzi ni dola milioni 46.96. Mkandarasi ni Kampuni ya Sogea Saton na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited.* Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 30 za tuta la barabara na km 27 za tabaka la chini zimekamilika.

*Peramiho – Mbinga (km78.00)*: Kazi za ujenzi zinaendelea. Mradi huu unagharamiwa na *MCC.* Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 79.80. Mkandarasi ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Limited* na Msimamizi ni kampuni ya *Nicholas O'Dwyer & Company Limited*. Hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 39 za tuta la barabara, km 17.20 za tabaka la chini, km 6 za tabaka la juu na km 6 za lami zimekamilika.

*Mbinga – Mbamba Bay (km 66.00):* Upembuzi Yakinifu na Usanifu umekamilika. Hatua inayofuata ni kutafuta fedha katika bajeti ya 2012/2013 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu inayoendelea ni:- Bagamoyo (Makurunge) – Saadani – Pangani - Tanga (km178); Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chamba – Kwamtoro - Singida (km 460); Mafinga - Igawa (km 140.60); *Flyover* ya *TAZARA;* barabara ya Same – Himo - Marangu na Mombo – Lushoto (km 104); Makambako – Songea (km 295); Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200); Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 140); Lusahunga –

Rusumo na Kobero - Nyakasanza (km 150); Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396).

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa *Flyover* ya *TAZARA* umekamilika kwa ufadhili wa *JICA.* Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka 2012/2013 na gharama zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu iliyokamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni Sumbawanga-Mpanda-Kanyani-Nyakanazi (km 562); Ipole-Koga-Mpanda (km 359); Chunya-Makongolosi-Rungwa-Mkiwa (km 455) na tathmini ya mazingira barabara ya Chalinze-Segera-Tanga (km 245).

Mheshimiwa Spika, miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu ambayo iko katika hatua za zabuni ni Sumbawanga-Matai-Kasanga Port sehemu ya Matai-Kasesya km 45); Ifakara-Mahenge (km 67); Kibondo-Mabamba (km 35); Mpemba-Isongole (Tanzania/Malawi) (km 49); Omugakorongo – Kigarama - Murongo (km 105); Kyaka – Bugene - Kasulo/Benaco (sehemu ya Bugene-Kasulo/Benaco (km 112); Daraja la Mto Wami, barabara ya Mtwara-Newala-Masasi (km 209) na Daraja la Mwiti; Kolandoto-Lalago-Mwanhuzi-Matala-*Oldean Junction (km 328);* na Tabora-Ipole-Rungwa (sehemu ya Ipole-Rungwa km 95).

Mheshimiwa Spika, Miradi Mikubwa ya Ujenzi wa Madaraja. Lengo la mradi huu ni kujenga daraja la

Nanganga na Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru; daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti; daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge; daraja la Maligisu kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi – Maligisu; daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga; daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga – Manonga; daraja la Ruhekei kwenye barabara ya Mbinga – *Mbamba Bay* na ununuzi wa Bailey Bridges za dharura.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umefikia hatua zifuatazo:-

*Madaraja ya Nanganga na Nangoo*Ujenzi wa daraja la Nanganga umekamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 2.54. Aidha, hadi kufikia Juni, 2012 ujenzi wa daraja la Nangoo unaendelea na gharama ni shilingi bilioni 4.8.

*Daraja la Sibiti.* Mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Daraja la Sibiti umekamilika na maandalizi ya kusaini mkataba wa ujenzi yanaendelea.

*(xlvi) Daraja la Kilombero.* Zabuni kwa ajili ya ujenzi tayari zimeitishwa na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2012/2013.

*Daraja la Maligisu*Hadi kufikia Juni, 2012 ujenzi wa mihimili ya daraja ulikuwa umekamilika.

*Daraja la Kavuu.* Kwa Daraja la Kavuu lengo ni kulijenga kwa daraja la chuma *Mabey Bridge. Quotation* kwa ajili ya ununuzi wa vyuma vya daraja zimepokelewa. Ununuzi na ujenzi wa daraja utafanyika mwaka 2012/2013.

*Daraja la Mbutu.* Kwa daraja la Mbutu, mkataba wa ujenzi umesainiwa Machi 2012 kati ya *TANROADS* na kampuni 13 za Kitanzania kwa gharama ya shilingi bilioni 12.34. Maandalizi ya kuanza ujenzi wa daraja yanaendelea na hadi mwishoni mwa Juni, 2012 maandalizi ya vifaa vya ujenzi na wafanyakazi yalikuwa yamekamilika. *Daraja la Ruhekei.*

Hadi kufikia Juni, 2012 kazi za ujenzi wa msingi wa daraja na mihimili yake *(abutments and intermediate piers)* zimekamilika. Maendeleo ya mradi wa jumla ni asilimia 90.

*Daraja la Ruhuhu.* Mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa daraja pamoja na Bwawa la umwagiliaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara ilikuwa na lengo la kuanza ujenzi wa Daraja la Kigamboni eneo la Kurasini. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 9 Januari, 2012 kati ya Mkandarasi *China Railway Construction Company Limited* kwa kushirikiana na *China Major Bridge Engineering Company Limited* na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(National Social Security Fund (NSSF).*

Mradi huu unagharamiwa na *NSSF* na Serikali ya Tanzania. Hadi kufikia Juni, 2012 ujenzi wa daraja hili umeanza kwa Mkandarasi kufanya maandalizi ya ujenzi. Daraja litagharimu shilingi bilioni 214.64.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Ruvu katika barabara ya Dar es Salaam – Morogoro, mkoani Pwani ulikamilika mwaka 2009. Fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho kwa Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kupunguza Msongamano wa Magari Katika Jiji la Dar-es-Salaam. Lengo la mradi huu ni kujenga, kufanya upanuzi na kukarabati barabara za Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari yanayotumia barabara katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na mpango wa kujenga *Fyovers* ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Usanifu wa *Flyover* eneo la makutano ya Barabara ya Mandela na Barabara ya Nyerere eneo la *TAZARA* umekamilika chini ya ufadhili wa *JICA,* mradi wa Mwenge-Tegeta unaendelea. Sehemu ya Mwenge-Morocco usanifu umekamilika na ujenzi utaanza mwaka 2012/2013 chini ya ufadhili wa *JICA* na mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni unaendelea; upanuzi wa barabara ya Kilwa, kazi ya ujenzi na upanuzi ili kumaliza kipande cha kilomita 1.5 kilichobaki kati ya Mbagala Zakhem na Mbagala Rangi Tatu imekamilika, ujenzi wa barabara ya Kimara – Ubungo – Magomeni – *"Fire"* – Feri/ Magomeni – Morocco/ *"Fire"* – Kariakoo (km 20.9)

umeanza pamoja na ujenzi wa vituo vya mabasi chini ya mradi wa *BRT* na barabara ya Mandela ukarabati umekamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata unaoendelea ukikamilika utapunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Wizara imefanya maandalizi ya awali ya mpango kwa ajili ya kujenga Dar es Salaam – Chalinze-Morogoro *Express Way* kwa utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP).* Aidha, Wizara kupitia TEMESA imeanza maandalizi ya kuanzisha usafiri wa majini kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo. Vile vile Wizara imezikasimu barabara za Jiji la Dar es Salaam ili zihudumiwe na *TANROADS.* Barabara hizo ni *Shekilango Road, United Nations,* Kifuru - *Pugu Station* (Mnadani), Kimara - Kinyerezi (Kimara mwisho), Kawe - *TPDF Firing Range* – Jangwani, Korogwe - Kilungule – *External, Mlimani City* - Ardhi - Makongo – Goba, Kigogo *Roundabout* – Jangwani, Ununio - *Mpiji Bridge, Tabata Dampo* – Kigogo, Temeke - Mtoni Mtongani, Buza - Kilungure – Nzasa, *Chang'ombe Road (Jct Kawawa Road/Nyerere Road - Police Chang'ombe), Taifa Road*, *Mgulani Road (DUCE* - Mgulani JKT), *Kinondoni Road, Shaurimoyo Road na Uhuru Road (Railway Station - Buguruni (Mandela Road).*

Mheshimiwa Spika, barabara za *Ubungo Bus Terminal – Mabibo-Kigogo Roundabout (km 6.4)* kazi ya ujenzi inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 82. Kigogo *Roundabout*-Bonde la Msimbazi – Twiga/*Msimbazi Junction (km 2.7)* kazi ya ujenzi inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 42. Tabata

Dampo – Kigogo-*Ubungo Maziwa External (km 2.25)* usanifu umekamilika na hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, barabara za *Old Bagamoyo* na *Garden Road (km 9.1)* usanifu unaendelea wakati barabara ya Jet Corner – Vituka – Davis Corner (km 10.3) hadi kufikia Juni, 2012 jumla ya km 7 za tuta la barabara, km 6.5 za tabaka la chini la msingi, km 6.5 za tabaka la juu la msingi na km 6.3 za lami zimekamilika. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 73.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara imekamilisha usanifu wa barabara za Mbezi Mwisho (Barabara ya Morogoro) – Maramba Mawili – Kinyerezi - Banana (km 14), Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (Barabara ya Morogoro) (km 20), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6) na Kimara – Kilungule – *External* – Mandela Road (km 9.0). Hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ina jukumu la kujenga miundombinu kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT). Awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa barabara ya Morogoro (Kimara – Kivukoni), Barabara ya Msimbazi *(Fire - Kariakoo)* na barabara ya Kawawa (Magomeni - Morocco) pamoja na ujenzi wa karakana *(Depots)* na Vituo vya Mabasi *(Bus Terminals).* Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 289.9. Mradi huu unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu Saba (7) kama ifuatavyo:-

*Ujenzi wa barabara ya Kimara – Magomeni (km 10.4) na Magomeni – Kivukoni, Kawawa na Msimbazi (km 10.5):-*

Mkataba ulikwishasainiwa na kazi zinatarajiwa kukamilika tarehe 8 Machi, 2015. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 240.9. Mkandarasi ni kampuni ya *Strabag International GmbH* kutoka Ujerumani na Mhandisi Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International* ya Australia. Kazi zimeanza na zinaendelea vizuri.

*Ujenzi wa Karakana (Depot) na Kituo cha Mabasi (Bus Terminal) Ubungo:*

Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 14.7 na umepangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 24. Mkandarasi ni kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd.* kutoka China na Mhandisi Msimamizi ni kampuni ya SMEC International ya Australia. Mkandarasi bado hajaanza kazi katika eneo hili kutokana na kushindwa kukabidhiwa eneo la mradi kwani ulipaji wa fidia haujakamilika. Wizara inaendelea kuwasiliana na wadau husika ili kukamilisha suala la upatikanaji wa eneo la mradi.

*Ujenzi wa Karakana ya Jangwani (Jangwani Depot):*

Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 12.9 na umepangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 24.

Mkandarasi ni kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation Ltd.* kutoka China na Mhandisi Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International* ya Australia. Mkandarasi anaendelea na kazi.

*Ujenzi wa Kituo cha Kivukoni (Kivukoni Terminal):*

Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 5.0 na umepangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 24. Mkandarasi ni kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd.* kutoka China na Mhandisi Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International* ya Australia. Hadi kufikia Juni, 2012 kazi ya ujenzi inaendelea na imefikia asilimia 80.

*Ujenzi wa Kituo cha Kariakoo (Kariakoo Terminal):*

Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 6.3 na kazi zilipangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi12. Mkandarasi ni kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd.* kutoka China na Mhandisi Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International* ya Australia. Kazi zimechelewa kutokana na mgogoro wa ardhi katika eneo hili baada ya wakazi wa eneo hili kufungua kesi mahakamani.

*Kujenga Vituo 6 (Six Feeder Stations) - Shekilango, Urafiki, Magomeni, Fire, Kinondoni 'A' na Mwinjuma:*

Gharama ya shilingi bilioni 4.4 na kazi zimepangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 12. Mkandarasi ni kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd.* kutoka China na Mhandisi

Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International* ya Australia. Hadi kufikia Juni, 2012 kazi zinaendelea na zimefikia asilimia 45.

*Kuhamisha Miundombinu ya Umeme Katika Eneo la Mradi:* Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 5.6 na kazi zilipangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 6.

Mkandarasi ni kampuni ya *Spencon Service Limited* ya Tanzania na Mhandisi Msimamizi ni kampuni ya *SMEC International* ya Australia. Kazi ya kuhamisha Miundombinu ya Umeme imekamilika (Substantailly Completed) na Mkandarasi anaendelea na kipindi cha uangalizi *(Defect Liability Period).*

Mheshimiwa Spika, Vivuko na Magali ya Serikali. Katika mwaka 2011/2012 Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) imekamilisha ujenzi wa vivuko vipya vya Rusumo, MV Ujenzi (Rugezi – Kisorya) na MV Musoma (Musoma – Kinesi). Wizara kupitia *TEMESA* inaendelea kukamilisha ujenzi wa vivuko vipya vya Msangamkuu na Kilambo. Aidha, taratibu za ununuzi wa kivuko kipya cha Ilagala zinaendelea na mwezi Mei, 2012 Mkataba ulisainiwa. *TEMESA* pia imekalilisha ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Rusumo na cha Rugezi – Kisorya (upande wa Kisorya). Ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Chato (Nkome), Rugezi – Kisorya upande wa Rugezi na Bugolora – Ukara unaendelea. Mkandarasi wa kukarabati maegesho ya kivuko cha Kilombero amepatikana na ataanza kazi baada ya kina cha maji kupungua. Mkandarasi wa ujenzi wa maegesho ya Msangamkuu pia

amepatikana na ataanza kazi wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa vivuko, Wizara kupitia *TEMESA* ilipanga kuvifanyia ukarabati vivuko vya MV Alina (Dar es Salaam) na *MV. Pangani* I (Tanga). Kivuko cha *MV. Alina* kilitengenezwa Ujerumani mwaka 1960 na kilifanya kazi nchini humo hadi kiliponunuliwa na Serikali mwaka 1991 na kivuko cha *MV Pangani* I kilinunuliwa na Serikali mwaka 1972. Vivuko hivi kwa sasa ni vichakavu sana vinafanyiwa ukaguzi mkubwa ili kuona kama vinafaa kutumika tena kwa kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* kwa kupitia makusanyo yake ya ndani ya vivuko ya mwaka 2011/2012 imeweza kuvifanyia ukarabati vivuko vya *MV Nyerere na MV Ukara.* Aidha, Wakala umevifanyia matengenezo ya kawaida vivuko vyake 19 vilivyoko nchi nzima. Mwaka 2011/2012 Wakala ulipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 5.00 baada ya kuongeza viwango vya nauli za vivuko Wakala umeweza kukusanya jumla ya shilingi 7,833,585,005.00 hadi Mei 2012. Baada ya kutoa gharama za uendeshaji, shilingi milioni 1,568.781 zimetengwa kununua kivuko/boti nyingine ya Dar es Salaam - Bagamoyo kwa ajili ya kupunguza msongamano Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 *TEMESA* ilitengeneza magari 6,299 na ilikamilisha miradi mipya ya umeme 65 na matengenezo makubwa ya umeme miradi 49 katika

ofisi za Serikali. Katika matengenezo hayo iliweza kukusanya kiasi cha shilingi milioni 1,646.892 ambazo zilitumika kuendesha Karakana zake 21 nchini.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wakala wa Majengo Tanzania *(Tanzania Buildings Agency (TBA)* umeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi: (i) Kutoa huduma ya Ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali na nyumba za kuishi watumishi wa umma, (ii) Kujenga nyumba za kuwapangisha na kuwakopesha watumishi wa Umma, (iii) Kupangisha baadhi ya majengo na nyumba za Serikali kibiashara. Idadi ya nyumba na majengo yaliyo chini ya miliki ya Wakala hadi sasa ni 2,713. Kati ya nyumba hizo, nyumba 1,353 zinapangishwa kibiashara, nyumba 748 zinapangishwa watumishi wa umma, 416 ni za viongozi, 103 nyumba za wageni *(Rest Houses),* 37 Ikulu Ndogo *(State Lodges)* na 56 ni majengo ya Ofisi, Maghala na Karakana.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Wakala umetoa huduma ya ushauri kwa miradi ipatayo 112 yenye thamani ya shilingi 243,311,834,224.00 na kujipatia ada ya ushauri kiasi cha shilingi 1,866,777,735.61. Katika kipindi hicho, Wakala umeweza pia kukusanya kiasi cha shilingi 1,365,153,905.30 zikiwa ni pango la nyumba za kibiashara, shilingi 4,202,511,111.00 kutokana na mauzo ya nyumba walizokopeshwa watumishi wa umma na shilingi 66,974,651.50 yakiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vingine mbali mbali. Kwa ujumla katika kipindi hicho, Wakala umeweza kukusanya jumla ya shilingi

12,665,432,379.87. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,743,936,863.87 ni kutokana na vyanzo vyake vya mapato. Takwimu hizi zinaonesha kuwa Wakala unazidi kujiimarisha kimapato na hatimaye kuweza kujitegemea wenyewe.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi iliyoendelea kutekelezwa na Wakala katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 ni pamoja na Majengo na Nyumba za kupangisha kibiashara, Nyumba za kuwauzia watumishi wa umma, Nyumba za Viongozi wa Serikali (ambazo hazitauzwa "*Tied Quarters*", pamoja na baadhi ya Majengo ya Ofisi za Serikali. Jumla ya miradi ya Majengo na nyumba iliyoendelea kutekelezwa katika kipindi hicho ni 45. Kati ya miradi hiyo, kuna nyumba za kuishi Mia mbili thelathini na nne (234) na majengo mengine nane (8). Thamani ya miradi hii yote ni shilingi 52,824,579,067.62. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Majengo na nyumba za kupangisha, Wakala unakamilisha ujenzi wa Majengo mawili ya ghorofa 10 kila moja yaliyoko katika Mitaa ya Semione (Goliondoi) na Wachaga/Wasukuma yote yakiwa katika Manispaa ya Arusha. Majengo mengine yenye nyumba za kuishi ni pamoja na jengo la ghorofa nane lenye nyumba *(flats)* 16 lililoko katika eneo la *Ada Estate* (kiwanja Na *93/1-Sida);* jengo la ghorofa 4 lenye nyumba *(flats) 8* linalojengwa katika eneo la *Mbezi Beach (Ex-NMC).* Majengo haya yamegharimu kiasi cha shilingi 9,535,215,923.20. Miradi mingine ya nyumba za kuishi ni pamoja na jengo la ghorofa 18 Mtaa wa Chimara na ghorofa 8 barabara ya Chole, yote yakiwa Jijini Dar-es-

Salaam. Majengo haya yana jumla ya nyumba *(flats) 60* na yamegharimu shilingi 27,738,705,600.00.

Mheshimiwa Spika, idadi ya nyumba 33 zinakaribia kukamilika kujengwa katika Mikoa 11 kwa gharama ya shilingi 990,000,000.00. Miradi ya majengo mengine ya kupangisha ni pamoja na jengo la Ofisi la ghorofa 5 linalojengwa katika Mtaa wa Moshi-Dodoma pamoja na Ukumbi wa Mikutano unaojengwa katika eneo la Keko Mwanga-Dar-es-Salaam. Majengo haya mawili yamegharimu shilingi 3,568,792,063.90. Jumla ya fedha zilizotumiwa na Wakala katika miradi ya uwekezaji ni shilingi 46,384,660,201.62.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya nyumba za kuwauzia watumishi wa umma, Wakala uliendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba 25 katika eneo la Bunju (Dar-es-Salaam) kwa gharama ya shilingi 1,312,128,84.00, nyumba 6 katika eneo la *Fire*-Arusha kwa gharama ya shilingi 165,000,000.00 na nyumba 21 katika mikoa 7 kwa gharama ya shilingi 630,000,000.00. Majengo haya yatagharimu jumla ya shilingi 2,107,128,848.00. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Majengo *(TBA)* iliendelea pia na ujenzi wa nyumba 10 za makazi kwa Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam (2), Iringa (1), Mbeya (1), Ruvuma (1), Tanga (1), Arusha (1), Dodoma (1), Tabora (1) na Mwanza (1); ujenzi wa nyumba za viongozi katika Wilaya za Urambo (1), Ukerewe (2), Bahi (2), Kondoa (1) na Mvomero (1) zote zikiwa ni jumla ya nyumba 17 ambazo hazitauzwa *(tied quarters).* Nyumba hizi zimegharimu jumla ya shilingi

4,227,363,516.00. Aidha, Wakala uliendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa zahanati ya Mwangaza (Dodoma) na zahanati ya Manispaa ya Lindi kwa jumla ya shilingi 90,000,000.00. Wakala pia umekamilisha awamu ya pili ya ukarabati wa jengo la *Old Boma* lililoko Bagamoyo na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bariadi kwa jumla ya shilingi 361,468,945.96. Aidha, Wakala uliendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi la ghorofa 3 la *TBA* Makao Makuu Jijini Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi 2,178,350,803.52. Majengo yote haya ni kwa matumizi ya Serikali na kwamba Wakala wa Majengo hawapati mapato yoyote kutokana na majengo na nyumba hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usalama Barabarani na Mazingira. Katika mwaka 2011/2012 Wizara iliendelea kutekeleza shughuli za usalama barabarani kwa kufanya yafuatayo: kudhibiti usalama wa Magari yanayobeba mizigo mikubwa "Abnormal Loads" na kudhibiti uzito wa Magari yanayotumia barabara, kuandaa rasmu ya sheria mpya ya usalama barabarani, kutoa ushauri wa masuala ya usalama kwa wadau wengine na kuchambua muswada wa sheria ya udhibiti uzito wa Magari kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Wizara imefanya upembuzi yakinifu wa vituo vya ukaguzi na kupumzikia madereva na abiria katika mtandao wa barabara kuu nchini. Maeneo yaliyopewa kipaumbele katika ujenzi wa vituo hivyo ni: Vigwaza, Manyoni na Lusahunga.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masuala ya mazingira, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa miradi yote ya barabara inatekelezwa kwa kuzingatia

uhifadhi wa mazingira. Katika mwaka 2011/2012 Wizara ilitoa mafunzo kuhusu tathmini na usimamizi wa mazingira katika sekta ya barabara kwa wahandisi 30 na mafundi sanifu 53 katika Halmashauri za Miji ya Pangani, Rufiji, Mkuranga, Magu, Ukerewe, Mvomero, Iringa, Makete, Arusha, Monduli, Manyoni, Iramba, Tunduru na Wakala wa Barabara Nchini *(TANROADS).* Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa athari za mazingira katika miradi inayoendelea ya Arusha – Namanga, Tanga – Horohoro, Babati – Singida na ile iliyokamilika ya Chalinze – Morogoro, Morogoro – Dodoma, Tanga – Segera, Barabara ya Nyerere, Mandela na Morogoro pamoja na kuandaa program ya elimu kwa umma ili kuzuia uchafuzi wa mazingira katika sekta. Elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya redio, televisheni, vipeperushi na magazeti.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishwaji wa Wababawake Katika Kazi za Barabara. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuhamasisha jamii hususani wanawake kujitokeza kushiriki katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara. Aidha, ukaguzi wa miradi umefanywa kubaini kiwango cha ushiriki wa wanawake katika miradi. Ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara imefikia asilimia 35. Wizara pia iliendelea kutayarisha miongozo ya ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara. Katika kuadhimisha Sikukuu ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi ya kila mwaka, mwaka 2011/2012 Wizara ilishiriki katika vipindi vya televisheni ili kuelezea majukumu ya kitengo na mafanikio yaliyopatikana kuhusu ushiriki wa wanawake katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na

kuongezeka kwa idadi ya kampuni za Makandarasi wa barabara yanayomilikiwa na wanawake toka 65 mwaka 2007 hadi kufikia 120 Juni 2012. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 5 ya kampuni za makandarasi wa barabara zinazomilikiwa na wanaume. Wizara inaendelea kuhamasisha na kuwajengea uwezo wanawake ili idadi ya kampuni za makandarasi zinazomilikiwa na wanawake iongezeke.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliwezesha kufanyika kwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake wa kujenga na kufanyia matengenezo barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvukazi yaliyofanyika Dodoma. Jumla ya wanawake 20 kutoka mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam na Dodoma walipatiwa mafunzo hayo na kutunukiwa vyeti ambavyo Bodi ya usajili wa Makandarasi inavitambua kama mojawapo ya vigezo vya kuweza kuwa Mkurugenzi wa Ufundi *(Technical Director)* kwa anayetaka kuanzisha kampuni ya daraja la *"Labour Based Specialist Road Contractors".*

Mheshimiwa Spika, Ushiriki Katika Jumuiya Mbalimbali. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuiwakilisha nchi katika masuala yanayohusu sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda. Jumuiya hizo ni *EAC, SADC* pamoja na majadiliano ya uanzishaji wa Eneo Huru la Biashara *(Free Trade Area)* katika nchi za *SADC, EAC* na *COMESA.* Lengo kuu ni kukuza ushirikiano katika kuendeleza sekta ya ujenzi hususani uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi ikiwemo ya barabara ili kufanikisha ufanyaji wa biashara katika nchi wanachama

wa jumuiya tatu. Wizara pia imeshiriki kikamilifu katika majadiliano ya utekelezaji wa miradi ya barabara zinazounganisha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ukiwemo mradi wa ujenzi wa barabara za Arusha – Namanga, Bagamoyo – Saadani - Tanga – Horohoro, Arusha – Himo – Holili/Taveta pamoja na Vituo vya pamoja vya mipakani *(One Stop Border Posts).* Aidha, majadiliano ya kutunga Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kudhibiti Magari yanayozidisha uzito na yasiyo ya kawaida *(abnormal)* yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watumihsi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuwaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka watumishi 27 katika mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi 11 walipelekwa mafunzo ya muda mrefu na 11 mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Watumishi watatu walipelekwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na watumishi wawili walipelekwa mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi. Aidha, watumishi 50 walibadilishwa vyeo, watumishi 38 walithibitishwa kazini. Katika miradi ya barabara, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali inayoendelea, Wizara iliweza kuwapatia ajira wafanyakazi 450,000 katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Kupambana na *UKIMWI.* Katika mwaka 2011/2012 Wizara iliendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI kwa njia ya vipeperushi mbalimbali kutoka *TACAIDS*. Aidha, watumishi wameendelea kuhamasishwa kupima afya zao na huduma ya lishe kwa waathirika waliojitokeza hadharani ilitolewa.

Mheshimiwa Spika, Vita Dhidi ya Rushwa. Wizara iliendelea kuwakumbusha watumishi kuhusu athari za vitendo vya rushwa. Elimu kuhusu suala hili ilitolewa kwa watumishi kupitia semina mbalimbali kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

MHeshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB).* Katika mwaka 2011/2012, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 316.551 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Hadi kufikia Mei, 2012, kiasi cha Shilingi bilioni 375.892 zilikusanywa. Hii ni sawa na asilimia 118.75. Hali hii ya makusanyo imetokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kupandishwa kwa bei ya mafuta ya taa ili kudhibiti uchakachuaji wa mafuta ya petroli na dizeli pamoja na juhudi nyingine za kuzuia uvujaji wa mapato. Bodi ya Mfuko wa Barabara ilitegemea kukusanya shilingi bilioni 400.00 hadi kufikia mwisho wa Juni, 2012. Bodi pia imepitisha Mpango Mkakati wa Miaka Mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012 wenye nia ya kuongeza kasi katika upatikanaji, utumiaji na ufuatiliaji wa fedha za Mfuko ili kuboresha hali ya barabara na madaraja nchini.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi *(ERB).* Bodi ya Usajili wa Wahandisi imepewa majukumu ya kuratibu na kusimamia mienendo na shughuli za kihandisi zinazofanywa na wahandisi na kampuni za kihandisi. Katika mwaka 2011/2012, hadi kufikia Mei, 2012 Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 855 na kufanya jumla ya Wahandisi waliosajiliwa kufikia 11,264. Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 31 zilisajiliwa

na hivyo kufanya jumla ya kampuni zilizosajiliwa na Bodi kufikia 227, ambapo 161 ni za kizalendo na 66 ni za kigeni. Aidha, katika kipindi hicho, Bodi ilisajili Wahandisi Washauri 41 na kufanya jumla ya Wahandisi Washauri waliosajiliwa na Bodi kufikia 369. Bodi ilifuta usajili wa kampuni tano za ushauri wa kihandisi na wahandisi washauri sita kwa makosa mbalimbali ikiwemo ukiukwaji wa maadili ya kihandisi na kufanya kazi bila kuzingatia taratibu za kihandisi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu, Bodi pia imeendelea kusimamia utekelezaji wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote. Aidha, Bodi imefanya ukaguzi katika miradi ya ujenzi wa barabara na majengo, ili kuhakikisha kuwa wahandisi katika miradi hiyo wamesajiliwa na Bodi. Bodi pia imekagua shughuli za kihandisi pamoja na maendeleo ya wahandisi katika Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji katika mikoa 17 ya Tanzania bara.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi *(AQRB).* Katika mwaka 2011/12, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili Wabunifu Majengo 31, Wakadiriaji Majenzi 28 na hivyo kufanya jumla ya wataalamu wa fani hizo waliosajiliwa na Bodi kufikia 548, ambapo wazalendo ni 500 na wataalamu wa fani hizo wa kigeni waliosajiliwa ni 48. Aidha, Kampuni 18 za Wabunifu Majengo na Kampuni 12 za Wakadiriaji Majenzi zilisajiliwa na kufanya jumla ya Kampuni zilizosajiliwa kufikia 269. Bodi pia iliwasajili wataalam wa

fani hizi wenye sifa za kati 82 na kufanya jumla ya wataalam wa kati waliosajiliwa kufikia 148 sanjari na usajili huo, Bodi imeweza pia kufuta Wabunifu Majengo watano (5), Wakadiriaji Majenzi wanne (4). Katika kipindi hicho, jumla ya kampuni nne (4) za Wabunifu Majengo na Kampuni moja (1) ya Wakadiriaji Majenzi zilifutwa. Ili kuhakikisha kwamba shughuli za majenzi zinasimamiwa na makampuni ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi waliosajiliwa, Bodi ilikagua miradi ya ujenzi 1,574 katika mikoa 21 ya Tanzania Bara. Aidha, ilisajili miradi ya ujenzi 611. Usajili wa miradi hiyo unasaidia kupatikana kwa taarifa za ujenzi kwa Serikali na pia wadau wote wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(CRB).* Katika mwaka 2011/2012, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilisajili Makandarasi 863 ambapo makandarasi 24 ni wa kigeni na makandarasi 839 ni wazalendo na kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia 9,041 hadi sasa. Aidha, Bodi ilikagua miradi ya ujenzi 2,760 na kati ya hiyo, miradi 848 ilikuwa na mapungufu ya kutozingatia sheria na usalama wa wafanyakazi. Makandarasi katika miradi yenye kasoro walichukuliwa hatua za kisheria zikiwa ni pamoja na kupewa onyo, kupelekwa mahakamani, kutozwa faini, kusimamishwa kwa muda na kufutiwa usajili. Makandarasi 357 walifutiwa usajili na kufanya idadi ya makandarasi waliofutiwa usajili kufikia 2,576.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bodi imeendelea kutekeleza mkakati wa kuwaendeleza makandarasi wa Kitanzania kwa kuendesha mafunzo katika mikoa ya Tanga, Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya na Singida.

Bodi pia imeendelea kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi Wadogo *(Contractors Assistance Fund)* ambapo hadi Desemba, 2011, Bodi imewekeza mtaji wa kiasi cha Shilingi 2.6 bilioni. Idadi ya Makandarasi wanachama wa Mfuko huu ni 781.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi *(NCC).* Katika mwaka 2011/2012, Baraza la Taifa la Ujenzi limeendelea kuteketeleza majukumu yake kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa msukumo wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ujenzi, kufanya tafiti mbalimbali za sekta, kutoa ushauri na kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi 50 kwenye Halmashauri za Wilaya 20 chini ya Ofisi ya Waizri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na kutoa mafunzo mbali mbali kwa wadau 239 wa sekta ya ujenzi kuhusu shughuli za zabuni, menejimenti ya mikataba, usuluhishi wa migogoro, menejimenti ya madai, gharama za ujenzi wa barabara, shughuli za matengenezo na ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Spika, Baraza pia limeendelea kuratibu utekelezaji wa majaribio ya mfumo wa kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma, yaani *Construction Sector Transparency Initiative (CoST)* pamoja na kuratibu utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika vijiji 45 vinavyozunguka mbuga za wanyama kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi. Kazi hii inafanywa kwa kushirikiana na *World Wide Fund (WWF) for Nature*. Aidha, Baraza limeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa 18 la ofisi Jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana

na Shirika la Nyumba la Taifa na kampuni binafsi ya *Lindi Express Limited* kwa gharama ya shilingi bilioni 17.8.

Mheshimiwa Spika, Vikosi vya Ujenzi *(Corporation Sole, Works – CSWS).* Katika mwaka 2011/2012, Vikosi vya Ujenzi vilitekeleza miradi 5 inayohusu ukarabati wa Jengo la Boma la Kale Bagamoyo (Awamu ya II), ujenzi wa nyumba za viongozi Dar es Salaam na Mwanza (Awamu ya I) zikiwemo nyumba za majaji, ujenzi wa Jengo la Ofisi za Kituo cha Hifadhi ya Bahari (Tanga), ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za watumishi Siha (Kilimanjaro) pamoja na ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Rusumo (Kagera). Miradi yote hii imegharimu shilingi milioni 1,726. Aidha, Vikosi vilianza utekelezaji wa maboresho ya kiutendaji *(restructuring)* ili kuwe na watumishi wenye sifa na wanaohitajika. Vikosi pia vimeanza kukarabati ofisi na karakana zake pamoja na kuongeza vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Usambazaji wa Tekinoloji Katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi *(Tanzania Transportation Technology Transfer Centre).* Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kituo kiliendelea kusambaza tekinolojia katika sekta ya Ujenzi na uchukuzi kwa ujumla hapa nchini. Kituo kilisambaza makala na taarifa 70 kwa wadau 90,000 zinazoelezea tekinolojia mbalimbali katika sekta ya uchukuzi. Aidha, wadau wa sekta ya uchukuzi waliendelea kutumia huduma ya Maktaba ya Kituo. Vilevile, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa tano (5) wa Kimataifa wa Usambazaji wa Tekinolojia katika Sekta ya Uchukuzi

Barani Afrika, uliokuwa na lengo la kuhamasisha usambazaji wa tekinolojia na utendaji wenye mafanikio kuhusu ujenzi na matengenezo ya miundombinu iliyo endelevu katika sekta ya barabara na uchukuzi kwa ujumla, pamoja na kubadilishana uzoefu, tekinolojia na kuongeza ujuzi kwa wataalamu, watafiti na watumiaji wa miundombinu katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Chuo Cha Ujenzi – Morogoro. Chuo cha Ujenzi Morogoro kina jukumu la kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu na stadi wanaoshiriki kazi za ujenzi kwenye sekta za umma na binafsi. Mwaka 2011/2012, jumla ya wanafunzi 516 wa fani mbalimbali za ujenzi walipata mafunzo ya *Basic Technical Course – 173, Basic Driving Course – 173; PSV Driving Course - 39 na Technician Maintenance Management Courses – 131.* Chuo cha Matumizi Stahiki ya Nguvu Kazi *(Appropriate Technology Training Institute – Mbeya).* Chuo cha ATTI kina jukumu la kuratibu kazi zote za miradi, kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kwa wadau na watendaji wa kazi za barabara kuhusu matumizi bora ya teknolojia stahiki ya nguvu kazi pamoja na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo makandarasi wanawake 43 kutoka mikoa mbalimbali nchini na pia Chuo kimeendesha mafunzo ya kimataifa kwa Wahandisi 9 kutoka nchini Somalia. Mafunzo hayo ambayo yalidhaminiwa na Shirika la Kimataifa la Misaada la Japani *(JICA)* na kuratibiwa na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* yalihusu usimamizi wa matengenezo na Ukarabati wa Barabara kwa kutumia Teknolojia

Stahili ya Nguvukazi *(LBT).* Aidha, kupitia ushiriki wake katika maonesho mbalimbali ya kitaifa, Chuo kilitoa mafunzo juu ya matumizi ya Teknolojia Stahili ya Nguvukazi kwa wananchi 665.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla miradi yote ya barabara, madaraja, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali inayoendelea kutekelezwa na Wizara ya Ujenzi imeenea nchi nzima na ina thamani isiyopungua shilingi bilioni 6,005.637 (Trilioni 6 na bilioni 5.637) kama inavyoelezwa hapa chini. Miradi mikubwa ya barabara inayoendelea kutekelezwa katika mkoa wa Mtwara na Ruvuma ina jumla ya shilingi bilioni 592.0583. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara za:-

(i) Masasi – Mangaka (km 54): shilingi bilioni 21.62.

(ii) Mangaka – Tunduru/Mtambaswala (km 202.5): shilingi bilioni 240.858.

(iii) Tunduru – Matemanga (km 58.70): shilingi bilioni 63.41.

(iv) Matemanga – Kilimasera (km 68.20): shilingi bilioni 64.02.

(v) Kilimasera – Namtumbo (km 60.70): shilingi bilioni 53.23.

(vi) Namtumbo – Songea (km 67.00): shilingi bilioni 62.88.

(vii) Peramiho – Mbinga (km 78.00): shilingi bilioni 79.81.

(viii) Mbinga – Mbamba Bay (km 66.00): shilingi bilioni 2.90.

(ix) Makambako – Songea (km 295): shilingi bilioni 0.979.

(x) Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200): shilingi bilioni 0.779.

(xi) Daraja la Nangoo; shilingi bilioni 0.578.

(xii) Daraja la Umoja: shilingi bilioni 0.2943.

(xiii) Mtwara – Newala – Masasi *(FS & DD) (km 209):* shilingi bilioni 0.70.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa wa Tabora na Kigoma, barabara ya Kigoma – Kidahwe na barabara ya Mwandinga – Manyovu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Miradi ya barabara na madaraja inayojengwa na Serikali kwa sasa ina thamani ya shilingi bilioni 623.02565. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi (km 300): shilingi bilioni 3.50.

(ii) Kidahwe – Uvinza (km 76.60): shilingi bilioni 78.24.

(iii) Daraja la Mto Malagarasi (Daraja la Kikwete na barabara zake (km 48): shilingi bilioni 78.91.

(iv) Tabora – Ndono (km 42): shilingi bilioni 51.35.

(v) Ndono – Urambo (km 52): shilingi bilioni 59.77.

(vi) Urambo – Kaliua – Ilunde (km 146): shilingi bilioni 2.50.

(vii) Tabora – Sikonge (km 70): shilingi bilioni 1.00.

(viii) Tabora – Nyahua (km 85.00): shilingi bilioni 93.41.

(ix) Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.40): shilingi bilioni 109.64.

(x) Mwandiga – Manyovu (km 60): shilingi bilioni 0.86565.

(xi) Nzega – Puge (km 56.10): shilingi bilioni 66.36.

(xii) Puge – Tabora (km 58.80): shilingi bilioni 62.74.

(xiii) Ipole – Koga – Mpanda (km 273 ): shilingi bilioni 1.20.

(xiv) Daraja la Mbutu: shilingi bilioni 12.34.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Rukwa na Katavi, miradi ya jumla ya shilingi bilioni 587.69 inatekelezwa na Wizara ya Ujenzi katika ujenzi wa kiwango cha lami. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Tunduma – Ikana: (km 63.70): shilingi bilioni 82.52;

(ii) Ikana – Laela (km 64.20): shilingi bilioni 76.10;

(iii) Laela – Sumbawanga (km 95.10): shilingi bilioni 130.10;

(iv) Sumbawanga – Kanazi (km 75.00): shilingi bilioni 78.84;

(v) Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.60): shilingi bilioni 82.84;

(vi) Kizi – Sitalike – Mpanda (km 95.00): shilingi bilioni 3.00;

(vii) Mpanda – Mishamo (km 100): shilingi bilioni 1.00; na

(viii) Sumbawanga – Matai – Kasanga (km 112): shilingi bilioni 133.29.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kagera na Geita, miradi inayoendelea kujengwa na ile iliyokamilika ambayo imepangiwa fedha katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 ina thamani ya shilingi bilioni 375.688. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Geita – Sengerema (km 90): shilingi bilioni 1.154;

(ii)Kagoma – Lusahunga (km 154): shilingi bilioni 191.46;

(iii) Ushirombo – Lusahunga (km 110): shilingi bilioni 114.56;

(iv) Kyaka – Bugene (km 59.10): shilingi bilioni 64.96;

(v) Uyovu – Biharamulo (km 112): shilingi bilioni 2.40;

(vi) Kyamyiorwa – Buzirayombo (km 120): shilingi bilioni 0.577; na

(vii) Buzirayombo – Geita (km 100): shilingi bilioni 0.577.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikoa ya Mwanza na Mara, baada ya barabara za Mwanza – Nyanguge, Mwanza – Ilula na Mwanza – Usagara – Geita kukamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Miradi inayoendelea kwa sasa ina jumla ya shilingi bilioni 100.761. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Makutano – Natta – Mugumu (km 100): shilingi bilioni 3.00;

(ii) Mwanza / Mara Border – Musoma (km 85.50): shilingi bilioni 85.368;

(iii) Nyanguge – Mwanza/Mara Border (km 85.50): shilingi bilioni 6.00;

(iv) Kisesa – Usagara Bypass (km 17.00): shilingi bilioni 1.50;

(v) Nyamswa – Bunda – Kisorya (km 118): shilingi bilioni 1.90;

(vi) Mwanza – Mwanza/Shinyanga Border (km 120): shilingi bilioni 0.55;

(vii) Daraja la Maligisu: shilingi bilioni 1.00;

(viii) Daraja la Kirumi: shilingi bilioni 0.289; na

(ix) Geita – Usagara (km 90): shilingi bilioni 1.154.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kujengwa kwa barabara ya Ilula – Shinyanga – Tinde/Isaka hadi Nzega kwa kiwango cha lami, kwa upande wa Mikoa ya Shinyanga na *Simiyu*, miradi ya barabara za lami, kwa sasa ina thamani ya shilingi bilioni 214.14. Miradi husika ni pamoja na:-

(i) Bariadi – Lamadi (km 71.80): shilingi bilioni 67.41;

(ii) Isaka – Ushirombo (km 132): shilingi bilioni 145.34;

(iii) Kahama Mjini (km 5): shilingi bilioni 0.760; na

(iv) Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala Oldeani *(km 328) (FS & DD):* shilingi bilioni 0.63.

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya Dodoma na Singida, miradi iliyokamilika kwa kiwango cha lami ni pamoja na barabara ya Shelui – Singida, Singida – Isuna, Manyoni – Isuna na Dodoma – Manyoni hivyo miradi inayoendelea na inayotegemewa kujengwa kwa kiwango cha lami ni ya gharama ya shilingi bilioni 424.4128. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Dodoma – Manyoni (km 127): shilingi bilioni 0.2308;

(ii) Manyoni – Isuna (km 54): shilingi bilioni 0.577;

(iii) *Dodoma University Road (km 12):* shilingi bilioni 0.577;

(iv) Singida – Kateshi (km 65.1): shilingi bilioni 51.63;

(v) Dodoma – Mayamaya (km 43.60): shilingi bilioni 40.61;

(vi) Mayamaya – Bonga (km 188.15): shilingi bilioni 263.958;

(vii) *Fufu Escarpment* – Dodoma (km 70.90): shilingi bilioni 64.33; na

(viii) Daraja la Sibiti: shilingi bilioni 2.50.

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya Arusha na Manyara, miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika mikoa hiyo ina jumla ya shilingi bilioni 328.235. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Bonga – Babati (km 19.20): shilingi bilioni 19.69;

(ii)Kateshi – Dareda (km 73.80): shilingi bilioni 64.14;

(iii) Dareda – Babati – Minjingu (km 84.60): shilingi bilioni 84.92;

(iv) Minjingu – Arusha (km 104): shilingi bilioni 75.51;

(v) Arusha – Namanga (km 105): shilingi bilioni 81.77; na

(vi) *KIA* – Mererani (km 23): shilingi bilioni 2.205.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya barabara katika *mikoa* ya Kilimanjaro na Tanga ina jumla ya shilingi bilioni 515.429. Miradi hiyo ni:-

(i) Korogwe – Handeni (km 65): shilingi bilioni 63.20;

(ii)Handeni – Mkata (km 54): shilingi bilioni 57.34;

(iii) Tanga – Horohoro (km 65): shilingi bilioni 69.894;

(iv) Korogwe – Mkumbara (km 76): shilingi bilioni 62.87;

(v) Mkumbara – Same (km 96): shilingi bilioni 65.13;

(vi) Chalinze – Segera – Tanga (km 245): shilingi bilioni 109.884;

(vii) Rombo Mkuu – Tarakea (km 32): shilingi bilioni 15.80;

(viii) Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 34): shilingi bilioni 25.10;

(ix) Kwa Sadala – Masama (km 12.5): shilingi bilioni 5.34

(x) Kibosho Shine – Kwa Rafael – International School (km 43.00): shilingi bilioni 8.93;

(xi) Rau Madukani – Mawela – Uru Njari (km 12.50): shilingi bilioni 4.88;

(xii) Kirua Nduoni – Marangu Mtoni (km 31.5): shilingi bilioni 9.10;

(xiii) Sanya Juu – Kamwanga – Bomang'ombe (km 75): shilingi bilioni 7.854;

(xiv) Same – Himo – Marangu & Mombo – Lushoto (km 132)- Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina shilingi bilioni 7.854; na

(xv) Tanga – Saadani – Bagamoyo (km 178) – Usanifu: shilingi bilioni 2.253.

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, miradi ya barabara inayoendelea ina jumla ya shilingi bilioni 961.072. Miradi hiyo ni:-

(i) Ujenzi wa barabara ya Kimara – Kivukoni (feri), *Fire – Kariakoo* na Magomeni – Morocco shilingi bilioni 240.90;

(ii)Ujenzi wa karakana na vituo vya mabasi yaendayo kasi (BRT) pamoja na kuhamisha nguzo za umeme, shilingi bilioni 47.90;

(iii) Ujenzi wa barabara ya Mwenge – Tegeta, shilingi bilioni 88.00;

(iv) Kuhamisha miundombinu sehemu ya Mwenge- Morocco, shilingi bilioni 13.801;

(v) Barabara ya Kilwa *(kilwa Road) (km 1.5),* shilingi bilioni 5.46;

(vi) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni, shilingi bilioni 214.64;

(vii) Ujenzi wa *Flyover TAZARA*, shilingi bilioni 60.00;

(viii) Ujenzi wa Barabara ya Gerezani *(Gerezani Road)* (Bendera Tatu – KAMATA), shilingi bilioni 6.60;

(ix) Barabara za pete *(ring roads)* ambazo ni *Ubungo Bus Terminal- Mabibo* – Twiga/Msimbazi Jct (km 9.1)shilingi bilioni 19.08;

(x) Barabara ya Kilwa *(Kilwa Road)* (Rangi Tatu – Zakhem, awamu ya kwanza (Mradi wa Kajima) shilingi bilioni 29.70;

(xi) Barabara ya Mandela, shilingi bilioni 61.25;

(xii) Usafiri wa vivuko/boti kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo, shilingi bilioni 3.50;

(xiii) *Jet Corner – Vituka – Davis Corner (km 10.30):* shilingi bilioni 12.474;

(xiv) Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60): shilingi bilioni 58.82;

(xv) Barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege Mafia (km14): shilingi bilioni 2.90;

(xvi) Daraja la Ruvu: shilingi bilioni 0.289;

(xvii) Mradi wa ujenzi wa barabara ya *Wazo Hill* – Bagamoyo – Msata, shilingi bilioni 89.61;

(xviii) Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14): shilingi bilioni 1.75; na

(xix) Barabara zilizokasimiwa Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS,* shilingi bilioni 4.398.

Barabara hizo ni Shekilango, *United Nations*, Kifuru – Pugu Stesheni (Mnadani), Kimara – Kinyerezi (Kimara

Mwisho), Kawe – *TPDF Firing Range* – Jangwani, Korogwe – Kilungule – *External, Mlimani City* – Ardhi – Makongo – Goba, Kigogo *Round About* – Jangwani, Ununio – Buza – Kilungure – Nzasa, Chang'ombe (Makutano ya Kawawa / Nyerere – Polisi Chan'gombe), *Taifa Road, Mgulani Road (DUCE* – Mgulani JKT), *Kinondoni Road,* Shaurimoyo *Road na Uhuru (Railway Station* – Buguruni *(Mandela Road).*

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya Lindi na Morogoro barabara ya Somanga – Nangurukuru- Lindi hadi Mingoyo ilikwishakamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Miradi inayoendelea ina thamani ya shilingi bilioni 149.7169 na inajumuisha miradi ya:-

(i) Nangurukuru – Mbwemkulu (km 95): shilingi bilioni 1.154;

(ii) Mbwemkulu – Mingoyo (km 95): shilingi bilioni 1.154;

(iii) Dumila – Rudewa (km 45): shilingi bilioni 41.93;

(iv) Magole – Turiani (km 48): shilingi bilioni 48.90;

(v) Turiani – Mziha (km 36.6): shilingi bilioni 0.05;

(vi) Daraja la Kilombero: shilingi bilioni 55.00; na

(vii) Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396) (Upembuzi yakinifu na usanifu): shilingi bilioni 1.5289.

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa, miradi inayoendelea ina jumla ya shilingi bilioni 422.493. Miradi hiyo inajumuisha:-

(i) Ibanda – *Itungi Port (km 26):* shilingi bilioni 0.657;

(ii) Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto – Mafinga (km 149.6): shilingi bilioni 127.70;

(iii) Iringa – Mafinga (km 69.4): shilingi bilioni 64.873;

(iv) Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152): shilingi bilioni 0.879;

(v) Mbeya – Lwanjilo (km 36): shilingi bilioni 27.464;

(vi) Lwanjilo – Chunya (km 36): shilingi bilioni 40.28;

(vii) Chunya – Makongolosi (km 43): shilingi bilioni 1.200;

(viii) Iringa – Migori (km 95.10): shilingi bilioni 84.22;

(ix) Migori – *Fufu Escarpment (km 93.80):* shilingi bilioni 73.61; na

(x) Njombe – Ndulamo – Makete (km 109.4): shilingi bilioni 1.610.

Mheshimiwa Spika, gharama za usimamizi wa miradi yote ya barabara na madaraja yanayojengwa katika nchi nzima ni shilingi bilioni 170.0.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa barabara na madaraja

inayoendelea katika nchi nzima ina thamani ya shilingi bilioni 6.612 ambazo zinagharamiwa na Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, miradi ya vivuko iko katika mikoa ya Geita, Mwanza, Mara, Dar es Salaam, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Morogoro, Tanga, Kagera na Pwani. Miradi hii ina jumla ya shilingi bilioni 28.068.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya Majengo na nyumba za Serikali katika mikoa yote ya Tanzania inayoendelea ina gharama ya shilingi bilioni 101.932.

Mheshimiwa Spika, ukichukua miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara na madaraja katika mikoa yote, ikajumuishwa na miradi ya nyumba na vivuko pamoja na miradi ya ukarabati na kazi za matengenezo maalum na ya dharura katika mikoa yote ya Tanzania Bara, Wizara na Serikali kwa ujumla inategemea kuajiri zaidi ya watu 650,000 ukiachia mama/baba lishe, wachimba kokoto, wafyatua matofali, watengeneza mbao za ujenzi, wachimba mchanga n.k. Wafanyakazi hawa wote watafanya kazi katika miradi niliyoitaja katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bodi za *CRB, ERB* na AQSRB, Bodi ya *CRB* imekwishasajili Makandarasi wa madaraja yote 9,041 na imewafutia usajili makandarasi 2,576; *ERB* imesajili Wahandisi 11,264 na imewafutia usajili Wahandisi Washauri 6 na kampuni 5 za ushauri wa kihandisi kwa makosa mbali mbali ikiwemo ukiukwaji wa maadili na *AQSRB* imesajili

wataalamu wa fani za uwabunifu majenzi na wakadiriaji majenzi 548 na kusajili kampuni 269 za ushauri katika fani hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bodi ya Mfuko wa Barabara katika mwaka wa 2012/2013 itakusanya shilingi bilioni 400 zitakazotumika katika matengenezo ya Barabara na Madaraja yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* na Barabara na Madaraja yaliyo chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine mtambuka yatakayoshughulikiwa na Wizara ni pamoja na masuala ya Usalama barabarani yaliyotengewa jumla ya shilingi bilioni 4.30288, masuala ya *NCC,* Utawala, ushirikishwaji wanawake katika kazi za barabara, Chuo cha Morogoro na Mbeya, Mazingira, UKIMWI na usimamizi wa sera na Sheria za nchi na hasa Sheria Na 13 ya mwaka 2007 inayohusu utunzaji wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, C: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013. Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Kawaida. Wizara ya Ujenzi inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 15,628,580 katika mwaka 2012/13 kutoka Idara za Utawala (shilingi 627,580), Huduma za Kiufundi (shilingi 15,000,000) na Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi (shilingi 1,000). Katika mwaka 2012/2013, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 329,085,354,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 300,764,800,000 ni fedha za Mfuko wa Barabara, shilingi 21,340,508,000 ni fedha za

mishahara kwa Wizara na Taasisi na shilingi 6,980,046,000 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013, Wizara imezingatia vipaumbele vya miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na wahisani na yenye kuhitaji mchango wa Serikali, Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na Utekelezaji wa Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali. Katika mwaka 2012/2013 Wizara ya Ujenzi imetengewa kiasi cha shilingi 693,948,272,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleao. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi 296,896,892,000 na fedha za nje ni shilingi 397,051,380,000. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2012/2013 ni kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na.1. Maelezo ya kila mradi ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya *Wazo Hill* – Bagamoyo – Msata (Km 107) – Shilingi Milioni 7,396.806. Lengo la mradi ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Bagamoyo – Makofia - Msata (km 64). Mkataba wa ujenzi unatekelezwa na kampuni ya ESTIM Construction kwa gharama ya shilingi milioni 89,610. Kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami inaendelea na imepangwa kukamilika katika kipindi cha miezi 24.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, jumla ya Shilingi milioni 7,108.260 za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bagamoyo

– Msata (km 64) kwa kiwango cha lami. Kiasi cha shilingi milioni 288.55 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Sadani – Tanga (km 178).

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Usagara – Geita – Kyamyorwa (Km 422) Sehemu ya Uyovu – Biharamulo (Km 112) – Shilingi Milioni 4,708.40. Lengo la mradi huu ni kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo – Geita hadi Usagara yenye urefu wa km 310 na sehemu ya Uyovu - Biharamulo yenye urefu wa km 112. Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa barabara ya Kyamyorwa - Geita (km 220) ambayo ilikamilika Februari 2008. Awamu ya pili ilihusisha ujenzi wa barabara ya Geita - Usagara (km 90) ambapo ujenzi wake ulianza Februari 2008 na umekamilika Januari 2010. Awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa barabara ya Uyovu - Biharamulo kupitia Bwanga (km 112). Jumla ya Shilingi milioni 2,400.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Uyovu – Biharamulo (km 112) katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 577.10 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo (km 120). Kiasi cha shilingi milioni 577.10 kimetengwa kwa ajili ya barabara ya Buzirayombo – Geita (km100) na kiasi cha shilingi milioni 1,154.20 kimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Geita – Usagara *(Lot 1 na Lot 2 ) (km 90).*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliuwa – Tabora (Km 443) – Shilingi Milioni 30,160.178. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kigoma hadi Tabora (km 443) kwa

kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja la Kikwete kwenye Mto Malagarasi na barabara za maingilio ya daraja (km 48). Kazi ya ujenzi wa daraja ilikwishaanza na inatarajiwa kukamilika Desemba 2013. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe - Uvinza (km 76.6) unaendelea na unatarajiwa kukamilika Oktoba 2013. Ujenzi wa barabara za Tabora-Ndono (km 42) na Ndono-Urambo (km 52) ulianza Januari, 2011 na unatarajiwa kukamilika Februari 2013. Aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Tabora – Sikonge (km 70) yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 1,385.093 fedha za ndani na shilingi milioni 6,693.00 fedha za nje zimetengwa ili kuendelea na ujenzi wa lami barabara ya Kidahwe –Uvinza (km 76.6). Kiasi cha shilingi milioni 2,039.70 fedha za ndani na shilingi milioni 6,130.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja la Malagarasi (Daraja la Kikwete). Kiasi cha shilingi milioni 4,767.255 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora - Ndono (km 42) na shilingi milioni 5,645.13 kwa sehemu ya Ndono – Urambo (km 52). Kwa upande wa barabara ya Tabora – Sikonge (km 70) na barabara ya Ilunde–Kaliua-Urambo (km 146) kiasi cha shilingi milioni 3,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/Bomang’ombe – Sanya Juu (Km 173) na Arusha – Moshi – Holili (Km 140) Shilingi Milioni 7,854.406. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya

Marangu –Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 96) kwa kiwango cha lami na kukarabati barabara ya Arusha – Moshi – Holili pamoja na Arusha by-pass (km 140) ili kuchochea maendeleo ya sekta ya utalii kuzunguka mlima Kilimanjaro na hivyo kukuza uchumi wa nchi. Ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32) ulikamilika Septemba 2009 na ujenzi wa sehemu ya Tarakea – Rombo Mkuu (km 32) ulikamilika Januari 2011. Kazi za ujenzi wa sehemu ya Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32 ) zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 488.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipia sehemu malipo ya mwisho ya mkandarasi wa Tarakea – Rombo na shilingi milioni 2,146.00 kwa ajili ya kukamilisha km 6 za lami kwa barabara ya Marangu – Rombo Mkuu na Mwika Kilacha (km 34). Aidha, kiasi cha shilingi milioni 2,926.00 kimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Kamwanga (km 75). Kiasi cha shilingi milioni 1,366 fedha za ndani zimetengwa kuanza ukarabati wa sehemu ya Arusha – Moshi – Holili kwa kiwango cha lami wakati shilingi milioni 28.90 fedha za ndani na shilingi milioni 900.00 fedha za nje zimetengwa kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Same – Himo na Mombo - Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nangurukuru – Mbwemkulu (Km 95) – Shilingi Milioni 1,154.20. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo ambayo ni kiungo muhimu kati ya Dar es

Salaam na mikoa ya kusini ambao ujenzi wake ulikamilika Januari, 2008. Katika mwaka wa fedha 2012/13, jumla ya shilingi milioni 1,154.20 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho kwa Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbwemkulu – Mingoyo (Km 95) – Shilingi Milioni 1,154.20. Mradi huu umehusisha kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbwemkulu - Mingoyo (km 95) kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design & Build)*. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo ambayo ni kiungo muhimu kati ya Dar es Salaam na Mikoa ya kusini (Lindi na Mtwara) na ujenzi wake ulikamilika Desemba, 2007. Katika mwaka 2012/2013, barabara hii imetengewa shilingi milioni 1,154.20 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Dodoma – Manyoni (Km 127) – Shilingi Milioni 230.84. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma - Manyoni (km 127) kwa utaratibu maalum wa kusanifu na kujenga (*Design & Build)*. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na ulikamilika mwezi Novemba 2009. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 230.84 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Manyoni – Singida (Manyoni – Isuna (Km 54)) Shilingi Milioni 577.10. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami

barabara ya Manyoni - Isuna (km 54) kwa utaratibu wa *Design & Build*. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi umekamilika. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, barabara hii imetengewa shilingi milioni 577.10 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi. Barabara ya Dumila – Kilosa (Km 78) – Shilingi Milioni 4,767.25. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Dumila – Kilosa (km 78). Kazi ya ujenzi wa sehemu ya Dumila - Rudewa (km 45) inaendelea. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na kwa mwaka 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 4,767.25 fedha za ndani kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Sumbawanga – Kasesya/Matai – *Kasanga Port* (Km 112) – Shilingi Milioni 7,303.34. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Sumbawanga –Matai-Kasanga Port (km. 158.82) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na unatekelezwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga. Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, kiasi cha shilingi milioni 7,303.34 fedha za ndani kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kutumia Bajeti ya maendeleo. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara ya Matai - Kasesya yenye urefu wa km 46.82 itafanyika.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Madaraja ya Nangoo, Kilombero, Maligisu, Kavuu, Mbutu, Ruhekei, na Ununuzi wa Madaraja ya Chuma kwa ajili ya

Dharura *(Bailey Emergency Bridge)* – Shilingi Milioni 9,963.62. Lengo la mradi huu ni kujenga Daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi - Ifakara – Mahenge, Daraja la Maligisu (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi - Maligisu, Daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto-Inyonga, Daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga-Manonga, Daraja la Ruhekei katika barabara ya Mbinga-Mbamba Bay, Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti na Daraja la Ruhuhu (Ruvuma) pamoja na ununuzi wa madaraja ya chuma kwa ajili ya dharura (Bailey *Compact Emergency Bridges)*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, kiasi cha shilingi milioni 577.62 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Nangoo, Daraja la Maligisu shilingi milioni 1,000.00, Daraja la Kilombero shilingi milioni 3,028.00, Daraja la Kavuu limetengewa shilingi milioni 1,000.00, Daraja la Sibiti limetengewa shilingi milioni 2,500.00, Daraja la Mbutu limetengewa shilingi milioni 300.00, na Daraja la Ruhekei shilingi milioni 577.00. Aidha, shilingi milioni 346.00 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa Bailey *Compact Emergency Bridges na crane lorry* na shilingi milioni 346.00 zimetengwa kwa ajili ya usanifu wa Daraja la Ruhuhu. Ujenzi wa Daraja la Kirumi umetengewa shilingi milioni 289.00.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya *New Bagamoyo (Kawawa JCT* – Tegeta (Km 17)) – Shilingi Milioni 55,661.324. Lengo la mradi huu ni kupanua barabara hii

kutoka njia mbili za sasa hadi njia nne kuanzia makutano ya Barabara ya Kawawa na Barabara ya Ali Hassan Mwinyi hadi Tegeta ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara hii. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la JICA. Jumla ya shilingi milioni 13,801.324 fedha za ndani na shilingi milioni 41,860.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi, kulipa fidia na kuhamisha huduma za jamii kwenye eneo la ujenzi (mabomba ya maji, nguzo na nyaya za umeme/simu n.k) katika mwaka 2012/2013.

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (Km 178) – Shilingi Milioni 4,572.17. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (Kyaka-Bugene) yenye urefu wa km 59.1 kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100. Kazi za ujenzi zilikwishaanza na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Jumla ya shilingi milioni 4,572.17 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Bugene – Kasulo yenye urefu wa km 124 itafanyika.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Isaka – Lusahunga – Rusumo (Km 242) na Nyakasanza – Kobelo (Km 150) – Shilingi Milioni 15,860.20. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242) kwa kiwango cha lami na kufanya Usanifu wa Kina wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobelo (km 150) chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Mradi wa ukarabati unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Mradi huu umegawanyika katika sehemu

mbili (2) ili kuharakisha utekelezaji; Isaka – Ushirombo (km 132) na Ushirombo – Lusahunga (km 110). Kazi ya ukarabati na inatarajiwa kukamilika Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, barabara hii imetengewa fedha za ndani shilingi milioni 8,779.00 kwa sehemu ya Isaka – Ushirombo na shilingi milioni 5,852.20 kwa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga kwa ajili ya kuendelea na ukarabati. Aidha, shilingi milioni 29.00 za ndani na shilingi milioni 1,200.00 za nje zimetengwa kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa sehemu ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobelo.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (Km 254) – Shilingi Milioni 16,584.00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora kwa kuanzia na sehemu ya Manyoni – Chaya (km 89.35) na sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85) kwa kutumia fedha za ndani. Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013 kwa sehemu zote mbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 8,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tabora – Nyahua na shilingi milioni 8,584.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Korogwe – Handeni (Km 65) – Shilingi Milioni 4,779.55. Lengo la

mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Korogwe – Handeni (km 65). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 4,779.55 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara za Mikoa Shilingi Milioni 20,410.00. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya ukarabati wa jumla ya km 337.60 kwa kiwango cha changarawe na kujenga km 23.70 kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za Bajeti ya maendeleo. Kazi za ukarabati kwa kiwango cha changarawe zitafanyika katika Mikoa yote. Aidha, ujenzi wa madaraja 14 utatumia fedha za Bajeti ya maendeleo katika Mikoa ya Morogoro (2), Mbeya (3), Manyara (1), Mtwara (1), Ruvuma (1), Simiyu (4), Lindi (1) na Rukwa (1). Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo imeoneshwa katika Kiambatisho Na 2. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, miradi ya maendeleo ya barabara za Mikoa imetengewa jumla ya shilingi milioni 20,410.00 zote zikiwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya *Mwanza/Shinyanga Border* – Mwanza (Km. 120) – Shilingi Milioni 50.00. Lengo la mradi huu ni kufanyia ukarabati kwa kiwango cha lami sehemu zilizoharibika za barabara ya mpaka wa Mwanza/Shinyanga – Mwanza. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 50.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Handeni – Mkata (Km 54) – Shilingi Milioni 4,213.04. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni – Mkata (km 54). Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi za ujenzi zinaendelea. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 4,213.04 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwandiga – Manyovu (Km 60) – Shilingi Milioni 865.65. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya kutoka Mwandiga hadi Manyovu inayounganisha Mkoa wa Kigoma na nchi jirani ya Burundi kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Ujenzi wa barabara hii umekamilika. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 865.65 fedha za ndani kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Umoja – Shilingi Milioni 294.32. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kujenga daraja katika Mto Ruvuma eneo la Mtambaswala / Negomane ili kuunganisha nchi za Tanzania na Msumbiji. Daraja hili lilijengwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga *(Design and Build).* Mradi huu unagharamiwa na Serikali za Tanzania na Msumbiji na ulikwishakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 294.32 fedha za ndani

zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kupunguza Msongamano wa Magari Katika Jiji la Dar-es-Salaam. Katika kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara inaendelea kutekeleza miradi ifuatayo yenye thamani ya shilingi bilioni 899.063:-

(i) Ujenzi wa barabara ya Kimara – Kivukoni (feri), *Fire – Kariakoo* na Magomeni – Morocco shilingi bilioni 240.90

(ii) Ujenzi wa karakana na vituo vya mabasi yaendayo kasi *(BRT)* pamoja na kuhamisha nguzo za umeme, shilingi bilioni 47.90;

(iii) Ujenzi wa barabara ya Mwenge – Tegeta, shilingi bilioni 88.00;

(iv) Kuhamisha miundombinu sehemu ya Mwenge- Morocco, shilingi bilioni 13.801;

(v) Barabara ya Kilwa (kilwa Road) (km 1.5), shilingi bilioni 5.46;

(vi) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni, shilingi bilioni 214.64;

(vii) Ujenzi wa Flyover TAZARA, shilingi bilioni 60.00;

(viii) Ujenzi wa Barabara ya Gerezani *(Gerezani Road)* (Bendera Tatu – KAMATA), shilingi bilioni 6.60;

(ix) Barabara za pete *(ring roads)* ambazo ni *Ubungo Bus Terminal* - Mabibo-Twiga/ Msimbazi Jct (km 9.1); shilingi bilioni 19.08;

(x) Barabara ya Kilwa *(Kilwa Road)* (Rangi Tatu – Zakhem, awamu ya kwanza (Mradi wa Kajima) shilingi bilioni 29.70;

(xi) Barabara ya Mandela, shilingi bilioni 61.25;

(xii) Usafiri wa vivuko/boti kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo, shilingi bilioni 3.50;

(xiii) *Jet Corner* Vituka-*Davis Corner (km 10.30):* Shilingi bilioni 12.474;

(xiv) Mradi wa ujenzi wa barabara ya *Wazo Hill – Bagamoyo* – Msata, shilingi bilioni 89.61;

(xv) Mbezi – Malamba mawili-Kinyereze-Banana (km.14): shilingi bilioni 1.75; na

(xvi) Barabara zilizokasimiwa Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS, shilingi bilioni 4.398. Barabara hizo ni :- Shekilango, *United Nations*, Kifuru – Pugu Stesheni (Mnadani), Kimara – Kinyerezi (Kimara Mwisho), Kawe – *TPDF Firing Range* – Jangwani, Korogwe – Kilungule – *External, Mlimani City – Ardhi* – Makongo – Goba, Kigogo *Round About* – Jangwani, Ununio – Buza – Kilungure – Nzasa, Chang'ombe (Makutano ya Kawawa / Nyerere – Polisi Chan'gombe), Taifa *Road, Mgulani Road (DUCE* – Mgulani JKT), *Kinondoni Road,*

Shaurimoyo *Road na Uhuru (Railway Station – Buguruni (Mandela Road).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara za Pete *(Ring Roads)* (Km 98.15) – Shilingi Milioni 10,577.00. Lengo la mradi huu ni kujenga, kufanya upanuzi, na kukarabati barabara za Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari.. Barabara hizo ni Ubungo Bus Terminal – Kigogo – Kawawa Roundabout (km 6.4), Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga Junction (km 2.7), Jet Corner – Vituka – Devis (km 10.3) na ujenzi wa mfereji wa Bungoni unaoanzia barabara ya Nyerere hadi Uhuru (Bungoni). Aidha, mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi *(Bus Rapid Transit Infrastructure)* na vituo vyake unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/2013, kiasi cha shilingi milioni 1,073.00 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobakia kwa barabara ya Ubungo Bus Terminal – Kigogo-Kawawa *Roundabout;* shilingi milioni 1,000.00 kwa barabara ya Kawawa *Roundabout* – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga Junction na shilingi milioni 1,200.00 kwa barabara ya *Jet Corner* – Vituka – *Devis Corner.*

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi milioni 577.00 kimetengwa kwa ajili ya ukarabati barabara ya

Ubungo Maziwa – *External na Tabata Dampo* – Kigogo, shilingi milioni 1,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Kimara – Kilungule – *External;* shilingi milioni 2,000.00 zimetengwa kwa ajili ya barabara ya Mbezi (Morogoro Road) –Malambamawili (pamoja na barabara iendayo Shule ya Msingi Malambamawili (km2) – Kinyerezi – Banana; shilingi milioni 2,100.00 kwa ajili ya barabara ya Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi *(Morogoro Road);* shilingi milioni 1,000.00 kwa ajili ya barabara ya Tanki Bovu – Goba; shilingi milioni 577.00 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Kimara – Baruti – Msewe – Changanyikeni na shilingi milioni 50.00 zitatumika kufuatilia na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo kwa kasi *(Bus Rapid Transit Infrastructure).*

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imezikasimu barabara za Jiji la Dar es Salaam ili zihudumiwe na *TANROADS,* barabara hizo ni: *Shekilango Road (km 3.8), United Nations*, Kifuru - *Pugu Station* (Mnadani), Kimara - Kinyerezi (Kimara mwisho), Kawe - *TPDF Firing* Range – Jangwani, Korogwe - Kilungule – *External, Mlimani City* - Ardhi - Makongo – Goba, *Kigogo Roundabout* – Jangwani, Ununio - *Mpiji Bridge, Tabata Dampo* – Kigogo, Temeke - Mtoni Mtongani, Buza - Kilungure – Nzasa, *Chang'ombe Road (Jct Kawawa Road/Nyerere Road- Police Chang'ombe), Taifa Road, Mgulani Road (DUCE - Mgulani JKT), Kinondoni Road, Shaurimoyo Road* na Uhuru *Road (Railway Station - Buguruni (Mandela Road).* Wizara pia ina mpango wa kujenga Dar es Salaam – Chalinze-Morogoro *Express Way* kwa utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP).*

Ujenzi wa *Flyovers* Dar Es Salaam na Barabara za Maingilio – Shilingi Milioni 2,000.00. Lengo la mradi huu ni kujenga *flyover* ya *TAZARA,* Dar es Salaam na barabara za maingilio ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kupunguza msongamano wa magari katika makutano ya barabara ya Mandela na Nyerere. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 2,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa *flyover*.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Kigamboni – Shilingi Milioni 2,788.55. Lengo la mradi huu ni kujenga daraja litakalounganisha Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Kigamboni. Kiasi cha shilingi milioni 2,788.55 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013. Mradi utajengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(National Social Security Fund (NSSF).*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Sam Nujoma (Km 4) – Shilingi Milioni 318.36. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kupanua barabara ya Sam Nujoma kutoka njia mbili kuwa njia nne pamoja na njia za waenda kwa miguu kuanzia Mwenge hadi Ubungo. Mradi huu umegharamiwa na serikali ya Tanzania na kazi za ujenzi wa barabara zilishakamilika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 318.36 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala *(Kilwa Road) (Km 12.9)* – Shilingi Milioni 8,100.00. Lengo la mradi huu ni kukarabati na kupanua barabara ya lami kutoka njia mbili hadi nne kati ya Gerezani na Mbagala kwa msaada kutoka Serikali ya Japan na Serikali ya Tanzania. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu nne ambapo awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Bendera Tatu – Mtoni kwa Azizi Ally (km 5), awamu ya pili inahusisha sehemu ya Mtoni kwa Azizi Ally – Mbagala Zakhem (km 5.1), awamu ya tatu inahusisha sehemu ya Mbagala Zakhem – Mbagala Rangi Tatu (km 1.5) na awamu ya nne inahusisha upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu – Gerezani (km 1.5). Awamu ya kwanza na ya pili imejengwa kwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan. Mkataba wa awamu ya tatu kwa ajili ya barabara yenye urefu wa km 1.5 ulisainiwa tarehe 19 Oktoba, 2010 na umekamilika Mei, 2012. Mradi huu umegharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 mradi wa Mbagala Zakhem – Mbagala Rangi Tatu umetengewa shilingi milioni 1,500.00 kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya kazi hizo. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 6,600.00 kimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Bendera Tatu – Gerezani (KAMATA).

Mheshimiwa Spika, Maegesho ya Vivuko Dar Es Salaam – Bagamoyo – Shilingi Milioni 2,000.00. Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 2,000.00 kwa ajili ya kuanza kujenga maegesho ya boti/kivuko kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa Barabara ya *Wazo Hill* – Bagamoyo – Msata (Km 107) – Shilingi milioni 7,396.806. Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 7,396.806 kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64).

Mheshimiwa Spika, Barabara zilizokasimiwa Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS (km 78.64)* - Shilingi bilioni 4.398.

Shilingi milioni 4.398 zimetengwa kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zilizokasimiwa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ndundu – Somanga (Km 60) – Shilingi Milioni 4,077.25. Llengo la mradi huu ni kujenga barabara sehemu ya Ndundu hadi Somanga (km 60) kwa kiwango cha lami. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 4,077.25 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (Km 396) – Shilingi Milioni 1,528.94. Lengo la mradi huu ni kuifanyia Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina barabara ya Kidatu hadi Lumecha/Songea chini ya msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na mchango wa Serikali ya Tanzania. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 28.94 fedha za ndani na shilingi milioni 1,500.00 fedha

za nje kwa ajili ya kuanza upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (Km 359) – Shilingi Milioni 1,200.00. Lengo la mradi huu ni kufanya Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mkataba wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulisainiwa tarehe 8 Juni, 2009 na kazi zimekamilika. Jumla ya shilingi milioni 1,200.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka 2012/2013 kwa sehemu ya Ipole – Koga – Mpanda yenye urefu wa kilometa 273.

Mheshimiwa Spika, Barabara ua Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (Km 328) – Shilingi Milioni 3,827.96. Lengo la mradi huu ni kufanya Usanifu wa Kina ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Usanifu wa Kina kwa sehemu ya Natta-Mugumu - Loliondo (km 115) na Mto wa Mbu – Loliondo (km 213) umeshakamilika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 3,000.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano - Natta – Mugumu (km 80) na shilingi milioni 827.96 kwa sehemu ya Mto wa Mbu - Loliondo. Aidha, mtatizo ya barabara katika eneo la Mto wa Mbu yatashughulikiwa. *(Makofi)*

Barabara ya Ibanda – *Itungi Port* (Km 26) – Shilingi Milioni 657.00. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2012/2013 mradi huu umetengewa shilingi milioni 657.00 fedha za ndani kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya mwisho kwa Mkandarasi aliyefanya kazi.

Barabara ya Tanga – Horohoro (Km 65) – Shilingi Milioni 12.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Tanga – Horohoro (km 65) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa *MCC* na mchango wa Serikali ya Tanzania. Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 22 Januari, 2010 na umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha shilingi milioni 12.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nzega – Tabora (Km 115) – Shilingi Milioni 10,000.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Nzega – Tabora (km 115) kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili kama ifuatavyo: Nzega-Puge (km 58.8) na Puge-Tabora (km 56.10). Kazi zilianza Februari 2011 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Kiasi cha shilingi milioni 5,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Nzega – Puge na shilingi milioni 5,000.00 kwa sehemu ya Puge – Tabora katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (Km 829) – Shilingi Milioni 16,800.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kanyani (km 497) kwa

kiwango cha lami. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Sumbawanga-Kanazi (km 75) na Kanazi-Kizi-Kibaoni (km 75.6) zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 6,400.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi kwa sehemu za Sumbawanga –Kanazi na shilingi milioni 6,400.00 kwa sehemu ya Kanazi – Kizi – Kibaoni. Kiasi cha shilingi milioni 3,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kizi – Sitalike – Mpanda na shilingi milioni 1,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Mishamo (km 100).

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyanguge – Musoma (Km 85.5) ma Mchepuo wa Usagara – Kisesa (Km 17) – Shilingi Milioni 7,500.00. Lengo la mradi huu ni kuikarabati barabara ya Nyanguge-Musoma (km 183) na kujenga kwa kiwango cha lami km 17 za mchepuo wa Usagara - Kisesa. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Mwanza/Mara Border – Musoma (km 85.5) ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 na kazi za ukarabati zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 mradi huu umetengewa shilingi milioni 6,000.00 kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ukarabati wa barabara ya Nyanguge - Musoma. Kiasi cha shilingi milioni 1,500.00 kimetengwa kwa sehemu ya barabara ya Kisesa – Usagara Bypass kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Magole – Mziha (Magole – Turiani (Km 48.8)) – Shilingi Milioni 4,110.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa

kiwango cha lami. Kazi zilianza tarehe 3 Machi, 2010 na zinaendelea. Kiasi cha shilingi milioni 4,110.00 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (Km 171) Bariadi – Lamadi (Km 71.8)) – Shilingi Milioni 7,000.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi - Lamadi yenye urefu wa jumla ya km 171 kwa kiwango cha lami. Kazi zilianza tarehe 8 Julai, 2010 kwa sehemu ya Bariadi – Lamadi yenye urefu wa km 71.80 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Kiasi cha shilingi milioni 7,000.00 kimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Km 95) – Shilingi 288.55. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kwa mwaka 2012/2013 mradi huu umetengewa shilingi milioni 288.55 kwa ajili ya kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (Km 310) – Shilingi Milioni 3,500.00. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 3,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kazi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia *(Mafia Access Road)* (Km 14) –

Shilingi Milioni 2,904.85. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa na Shirika la Misaada la Marekani *(MCC*) ambao wametoa fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia kwa makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kiasi cha shilingi milioni 2,904.85 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma *(Dodoma University Road)* (Km 12) – Shilingi Milioni 577.10. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Dodoma – Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Kiasi cha shilingi milioni 577.10 kimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kuanza kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (Km 231) – Shilingi Milioni 57.88. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Tunduma – Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 231 kwa kiwango cha lami.

Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Mfuko wa *Millennium Challenge Corporation (MCC)* na mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni:- Tunduma – Ikana (km 64); Ikana – Laela (km 64) na Laela – Sumbawanga (km 96.5).

Katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 17.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi kwa sehemu ya Tunduma – Ikana, shilingi milioni 17.00 kwa sehemu ya Ikana-Laela na shilingi 23.88 kwa sehemu ya Laela – Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kagoma – Lusahunga (Km 154) – Shilingi Milioni 10,705.01. Mradi huu ni sehemu ya barabara ya Mutukula – Bukoba – Biharamulo – Lusahunga yenye urefu wa km 294 iliyofanyiwa usanifu mwaka 1996 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Ujenzi wa sehemu ya barabara ya Mutukula – Muhutwe – Kagoma ulikamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Mfuko wa *OPEC.*

Awali Benki ya Maendeleo ya Afrika ilitoa mkopo wa ujenzi wa sehemu ya Kagoma – Lusahunga (km 154) kwa kiwango cha lami. Baada ya Mkandarasi *China State Construction Engineering Corporation Ltd. (CSCEC)* wa China kushindwa kutekeleza mkataba wa awali na kuondolewa, mkataba mpya wa kumalizia ujenzi wa barabara ya Kagoma – Lusahunga yenye urefu wa km 154 kwa kiwango cha lami ulisainiwa tarehe 18 Juni, 2009. Kazi za ujenzi zilianza Septemba 2009 na zinaendelea. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 10,705.01 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Arusha – Namanga (Km 105) – Shilingi Milioni 32,608.89. Mradi wa

Arusha – Namanga (km 105) – *Athi River* ni sehemu ya miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki unaojumuisha nchi za Tanzania na Kenya ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(African Development Bank (ADB))* na Benki ya Maendeleo ya Japan *(Japan Bank for International Cooperation (JBIC)* kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Kenya.

Lengo la mradi ni kukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi milioni 797.89 fedha za ndani na shilingi milioni 31,811.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ukarabati katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Singida – Babati – Minjingu – Arusha (Km 321) 29, 717.56. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara ya Singida - Babati -Minjingu yenye urefu wa kilomita 223 na kukarabati kwa kiwango cha lami sehemu ya Minjingu-Arusha yenye urefu wa km 98. Ujenzi wa barabara ya Singida - Babati - Minjingu umegawanywa katika sehemu tatu za Singida – Katesh (km 65.1), Katesh – Dareda (km 73.8 ) na Dareda – Babati – Minjingu (km 84.6). Kazi za ujenzi zimefikia asilimia 88.

Miradi hii inagharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA)* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkataba wa ukarabati wa sehemu ya Minjingu-Arusha umesainiwa tarehe 12 Mei, 2011 na

kazi inatarajiwa kukamilika Mei, 2014. Sehemu hii inakarabatiwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 240.56 fedha za ndani na shilingi milioni 1,340.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Singida – Katesh; shilingi milioni 336.00 fedha za ndani na shilingi milioni 1,490.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Katesh – Dareda na shilingi milioni 375.00 fedha za ndani na shilingi milioni 2,330.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Dareda – Babati – Minjingu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa sehemu zote tatu. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 289.00 fedha za ndani na shilingi milioni 23,317.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Minjingu - Arusha.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Msimba – Ruaha/Ikokoto – Mafinga (Km 219) – Shilingi Milioni 18,425.78. Lengo la mradi huu ni kufanya ukarabati wa barabara ya lami ya Dar es Salaam – Tunduma *(TANZAM).* Mradi huu unahusisha ukarabati wa sehemu ya Iyovi - Kitonga Gorge (km 86.3), Ikokoto - Iringa (km 60.9), barabara ya mchepuo kuingia Iringa mjini (km 2.1) na Iringa - Mafinga (km 68.9). Mradi huu unagharamiwa kwa mkopo kutoka Serikali ya Denmark pamoja na mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 3,584.00 fedha za ndani na shilingi milioni 13,962.38 za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na

ukarabati wa km 68.90 za Iringa - Mafinga. Aidha, jumla ya shilingi milioni 29.40 fedha za ndani na shilingi milioni 850.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya usanifu wa barabara ya Mafinga-Igawa yenye urefu wa km. 146.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Korogwe–Mkumbara (Kilomita 172), Shilingi Milioni 52,144.71. Barabara ya Korogwe-Mkumbara–Same (kilomita 172) ambayo ni sehemu ya barabara ya Segera – Moshi – Arusha iliyojengwa kwa kiwango cha lami katika miaka ya sabini imechakaa na inahitaji kufanyiwa ukarabati. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Katika utekelezaji, mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

(i) Korogwe – Mkumbara (kilomita 76). Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 72.41 fedha za ndani na shilingi milioni 26,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ukarabati wa sehemu hii ya barabara.

(ii) Mkumbara – Same (kilomita 96). Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 72.30 fedha za ndani na shilingi milioni 26,000.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ukarabati wa sehemu hii ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbeya–Makongolosi (Kilomita 115), Shilingi Milioni 9,544.95. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya Mbeya hadi Makongolosi (Kilomita 115) kupitia Chunya kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii

umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya–Lwanjilo (Kilomita 36); Lwanjilo-Chunya (Kilomita 36) na Chunya-Makongolosi (Kilomita 43). Ujenzi wa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (Kilomita 36) ulianza mwezi Septemba, 2007 na ulitegemewa kukamilika Machi, 2010. Hata hivyo, mkataba wa ujenzi ulisitishwa Aprili 2009, baada ya Mkandarasi kushindwa kutimiza matakwa ya mkataba. Mkataba na Mkandarasi mwingine ulisainiwa Desemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, kazi kwa sehemu ya Lwanjilo-Chunya (Kilomita 36) zinatarajiwa kukamilika Agosti, 2013. Barabara hii imetengewa kiasi cha shilingi milioni 4,891.33 kwa sehemu ya Mbeya–Lwanjilo; shilingi milioni 3,253.62 kwa sehemu ya Lwanjilo-Chunya na shilingi milioni 1,200.00 kwa sehemu ya Chunya–Makongolosi kwa ajili ya kuendelea na ujenzi katika mwaka 2012/2013. Aidha, shilingi milioni 200.00 zimetengwa ili kukarabati kwa kiwango cha changarawe sehemu ya Makongolosi–Rungwa–Itigi– Mkiwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Chalinze–Segera – Tanga (Kilomita 248), Shilingi Milioni 12,696.34. Lengo la mradi huu ni kuifanyia ukarabati na upanuzi barabara ya Chalinze-Segera hadi Tanga. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni:- Chalinze-Kitumbi (Kilomita km 125) na Kitumbi-Segera-Tanga (Kilomita 120). Ujenzi wa sehemu ya Chalinze-Kitumbi ulianza Aprili, 2008 na ulikamilika Oktoba, 2010. Mkataba wa sehemu ya Kitumbi-Segera-Tanga ulisainiwa tarehe 24 Desemba, 2010. Katika mwaka wa fedha 2012/13, jumla ya Shilingi milioni 3,121.00 fedha za ndani na shilingi milioni 9,575.00

fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Kitumbi–Segera–Tanga.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Ruvu, Shilingi Milioni 288.55. Lengo la mradi huu ni kujenga daraja jipya katika Mto Ruvu katika barabara ya Dar es Salaam–Tunduma *(TANZAM)*. Mradi huu ulikamilika mwaka 2009. Jumla ya shilingi milioni 288.55 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma – Iringa (Kilomita 260), Shilingi Milioni 57,930.00. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma–Mtera–Iringa (Kilomita 260). Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Shirika la Misaada la Japan *(JICA)*. Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni: Iringa–Migori (Kilomita 95.1), Migori–Fufu *Escapment* (Kilomita 93.8) na Fufu *Escapment*–Dodoma (Kilomita 70.9).

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/2013, kiasi cha shilingi milioni 400.00 fedha za ndani na shilingi milioni 20,050 fedha za nje zimetengwa kwa sehemu ya Iringa–Migori; shilingi milioni 350.00 fedha za ndani na shilingi milioni 17,550 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Migori–Fufu *Escapment* na shilingi milioni 380.00 fedha za ndani na shilingi milioni 19,200 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Fufu *Escapment* Dodoma kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Dodoma–Babati (Kilomita 261), Shilingi Milioni 36,875.91. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dodoma–Kondoa– Babati (Kilomita 261). Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Dodoma–Mayamaya (Kilomita 43), Mayamaya–Bonga (Kilomita 199 ) na Bonga–Babati (Kilomita 19.20).

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa sehemu ya Dodoma–Mayamaya unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Bonga–Babati (Kilomita 19.2) unatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Ujenzi wa sehemu hizi mbili unagharamiwa na Serikali ya Tanzania. Aidha, sehemu ya Mayamaya–Bonga inatarajiwa kujengwa kwa fedha za mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB)* na *JICA*. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha shilingi milioni 4,291.91 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Dodoma–Mayamaya na shilingi milioni 2,200.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Bonga–Babati. Kazi za ujenzi wa barabara ya Mayamaya–Bonga kwa kiwango cha lami imegawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:-

(i) Mayamaya–Mela (Kilomita 99.35). Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 577.00 fedha za ndani na shilingi milioni 14,380.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa sehemu hii ya barabara.

(ii) Mela–Bonga (Kilomita 88.80). Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 577.00 fedha za ndani na shilingi milioni 14,850.00 fedha za nje

zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa sehemu hii ya barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masasi–Songea–*Mbamba Bay* (Kilomita 649), Shilingi Milioni 125,496.85. Lengo la mradi huu ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Masasi-Songea–Mbamba Bay yenye jumla ya Kilomita 649. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu zifuatazo:- Masasi–Mangaka (Kilomita 54), Mangaka–Tunduru (Kilomita 137), Mangaka–Mtambaswala (Kilomita 65.5), Namtumbo-Kilimasera (Kilomita 60.7); Kilimasera–Matemanga (Kilomita 68.2), Matemanga–Tunduru (Kilomita 58.7), Songea-Namtumbo (Kilomita 67), Peramiho–Mbinga (Kilomita 78) na Mbinga-Mbamba Bay (Kilomita 66).

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi huu kwa barabara ya Masasi–Mangaka umekamilika. Sehemu hii inagharamiwa na Serikali za Japan na Tanzania. Kwa barabara ya Mangaka–Tunduru na Mangaka–Mtambaswala kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika na taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami zinatarajiwa kuanza katika mwaka wa 2012/2013, chini ya ufadhili wa *ADB* na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo *(JICA)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu za Namtumbo–Kilimasera (Kilomita 60.7); Kilimasera–Matemanga (Kilomita 68.2) na Matemanga–Tunduru (Kilomita 58.7) kazi zinaendelea chini ya ufadhili wa *ADB* na *JICA*. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Songea–

Namtumbo (Kilomita 67), ulisainiwa tarehe 25 Mei, 2010 na muda wa utekelezaji ni miezi 27 chini ya ufadhili wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Peramiho–Mbinga–Mbamba Bay, ujenzi wa sehemu ya Peramiho Junction–Mbinga (Kilomita 78) unagharamiwa kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa *MCC* na mchango wa Serikali ya Tanzania na kazi za ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, zimetengwa jumla ya shilingi milioni 346.85 fedha za ndani na shilingi milioni 7,300 fedha za nje kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mangaka–Nakapanya; shilingi milioni 346.00 fedha za ndani na shilingi milioni 6,500.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Nakapanya–Tunduru; shilingi millioni 346.00 fedha za ndani na shilingi milioni 6,909.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mangaka–Mtambaswala; shilingi milioni 3,617.00 fedha za ndani na shilingi milioni 33,616.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Tunduru–Matemanga.

Mheshimiwa Spika, pia shilingi milioni 3,040.00 fedha za ndani na shilingi milioni 28,359.00 fedha za nje, zimetengwa kwa ajili kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Matemanga–Kilimasera; shilingi milioni 3,040.00 fedha za ndani na shilingi milioni 27,685.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya sehemu ya Kilimasera–Namtumbo; shilingi milioni 17.00 fedha za ndani

zimetengwa kwa ajili ya Songea–Namtumbo; shilingi milioni 17.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya Peramiho–Mbinga;

Mheshimiwa Spika, vile vile shilingi milioni 2,600.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Mbinga–Mbamba Bay; shilingi milioni 29.00 fedha za ndani na shilingi milioni 950.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa sehemu ya Makambako–Songea na shilingi milioni 29.00 fedha za ndani na shilingi milioni 750.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa sehemu ya Mtwara–Mingoyo–Masasi.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* – Shilingi Milioni 120.50. Lengo la mradi huu ni kujenga Jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za ndani. Usanifu wa jengo umekamilika. Kiasi cha shilingi milioni 120.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Barabara za *Uongozi Institute* (Kilomita 8.8), Shilingi Milioni 405.50. Lengo la mradi huu ni kujenga barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia Uongozi *Institute* pamoja na barabara zilizoko ndani ya Uongozi *Institute* kitakachojengwa Bagamoyo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 405.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya

Bagamoyo kuingia Chuoni pamoja na barabara zilizoko ndani ya Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/13, Wizara imetenga kiasi cha shilingi milioni 4,800.00 kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya vivuko. Wizara kupitia *TEMESA* imepanga kuendelea na ujenzi wa maegesho *(ramps)* katika vivuko vya Msangamkuu (shilingi milioni 478.48), Rugezi-Kisorya (shilingi milioni 111.32) na kulipia sehemu ya gharama ya ujenzi wa maegesho ya Utete (shilingi milioni 954.00). Aidha, Wizara kupitia *TEMESA* imepanga kuanza ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Maisome-Kahunda (shilingi milioni 400.00), Ruhuhu (shilingi milioni 400.00) na kivuko cha Chato, maegesho yake matano ya Muharamba, Kikumbiitale, Bukondo, Senga na Zumacheli (shilingi milioni 456.2).

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na juhudi za kuanzisha usafiri wa boti au kivuko katika mwambao wa Bahari ya Hindi kuanzia Dar es Salaam hadi Bagamoyo kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Mradi huu utatekelezwa hatua kwa hatua ambapo shilingi milioni 2,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maegesho katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka wa fedha 2012/13 imetenga jumla ya shilingi milioni 2,571.149 kutoka Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipya na vifaa vya Karakana. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 1,939.050 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipya cha Ilagala (Kigoma)

na kiasi cha shilingi milioni 632.099 zimetegwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha 2012/13, Wizara imetenga kiasi cha shilingi milioni 799.415 kwa ajili ya ukarabati wa vivuko. Wizara kupitia TEMESA imepanga kukarabati vivuko vya *MV* Chato (shilingi milioni 129.00), *MV* Geita (shilingi milioni 100.00), MV Kome I (shilingi milioni 100.00), *MV* Kilombero I (shilingi milioni 180.84), *MV* Sabasaba (shilingi milioni 250.00) na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi (shilingi milioni 39.575). Ukarabati wa vivuko hivi utaviwezesha viendelee kutoa huduma kwa uhakika na usalama kwa wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali zimetengwa Shilingi Milioni 5,978.772. Mradi huu umelenga kujenga nyumba za makazi ya viongozi na watumishi wa Serikali wenye stahili hiyo. Kipaumbele kwa sasa ni katika ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji pamoja na viongozi wengine wa Serikali wenye stahili ya kupewa nyumba na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 2,364.83 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji katika Mikoa ya Kilimanjaro (1), Mtwara (1), Kagera (1) na Shinyanga (1) pamoja na umaliziaji wa nyumba za Waheshimiwa Majaji katika Mikoa ya Tabora (1), Dar es Salaam (2) Mbeya (1), Mwanza (1), Iringa (1), Tanga (1), Dodoma (1), Ruvuma (1) na Arusha (1). Aidha, jumla ya shilingi milioni 475.00 zimetengwa kwa ajili ya

kuanza ujenzi wa nyumba za viongozi wa Serikali katika Wilaya za Kasulu (1) na Ilala (1) pamoja na umaliziaji wa nyumba za Viongozi katika Wilaya za Urambo (1), Ukerewe (2), Bahi (2), Kondoa (1) na Mvomero (1). Kiasi cha shilingi milioni 400.00 zimetengwa kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bariadi, Mkoani Simiyu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 260.942 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Mwangaza (Dodoma) na zahanati ya Lindi (Manispaa). Miradi mingine iliyotengewa fedha ni pamoja na shilingi milioni 200.00 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za viongozi wa Serikali katika Wilaya ya Siha; shilingi milioni 374.400 kwa ajili ya uhifadhi wa jengo la Boma la Kale Bagamoyo; shilingi milioni 542.00 kwa ajili ya uboreshaji wa mazingira ya nje na ndani pamoja na ujenzi wa uzio kuzunguka nyumba za viongozi Dar es Salaam. Aidha, ukarabati wa karakana za *TEMESA*, karakana za useremala na ofisi za vikosi vya ujenzi zimetengewa shilingi milioni 565.77.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetenga kiasi cha shilingi milioni 375.83 kwa ajili ya kazi za ushauri, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi. Wizara pia imetenga jumla ya shilingi milioni 420.00 kwa ajili ya kufanya maandalizi ya ujenzi wa nyumba 10,000 za Watumishi wa Serikali katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara. Aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)*, imepanga kujenga nyumba 2,500 katika Mikoa yote Tanzania Bara. Jumla ya shilingi milioni 180,000.00 zitatumika kukamilisha mradi huu. Fedha hizi zitatokana na mkopo

ambao *TBA* wataupata kutoka mabenki ya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za maandalizi, *TBA* imepata jumla ya viwanja 2,253 katika Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara ikiwemo mikoa mipya minne ya Njombe, Katavi, Simiyu na Geita. Katika mikoa hiyo mipya, Wakala umeahidiwa kupewa jumla ya viwanja 600 kwa mchanganuo wa viwanja 100, Mkoa wa Katavi; viwanja 100; Mkoa wa Njombe; viwanja 100; Mkoa wa Geita na viwanja 300; Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, usalama Barabarani umetengewa Shilingi Milioni 4,302.88. Mradi huu una lengo la kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani. Katika mwaka wa fedha 2012/13, kiasi cha shilingi milioni 1,802.88 fedha za ndani na shilingi milioni 2,500.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya usalama barabarani. Miradi itakayotekelezwa ni ujenzi wa mizani ya kisasa inayopima uzito wa gari ikiwa katika mwendo (*Weigh-in-Motion)* Vigwaza. Aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013 shilingi milioni 1,358.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu itakayoendelea ikiwa ni pamoja na ulipaji wa fidia kwa baadhi ya maeneo ambapo mradi wa ujenzi wa mizani utatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi milioni 245.88 fedha za ndani na shilingi milioni 1,000 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha Wakala wa Usalama Barabarani *(National Road Safety Agency)*; shilingi milioni 22.00 fedha za ndani na shilingi milioni 1,500.00

fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa kitaalam wa utoaji wa taarifa za ajali barabarani *(Road Accident Information System)*; shilingi milioni 177.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa usimamizi, utathmini na udhibiti wa uharibifu wa barabara *(establishment of overloading management system and harmonization of road damage control and evaluation)* pamoja na ukaguzi wa usalama wa barabara *(Road Safety Audit)* wakati wa usanifu, ujenzi na baada ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Usalama, Mazingira na Marekebisho ya Mfumo, umetengewa Shilingi Milioni 800.00. Mradi huu una lengo la kugharamia shughuli za usalama na mazingira pamoja na marekebisho ya mfumo wa utekelezaji. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania na Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark, yaani *DANIDA*. Katika mwaka 2012/13 mradi huu umetengewa fedha za ndani shilingi milioni 350.00 na shilingi milioni 450.00 fedha za nje kwa ajili ya kulipia gharama za ushauri wa kitaalam *(Technical Assistance)* katika kuandaa programu za maendeleo ya sekta, kujenga uwezo wa watumishi wa Idara *(capacity building)*, kutoa elimu ya usalama barabarani *(road safety education)* shuleni na vyuoni pamoja na kugharamia matangazo na machapisho yanayohusu usalama barabarani kwa njia ya luninga, magazeti, vipeperushi, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira, imetengewa Shilingi Milioni 357.00. Mradi huu una lengo la kuelimisha utekelezaji wa Sheria ya

Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004 katika sekta ya ujenzi. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 73.00 fedha za ndani na shilingi milioni 284.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004 kwa miradi inayotekelezwa katika sekta ya ujenzi. Fedha hizo pia zitatumika kutoa mafunzo kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu ili kuwawezesha kutathmini na kusimamia utunzaji wa mazingira katika sekta ya ujenzi. Kazi nyingine ni kuandaa programu mbali mbali za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta ya ujenzi *(pollution control programmes)* na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi walioko katika sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, *Institutional Support* imetengewa Shilingi Milioni 992.472. Lengo la mradi huu ni kujenga uwezo *(capacity building)* wa wataalam wa Wizara na Taasisi zake. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 mradi huu umetengewa shilingi milioni 232.472 fedha za ndani na shilingi milioni 760.00 fedha za nje. Fedha hizo zitatumika kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani zao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, kiasi cha shilingi 300,764,800,000.00 fedha za Mfuko wa Barabara zitatumika kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara; utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara na vivuko na usimamizi wa utekelezaji wa miradi hiyo. Kati ya fedha hizo Wizara ya Ujenzi imetengewa shilingi 29,775,720,000.00 na *TANROADS* shilingi 267,981,436,800.00. Aidha, Bodi ya Mfuko wa

Barabara imetengewa shilingi 3,007,643,200.00. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 728.848 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi milioni 1,091.285 ni kwa ajili ya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya barabara nchi nzima ikiwemo ile ya Halmashauri za Wilaya, shilingi milioni 192.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Jengo la Ofisi Dodoma na shilingi milioni 995.51 ni kwa ajili ya uendeshaji. Fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi zitatumika kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Miradi ya Barabara za Mikoa ambayo imetengewa shilingi milioni 15,524.90 kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 3;

(ii) Miradi ya Barabara Kuu ambayo imetengewa shilingi milioni 9,011.71 kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na. 4;

(iii) Miradi ya vivuko kama ifuatayo: ununuzi wa kivuko kipya cha Maisome-Kahunda (Geita) shilingi milioni 1,159.05, ununuzi wa kivuko kipya cha Itungi *Port* (Kyela) chenye uwezo wa kubeba tani 50 shilingi milioni 963.74 na ununuzi wa vipuri vya vivuko 19 nchini shilingi milioni 840.95; na

(iv) Kazi za dharura za barabara na madaraja pamoja na shughuli za usalama barabarani na mazingira shilingi milioni 1,150.00.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Matengenezo ya Barabara kwa Mwaka 2012/2013. Fedha za matengenezo ya Barabara Kuu na Barabara

za Mikoa kwa mwaka 2012/2013 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni jumla ya shilingi 267,981,436,800.00. Fedha hizi zitatumika kwa kazi zifuatazo:-

(i) Shilingi milioni 220,776.797 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu zenye urefu wa kilomita 10,644.88 na madaraja 1,154 katika barabara kuu; pia kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Mikoa zenye urefu wa kilomita 21,706.27 na madaraja 1,251 pamoja na shughuli zinazohusiana na matengenezo ya barabara;

(ii) Shilingi milioni 4,398.272 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Dar es Salaam zilizokasimishwa pamoja na nyingine zitakazopandishwa madaraja katika mwaka 2012/2013;

(iii) Shilingi milioni 4,696.353 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya dharura na tahadhari;

(iv) Shilingi milioni 6,710.02 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa majaribio wa kufanya matengenezo ya muda mrefu katika Mikoa ya Mwanza, Rukwa na Tanga *(PMMR)* zitahusisha kilomita 1,092;

(v) Shilingi milioni 9,500.00 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo, ukarabati, ujenzi na shughuli za uendeshaji wa mizani; na

(vi) Shilingi milioni 21,900.00 zimetengwa kwa ajili ya usimamizi na kazi za utawala.

Mheshimiwa Spika, mpango wa matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa kwa mwaka 2012/2013 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara umeoneshwa katika Viambatisho Na. 5A hadi 5E. Viambatisho hivyo ni:-

- Kiambatisho 5: Mpango wa Matengenezo ya Barabara kwa Kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara Mwaka 2012/13 Jumla shilingi milioni 216,506.792;

- Kiambatisho 5 (A-1): Matengenezo ya Kawaida kwa Kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara 2012/2013 - Barabara Kuu, Jumla shilingi milioni 22,234.990;

- Kiambatisho 5 (A-2): Matengenezo ya Kawaida Kwa Kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2012/13 - Barabara za Mikoa, jumla shilingi milioni 28,868.170;

- Kiambatisho 5 (B-1): Matengenezo Maalum *(Periodic Maintenance)* kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2012/2013 – Barabara Kuu, Jumla shilingi milioni 59,920.831;

- Kiambatisho 5 (B-2): Matengenezo Maalum *(Periodic Maintenance)* kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2012/2013 - Barabara za Mikoa, jumla shilingi milioni 69,740.222;

- Kiambatisho 5(C-1): Matengenezo Sehemu Korofi *(Spot Improvement)* kwa kutumia Fedha za

Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2012/2013 – Barabara Kuu, Jumla shilingi milioni 1,015.025;

- Kiambatisho 5(C-2): Matengenezo ya Sehemu Korofi *(Spot Improvement)* kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2012/2013 – Barabara za Mikoa, jumla shilingi milioni 10,705.818;

- Kiambatisho 5(D): Matengenezo ya Kukinga Madaraja *(Preventive Maintenance)* kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara – Barabara Kuu na za Mikoa, jumla shilingi milioni 2,907.267;

- Kiambatisho 5(E): Matengenezo Makubwa ya Madaraja na Makalvati *(Bridge Major Repair)* kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Barabara; Barabara Kuu na za Mikoa, jumla shilingi milioni 18,124.845; na

- Kiambatisho 6: Ramani za Mikoa zinazoonesha Mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango Maalum wa Kitaifa wa Kuinua Matumizi ya Teknolojia ya Nguvu Kazi uliotengewa Shilingi Milioni 140.00 (Kutoka Mfuko wa Barabara). Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo cha Matumizi Stahiki ya Nguvu Kazi *(Appropriate Technology Training Institute -ATTI)* kimepanga kuendelea na utoaji wa mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa makandarasi wadogo katika Mikoa ya Dodoma (Bahi na Chamwino); Iringa (Mufindi na Iringa Vijijini) kwa washiriki watano kwa kila Wilaya kwa ufadhili wa *JICA*.

Mheshimiwa Spika, aidha, mafunzo yatatolewa kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu *(Technicians)* 10 kutoka Somalia kwa ufadhili wa *JICA*. Chuo kitatoa pia mafunzo ya kutengeneza barabara za lami kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi kwa mafundi sanifu 20 kutoka Halmashauri mbalimbali nchini. Chuo kitatoa mafunzo ya kufanyia matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa viongozi wa vikundi vijijini *(village gang leaders)* kutoka Wilaya ya Rungwe, Mkoani Mbeya katika Vijiji vya Kyimo kwa washiriki 30 na Ilalagwe washiriki 40.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara nchini, zimetengwa Shilingi Milioni 79.90 (Kutoka Mfuko wa Barabara). Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara itakamilisha uandaaji wa mwongozo wa ushirikishwaji wa wanawake katika kazi ya barabara, kutoa mafunzo ya kutengeneza na kukarabati barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi kwa wanawake 15. Aidha, Wizara kupitia kitengo cha ushirikishwaji wanawake katika kazi za barabara itatembelea mikoa 12 kuona ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara na pia kuhamasisha wanawake wengi zaidi washiriki kama makandarasi na wafanyakazi katika ngazi mbalimbali za kazi za barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2012/2013 watumishi 132 wanatarajiwa kupewa mafunzo, kati ya hao watumishi 29 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na watumishi 103 watahudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Aidha, wafanyakazi wa muda

mfupi na muda mrefu wanaokadiriwa kuwa 600,000 wanatarajiwa kupata ajira katika miradi ya barabara, vivuko na katika miradi ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikakati ya kupambana na UKIMWI, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na Tume ya Kudhitibi UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kutoa elimu na kuwahamasisha Watumishi kupima afya zao ili kujikinga na maambukizi mapya. Wizara itaendelea kutoa msaada wa lishe bora kwa Watumishi waliojitokeza kupata msaada.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya rushwa, katika mwaka 2012/13, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) itaendelea kuwaelimisha Watumishi juu ya athari za rushwa katika sehemu za kazi na katika jamii kwa ujumla. Watumishi wataendelea kukumbushwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa Umma katika utendaji kazi na usimamiaji mikataba mbalimbali ya sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Habari, Elimu na Mawasiliano. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa elimu na taarifa kwa umma kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara. Taarifa hizo zitatolewa kupitia vipindi vya Televisheni na Redio, Tovuti *(www.mow.go.tz)*, machapisho pamoja na makala za magazeti na vijarida. Aidha, nachukua fursa hii kuvipongeza vyombo vya habari kwa namna ambavyo vimekuwa vikifuatilia na kuripoti shughuli

zinazohusu sekta hii ya ujenzi. Wizara inaahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo hivyo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa malengo, sera, sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi zinafahamika vema kwa umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Utekelezaji Kazi Katika Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2012/2013; Wakala wa Barabara umekabidhiwa jukumu la kujenga, kukarabati na kufanyia matengenezo barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa Kilomita 35,000. Katika mwaka 2012/2013, Wakala utaendelea kusimamia kazi za kukarabati, kujenga na kufanya matengenezo ya barabara kuu (Kilomita 12,786), barabara za mikoa (Kilomita 22,214) na barabara za Jiji la Dar es Salaam (Kilomita 79.44) kulingana na bajeti iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara kuu na mikoa yanayotarajiwa kufanyika yatahusisha matengenezo ya kawaida *(routine maintenance)* Kilomita 28,496.49, matengenezo ya muda maalum Kilomita 3,854.66 na madaraja 2,405. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za utawala na usimamizi wa kazi, udhibiti wa uzito wa magari, kazi za dharura, mradi wa matengenezo ya muda mrefu na kazi zinazosimamiwa toka Makao Makuu za mipango, usalama barabarani na hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Wakala pia utaendelea kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara kuu ambapo Kilomita 414.00 ni ujenzi mpya kwa kiwango cha lami na Kilomita 135.00 ni za ukarabati

kwa kiwango cha lami na kuendelea na ujenzi wa madaraja 11. Kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala umepanga kukarabati Kilomita 573.60 kwa kiwango cha changarawe, kujenga Kilomita 31.90 kwa kiwango cha lami na madaraja 27.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali uko katika mchakato wa kutekeleza mradi maalum wa ujenzi wa nyumba 10,000 katika mikoa yote kwa ajili ya kuishi watumishi wa umma. Katika kufanikisha hili, Wakala tayari umenunua viwanja 2,254 katika mikoa 21, maeneo yenye ukubwa wa takribani ekari 1,672 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Kilimanjaro. Hivi sasa, kazi za kufanya upembuzi yakinifu pamoja na ubunifu wa majengo (maandalizi ya michoro) kwa baadhi ya viwanja na maeneo yaliyopo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania imepanga kujenga nyumba 2,500 katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya shilingi milioni 180,000 zitatumika kukamilisha mradi huu. Fedha hizi zitatokana na mkopo ambao *TBA* wataupata kutoka mabenki ya hapa nchini. Hivi sasa, Wakala umeanza na unaendelea kufanya mazungumzo na mabenki mbali mbali kwa ajili ya kupata mikopo ya muda mrefu na yenye masharti nafuu. Kutokana na juhudi hizo, Wakala umekubaliwa na Benki Kuu ya Tanzania kuwa miongoni mwa taasisi zitakazonufaika na programu maalum inayodhaminiwa na Benki hiyo ya kujenga uwezo wa watumishi kuhusiana na suala zima la *Mortgage Re-Financing*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wakala utaimarisha Idara za Ushauri na Miliki ili kuzifanya ziendane na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji halisi ya Serikali. Hatua hii itausaidia Wakala kusimamia kwa karibu ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo vyake, kubuni na kuibua vyanzo vipya pamoja na kuendelea kufanya matengenezo na kujenga majengo na nyumba za Serikali kwa utaalam zaidi na hatimaye kuboresha mazingira ya ndani na nje ya majengo na nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* imepanga kutengeneza magari 12,296 katika karakana zake zote, kuendelea na mchakato wa ununuzi wa vivuko vipya vya Ilagala (Kigoma), Itungi Port (Mbeya) na Kahunda-Maisome (Geita) pamoja na kukamilisha ukarabati wa vivuko vya *MV* Chato (Geita), *MV* Kome I (Mwanza), *MV* Kilombero I (Morogoro) na *MV* Geita (Mwanza). Aidha, *TEMESA* imepanga kujenga maegesho ya vivuko katika maeneo ya vivuko vya Msangamkuu (Mtwara), Chato (Geita), Ruhuhu (Ruvuma), Maisome-Kahunda (Geita), Rugezi-Kisorya kwa upande wa Ukerewe (Mwanza) na Dar es Salaam - Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, *TEMESA* pia itaendelea kutoa ushauri wa kihandisi, kufanya matengenezo na usimikaji wa mifumo ya umeme, elektroniki, viyoyozi na mabarafu katika majengo ya Serikali na kuendelea na ukarabati wa karakana pamoja na kuzipatia vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara. Katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Mfuko wa Barabara imepanga kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya kuongeza wigo wa vyanzo (vipya) vya mapato ya Mfuko pamoja na mapendekezo ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Barabara. Bodi, kwa kushirikiana na *EWURA*, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, itaweka mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato na uchakachuaji wa mafuta pamoja na kushirikiana na *TANROADS* katika kudhibiti wa uzito wa magari na mizigo inayosafirishwa kwa barabara. Aidha, Bodi itaanza kutumia mwongozo wa matumizi ya fedha za Mfuko ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Barabara na kuweka mikakati ya kuongeza uwezo na ufanisi wa Taasisi zinazotumia fedha ili ziweze kutumia fedha hizo vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Bodi ya Usajili wa Wahandisi imepanga kusajili wahandisi 995, Mafundi Sanifu 200, kampuni za ushauri wa kihandisi 30 pamoja na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu 1,000. Bodi pia itafanya ukaguzi wa kina katika miradi ya ujenzi, viwanda, taasisi za elimu ya juu zinazofundisha uhandisi pamoja na makampuni yanayoajiri wahandisi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kubaini kama kazi za kihandisi zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa na Bodi pamoja na kupata idadi kamili ya wahandisi walio katika shughuli za kihandisi nchini. Aidha Bodi itafanya ukaguzi wa kina katika taasisi za elimu ya juu zinazofundisha uhandisi ili kubaini kama vyuo hivyo vina

sifa stahiki za kufundisha wahandisi na iwapo wahadhiri wanaofundisha wahandisi wamesajiliwa na Bodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 4 ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2010. Ili kufanikisha lengo hilo, msukumo mkubwa utakuwa kwenye kuimarisha rasilimali watu na elimu kwa umma. Aidha, Bodi imepanga kusajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi 39, kuwasajili wataalam wenye sifa za kati 146 na Makampuni ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi 23. Bodi pia imepanga kutembelea mikoa yote ya Tanzania Bara kuelimisha waendelezaji wa miradi ya ujenzi kuhusu umuhimu wa kutumia wataalam waliosajiliwa na Bodi katika miradi yao. Bodi itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watakaokiuka taratibu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili Bodi, kwa kuendelea kuwawezesha wahitimu wengi zaidi kupata mafunzo kwa vitendo, wataalam kujihusisha na ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa barabara, pamoja na kuwapatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Usajili wa Makandarasi imepanga kusajili jumla ya makandarasi 807 wa fani mbalimbali na kutathmini utendaji wa makandarasi 587 ili kujiridhisha kama bado wana sifa na uwezo wa kuendelea kuwa katika madaraja waliyopo. Baadhi ya sifa zitakazohakikiwa ni uwepo wa Wakurugenzi wa Ufundi *(Technical*

*Directors)*, Wahandisi waliosajiliwa, vitendea kazi na ofisi zinazotambulika. Aidha, Bodi itakagua miradi ya ujenzi 3,090 nchi nzima kwa lengo la kuhakikisha kwamba kazi zote zinafanywa na makandarasi waliosajiliwa, wanaofuata sheria na taratibu za ujenzi katika utekelezaji wa miradi, pamoja na kuendesha kozi sita za mafunzo katika mikoa mbalimbali ya Tanzania. Zaidi ya makandarasi 180 wanatarajiwa kuhudhuria mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, mafunzo yatalenga maeneo ya usimamizi wa miradi, ukadiriaji wa gharama za ujenzi na uandaaji zabuni na afya na usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi. Bodi pia itasimamia ujenzi wa daraja la Mbutu unaojengwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga *(design and build)*. Mradi huu unatekelezwa kwa ubia na Makandarasi wazalendo 13 na Wahandisi Washauri wazalendo wawili kwa lengo la kukuza uwezo wa wazalendo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Baraza la Taifa la Ujenzi limepanga kushiriki katika uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Ujenzi ya mwaka 2003, kuandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha Baraza la Taifa la Ujenzi, kuendelea na jitihada za kuanza kazi kwa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi *(Construction Industry Development Fund – CIDF)*, kuratibu mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji *(Construction Sector Transparency Initiative – CoST),* kufanya tafiti nne (4) kuhusiana na sekta, kuratibu na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri wa kiufundi na

utatuzi wa migogoro pamoja na kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza la Taifa la Ujenzi litaendelea na ujenzi wa Jengo la Ghorofa 18 la Ofisi lililoko Barabara ya Samora, Dar es Salaam kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* na Lindi *Express Limited* pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kitega uchumi maeneo ya *Regent Estate* na Mbezi *Beach*, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Vikosi vya Ujenzi vinategemea kutekeleza miradi minne (4) yenye thamani ya shilingi milioni 2,325. Miradi hiyo inahusu awamu ya tatu ya Ukarabati na Uhifadhi wa Jengo la Boma la kale Bagamoyo (*Phase III*), ujenzi wa nyumba za viongozi Dar es Salaam na Mwanza, ujenzi wa maegesho ya Kivuko cha Rugezi, Ukerewe (Mwanza) na kuendelea kufanya maboresho hasa ya vitendea kazi, kukarabati ofisi na karakana za Kikosi pamoja na kuanzisha mradi wa Kituo cha Vifaa vya Ujenzi *(Building Materials Centre)* Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ujenzi, Morogoro kimetengewa Shilingi Milioni 160.00 (Kutoka Mfuko wa Barabara). Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi 780 katika fani za ufundi stadi wa kazi za barabara, majengo pamoja na udereva. Aidha, Chuo kimepanga kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la madarasa na karakana ya ufundi, kukarabati majengo matatu pamoja na kununua samani na zana za kufundishia.

Utaratibu wa kukisajili Chuo kisheria unaendelea. Mchakato wa kukisajili utaendelea katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia katika Sekta ya Uchukuzi *(Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)*. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya barabara na uchukuzi hapa nchini. Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Taifa cha Morgan *(Morgan State University)* cha Marekani pamoja na wadau wengine, Kituo kimepanga kuanza kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na uchukuzi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kituo kwa kushirikiana na wadau, kimepanga kuandaa warsha na kozi zinazolenga kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya barabara na uchukuzi. Warsha na kozi hizi zitahudhuriwa na wadau wapatao 340 na kusambaza kwa wadau 100,000 jumla ya makala na taarifa 150 zinazohusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya barabara na uchukuzi kwa ujumla pamoja na kuendelea kutoa huduma ya Maktaba ya Kituo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wabunge wote, nikielekeza shukrani maalum kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kwa michango,

ushauri na ushirikiano waliotupa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Wizara inaahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukurani zetu ziwaendee Washirika wetu wa Maendeleo waliochangia katika kutekeleza programu na mipango yetu ya sekta. Nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyochangia kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta yetu ni pamoja na Abu Dhabi, Canada *(CIDA)*, Demark *(DANIDA)*, Japan *(JICA)*, Korea, Marekani *(MCC)*, Uingereza *(DFID)*, Benki ya Dunia *(WB)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Kuwait *Fund* na *OPEC Fund*. Aidha, tunawashukuru wadau wengine mbalimbali hususani wa sekta binafsi, kwa ushiriki wao katika ujenzi wa barabara, madaraja, nyumba na vivuko pamoja na ushirikiano wanaotupa katika kutekeleza malengo ya sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara nikianza na Mheshimiwa *Engineer* Gerson H. Lwenge, Naibu Waziri; Balozi Herbert E. Mrango, Katibu Mkuu; *Engineer* Daktari John S. Ndunguru, Naibu Katibu Mkuu; Wenyeviti wa Bodi za Mfuko wa Barabara, Usajili wa Makandarasi, Usajili wa Wahandisi, Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Baraza la Taifa la Ujenzi, *TANROADS, TEMESA* na *TBA* kwa ushirikiano walionipa. Aidha, nawashukuru Watendaji Wakuu wa *TANROADS, TBA, TEMESA*, Mfuko wa Barabara, Bodi za Usajili wa

Makandarasi, Usajili wa Wahandisi, Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Baraza la Taifa la Ujenzi, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kipindi cha uongozi wangu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu pamoja na uvumilivu walionao kwangu wakati nikitekeleza majukumu ya Kitaifa. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara ya Ujenzi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 329,085,354,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 21,340,508,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, shilingi 300,764,800,000.00 ni fedha za Mfuko wa Barabara na shilingi 6,980,046,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Wizara ya Ujenzi inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 693,948,272,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 296,896,892,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 397,051,380,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka 2012/2013.

**MAELEZO** **KIASI (SHILINGI)**

Mishahara… … … … … … … … … … … … 21,340,508,000

Mfuko wa Barabara… … … … … … … … …300,764,800,000

Matumizi Mengineyo… … … … … … … … … 6,980,046,000

Jumla ya Fedha za Matumizi ya Kawaida… … 329,085,354,000

Fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo… ...296,896,892,000

Fedha za nje kwa Miradi ya Maendeleo… … ..397,051,380,000

Jumla Fedha za Maendeleo… … … … … … 693,948,272,000

**JUMLA KUU… ... ... ... ... ... ... ... ... ... …1,023,033,626,000**

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono hivyo nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii. Mheshimiwa Anne K. Malecela, Makamu Mwenyekiti!

**MHE. ANNE K. MALECELA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa yangu naomba nianze kwa kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa uwasilishaji mzuri sana wenye vielelezo na kutoa picha kamili ni kiasi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajitahidi kutatua tatizo la miundombinu Tanzania. Kipekee niipongeze *TANROAD* kwa kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa maandalizi, ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hiyo mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2012/2013

ikiwa ni pamoja na Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, nitaomba speech yangu iende moja kwa moja kwenye *Hansard* kwa sababu kulingana na wakati kuna sehemu nyingine nitaziruka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2011/2012. Wizara ya Ujenzi imejitahidi kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Kamati. Kwa ujumla Kamati imeridhika na utendaji wa Wizara hii isipokuwa kwa maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ucheleweshaji na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Wizara ilikusudia kukusanya mapato ya shilingi 41,873,788/=. Mpaka kufikia Aprili 2012, jumla ya shilingi 16,606,114/= ikiwa ni 39.7% ya makadirio ya fedha zilizokusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ilitengewa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida shilingi 245,440,294,000/= ikiwa ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2012 Wizara ilikuwa imepokea sh. 250,075,053,989.50/= ikiwa ni 101.89% ya makadirio yote. Ongezeko hili linatokana na makusanyo ya kodi ya mafuta ya taa baada ya

kuondoa punguzo la kodi katika bidhaa hii kwa lengo la kuepusha uchakachuaji wa mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2011/2012 Serikali ilitenga shilingi 1,155,976,940,000/= kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Mpaka kufikia Mei, 2012 shilingi 565,037,330,000/= zilikuwa zimetolewa sawa na 48.8%.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwelekeo wa bajeti na mpango wa bajeti kwa mwaka wa 2012/2013. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Wizara kupitia Idara mbalimbali na Vitengo vyake inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 15,628,580/=.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Wizara imetengewa jumla ya sh. 329,085,354,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 693,948,272,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hivyo makadirio kwa ajili ya matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 jumla ni sh. 1,023,033,626,000/=.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kuhusu Miradi ya Ujenzi wa Barabara; katika Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka uliopita Kamati hii iliwahi kushauri kuwa ujenzi wa baadhi ya barabara katika ngazi ya Wilaya katika Halmashauri zetu zisimamiwe na *TANROADs*. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanza kutekeleza ushauri huu ambapo kwa sasa imepandisha hadhi barabara 22 za Jiji la Dar es salaam na zingine 18 zinakusudiwa kupandishwa hadhi ambazo zilikuwa chini ya Manispaa za Jiji la Dar es Salaam na sasa kuwa

chini ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Barabara 22 ambazo tayari zimeshapandishwa hadhi ni:-

(1) Kwembe- Malambamawili;

(2) Kifuru-Pugu Stesheni;

(3) Kimara-Kinyerezi;

(4) Kawe-*TPDF Firing Range*;

(5) Chanika –Zingiziwa;

(6) Banana – Kitunda- Msongola;

(7) Korogwe- Kilungule- Kisukuru-*External*;

(8) Kimara –Nzasa- Binyokwa- Kinyerezi;

(9) Mlimani *City*- Ardhi-Makongo-Goba;

(10) Kigogo *Roundabout* Jangwani;

(11) Ununio- Mpiji Bridge;

(12) Uhuru *Road- Railway Station*- Buguruni-Mandela Road;

(13) Tabata Dampo-Kigogo;

*(14) United Nations Road*;

(15) Kibada –Tungi;

(16) Temeke- Mbagala;

(17) Buza- Kilungule- Nzasa;

(18) Barabara ya Chang'ombe (Kawawa/Nyerere *Junction-Police* Chang'ombe);

(19) Barabara ya Mgulani (*TAMECO*- Kilwa *Road* kupitia *DUCE*);

(20) Barabara ya Shekilango;

(21) Barabara ya Kinondoni; na

(22) Barabara ya Shaurimoyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri barabara zote hizi zijengwe kwa kiwango cha lami. Ni matumaini ya Kamati kuwa utaratibu huu utaendelea kwa barabara za Majiji ya Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya na baadaye kwenye Manispaa kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara zinazohitajika kujengwa ni nyingi na kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosha, Kamati iliishauri Serikali kutumia mpango wa BOT *(Build - Operate and Transfer), BOOT (Build – Own - Operate and Transfer)* na ule wa *PPP (Public Private Patnership)* na kuharakisha kutunga Sera husika. Wizara ilieleza kuwa imeshafanya utafiti wa awali kubaini miradi inayoweza kutekelezwa kwa utaratibu huo ikiwemo ujenzi wa barabara ya Dar es

Salaam- Chalinze, Arusha-Moshi, Chalinze-Morogoro na usafiri wa majini katika bahari ya Hindi kuanzia Bagamoyo hadi Magogoni, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia hiyo njema, Kamati inashauri Serikali iweke muda maalum wa utekelezaji *(Timeframe)* badala ya kutumia kauli za "inaangalia uwezekano, iko mbioni, juhudi zinafanywa, na maneno mengine kama hayo". Iwapo utafiti umeshafanywa miradi hiyo itangazwe ili wawekezaji wenye nia na uwezo wa kujenga barabara hizo wafanye hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwa na barabara zinazojengwa na kusimamiwa na watu au makampuni binafsi umeshazoeleka katika nchi zingine kama vile nchi nyingi za Mashariki ya Mbali za Singapore, Malaysia, Thailand na kadhalika. Hivyo, kama ilivyo katika nchi zingine, Kamati inashauri kuwe na hamasa na ushawishi kwa wawekezaji binafsi kujenga barabara mijini ili watumiaji wa barabara hizo wazitumie kwa malipo. Utaratibu huu utachangia kupunguza ama kuondoa kabisa msongamano wa magari katika miji yetu hasa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufika mwezi Machi, 2012, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 351.977 kati ya shilingi bilioni 609.743 zilizoko kwenye bajeti ya mwaka wa 2011/2012. Hata hivyo, sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa imetumika kulipa madeni ya mwaka wa 2011/2012 ambayo yalikuwa ni shilingi bilioni 420. Tafsiri yake ni kwamba, sehemu kubwa ya miradi inayoendelea sasa inafanywa kwa mkopo kwani fedha

iliyokasimiwa kuigharamia imetumika kulipa madeni yaliyopita. Kamati inashauri kuwa wakati wa majumuisho ya mjadala wa bajeti ya mwaka 2012/2013 ya Wizara hii ni vizuri Bunge lako Tukufu lielezwe Serikali inadaiwa kiasi gani katika sekta ya barabara kutokana na bajeti ya mwaka uliopita wa 2011/2012 ili kujua iwapo bajeti inayopitishwa sasa itakwenda kujenga miradi iliyokusudiwa au ni kwa ajili ya kulipa madeni.

Kwa mfano, mwezi Mei, 2012 Kamati ilipofanya ziara ya kukagua miradi katika Kanda ya Ziwa ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012 miradi ya barabara kwa Mkoa wa Shinyanga peke yake ilikuwa na madeni ya karibu sh. 80,095,829,177.98/= na riba inayotokana na madeni hayo ilikuwa karibu shilingi 8,929,361,938/=, inawezekana hali katika mikoa mingine ikawa ni mbaya zaidi. Hali hii ni lazima iwekewe mkakati maalum wa kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya ziara katika Kanda ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini na kubaini kuwa kuna barabara zimekwama katika ujenzi kutokana na tatizo la utawala zaidi kuliko tatizo la fedha. Mfano wa barabara hizo ni barabara ya Namtumbo-Kilimasera, Kilimasera-Matemanga na Matemanga-Tunduru. Utekelezaji wa miradi hii umekwama kwa muda mrefu. Kamati inashauri Wizara ichukue hatua za kimkataba mara moja kwa mkandarasi wa miradi hii. Hata hivyo hatua hizo za kimkataba zisitoe mwanya kwa ujenzi wa barabara hizi kusimama kabisa, jambo la muhimu ni kumsimamia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri pia kuwa Mameneja wote wa Wakala wa Barabara (*TANROADS*) katika ngazi ya Mikoa wawe sehemu ya usimamizi wa ujenzi wa miradi ya barabara unaotekelezwa ndani ya mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inakusudia kupanua barabara na hivyo kulazimika kuwaondoa wananchi waliojenga ndani ya eneo linalokusudiwa kuwa sehemu ya barabara ni vema wananchi hao, kwa kuzingatia sheria husika, walipwe mara baada ya maeneo yao kuthaminiwa ili kuepuka kupanda gharama za ujenzi pamoja na kuondoa manung'uniko kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa barabara inaligharimu Taifa letu fedha nyingi sana. Kamati inaendelea kushauri kuwa ujenzi wa barabara, hasa zinazojengwa kwa fedha za ndani, zifanywe na Wakandarasi na Wakandarasi Washauri wa ndani au Wakandarasi na Wakandarasi Washauri wa nje kwa kuingia ubia na Wakandarasi wa ndani. Uamuzi huu utasaidia kubakiza fedha zetu nchini na kuwaongezea uwezo Wakandarasi wa ndani pamoja na kuhawilisha teknolojia *(technology transfer)* kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya kulipa madeni na hati za malipo zinazopokelewa kutoka kwa Wakandarasi na Wahandisi Washauri wanaotekeleza kazi za kandarasi nchini. Kamati inaishauri Wizara iweke vipaumbele vichache vya barabara za kujengwa kutokana na

umuhimu wake kiuchumi na kijamii ili kuleta tija na kuweza kurejesha gharama ya ujenzi wa barabara husika. Barabara za vipaumbele ziwe ni zile zinazounganisha nchi yetu na nchi za jirani, Mikoa, Wilaya na maeneo ya uzalishaji kama vile unaotokana na kilimo, madini na viwanda. Vipaumbele hivi vitaifanya Serikali kutoelemewa na madeni yanayotokana na riba na adhabu zingine zinazotokana na Mikataba ya kazi za ujenzi.

Mifano ya barabara hizo muhimu ni:-

(i) Kidahwe-Kasulu- Nyakanazi;

(ii) Kanyani- Mpanda- Sumbawanga;

(iii) Bunda- Kisolya-Nansio;

(iv) Dodoma- Babati;

(v) Dodoma- Iringa;

(vi) Kyela- Kasumulu;

(vii) Mtwara-Tunduru-Songea- Mbamba Bay;

(viii) Bagamoyo- Saadani- Tanga;

(ix) Arusha- Musoma;

(x) Mbeya-Chunya- Tabora;

(xi) Manyoni-Tabora- Kigoma;

(xii) Tabora- Sikonge- Mpanda;

(xiii) Mwigundi - Maswa-Bariadi-Lamadi; na

(xiv) Mpanda- Kaliua-Kahama.

Mheshimiwa Spika, alama za barabarani ni muhimu sana kwa usalama wa watumiaji wa barabara. Hata hivyo, kumekuwa na wimbi kubwa la watu kuiba au kuharibu alama hizi za barabarani. Baadhi ya alama hizi pamoja na mifuniko ya mifereji ya maji machafu, vyuma vinavyowekwa kwenye kingo za barabara na madaraja kuibwa na kuuzwa kama chuma chakavu. Kamati inashauri itungwe sheria ya kudhibiti uuzaji wa chuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu. Aidha, Kamati inashauri vile vile kuwa, kila barabara inayojengwa iwe na alama kwa ajili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi nchini ni za kiwango cha udongo au changarawe. Barabara hizi hugharimu fedha nyingi kuzikarabati hasa wakati wa kipindi cha mvua. Ili kuepuka hali hii, Kamati inashauri Serikali iongeze jitihada kwa ajili ya ujenzi wa barabara za kudumu za lami na kupunguza barabara za udongo au changarawe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ni tatizo kubwa sana.

Kama ilivyoelezwa katika taarifa ya Kamati hii mwaka uliopita wa 2011/2012 zaidi ya 84% ya kodi za ndani zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania zinatoka katika Jiji la Dar es Salaam. Tafsiri yake ni kwamba uchumi wa nchi hii kwa sehemu kubwa unategemea shughuli za kiuchumi zinazofanyika Jijini Dar es Salaam ambazo kwa bahati mbaya zinatatizwa na usafirii na hivyo kutatiza uchumi wa nchi pia. Aidha, taarifa hiyo pia ilieleza kuwa tafiti zilibaini kuwa Tanzania inapoteza kiasi cha bilioni nne kila siku (kiasi cha trilioni 1.44 kwa mwaka) kutokana na adha hii ya usafiri Jijini Dar es salaam. Fedha hizi ni nyingi na Serikali inaweza kuziokoa kwa kutekeleza mipango yote iliyopendekezwa na wataalam na watafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali itatue kero hii kwa kujenga na kuimarisha barabara za pembezoni *(feeder roads),* kujenga barabara za juu *(fly overs),* usafiri wa boti kutoka Bagamoyo mpaka feri pamoja na usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam. Serikali ilieleza mipango yake ya kujenga *flyovers* na kuanzisha usafiri wa boti katika bahari ya Hindi kutoka Bagamoyo hadi Magogoni Jijini Dar es Salaam, mwaka wa fedha wa 2012/2013 bado inaelezea mipango hiyo.

Kamati inashauri mipango hiyo ianze kutekelezwa badala ya kuishia kwenye makabrasha. Kwa mfano, wakati wa kujadili mapendekezo ya bajeti hii mwezi Juni 2012, Jijini Dar es Salaam, Serikali iliieleza Kamati kuwa mwaka 2012/2013, imepanga kuanza taratibu za kununua boti au vivuko na kujenga maegesho katika eneo litakalokubalika. Hata hivyo, hakuna mpango uliowekwa utakaoweza kufuatiliwa na kufanyiwa

tathmini. Kamati inashauri itolewe taarifa mahsusi kuhusu mipango hii, ilieleze Bunge lako Tukufu mpango wa utekelezaji, muda wa utekelezaji, gharama na hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa kuanzia *Flyover* itaanza kujengwa eneo la *TAZARA* kwenye makutano ya barabara ya Nyerere na barabara ya Mandela, pamoja na kuwa ni jambo jema madhara yake ni kuwa baada ya kukamilika kwa ujenzi huo kutakuwa na msongamano wa kutisha pande zote mbele ya daraja hilo kwani magari yote yatajazana katika makutano yanayofuata baada ya makutano ya *TAZARA*. Kamati inashauri kuwa ujenzi wa *flyovers* katika makutano ya Ubungo na Chang'ombe uharakishwe kama ilivyo katika mpango wake wa kujenga *flyovers* hizo vinginevyo *flyover* ya *TAZARA* itaongeza tatizo badala ya kutatua.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati hii mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012, tulisema kuwa, tulipokea taarifa kutoka Wizarani iliyoeleza kwamba daraja la Kigamboni lingejengwa na *NSSF* na mpaka mwezi Februari, 2011, shirika hilo lilikuwa limeshapata 60% ya fedha ambazo zingetumika katika ujenzi wa daraja hilo. Kama ilivyo katika mipango ya Serikali iliyoelezwa hapo juu, ujenzi bado haujaanza na katika mipango yake ya mwaka 2012/2013, ujenzi huo umeelezwa na kwamba Mkataba wa Ujenzi wake ulisainiwa mwezi Januari mwaka huu wa 2012. Kamati inaitaka Wizara wakati wa majumuisho ya bajeti hii ilieleze Bunge lako Tukufu iwapo 40% ya fedha iliyosalia imepatikana na kwamba wananchi wa Kigamboni na

wakazi wa Dar es Salaam kwa ujumla wataanza kushuhudia ujenzi ukianza mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 na siyo kuendelea kusikia mipango mikakati ya ujenzi huo ikielezwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari uliopo Jijini Dar es Salaam pia limeanza kujitokeza katika Majiji ya Mwanza na Arusha. Kamati inashauri hatua za kutatua tatizo hilo zichukuliwe mapema kabla ya kuwa kubwa kama ilivyo Dar es Salaam. Mji wa Dodoma pia unakuwa kwa kasi sana na hivyo kupelekea ongezeko kubwa la magari. Ni vema mamlaka husika zianze kuboresha miundombinu ili kuzuia tatizo hilo lisijitokeze.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara na usimamizi wa usafiri na usafirishaji katika miji yetu unafanywa na wadau wengi na hivyo kuleta migongano inayochelewesha maamuzi na utekelezaji wa maamuzi yanayofikiwa. Ili kuondoa hali hii Kamati inaendelea kushauri kuwa masuala ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam yasimamiwe na mamlaka moja itakayokuwa na mamlaka kamili.

Mheshimiwa Spika, katika barabara zetu kuna mashimo mengi ambayo wakati mwingine yanakuwa chanzo cha ajali za barabarani, uharibifu wa magari na pia kuongeza msongamano wa magari hasa katika Jjiji la Dar es Salaam. Kamati inashauri kuwa ukarabati wa barabara ufanywe mara kwa mara na kwa wakati, pia fedha za ukarabati wa barabara hizo zitengwe ili zitumike kila inapohitajika. Aidha, kuwe na utaratibu mahsusi wa kusafisha mifereji ya maji ya mvua katika

barabara zetu kwani mara nyingi mvua zikinyesha hasa Jijini Dar es Salaam kunakuwa na kero kubwa sana ya magari kushindwa kupita barabarani au kusababisha msongamano mkubwa sana. Katika kutekeleza hili Wizara ishirikiane na wadau wengine kuhamasisha wananchi kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri pia kuwa barabara zote zinazoingia Jijini Dar es Salaam, barabara za Kilwa, Morogoro, Nyerere, Bagamoyo pamoja na barabara ya Mandela zipanuliwe ili kuwa na njia nne. Kamati inashauri kuwa, Serikali inapopanga kujenga barabara ifikirie miaka mingi ijayo kwa kujenga barabara pana zitakazohimili wingi wa magari kwa miaka mingi mbele. Kwa mfano, ni jambo la kushangaza kuwa, mwaka 1976 wakati Dar es Salaam ilipokuwa na watu wachache na eneo kubwa likiwa pori Mwalimu Nyerere alifikiria kujenga barabara ya Mandela ikiwa na njia mbili *(double lane),* leo miaka 36 baadaye bado tunajenga barabara za njia mbili, maana yake ni kwamba, mawazo yetu hayaendi mbele badala yake yanarudi nyuma kwa miaka 36. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria mtengenezaji mkuu wa magari ya Serikali ni Wakala wa Ufundi na Umeme. Hata hivyo, Wakala huyu hana wataalam na vifaa vya kutosha na hivyo wakati mwingine kulazimika kuelekeza magari ya Serikali yakatengenezwa kwenye gereji binafsi, Kamati inashauri Wakala huyu aimarishwe kwa kupewa vifaa vya kutosha na wataalam ili lengo la Serikali la kuanzisha Wakala huu litimie.

Mheshimiwa Spika, ni Wakala huo pia ndiyo unaoidhinisha kuwa gari fulani haliwezi kutengenezeka au iwapo utengenezaji wake utaigharimu sana Serikali kiasi ambacho ni nafuu zaidi kuliuza na kununua gari jipya kuliko kulitengeneza. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikipata hasara kubwa kutokana na magari yanayopelekwa huko kutotengenezwa na hata uamuzi wa kuyauza hautolewi kwa wakati, hivyo magari kuendelea kuwepo huko mpaka yanaoza na kuwa chuma chakavu. Kwenye Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali pia kuna magari yaliyotelekezwa kwa muda mrefu na mengine mpaka yameoza. Kamati inashauri Wakala kuwa uamuzi wa kutengeneza au kuuza utolewe mapema ili Serikali isipate hasara. Aidha, iwe ni lazima kuwa kila Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zisiruhusiwe kununua magari mengine mpaka yaliyokuwepo hatma yake imejulikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mizani za barabarani, mizani ni muhimu sana katika kudhibiti uzito wa magari unaopelekea uharibifu wa barabara zetu. Hata hivyo, inaelekea ufanisi wa vituo vya mizani tulivyonavyo ni mdogo kwani pamoja na kuwa na vituo vingi vya mizani bado barabara zetu zinaharibika kutokana na uzito wa magari yanayopita. Kwa sasa hali ni mbaya zaidi katika sehemu za milima ambapo upande wa barabara wenye uelekeo wa kupanda milima unaharibika na kutengeneza migongo kudhihirisha kuwa uzito wa magari ni mkubwa kuliko uwezo wa barabara. Kamati inashauri kuwa wasimamizi wa

mizani hizi wawe waadilifu na makini zaidi katika upimaji wa magari ili kulinda barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, malori yanayosafirisha mizigo kwenda nje ya nchi *(Transit goods)* yawe na vituo vichache vya mizani ili kutoyapotezea muda mwingi njiani kwani yaliyo mengi yamefungwa lakiri (*seal*) na hivyo ni vigumu kupakia na kupakua mizigo njiani jambo ambalo linaweza kuongeza mizigo baada ya kupima mizigo katika mizani za mwanzo. Kwa mfano, lori linalokwenda Rwanda likipimwa Dar es salaam lipimwe tena Dodoma na mzani wa Mwendakulima badala ya hali ya sasa ambapo linapimwa Dar es Salaam, Kibaha, Mikese, Kihonda, Dodoma, Singida, Tinde, Mwendakulima, Nyakahura na Benaco.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe pia katika vituo hivi kuna foleni kubwa ya malori na mabasi wakati huo huo kuna vituo vingine njiani vinavyosimamiwa na mamlaka nyingine kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na askari wa usalama barabarani ambavyo pia pamoja na kazi nzuri wanazofanya wanachangia kuchelewesha muda wa malori haya na hivyo kupunguza mzunguko wa biashara. Aidha, mizani zijengwe kando ya barabara kuu ili kuruhusu kupita magari mengine ambayo hayahitaji kupima uzito.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa majengo Tanzania (*TBA*) unahusika zaidi na ujenzi na usimamizi wa nyumba za Serikali. Kutokana na ukosefu wa nyumba kwa ajili ya watumishi wa Serikali, Kamati inashauri Wakala huu ujenge nyumba kwa ajili ya kuwauzia au kuwakopesha watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili Wakala huyo atekeleze majukumu yake ipasavyo Kamati inashauri taasisi zinazoshughulika na upimaji na utoaji wa viwanja zipunguze urasimu katika upimaji na ugawaji wa viwanja hivyo. Aidha, taasisi zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ya umeme na maji pia zipunguze urasimu kwani urasimu unapunguza ufanisi wa miradi ya ujenzi wa nyumba zinazokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala huu unakabiliwa na uhaba mkubwa wa fedha ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inashauri kuwa ni vema sasa waanze kujiendesha kibiashara kwa kujihusisha na usanifu wa majengo, kuchora ramani, kukopa benki kwa kuweka dhamana mali zake ikiwemo majengo na viwanja, kuingia ubia na wawekezaji wengine na mengineyo ili kujiongezea kipato. Ili kufanikisha ukopaji kutoka vyombo vya fedha ni muhimu mali zote za Wakala huu ziwe na Hatimiliki za majengo na viwanja vyake vyote. Aidha, Wizara isimamie sheria ili wote wanaodaiwa na Wakala huu wahakikishe kuwa wanalipa madeni yao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*), miradi mingi yenye thamani kubwa, hususan ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami hufanyika na Wakandarasi wageni kwa kuwa Wakandarasi wa Kitanzania hawana uwezo wa kutekeleza miradi hiyo ikiwa ni pamoja na uzoefu, mitambo, utaalam na mitaji. Ili kukuza uwezo wa Wakandarasi wa kizalendo, Kamati inaishauri Wizara kuwa, Bodi hiyo, kwa kushirikiana na Serikali na wadau

wengine ibuni mkakati maalum wa makusudi wa kuendeleza Wakandarasi wazalendo. (*Makofi*)

Kutokana na uhaba wa mitambo katika sekta ya ujenzi hususan kwa Wakandarasi wa kizalendo ambayo ni kero kubwa kwa Wakandarasi, Kamati inashauri kuwa Serikali iwezeshe upatikanaji wa mitambo hiyo kwa gharama nafuu, kuhamasisha makampuni yanayokodisha na kuuza mitambo kuja kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ujenzi ni sekta muhimu inayochangia ajira nchini. Aidha, shughuli za ujenzi kwa asili yake zinahitaji Mkandarasi awe na mtaji mkubwa kutekeleza kazi jambo ambalo limesababisha Wakandarasi wa Kitanzania wengi wenye mitaji midogo kutoshiriki kikamilifu kutumia fursa za ujenzi. Kamati inashauri Serikali ifanye juhudi kuwawezesha Wakandarasi na Wakandarasi Washauri wa Kitanzania wenye mitaji midogo kushiriki katika kazi za ujenzi ili kuongeza ajira kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwiano wa Wahandisi na Mafundi Sanifu; kumekuwa na wimbi la kubadilisha Vyuo vya Ufundi na kuwa Vyuo Vikuu na hivyo kusababisha Taifa kukosa idadi ya kutosha ya mafundi sanifu watakaokidhi mahitaji ya soko. Kamati inashauri kuwa Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Mamlaka ya Ufundi (*VETA*) ijipange katika kupanga mikakati ya kuendeleza mafundi stadi katika sekta ya ujenzi. Aidha, Serikali isitishe utaratibu wa kubadilisha Vyuo vya Ufundi vya kati kuwa Vyuo Vikuu

kwani kwa kufanya hivyo tunaondoa uwiano unaotakiwa baina ya Wahandisi na Mafundi Sanifu.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2012/2013, Wizara ya Ujenzi inaomba iidhinishiwe jumla ya shilingi 1,023,033,626,000/=. Kati ya hizo shilingi 329,085,354,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 693,948,272,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na kupitia kifungu kwa kifungu na kuipitisha na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu kuyajadili na kuyapitisha maombi hayo ya fedha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mheshimiwa Daktari John P. Magufuli, Waziri wa Ujenzi; Mhe. *Engineer* Gerson H. Lwenge, Naibu Waziri wa Ujenzi; Balozi Herbert E. Mrango, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa wa kupitia na kuchambua Mipango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. Kwa nafasi ya kipekee napenda kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mjumbe; Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mjumbe; Mheshimiwa Herbet James Mtangi, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mjumbe; Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mjumbe; Mheshimiwa Inocent Edward Kalogeresi, Mjumbe; Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikira, Mjumbe; Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mjumbe na Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mjumbe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mjumbe; Mheshimiwa *Engineer* Ramo Matala Makani, Mjumbe; Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mjumbe; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mjumbe; Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mjumbe; Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu Mjumbe; Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu,

Mjumbe; Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mjumbe; Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mjumbe; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Juma Athman. Kapuya, Mjumbe na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Daktari Thomas Didimu Kashillilah, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi pamoja na Katibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kuihudumia Kamati ya Miundombinu kwa ufanisi mkubwa na kuandaa taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi. Namwomba Mheshimiwa Pauline Gekul. Hii Wizara sijui ni ya akinamama!

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. SAID A. ARFI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Wizara ya Ujenzi

kuhusu mapitio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mdogo naomba hotuba hii iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuendelea kunipigania siku zote na sasa nimesimama hapa ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa Fedha 2012/2013. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, kipekee, nitoe shukrani kwa familia yangu kwa kuniwezesha kutimiza majukumu yangu ya Kibunge na Kichama. Aidha, pongezi ziende kwa viongozi wenzangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kazi kubwa wanayoifanya bila kuchoka katika kukidhi matarajio ya Watanzania kuwa CHADEMA ndio chama mbadala kuongoza nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Kiongozi wa Upinzani, Bungeni kwa kutupa dhamana ya kuisimamia Wizara hii yenye changamoto nyingi mimi pamoja na Waziri kivuli Mheshimiwa Said Arfi. Tunapenda kumhakikishia kuwa tutatekeleza wajibu wetu kwa uwezo na nguvu zetu

zote kama yalivyo matarajio ya Watanzania kwa Chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini kwa umuhimu, niipongeze Kamati ya Miundombinu pamoja na Mwenyekiti wake kwa ushirikiano na kazi kubwa tunayoifanya katika kuhakikisha thamani halisi ya fedha za walipa kodi inaonekana katika miradi ya maendeleo kwenye sekta ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na ubora wa barabara; kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi kwa mwaka 2011, kasi ya ujenzi wa mtandao wa barabara ilipungua kutoka asilimia 10.2 mwaka 2010 hadi asilimia 9.0 na inaendelea kuainisha kuwa mwaka 2011, jumla ya kilomita 29,369 zilifanyiwa tathimini, kati ya hizo kilomita 5,727 sawa na asilimia 59.1 za barabara kuu zilikuwa katika hali nzuri, ikilinganishwa na kilomita 8,364.73 sawa na asilimia 65 mwaka 2010. Hii ina maana kuwa ubora wa barabara umepungua kwa asilimia 5.9 mwaka 2011. Aidha, kilomita 862, sawa na asilimia 9.0 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilomita 842.93 sawa na asilimia 7.0 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ni kwa nini hali hii ilitokea na hasa ikizingatiwa kuwa bajeti ya Wizara ya Ujenzi iliongezeka kwa zaidi ya asilimia mia moja ukilinganisha na mwaka 2010, wakati huo huo ubora wa barabara zetu kupungua? Kuna uhusiano gani kati ya fedha kuongezeka na barabara kupungua ubora?

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo taarifa hiyo inavyojionesha ni ukweli ulio wazi kuwa barabara nyingi zimekuwa zikijengwa chini ya kiwango na mfano mzuri ni barabara ya Misigiri-Shelui (Iramba Magharibi). Itakumbukwa kuwa Mbunge wa Iramba Magharibi wa wakati huo Mheshimiwa Juma Kilimba aliitahadharisha Serikali kuhusiana na ujenzi wa barabara hiyo kuwa uko chini ya kiwango, kwa kuwa, alikuwa mfuatiliaji wa masuala ya msingi, lakini Serikali haikuchukua hatua yoyote kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Serikali kutochukua hatua wakati huo taarifa zilizopo ni kuwa barabara hiyo inapaswa kujengwa upya na sio kufanyiwa ukarabati. Hii ni hasara kubwa sana kwa Serikali kwani kwa kipindi cha chini ya miaka mitatu tunakwenda kujenga barabara ambayo tayari ilishajengwa badala ya kutumia fedha hizo kujenga barabara mpya.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani, inataka kupata majibu ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kwa Mkandarasi pamoja na mshauri mwelekezi ambao walihusika na ujenzi huu. Pia tunawataka Wabunge wawe wanafuatilia miradi ya barabara ambayo inajengwa kwenye Majimbo yao ili kuliepusha Taifa na hasara kubwa kama hii na hasa kufuatilia viwango. Aidha, Serikali ichukue hatua kila taarifa inapotolewa ili kuepuka hali hii isijirudie tena.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyamyorwa-Buzirayombo (kilomita120) nayo ilijengwa chini ya kiwango kilichopelekea barabara hii kukataliwa

kupokelewa na kutakiwa Mkandarasi kurudia kufanya marekebisho kwa viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua hatua iliyofikiwa hadi sasa kwani ni takriban miaka minne imepita. Pia tunataka kujua ni hatua gani iliyofikiwa katika ujenzi wa barabara ya Kilwa (Dar es Salaam) ambayo ilijengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, katika kupitia kitabu cha pili cha mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka kwa kipindi kinachoishia mwezi Juni, 2012, inaonesha fedha za maendeleo zilizotolewa na Serikali hadi mwezi wa April 2012. Kati ya miradi 61 iliyotengewa fedha, miradi 26 haikupelekewa fedha kabisa pamoja na kwamba Bunge lilipitisha fedha kwa miradi hiyo. (Kiambatisho: katika Randama ya mapitio ya utekelezaji na mpango wa bajeti 2011/2012).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwanini miradi hiyo haikutengewa fedha kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya barabara; Kambi ya Upinzani inapenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwa mikataba mingi ya ujenzi wa barabara iliwekwa mwaka 2009/2010 tukielekea kwenye Uchaguzi Mkuu na muda wa kukamilika miradi hiyo si zaidi ya miezi 36. Mikataba yote iliyosainiwa mwaka 2009 inapaswa kukamilika mwaka 2012 na ile ya mwaka 2010 inapaswa

kukamilika mwaka 2013 na takriban miradi yote ya ujenzi wa barabara hadi sasa imeshatekelezwa chini ya asilimia hamsini.

Mheshimiwa Spika, kwa uchache miradi inayotakiwa kukamilika mwaka huu ni pamoja na barabara ya Sumbawanga hadi Kibaoni, Sumbawanga hadi Matai na Kasanga. Pia barabara ya Handeni–Mkata, Tunduma-Sumbawanga na nyinginezo nyingi hazitakuwa zimekamilika mwaka huu kwa mujibu wa mkataba. Matokeo yake barabara hizi zitachukua muda mrefu kukamilika na kuligharimu Taifa fedha nyingi zaidi kwa malengo ya mafanikio na kisiasa na gharama hizo zitabebwa na Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyosainiwa mwaka 2010 na kutarajiwa kukamilika mwaka 2013, ni pamoja na: barabara ya Manyoni - Itigi- Chaya yenye urefu wa kilomita 89.30; tarehe ya kuanza kazi rasmi ilikuwa 20 Disemba 2010 na tarehe ya kumaliza kazi ni 20 Disemba 2013. Mkandarasi wa mradi huu ni *Sinohydro Coorporation Limited*, China. Mpaka mwezi May 2012 hali ya utekelezaji wa Mradi huu ilikuwa imefikia kuwa, kusafisha eneo la ujenzi 46%, kujenga tuta la barabara 13.7%, kujenga tabaka la sementi 0%, kujenga tabaka la kokoto 0%, kujenga tabaka la lami nyepesi 0%.

Mheshimiwa Spika, hali ni hiyo hiyo kwa barabara ya Tabora–Nyahua yenye urefu wa kilomita 85.0, barabara ya Tabora–Urambo yenye kilomita 94.0, Tabora-Nzega yenye kilomita 116. Changamoto kubwa ni kuwa kila mradi wa ujenzi Wakandarasi wanaidai Serikali fedha na Serikali haijaweza kulipa na

hivyo katika miradi hiyo wakandarasi wamepunguza kasi na kutoa tangazo la dhamira ya kusimamisha ujenzi katika baadhi ya barabara mwezi Mei, 2012 kwa kutokulipwa madai yao kwa wakati.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata taarifa ni kwa nini Wakandarasi hawa hawajalipwa kwa wakati ili waweze kutekeleza miradi hii kama ilivyokusudiwa wakati Fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge kiasi cha shilingi 14,415,640,000 (*Volume Four (4) Development*) mwaka jana kwa ajili ya mradi huu zilikwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Geita-Sengerema umekamilika kwa asilimia mia moja tangu Februari 2010, lakini Mkandarasi bado anadai shilingi 273,702,658.35 ambayo inasababisha matatizo mengi ya kimkataba ikiwemo kuongezeka kwa riba ya ucheleweshaji malipo na kuongeza mzigo wa deni. Hivyo hivyo, barabara ya Sengerema–Usagara kilomita 40 ambayo imekamilika na kupokelewa Serikalini mwaka 2010; iliyokuwa inajengwa na Mkandarasi *Sinohydro Cooperation Limited* ambaye anadai shilingi 5,728,347,080.97 na Mhandishi Mshauri anadai shilingi 637,866,136.29 na hivyo kulifanya deni kuwa shilingi 6,366,213,217.26. Kutokana na deni hili linasababisha riba ya deni kuendelea kuongezeka kutokana na masharti ya mkataba. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ni lini deni hili litalipwa na je, fedha za kulipia deni hili zipo kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyaka-Bugene kilomita 59.1 mkataba ulisainiwa mwaka 2010 hadi sasa asilimia 57 ya mkataba imepita na kazi za ujenzi zinasuasua na hivyo kufanya hadi sasa utekelezaji kuwa ni asilimia 20 tu, kutokana na tatizo la malipo. Aidha, Kambi ya Upinzani inataka kujua hatua madhubuti zilizochukuliwa ili kukamilisha mradi huu sambamba na kipande cha Ndundu-Somanga kilomita 60 kwenye barabara itokayo Dar es Salaam kwenda Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Ushirombo-Lusaunga kilomita 110, kazi zimesimama tangu tarehe 23 Agosti, 2011 hadi sasa kutokana na madeni. Kama tulivyotangulia kusema awali miradi hii ilikuwa na lengo la kisiasa kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2010, kuliko uwezo halisi wa Serikali kuhimili kulipia huduma kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kagoma-Lusaunga kilomita 154 ni miongoni pia ya mikataba ya ujenzi iliyosainiwa mwaka 2009; pamoja na kuongezewa muda zaidi ya miezi 36 ya awali inatakiwa ikamilike Januari 2013. Lakini Mkandarasi ametoa taarifa ya kupunguza kasi ya ujenzi kwa sababu anadai jumla ya shilingi bilioni 12.56 na dola za Kimarekani milioni 14.56. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu mkakati wa Wizara wa kulipa deni hili kwa kazi ambayo tayari imefanyika ili mradi ukamilike kwa wakati na hatua zilizochukuliwa za kuhamisha nguzo za umeme, simu na mabomba ya maji katika Mji wa Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa barabara na utayarishaji wa vitabu vya zabuni barabara ya Kidahwe-Kasulu-Kibondo-Nyakanazi (kilomita 310) uliahirishwa kutokana na tatizo la fedha. Kambi ya Upinzani inataka kujua hatua iliyofikiwa hadi sasa, kwani barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa na kiungo kwenda Kanda ya Ziwa na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Miradi Maalum ya Barabara. Bajeti ya serikali ya mwaka jana ilionesha kuwa zilikuwa zimetengwa fedha kiasi cha shilingi 348,075,000,000 kwa ajili ya kitu kinachoitwa *Special road construction Projects* (fungu 4168), na katika hotuba ya Kambi ya Upinzani tulihoji hapa Bungeni kuhusiana na fedha hizi .

Mheshimiwa Spika, naomba kununukuu: "Mheshimiwa Spika, kitabu cha Miradi ya Maendeleo (sehemu-A juzuhu iv) katika fungu 98, kasma 4168 utaona kuwa kuna mradi unaitwa Miradi ya ujenzi wa barabara maalum (*special road construction projects)* na fungu hili limetengewa kiasi kikubwa kuliko mradi mwingine wowote wa ujenzi wa barabara katika mwaka huu wa fedha kwani zipo jumla ya shilingi 348,075,000,000 na hizi zote ni fedha za ndani.

Kwa hakika hizi ni fedha nyingi sana na hasa ikizingatiwa kuwa kitabu hicho kimeonesha miradi yote ya ujenzi wa barabara ambayo itatekelezwa katika mwaka huu wa fedha, ila hii miradi maalum haijaoneshwa ni miradi ya barabara gani na zitajengwa wapi. Kasma hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011 haikuwa imetengewa kiasi

chochote cha fedha na ndio maana imetustua kuona mwaka huu fedha nyingi kiasi hicho kinatengwa kwa miradi isiyojulikana kuwa itajengwa wapi.

Kambi ya Upinzani tunataka kupata maelezo ya kina ni miradi gani hii ambayo haiwezi kuandikwa na inatengewa fedha nyingi kiasi hicho? Kwani hii italiwezesha Bunge kuweza kupitisha bajeti inayoifahamu, na kuisimamia serikali kwa kuweza kufuatilia utekelezaji wa miradi hii. Pili, fedha hizi zipangwe kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za kimkakati ambazo Kambi ya Upinzani imependekeza ili ziweze kuunganisha mikoa husika na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali yalikuwa kama ifuatavyo: "Fedha hizi ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi tunayotakiwa tuchangie fedha ili tupewe mikopo. Sehemu kubwa ya miradi yetu ya barabara inatekelezwa kwa fedha za mikopo." Mwisho wa kunukuu. (Chanzo: majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa na Wizara ya Ujenzi).

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2012/2013, hakuna fedha yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya kasma hii na hili linaendelea kuzua maswali na hasa kutokana na majibu yaliyotolewa mwaka jana kuhusiana na fedha hizi. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kuhusiana na mambo yafuatayo:-

(a) Je, mwaka huu wa fedha hatutegemei kukopa fedha kwa ajili ya miradi ya barabara na hivyo kulazimika kuchangia?

(b) Fedha zilizokuwa zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 zilitumika kugharamia mikopo ipi na kwa ajili ya miradi ipi ya barabara?

(c) Fedha hizi ziliwekwa kwenye akaunti ipi kwani kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011, inaonesha kuwa *TANROADS* walikuwa hawajafungua akaunti maalum kama ambavyo sheria inataka kwa ajili ya *Counterpart funds.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa mapendekezo na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe kwanza inalipa madeni yote yaliyopo ili kuwezesha miradi ya ujenzi wa barabara ukamilike kwa haraka;

(ii) Serikali ikamilishe utaratibu wa kupata Wakandarasi katika vipande ambavyo havijaanza kujengwa katika barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora na Tabora-Urambo-Kigoma na kukamilisha kipande cha Ndundu-Somanga, barabara ya Dar-Lindi hadi Mtwara na Kibaoni–Mpanda, barabara ya Sumbawanga–Mpanda, ili barabara hizi zikamilike kwa pamoja na kukamilisha miradi husika;

(iii) Serikali itoe kipaumbele kwa barabara ambazo zinatumika kuhamisha shehena kubwa ya

mazao ya chakula kutoka maeneo ya uzalishaji, kama vile barabara ya Mpanda-Tabora na nyinginezo;

(iv) Kuongeza kasi katika kuhakikisha upanuzi wa barabara ya Dar es Salaam-Chalinze ili kupunguza msongamano na ajali katika barabara hiyo;

(v) Itenge fedha za kutosha kwa ajili ya barabara kuu ya kutoka Iringa-Dodoma-Kondoa-Babati hadi Arusha kwani barabara hii ndiyo inaunganisha kusini na kaskazini mwa nchi yetu; na

(vi) Kutengeneza mpango mkakati na mpango wa utekelezaji katika Majiji ya Mwanza, Arusha na Mbeya ili kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari kama ilivyo Dar es Salaam leo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sakata la bomoa bomoa nchini; mwanzoni mwa mwaka uliopita 2011 karibu nchi nzima liliendeshwa zoezi la kuweka alama ya *X* nyumba na mali zote zilizopo katika hifadhi ya barabara ili kupisha nafasi hizo kuwa wazi au kupisha upanuzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili limezua malalamiko mengi sana miongoni mwa wananchi walioathirika na hali hiyo na jambo hili likamfanya Mheshimiwaa Waziri Mkuu kutoa kauli kama ilivyonukuliwa na vyombo vya habari tarehe 6/3/2011, naomba kununukuu: “Rais aliona sekta ya barabara panalegalega na kumrudisha Daktari Magufuli kwenye Wizara hii, lakini ameanza kwa spidi kubwa, hivyo tumemwagiza asimamishe

operesheni hii hadi suala hili litakapojadiliwa na Baraza la Mawaziri na kuongeza kuwa kasi hiyo imeitisha."

Mheshimiwa Spika, kutekeleza agizo hilo katika Jiji la Dar es Salaam juu ya bomoabomoa katika barabara ya Morogoro Waziri Mkuu aliagiza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kufanya tathmini ya zoezi hilo kabla halijaanza kutekelezwa na kutoa taarifa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kufanya tathmini ya kina kabla ya kuanza kutekeleza zoezi hilo kwa sababu lina mkanganyiko mkubwa sana ukizingatia kuwa wapo wananchi waliokuwa wanaishi katika baadhi ya maeneo hata kabla ya Sheria ya Hifadhi ya Barabara ya Mwaka 2007 haijatungwa. Pia Halmashauri nyingi nchini pamoja na Wizara ya Ardhi wametoa leseni za makazi, ramani, vibali na hati za ardhi katika maeneo ambayo yapo kwenye hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kuboresha miundombinu ya barabara nchini, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kufanya maamuzi ya pamoja kama Serikali (*collective responsibility*) kuanzia Serikali Kuu mpaka Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa zoezi la bomoa bomoa na sio kutumia sababu moja tu ya utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Barabara ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wananchi; katika miradi mingi ya ujenzi wa barabara kumejitokeza ulipuaji wa baruti miamba karibu na makazi ya

wananchi na athari zake hujitokeza baada ya kazi kumalizika jambo ambalo huwapa hasara wananchi na usumbufu, wakati wa kudai fidia zao huleta kero kwa wananchi. Maeneo mengi nchini kama barabara ya Minjingu-Babati-Dareda, Nyahua hadi Tabora, Kagoma-Lusaunga hadi Biharamulo wameathirika na hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili kwa kiasi kikubwa linatokana na ukweli kwamba Wahandisi Washauri wengi hawafanyi upembuzi yakinifu kwa madhara ambayo yanaweza kutokea katika zoezi la ulipuaji wa miamba. Tukumbuke kuwa tatizo hili la fidia ya ulipuaji wa miamba imekuwa ni adha kubwa kwa wananchi wa maeneo husika. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya upembuzi yakinifu kwa maeneo tajwa yaliyoathirika na ulipuaji na hivyo kutoa fidia stahiki kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, masuala ya utoaji wa fidia hapa nchini kwa muda mrefu sasa yamekuwa hayazingatii Katiba ya Nchi, Sera, Sheria, Kanuni za ardhi na maslahi ya wamiliki wa ardhi husika. Hii ni kutokana na manung'uniko ya wananchi wanaohamishwa katika maeneo yao kulipwa viwango vidogo vya fedha kama fidia. Vilio vya wananchi vimekuwa vikisikika katika vyombo mbalimbali vya habari na hata kesi mbalimbali kufunguliwa katika Mahakama za Ardhi nchini kuashiria wananchi kutoridhika na michakato ya fidia inayofanyika katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, fidia ya ardhi ni gharama ambazo mmiliki halali wa ardhi hulipwa kwa kuzingatia haki zake juu ya ardhi husika, yaani; thamani ya ardhi, maendelezo katika ardhi husika na maslahi mengine juu ya ardhi kwa mmiliki. Endapo mwananchi ambaye eneo lake linachukuliwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara, ni haki yake ya msingi kushiriki katika hatua zote ikiwa ni pamoja na kupewa fidia kwa mujibu wa kifungu cha 3(g) cha Sheria za Ardhi Na. 4 na Na. 5 za 1999.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa utaratibu huu wa kuwashirikisha wananchi katika hatua zote muhimu kwa ajili ya kuweza kupata fidia kwa mujibu wa sheria kama ambavyo tumeelezea hapo juu haufuatwi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na taarifa kwamba Serikali imetenga kiasi cha zaidi ya Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya shughuli ya kuwalipa fidia wananchi ambao nyumba zao zitabomolewa kwa ajili ya kupisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi na upanuzi wa barabara kati ya Tandika Devis Kona Manispaa ya Temeke hadi Jet-Kona Manispaa ya Ilala. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge juu ya matumizi halisi ya fedha tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na malalamiko ya wananchi wa maeneo mbalimbali kama vile Vijiji vya Mazingara, Mkata, Vibaoni, Kilole Wilaya ya Bagamoyo, Wilaya ya Handeni, Wilaya ya Ruangwa na maeneo mbalimbali katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Tabora, Rukwa na maeneo mengine ambayo miradi

ya ujenzi wa barabara inatekelezwa hapa nchini kuhusiana na fidia ama kuwa ndogo, kutokulipwa kwa wakati au kutokulipwa kabisa na kuwafanya Watanzania hawa kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria na taratibu ni kuwa msingi wa kukadiria thamani ya ardhi yoyote na uboreshaji kwa ajili ya ulipaji wa fidia, vigezo vinavyotumika ni pamoja na thamani ya ardhi hiyo katika soko, maendelezo yanayofanyika katika ardhi kama vile majengo na mazao yanatakiwa kulipwa kwa mmiliki wa ardhi kama gharama halali na halisi alizotumia kufanya maendelezo katika ardhi husika, posho ya usumbufu, gharama za nauli pamoja na riba ya miezi kumi na mbili kulingana na viwango vya riba vya kibenki. Riba kwenye fidia yoyote italipwa na Serikali Kuu au Mamlaka ya Serikali za Mitaa pale tu ambapo malipo ya fidia hayakulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba miliki ya mtu inapoingiliwa, mabadiliko ya kimaisha lazima yatatokea. Mfano, ni wahanga wengi ambao wamekuwa wakiishi katika maeneo yao kwa muda mrefu. Kwa sehemu kubwa, wanapohamishwa pasipo kupatiwa ardhi mbadala, matokeo yake ni kuwafanya waishi maisha ya kutangatanga katika nchi yao. Ni haki yao kupatiwa ardhi katika maeneo mengine na ardhi hiyo iwe imepimwa ili kuongeza uhakika wa ardhi husika na pasipo kufikwa na bomoa bomoa nyingine au kuhamishwa, jambo ambalo limekuwa halifanyiki hapa nchini na hivyo kuwafanya wananchi ambao wanakumbwa na bomoa bomoa kujikuta katika

wakati mgumu sana wa kuweza kuendeleza maisha yao.

Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali iwe na utaratibu wa kuwalipa wananchi fidia timilifu na kwa wakati na wawe wanalipwa kabla ya bomoa bomoa kufanyika kwani kitendo cha kubomoa kabla ya fidia kinawafanya wananchi husika kuathirika sana na hivyo kushindwa kuendesha maisha yao. Kambi ya Upinzani inapendekeza hatua zifuatazo ziweze kuchukuliwa na Serikali ili kuondokana na hali hii:-

(a) Wizara ya Ardhi kurejelea ramani (*Master plan*) ya Jiji la Dar es Salaam na nchini kote kufahamu bayana barabara za Wilaya na Mikoa na mikakati ya mpango wa uendelezaji wa barabara na pia kuwafahamisha wananchi kuhusiana na mipaka hiyo;

(b) Serikali iwachukulie hatua watendaji wanaokiuka utaratibu wa matumizi ya hifadhi ya barabara na kusababisha usumbufu kwa wananchi. Hali halisi inaonesha kwamba, wenye taaluma hii ndio wamekuwa wakipotosha Watanzania kwa kuruhusu umiliki wa ardhi kwa matumizi mengine tofauti na yaliyopangwa mathalani ardhi kwa ajili ya barabara. Pia, wamekuwa wakipima na kugawa viwanja mijini kiholela bila kujali kama kuna umuhimu wa kuwa na maeneo ya barabara, shule, zahanati, soko, nyumba za ibada, viwanja vya michezo na matumizi mengine;

(c) Serikali iwajibike na sio kufumbia macho uvunjwaji wa utaratibu uliowekwa katika hifadhi za barabara na matumizi mengine kwa manufaa ya

wananchi. Mfano hai ni katika miji ambayo ina hadhi ya Majiji na Manispaa kama Dar es Salaam, Mwanza, Iringa, Mbeya na Arusha. Mipango mikuu ya Majiji na Manispaa hizi hazifuatwi kabisa;

(d) Maafisa Mipango Miji wakaguliwe utendaji wao unaotakiwa kufuata maadili ya kazi. Hii ni kutokana na kuwa ni maafisa wanaolalamikiwa sana na wananchi kwa tabia yao ya kudai na kupokea rushwa. Kinachotakiwa ni kuangalia Mipango Mikuu ya Miji na kuangalia hali halisi ya ujenzi; na

(e) Pale inapolazimika kuvunja pande zote mbili za barabara basi walipwe fidia wote na si upande mmoja wa barabara na mwingine kutokulipwa ili kuondoa malalamiko ya wananchi na kuwatendea haki sawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu miradi inayofadhiliwa na wafadhili ya mwaka 2010/2011 inaonesha kuwa kiasi cha dola za Kimarekani 73,520.38 kililipwa kama kodi kwa *Airtel Tanzania Limited* kwa ajili ya mwezi Aprili ambazo ni sawa na sh. 110,280,000. Fedha hizi zilitumika kutoka kwenye fungu la fedha za miradi ambayo inafanywa kwa ubia baina ya Serikali na wafadhili kinyume na mikataba na hati ya makubaliano. Kambi ya Upinzani inahitaji kupata maelezo ya ukiukwaji uliofanywa; pia kodi hiyo ni kwa ajili ya mwezi Aprili tu au kwa ajili ya mwaka mzima?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye randama ya Wizara ya Ujenzi, fungu 6383, utaona kuwa Wakala wa Barabara kwa mwaka huu wa fedha wametenga kiasi cha shilingi milioni 120.5 kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi wa Makao Makuu. Kambi ya Upinzani inaona kiasi kilichotengwa ni kidogo sana bila ya kuangalia athari ya kuendelea kupangisha ofisi za Wakala katika jengo la *Airtel.* Aidha, tunashauri Wakala wa Barabara kujenga ofisi zao wenyewe katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka maelezo ni kwa nini Wakala ukapangishe jengo la ofisi kutoka miongoni mwa wateja ambao anapaswa kuwahudumia na kuwasimamia (hasa kwenye suala la kuweka mabango ya matangazo kandokando mwa barabara). Makampuni mengine ya simu yatatendewa haki? Je, *Airtel* akiweka bango vibaya Wakala utaweza kumwajibisha ama utakuwa na hofu ya kuondolewa kwenye jengo hilo?

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa, Wakala wa Barabara alitumia kiasi cha shilingi 49,581,000 kwa ajili ya ukarabati wa dharura kwenye eneo la Same –Himo na fedha hizi kiasi cha shilingi 46,958,975 zililipwa kutoka Makao Makuu ya Wakala na kiasi cha shilingi 2,471,525 kililipwa na *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro bila fedha hizo kuidhinishwa na Benki ya Dunia. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu je, ni utaratibu gani unatumika katika kukarabati barabara? Je, fedha hulipwa na Wakala moja kwa moja au hutumwa kwa Wakala kwenye mkoa husika?

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa Wakala ulilipa malipo ya awali ya kiasi cha dola za Kimarekani 7,495,658.50 ambazo ni sawa na shilingi 10,068,269,000 kwa kiwango cha shilingi 1,550 kwa dola moja, kabla ya mkataba *No.TRD/HQ/1064/2010/11* kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Arusha–Minjingu (kilomita 98) kabla mkataba wa ujenzi kuidhinishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma kifungu cha 55(6) No. 21 ya mwaka 2004.

Kambi ya Upinzani tunataka kupata maelezo ya kina juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliohusika kuvunja sheria na kupuuza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo ipo kikatiba na kisheria, kwani kama hatua hazitachukuliwa jambo hili linaweza kuisababishia Serikali hasara kutokana na mikataba kutokidhi viwango vya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali au Wakala kuangalia upungufu wa wataalam Wahandisi na Mafundi Mchundo katika ofisi zao nyingi mikoani na kuajiri wataalam wa kutosha ili kuwezesha usimamizi mzuri wa miradi na kazi nyingine za kitaalam zifanyike kwa ufanisi. Kadhalika, tunaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi kuangalia uwezekano wa kuanzisha Wakala wa Ujenzi wa Barabara Vijiji (*Tanzania Rural Roads Agency*) na kuajiri wataalam wa kutosha kwa usimamizi bora wa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Mfuko wa Barabara; mwaka 2011 Mfuko wa Barabara ulikusanya mapato ya shilingi bilioni 401.935 ikilinganishwa na shilingi bilioni 278.231 zilizokusanywa mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 44.5; ongezeko hilo linatokana na kupungua kwa uchakachuaji wa mafuta kutokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta ya taa ambalo limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilianzishwa mwaka 2000 ikiwa ni moja ya mikakati ya kuboresha Sekta ya barabara hususani katika kukusanya, kutoa na kuratibu matumizi ya fedha za matengenezo ya barabara. Sheria ya Ushuru wa Barabara (Marekebisho Na. 2) ya mwaka 1998, iliyounda Bodi ya Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Barabara, ilifanyiwa marekebisho mwaka 2006 na kuitwa *Road and Fuel Tolls Act, Cap 220, Revised Edition 2006.* Hadi sasa vyanzo vya mapato kwa mujibu wa sheria ni kama ifuatavyo: ushuru wa barabara unaotozwa katika mafuta ya petroli na dizeli, ushuru wa magari ya kigeni mipakani na tozo ya magari yaliyozidisha uzito.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Waziri wa Ujenzi ya mwaka 2011/2012 katika ukurasa wa 97 kuhusu Bodi ya Barabara alisema, nanukuu: “Bodi itaanzisha utaratibu wa kuwatumia wataalamu washauri waliopo maeneo husika *(local consultants)* kwa ajili ya kukagua ubora wa kazi *(value for money) wakati miradi ya* matengenezo inapoendelea.” Kambi ya Upinzani

inahoji kama ahadi hii ya Serikali imetekelezwa kwa kiwango gani ikiwa sote tumeshuhudia barabara zikiendelea kujengwa bila ubora kwa kuzingatia thamani ya pesa na mifano ya barabara hizi ni mingi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la magari kuzidisha mizigo halitaweza kutatuliwa kwa kutoza faini magari yanayozidisha viwango vya mizigo. Serikali kuendelea kutegemea mapato kutokana na uvunjifu wa sheria ni kuruhusu uvunjaji wa sheria kwa makusudi. Pia kuruhusu uharibifu wa barabara zinazojengwa kwa kodi za Watanzania ni utaratibu wa ajabu wa kutunza barabara.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuendelea kutoa adhabu za tozo au faini kwa wanaozidisha uzito hakutaweza kutatua tatizo hili. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kubadili mfumo wa kuongeza mapato ya Mfuko wa Barabara kwa kutegemea faini na tozo hizi na kuandaa sheria maalum ya kudhibiti uzidishaji wa mizigo kwa magari na iweke adhabu kali zaidi ili kuweza kuzilinda barabara zetu na madaraja ambavyo vyote hivi tunavijenga kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Serikali ni kuwa hadi Aprili, 2011 magari yapatayo 732,307 yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo magari 168,041 yalikuwa yamezidisha uzito ambapo ni sawa na asilimia 22.95 ya magari yote yaliyopimwa. Fedha zilizokusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana ilikuwa shilingi milioni 1,094.718.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kiwango cha fedha zilizotozwa kama faini na tozo mbalimbali na ukaangalia uharibifu wa barabara uliofanywa na magari hayo na kisha ukawianisha na gharama inayohitajika kwa ajili ya kujenga kilomita moja ya lami, ni wazi kuwa kuendelea na utaratibu wa kutoza faini hakulisaidii Taifa bali ni kuendelea kuharibu barabara zetu ambazo tunazijenga kwa gharama kubwa sana. Kwa mfano, gari iliyokuwa inatoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza ikiwa na mzigo uliozidi ni hakika kuwa kiwango cha uharibifu wa barabara na madaraja yetu kitakachotokea hakiendani na faini itakayotozwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, tunaendelea kushauri kuwa pamoja na faini na tozo hizi, pawepo na utaratibu wa kisheria kwa zile kampuni ambazo zitabainika kuwa wanaongoza kwa kuongeza uzito wa mizigo kwenye magari yao wawe wanafungiwa kupita barabarani kwa vipindi kama vile kwa miezi mitatu, sita au hata mwaka mmoja ili liwe fundisho na itasaidia kuzinusuru barabara zetu na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu na ambao kulipa faini sio tatizo kwao kwani fedha wanazo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ukusanyaji wa mapato ya Mfuko wa Barabara kwenye ushuru wa barabara katika mafuta ya petroli na dizeli chini ya mkakati wa kudhibiti uchakachuaji wa mafuta ya petroli na dizeli ulivyoainishwa na Waziri katika hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012 ukurasa 97, nanukuu: “Kudhibiti

uchakachuaji wa mafuta kwa kuongeza kodi kwenye mafuta ya taa.” Hatua zilizochukuliwa zimeendelea kuwaumiza wananchi na hasa waishio vijijini. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kupunguza kodi hii kwenye mafuta ya taa ili wananchi waweze kupunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi ni kuwa ajali za barabarani zimekuwa zikiongezeka kwa kasi tangu Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani mwaka 2005 na hii inatokana na takwimu zinazoonesha kuwa mwaka 2005, ajali za barabarani zilikuwa 16,388, mwaka 2006 ajali 17,039, mwaka 2007 ajali 17,753, mwaka 2008 ajali 20,615, mwaka 2009 ajali 22,739, mwaka 2010 ajali 24,665 na mwaka 2011 ajali 23,986.

Mheshimiwa Spika, ajali hizi ni dhahiri kuwa zimelisababishia Taifa hasara kubwa sana kama vile kupoteza nguvu kazi kutokana na vifo vya ajali hizi, watu kupata ulemavu wa kudumu na hivyo kuwafanya wengine kuwa tegemezi kutokana na ulemavu walioupata na kadhalika. Miongoni mwa vyanzo vya ajali hizi ni pamoja na barabara kujengwa chini ya kiwango na nyingine kuwa na utelezi kama mvua zinanyesha na hivyo kuyafanya magari kushindwa kutulia barabarani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupitishwa kwa Sera ya Usalama Barabarani Januari, 2008 lakini jambo la kushangaza ni kuwa mpaka sasa Wizara inaendelea na maandalizi ya mikakati ya utekelezaji wa sera na bado sheria ipo kwenye hatua ya rasimu. Kambi ya

Upinzani inataka kujua ni lini Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani utawasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni mikakati gani ambayo Wizara na Serikali imechukua ili kukabiliana na Wakandarasi hawa wanaojenga barabara chini ya kiwango na hatimaye kuchangia ongezeko la ajali za barabarani? Kwani kuna taarifa kuwa baadhi yao ndio hao hao wanaopewa kandarasi za kujenga barabara nyingine nchini hata baada ya kubainika kuwa baadhi ya maeneo wamejenga barabara kwa kiwango cha chini. Kadhalika Kambi ya Upinzani inataka kujua ni lini Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani utawasilishwa Bungeni?

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo Tanzania ulianzishwa mwezi Mei mwaka 2002 chini ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1997 ya Wakala za Serikali. Lengo la kuanzisha Wakala huu ni kuwezesha kuwa na nyumba bora zaidi za kuishi watumishi wa Serikali wakiwa kazini na baada ya kustaafu kwa kujenga nyumba na kuwakopesha; kujenga majengo ya Serikali kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na kuyatunza na pia kutoa huduma za ushauri wa kitalaam kuhusiana na majengo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo mbali na dhana nzuri ya uanzishwaji wake, lakini Wakala umekuwa haupatiwi fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake. Mfano mzuri ni kwamba, mwaka wa fedha uliopita zilitengwa shilingi bilioni 5.3, lakini fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 2.8. Mwaka huu wa fedha

Wakala wa Majengo wametengewa shilingi bilioni 5.98. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa nini fedha zinazotengwa kwa Wakala huyu hazitoshi kutimiza majukumu yake au ni mtindo ule ule wa taasisi kuwepo tu lakini hazitoi tija yoyote kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kama kweli Wakala wa Majengo alitakiwa kujenga nyumba za watumishi wa Serikali, basi ni dhahiri kuwa Wakala huyu anashindwa kuelewa vizuri majukumu yake. Tatizo sugu la ukosefu wa nyumba za Walimu, Madaktari na watumishi wengine, majengo ya mashule na majengo kadhaa ya Serikali ambayo ujenzi wake ndilo jukumu lake la msingi wanakiacha badala yake ujenzi wa majengo hayo unajengwa na Wakandarasi binafsi jambo linalopelekea majengo hayo kujengwa kwa ubora wa viwango vya chini kabisa. Hii ni hasara kwa Serikali na kwa wananchi ambao wanachangia katika ujenzi wa shule na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo lengo lake halikuwa ni kufanya biashara, lakini kwa sasa Wakala umejikita katika kufanya biashara zaidi kuliko kujenga nyumba za watumishi wa umma. Shirika la Nyumba la Taifa nalo lina majukumu ya ujenzi wa nyumba za kuishi, majengo kwa ajili ya kuuza kama itakavyoamuliwa na Bodi, kujenga majengo kama sehemu ya mradi ulioidhinishwa na Bodi na pia kutoa na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya ujenzi kwa kuanzisha vifaa au njia nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia majukumu hayo ni dhahiri taasisi hizo zote mbili inakuwa ni kama wanashindana kwani wote wanajenga nyumba na wote wanauza nyumba. Hizi zote ni taasisi za Serikali ni kwa nini zisiwe taasisi moja? Aidha, Serikali ilibinafsisha viwanda karibu vyote vilivyokuwa vinatengeneza mali ghafi za ujenzi kama vile matofali, vigae na mabati. Sasa kama wanaamini sekta binafsi inaweza kufanya kazi ambazo ni majukumu ya Serikali na kwa kuwa taasisi hizo kwa sasa zinafanya biashara zaidi ni bora kazi za kujenga na kuuza nyumba zirudi kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za hali ya uchumi wa Taifa inaeleza kuwa Wakala uliendelea kusimamia miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za viongozi ambazo ni za Waheshimiwa Majaji katika Mikoa ya Ruvuma, Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Tabora, Mwanza, Mbeya na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo inaendelea kueleza kuwa Wakala uliendelea na ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Wilaya za Bariadi, Urambo na Siha pamoja na nyumba nyingine za viongozi wa Serikali Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2011/2012, Kambi ya Upinzani ilihoji ni Wilaya zipi ambako nyumba za *DSO, DAS, OCD* na *DMO* zingejengwa. Katika kitabu cha majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kilichotolewa na Wizara ya Ujenzi mwezi Agosti, 2011 ukurasa wa 14, kwenye hoja hiyo majibu yalikuwa, naomba kunukuu: “Nyumba za

DSO, DAS, OCD *na* DMO zinajengwa katika Wilaya zifuatazo: Bahi mbili (*OCD* na *DSO)*, Ukerewe mbili *(OCD* na *DSO)*, Mvomero moja *(DAS)* na Kondoa moja (Hakimu)".

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu sahihi kuwa ni taarifa zipi sahihi kuhusiana na nyumba zilizojengwa na kusimamiwa na Wakala wa Ujenzi na hasa kwenye Wilaya. Je, ahadi hii ya Serikali ilitekelezwa?

Mheshimiwa Spika, mbali ya usahihi wa takwimu kuwa na utata, inaonesha kuwa Wakala wa Majengo umejikita zaidi kujenga nyumba za Viongozi Wakuu katika Mikoa na Wilaya na kuwauzia nyumba pindi wanapostaafu. Maana yake ni kwamba watumishi wa kada ya chini wao hawajengewi nyumba kama ambavyo niliainisha awali aina ya kada ya utumishi wa umma ambao wanahitaji sana kupatiwa nyumba wawapo katika utumishi na wamalizapo muda wa utumishi. Ukisoma randama ya Wizara, kasma 220703 inaonesha kuwa kiasi cha shilingi 288,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kulipia pango la ofisi Holland ambako Wizara imepanga.

Kambi ya Upinzani, inauliza hivi ni sahihi kweli kwa Wizara ambayo imechukua jukumu la kujenga nyumba na Ofisi za Serikali kushindwa kuwa na jengo lake la ofisi na badala yake inapanga? Ni lini Wizara hii itajenga jengo lake kwa ajili ya ofisi zake pamoja na taasisi mbalimbali zilizopo chini yake utaanza? Je, ahadi hii ya Serikali ilitekelezwa?

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge namba 20 ya mwaka 1979 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2008 (*National Construction Council Act, CAP 162, R.E.* 2008). Baraza lilianzishwa ili kusimamia maendeleo ya sekta ya ujenzi na pia kutoa uongozi mkakati unaolenga katika maendeleo ya sekta ya ujenzi kwa kutilia mkazo ukuzaji wa uwezo wa ndani.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu ya msingi ya Baraza ni kusimamia na kuongoza juhudi za kukuza na kuendeleza sekta ya ujenzi nchini Tanzania kwa kuzingatia ukuzaji wa uwezo wa ndani ya nchi ili kwenda sambamba na maendeleo na ushindani wa Kimataifa; kusimamia na kuratibu maendeleo na utekelezaji wa viwango, kanuni na miongozo ya kiufundi inayohusiana na sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Baraza linatakiwa kufanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi ya ujenzi ili kupata maelezo kuhusu mwenendo na utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na mapungufu yaliyopo na utatuzi wake. Ukaguzi unaweza kufanyika katika hatua yoyote ya mradi ikiwa ni pamoja na matayarisho ya utekelezaji, wakati wa utekelezaji na baada ya mradi kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa watumiaji wa barabara kuwa zinajengwa chini ya kiwango kiasi kwamba ajali nyingi chanzo chake ni ubora hafifu wa barabara. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa hadi sasa toka

kandarasi nyingi zilipoanza kazi ukaguzi umekwishafanyika katika miradi mingapi ya barabara?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezo wa Wahandisi Washauri. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina wa Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara ya Namtumbo-Tunduru juu ya uwezo na utaalam wao. Inasemekana kuwa wataalam wengi katika mradi huo hawana sifa, hivyo basi, ili kuondoa mashaka hayo, tunashauri uhakiki ufanyike katika mradi huo na miradi yote ya ujenzi wa barabara nchini na ikithibitika ndivyo hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TEMESA*; Serikali ina tatizo lingine kubwa la matumizi makubwa yasiyoratibiwa katika matengenezo na manunuzi ya magari. Sambamba na matumizi makubwa ya Serikali katika posho mbalimbali na mbali na kutokuwepo kwa sera madhubuti inayosimamia ununuzi na aina ya magari kwa kada mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Serikali ina tatizo lingine kubwa la matumizi makubwa yasiyoratibiwa katika matengenezo na ununuzi wa mafuta ya magari. Kwa mujibu wa Ripoti ya Kiufanisi na Kiuchunguzi kama ilivyotolewa na *CAG* ya tarehe 31 Machi, 2012 ni kwamba, Wizara ya Ujenzi ndio yenye jukumu la kununua, kusajili na kufanya matengenezo ya magari ya Serikali, ikisaidiana na Wakala wake *TEMESA* (*Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency).*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya *CAG* inaonesha kwamba Wizara ya Ujenzi haijaweka mfumo wa

kusimamia matengenezo ya magari. Pia hakuna sera yoyote ya ununuzi na matengenezo ya magari na hivyo hakuna mwongozo toshelezi juu ya usimamizi wa ununuzi na matengenezo ya magari. Wizara haijatoa mwongozo kwa *TEMESA* juu ya hatua na michakato ya kufuata na wala Wizara haisimamii utendaji wa *TEMESA* ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia haina kumbukumbu za kila wakati kama chombo cha usimamizi wa matengenezo ya magari. Mfumo wa matengenezo ya magari ya Serikali hausimamiwi ipasavyo na *TEMESA* kwa kuwa magari ya Serikali hayakaguliwi kabla na baada ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, mapungufu haya ya Wizara na *TEMESA* katika kusimamia matengenezo ya magari ya Serikali kunapelekea Serikali kupoteza fedha nyingi sana kwani licha ya kuwa hakuna usimamizi wa kutosha lakini pia hakuna taarifa au kumbukumbu za matengenezo ya magari na gharama zake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na matumizi makubwa ya fedha za walipa kodi kwa matengenezo ya magari ya Serikali ambayo hayana usimamizi madhubuti. Gharama kubwa sana inatumika kwa mafuta na matengenezo ya magari.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ieleze ni lini itakamilisha sera ya ununuzi na matumizi ya magari ya Serikali na kuanza kutumika ili kuliepusha Taifa na hasara ambayo inaweza kuepukika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzan, na kwa niaba ya Waziri Kivuli, naomba kuwasilisha. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani umesoma yote na nilipenda nisiwafanyie *interruption* kusudi hotuba yao isikike kama ilivyo. Sasa nitapenda niwakaribishe wageni maana sikuwatambulisha pale mwanzo kwa sababu watu wangu hawakuniletea orodha yao. Sina hakika, wengine watakuwa wameondoka lakini wengine wapo. *(Makofi)*

Wapo wanachuo 80 kutoka Chuo Kikuu cha *RUCO* Iringa. Walipo naomba wasimame tuwatambue kuwepo kwao, tunashukuru na nina hakika mmekatisha njia ya Mtera, tunaendelea kuijenga tumeiona jana ma-*contractor* wako barabarani na tunaomba hiyo barabara iishe haraka kwa sababu hawa saa hata mbili zisingefika. Karibuni sana na mjisikie mko nyumbani. *(Makofi)*

Wanafunzi wengine 90 na walimu wao kutoka shule ya Msingi Nzasa iliyopo Wilayani Temeke, Dar es Salaam, naamini labda watakuja tena baadaye. Halafu kulikuwepo wanafunzi 100 na walimu wao kutoka shule ya Mgulani iliyopo pia Temeke, Dar es Salaam. Halafu tulikuwa na wanafunzi 64 na walimu wao kutoka shule ya msingi Ebony, hii ni ya Kondoa Singida. *(Makofi)*

Pia kuna wataalam wa Wizara, sasa sina hakika kama wapo, lakini napenda hata kama wamechukua

nafasi zao za kazi, maana wageni wetu wanakaa pale, ikifika wakati nyie mnachangia inabidi wakakae kwenye maeneo wanayopaswa kuandika. Kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni zetu mgeni hapaswi kuandika aliko wala kusoma kitu ambacho sisi hatujamgawia. Kwa hiyo, ndiyo maana wale wataalam wakishafika wakati wa mjadala inabidi warudi kwenye viti vyao kusudi waweze kuandika, kuchukua *notice* na kumshauri Waziri. Kwa hiyo naisema hili mlifahamu kwamba kuna Kanuni ya namna hiyo.

Nitawataja wale wataalam wote wa Waziri kusudi mnapojadili hapa mjue mnamsema nani na si vizuri kuwataja watu majina mnapojadili. Sisi hatujadili watu, tunajadili *issues,* napenda sana Waheshimiwa mjifunze tujadili *issues not people*. Unakuta mtu amemkakamalia mtu kwa jina hatufanyi hivyo. Mjadili *issues* kama kuna kitu kisichokwenda sawasawa, semeni hicho.

Kwa hiyo, hawa nawataja kwa sababu ndiyo wanaomsaidia Waziri. Yupo Balozi Herbert Mrango yeye ni Katibu Mkuu, yupo Daktari *Engineer* John Ndunguru, yeye ni Naibu Katibu Mkuu, halafu wapo Wenyeviti wa Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara. *(Makofi)*

Pia yupo Daktari James Wanyancha yeye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, yupo *Engineer* Consolata Mgimbwa Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi; yupo Profesa *Engineer* Nenatubu Lema yeye ni Mwenyekiti Bodi ya Wasajili wa

Wahandisi; yupo Profesa Idrisa Mshoro yeye ni Mwenyekiti wa Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* amemaliza kusoma sasa hivi. Yupo pia Profesa Burton Mwamila, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Ujenzi na yupo *Archtecturer Doctor* Ambwene Mwakyusa, yeye ni Mwenyekiti Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiliaji Majengo. Hawa ndiyo Wenyeviti wa Bodi za taasisi. *(Makofi)*

Halafu wapo Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara; yupo *Doctor Engineer* William Mshama, Mkurugenzi wa Huduma za Kiufundi; yupo *Engineer* Joseph Nyamhanga, Kaimu Mkurugenzi wa Barabara; yupo Bi. Elizabeth Tagora Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango; yupo *Engineer* Madeni Kipande, Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira na yupo Bi Agnes Tirumanywa, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Utawala.

Vile vile yupo Bwana Projestus Pastory, Kaimu Mhasibu Mkuu; yupo Bi. Nuru Mhando, Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi; yupo, *Engineer* Martin Temo, Mkuu wa Kitengo cha Habari; yupo Bwana Donald Chidou, Mkuu wa Kitengo cha Sheria; yupo Bwana Michael Liwanda, Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na yupo Bwana Steven Nchimbi, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. *(Makofi)*

Wapo wakuu wa Taasisi chini ya Wizara; yupo *Engineer* Bi Macelina Magesa, yeye ni Mtendaji Mkuu Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA); yupo *Engineer* Patric Mfugale, Mtendaji Mkuu wa Barabara *(TANROAD);* yupo Bwana Elius Mwakalinga, Kaimu Mtendaji Mkuu, Wakala wa Majengo *(TBA)* na yupo

Bwana Joseph O. Haule, Meneja Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

Yupo *Engineer* Kasoguwele Msita, Mtendaji Mkuu Baraza la Taifa la Ujenzi na yupo *Engineer* Boniface Mhegi, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi yuko *Archtecturer Doctor* Jehadi Jehadi, Msajili Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majengo. Yupo *Engineer* Steven Mlote, huyu ni Msajili Bodi ya Msajili wa Wahandisi na yupo *Engineer* Dismas Mgani, Mkuu wa Vikosi vya Ujenzi na yupo Bwana Hussein A. Mmomba, Kaimu Mkuu wa Chuo cha *ATTI* Mbeya. *(Makofi)*

Vile vile wapo Mameneja wa Mikoa, Mameneja wa *TANROADS* wa Mikoa yote na nafikiri na wa Njombe naye yupo. Wapo Mameneja wa *TBA,* Mkoa wa Dodoma, Manyara, Simiyu na Morogoro. Yupo Kaimu Meneja wa *TEMESA,* Mkoa wa Dodoma, halafu wapo Wawakilishi wa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, Bwana Exon Kipole.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi; yupo *Engineer* Doctor Malima Bundala, yeye ni Rais Taasisi ya Wahandisi Tanzania; yupo Bwana Yohane Kaduma, Mtendaji Mkuu wa *Commercial Bank of Africa* akifuatana na Mtendaji mwingine wa Benki hiyo. Halafu anaeleza kwamba Benki hii ni *Commercial Bank of Africa* inatoa dhamana ya zabuni kwa Wakandarasi wa ndani wanaojenga daraja la Mbutu lililoko Wilaya ya Igunga Mkoani Tabora. Kwa hiyo, nimewatajia hao kusudi mkisema hapa mjue wanasikia na wapo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa tunaendelea na wachangiaji. Kama kawaida yetu, tunaanza na wale walioomba kuchangia, lakini hawajachangia hata mara moja. Wakiisha hao tunaingia wale walioomba kuchangia lakini wamechangia mara moja. Hii ni Wizara inachukua siku mbili, kwa hiyo haitakuwa na wachangiaji wengi.

Naanza na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, atafuatiwa na Daktari Haji Hussen Mponda, Mheshimiwa Zabein Mhita na Mheshimiwa Katagira atafuatiwa. Hawa hawajachangia hata mara moja, Mheshimiwa Rweikiza!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii hasa nafasi ya kwanza kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Niseme kabisa kwamba, siungi mkono hoja kwa sababu ambazo nitasema baadaye.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kusema kwa nini siungi mkono hoja niseme kwamba, natambua kazi ambayo imefanywa na Wizara hii ya kujenga barabara nyingi nchini hapa kwa ufanisi na kama mlivyosikia kwenye maelezo ya Waziri kazi zinafanyika vizuri. Lakini nitangulie pia kusema kwamba niombe Wizara hii ishirikiane sana na Wizara ya Uchukuzi kuimarisha miundombinu ya reli. Kwa sababu bila kufanya hivyo barabara zinajengwa lakini zitakuwa zinaharibika haraka.

Mheshimiwa Spika, mizigo ambayo inapita kwenye barabara hizi ni mikubwa sana, malori yenye mizigo mikubwa ya tani 40 lenyewe lina tani, labda 20 jumla tani 60, barabara nzuri inaharibika, madaraja yanaharibika. Kwa hiyo ni muhimu sana kwa Wizara ya ujenzi kushirikiana sana na Wizara ya Uchukuzi ili miundombinu ya reli iimarishwe na iboreshwe na mizigo mikubwa ipite kwenye reli. Hii itakuwa na manufaa kama nilivyosema, barabara zitadumu lakini pia sisi tunaokaa Mikoa ya Kanda ya Ziwa tutapata unafuu wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, hivi leo tunapata bidhaa zote kutoka Dar es Salaam kwa mfano, kupitia njia ya barabara. Mfuko wa *cement* pale Bukoba shilingi 22,000/= wakati Dar es Salaam shilingi 13,500/= au 14,000/=. Hii inatokana na sababu ya kupeleka mizigo hii kwa njia ya barabara ambayo ina gharama kubwa. Kwa hiyo, reli ikianza kufanya kazi vizuri tutapata unafuu pia kwenye kumudu bidhaa hizi.

Mheshimiwa Spika, hili sio linalonizuia kuunga mkono hoja. Linalonizua ni kwamba Bukoba sina barabara. Tumesikia maelezo mengi, tumesoma kwenye kitabu humu miaka iliyopita na mwaka huu katika bajeti hii, Bukoba hatuna barabara kabisa. Bukoba vijijini tuna lami kilomita 20 peke yake. Nafikiri sasa hivi Tanzania tuna lami kilomita 7000 au 8000 ambazo zimekamilika. Zile ambazo ziko chini ya Wakandarasi sasa hivi hazipungui kilomita 11,000 au 12,000, lakini Bukoba haimo, ina kilomita 20 peke yake.

Mheshimiwa Spika, ni kuanzia pale Kata Karabagaine, Kijiji cha Tawa hadi pale nyuma ya Kemondo Kanyinya na kuanzia Kijiji cha Katoma hadi pale Mwanzo Mgumu kuelekea Kyaka na Mtukula kama kilometa 20 au 18 peke yake Wilaya nzima. Sasa hii ni ndogo sana. Zilizobaki ni za vumbi na hakuna barabara ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha mwaka 2008, Serikali iliingia Mkataba na Mkandarasi wa kujenga barabara chini ya Mradi wa Kabanga *Bay* kutoka Bukoba Mjini kwenda hadi Rubafu na kuweka *ferry* pale kuunganisha Tanzania na Uganda kwa thamani ya shilingi bilioni 47 hadi leo hakuna kazi iliyofanyika miaka minne, miaka mitano. Serikali imetambua umuhimu huu na imefanya uchambuzi yakinifu na imesaini mikataba. Kazi haijafanyika na ndiyo maana siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa nini barabara hii haipewi au mradi huu haupewi pesa, milioni 47 za thamani ya mkataba tangu mwaka 2008 inahusisha urefu wa kilomita 42 na *ferry* kama bilioni tatu au bilioni nne, kazi haianzi miaka nenda miaka rudi? Barabara hii ni muhimu sana, inaunganisha Tanzania na Uganda, nchi jirani. Barabara hii ina umuhimu wa kibiashara nawa kimahusiano hata wa kiulinzi. Kipindi cha vita ya Uganda na Tanzania mwaka 1978, Iddi Amin alipobomoa daraja la Kyaka pale tulikuwa hatuna mawasiliano na Uganda.

Mheshimiwa Spika, tungekuwa na barabara ya pili kama hii tungekuwa na barabara mbadala na nafikiri ndiyo maana Serikali ikaona umuhimu ikasema ijengwe kwa kiwango cha lami, lakini kazi haianzi. Miaka ya nyuma kidogo hapa alikwenda Mheshimiwa Waziri Magufuli akiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi alikuwa anafungua Bandari kule kule eneo hilo hilo, Bandari ya Malee. Akafungua bandari ile nzuri ya kisasa akasema atamwomba Waziri wa Ujenzi wakati huo ajenge barabara hiyo, mkataba upo umesainiwa.

Mheshimiwa Spika, alisema barabara hiyo ijengwe kusudi itumike na hata samaki wanaovuliwa pale waweze kuletwa Kemondo kwenye kiwanda na sehemu nyingine kwa ufanisi zaidi. Akasema nitamwomba Waziri wa Ujenzi, leo hii yeye ndiye Waziri wa Ujenzi mbona hajengi barabara hii? Alisema atamwomba nani? Maana yeye sasa ndiye mwenyewe, hamwombi mtu, anajenga mwenyewe lakini hatuwekei pesa.

Mheshimiwa Spika, wakati nasoma kwenye kitabu cha Bajeti; mwaka juzi 2010/2011 ilitengewa shilingi milioni 700, zikaishia kujenga kambi ya Mkandarasi na nyumba mbili pale ziwani, barabara haikujengwa. Mwaka jana mmeandika milioni 250 ambayo si kweli. Ilikuwa ni milioni 50 tu, lakini mmendika milioni 250. Mwaka huu mmeweka milioni 75 katika bilioni 47. ndogo sana na hazina maana yoyote. Tupe pesa tujenge barabara hii, ni ya muhimu na kwa bahati eneo hilo lina watu wengi sana.

Mheshimiwa Spika, inapita katika Vijiji vingi sana, Nyakato, Kashozi, Kibengwe, Kagya, Katale mpaka kule Rubafu mwishoni. Watu wanapata taabu sana ikija mvua kwani huwa haipitiki na kule kuna mvua nyingi sana. Barabara hii ina umuhimu wa kipekee, tunaomba tupate pesa angalau kidogo, mwaka huu na mwakani kidogo basi, angalau barabara hii ikamilike na ile *ferry* ijengwe tuwe na usafiri mzuri wa kwenda Uganda ili tupeleke mazao, tupeleke ndizi, maharage na watu wanufaike na uwepo wa barabara hii na Serikali imeona umuhimu wake ndiyo maana iliweka mkataba. Lakini sasa inakuwa kama vile kitendawili, mkataba umesainiwa pesa haitoki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siungi mkono hoja hii ya Wizara ya Ujenzi kwa sababu hiyo, hadi nitakapopata maelezo ya ziada kwenye majumuisho ya Waziri kwamba amefanya maarifa gani kwenye bajeti yake angalau bilioni 15 au 20 kazi pale ianze mwaka huu. Mwezi wa Pili nilikaa naye nikamwomba Mheshimiwa Waziri tusaidie barabara hii akaniambia tutafanya hivyo, nitatekeleza yote, lakini naangalia kwenye kitabu humu juzi, hakuna kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasikitika kwamba sitaunga mkono hoja ya Wizara ya Ujenzi. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya pili kuzungumza. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema ya kuwepo hapa leo. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Ninaunga mkono hoja hii kwa sababu wamefanya kazi nzuri sana, tumesikia habari mbalimbali za kuendeleza barabara na madaraja Tanzania. Watu wengi wameridhishwa na kazi inayofanywa hasa ukizingatia kwamba, Daraja la Mto Malagarasi, Daraja la Mkapa, barabara za lami kutoka Dodoma – Mayaya, Barabara za Kibiti – Lindi na barabara nyingine, jinsi zinavyokwenda vizuri. Sisi tunamwombea Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, aendelee kufanya kazi nzuri ambayo ameianza kwa *speed* nzuri na hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa jitihada zinazofanywa, ninaunga mkono hoja ili na sisi katika Mkoa wa Lindi, Barabara yetu ya Kibiti - Lindi iweze kwisha kwa sababu hatua iliyofikia sasa hivi inaridhisha. Tunaomba Wizara ituambie mpaka sasa imefanya kazi kiasi gani na bado kiasi gani ili na sisi Mkoa wa Lindi tuweze kufurahia, tunaona matokeo mazuri ambayo yanaendelea hasa wiki hii kule ni vumbi tupu, kazi inafanyika.

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme tu kuwa, Barabara ya Kibiti – Lindi ikifunguka ikawa inapitika ni kichocheo kikubwa cha maendeleo katika Mkoa wa Lindi na Mikoa yote ya Kusini. Barabara ile ikifunguka, uchumi utakuja juu. Watu wanashindwa kwenda Lindi kuna mambo mengi sana, kwa mfano, suala la biashara kule kuna *gypsum, gas,* korosho, madini, mbao, kuna Bahari Kuu inayotoka Msumbiji kwenda Dar es Salaam mpaka Kenya, ambayo kuna samaki wakubwa wangeweza kutengeneza viwanda vya minofu. Samaki hao wapo Lindi, barabara ikipitika hizo kazi zote zitafanywa na siyo hiyo tu kuna masuala ya

Utalii na kuna Mji Mkongwe wa Kilwa, masuala ya *dinosaurs* na pango kubwa katika Afrika lipo Lindi.

Mheshimiwa Spika, Barabara hiyo ikifunguka kutakuwa na mawasiliano mazuri ya kwenda Mashariki, Magharibi, Msumbiji, Malawi na kadhalika. Mimi ninashudia watu wengi wanatoka Dar es Salaam, wengine wanatoka nchi za nje, wanapita Lindi kwa tabu wanakwenda Mtwara wakisema kuna *shortcut* inayokwenda Afrika ya Kusini. Kwa hiyo, wanaingoja ile Barabara wote hao, ninaomba Wizara tafadhali imalize maeneo ambayo hayajamalizika. Hiyo ilikuwa ni kuunga mkono mia kwa mia na hili litafanyika Barabara hizi za Kibiti – Lindi zikiisha.

Mheshimiwa Spika, nije sasa kwenye masuala ya *OPEC Fund.* Mwaka jana nilizungumzia hili kwamba, hizi barabara ni msaada wa *OPEC Fund,* kwa maana ya nchi zinazochimba mafuta kusaidia nchi maskini. Wao waliona kwamba, nchi maskini zipo mojawapo ikiwa Tanzania na walichagua Mikoa ya Kagera, Singida, Kigoma na Lindi. Sasa upande wangu wa Lindi tukiacha Mikoa mingine, hizi barabara zimejengwa kiasi gani na bado kiasi gani? Tunataka Serikali ituambie, hapa nimeona barabara hizo hizo zimetajwa ukurasa wa 200 katika Kitabu hiki cha Bajeti na ukurasa wa 204 na 205; hizi barabara zilizotajwa humu ni hizo hizo ambazo Mkoa wa Lindi tulipewa katika *OPEC Fund?*

Mheshimiwa Spika, tunataka kufahamu fedha zilizotumika katika ukurasa wa 204 na 205 ni za *OPEC* au ni fedha zingine za Serikali ya Tanzania. Vilevile

ninataka kufahamu Barabara za *OPEC Fund* kwa Mkoa wa Lindi tulipewa kilomita 200 za barabara kwa kiwango cha changarawe, ilikuwa ianze Septemba 2006 na kwisha mwaka 2008. Lindi tulipewa Barabara ya Tingi - Kipatimu kilomita 50, Barabara ya Nanganga – Ruangwa kilomita 60, Barabara ya Nachingwea – Kilimarondo kilomita 60 na Barabara ya Nachingwea - Liwale kilomita 30. Ninataka Wizara ituambie kama barabara hizi zipo tayari au bado ili na sisi tuone tumepiga hatua kiasi fulani au bado tupo nyuma katika hali ya umaskini ambao wenzetu wa *OPEC* wametuona kwamba sisi ni maskini.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuzungumzia Barabara za Mkoa. Tunaomba sana Wizara itusaidie Barabara za Mkoa ambazo zilipandishwa hadhi zitengewe fedha kwa ajili ya ukarabati. Zimepandishwa hadhi lakini je, zinaendeleaje? Serikali imetusaidia vipi katika kuendeleza barabara hizo kwa sababu zinatusaidia sana katika kusafirisha mazao ya wananchi?

Nikija suala la kupandishwa daraja barabara; Mkoa wa Lindi tunazo barabara ambazo tunaiomba Serikali itusaidie kupandisha daraja; kwa mfano, kuna Barabara hii ya Nyengedi - Rondo na Mandawa, tunaomba Serikali itusaidie. Kuna Barabara ya Mchinga – Kijiweni - Jiwe la Mzungu hadi Lushungi, tunaomba Serikali itusaidie kupandisha hadhi kwa sababu ni barabara ambazo zinafanya kazi nzuri sana ya kusafirisha mazao ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna Barabara ya Liwale - Kilimarondo mpaka Tunduru na Barabara ya Nachingwea - Chiola hadi Ruangwa, tunaiomba sana Serikali itusaidie kupandisha hadhi barabara hizi.

Kuunganisha barabara Mkoa hadi Mkoa; Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005 ilisema kwamba, itasaidia kuunganisha barabara Mkoa hadi Mkoa kuweka barabara nyingine. Kwa mfano, ukitoka Mkoa wa Lindi kwenda Mkoa wa Morogoro kuna barabara inayotoka Liwale, inatoka Liwale - Mpigamiti inakwenda Mbuga mpaka Morogoro.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali kama ilivyozungumzia kwenye Ilani yake kwamba itaunganisha barabara Mkoa hadi Mkoa, barabara hii iunganishwe kutoka Mkoa wa Lindi, kutoka Kijiji cha Liwale Mpigamiti kwenda Mkoa wa Morogoro. Barabara nyingine ni ya kutoka Liwale - Kilimarondo hadi Tunduru, kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Lindi kwenda Mkoa wa Ruvuma.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa ugunduzi wa barabara mpya.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, naunga Mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita na Mheshimiwa Eustace Katagira atafuatia.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu, ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, aliyenijalia kuwa mwingi wa afya leo nami nipate nafasi ya kutoa mchango katika Hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi. Naomba pia nitumie nafasi hii, kuwashukuru sana Wakazi, Wadau na Wapiga Kura wa Jimbo la Ulanga Magharibi, ambao bado wana mapenzi mema na mimi na bado wananipa ushirikiano mkubwa katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Ulanga Magharibi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa mfupi na utajikita katika sehemu mbili. Nitaoanisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ambayo imetoa vipaumbele kimojawapo ni miundombinu na vilevile changamoto ambayo nchi hii imepata ya chakula katika suala la uchumi na vilevile ni namna gani Wizara ya Ujenzi inaweza kuchangia kutatua tatizo hili la Kitaifa. Katika Bajeti ya Serikali imeonesha wazi kabisa na imeeleza na wengi tunashuhudia changamoto kubwa ya uhaba wa chakula, lakini habari njema ambayo Watanzania wengi mnafahamu, naomba nichukue nafasi hii kuwaeleza kwamba Mkoa wa Morogoro tumebarikiwa kuwa na mabonde makubwa ambayo yana rutuba, yakiwezeshwa yanaweza kutatua tatizo la chakula na mfumko wa bei upande wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliliona hili toka mwaka 2006, ambapo alikaa na Wadau wa Mkoa wa Morogoro tukaanzisha Mpango wa FAMOGATA ulioifanya Morogoro kuwa Ghala la Chakula la Taifa.

Tayari Wadau wa Mkoa wa Morogoro tumeshajipanga, kwa kutumia wataalamu wetu wa *SUA* tumetengeneza *proposals* mbalimbali ambapo kutumia vyanzo tulivyonavyo vya Mabonde haya mawili; Bonde la Kilombero na Bonde la Wami, vinatosha kabisa kuwalisha Watanzania chakula cha mchele, maana yake mpunga na kilimo cha miwa kwa kuwapa Watanzania sukari ya kutosha nchi nzima; namna gani sasa Wizara hii ya Ujenzi inaweza kusaidia huu Mpango ambao Rais pia ameuona na tayari sisi Wadau wa Mkoa wa Morogoro tumejipanga jinsi ya utekelezaji wake.

Changamoto inayoukabili Mpango huu ni miundombinu kama nilivyosema, mahali penye bonde maana yake pana mvua nyingi. Wilaya ya Ulanga ni kisiwa, kwa maana nyingine tunatenganishwa na Wilaya ya Kilombero na Mto Kilombero kipindi cha masika kwa sababu pale tunahudumiwa na kivuko mara nyingi kivuko kile hakifanyi vizuri kama inavyostahili, sasa wakati mwingine unajikuta unataka kutoka nje ya Wilaya inakuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, Wabunge wenzangu sisi tunapolalamika kuhusu ujenzi wa Daraja la Mto Kilombero si kwa sababu tunataka tupite kirahisi hapana ni kwamba tupo kwenye mazingira magumu, tupo kwenye kisiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1999 tulipoteza wenzetu 100 pale wakati Kivuko cha Kilombero One kilipozama. Kwa hali hiyo, ninashukuru Serikali wameona na wameweka dhamira za dhati kabisa kwamba wanataka waanze kujenga Daraja la Mto

Kilombero. Daraja hili ni kero kubwa siyo tu kiuchumi bali pia katika kusafirisha mazao, pembejeo na adha kwa Watanzania wanaoishi kwenye Bonde la Kilombero na maeneo ya Wilaya ya Ulanga.

Changamoto nyingine ambayo tunakutana nayo katika Mpango huu wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa la chakula ni suala la barabara maana huwezi kwenda shambani au huwezi kusafirisha mazao kama huna barabara ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, barabara ninazozizungumzia na ninaiomba Serikali waangalie zaidi na katika kipindi cha bajeti hii wameelezea lakini kidogo, ninaomba wakazie zaidi na waanze kuitekeleza. Barabara ambazo zinatutesa hasa ni mbili; barabara ya kuanzia Ifakara kwenda Mlimba, ambako tumetenga bonde kubwa sana linazalisha miwa na mpunga. Barabara hii haipitiki kipindi cha masika na hiyo ndiyo inayosababisha usafirishaji wa mazao kwenda kwenye soko Ifakara na Dar es Salaam, gharama zinakuwa kubwa kiasi kwamba gunia moja kulitoa maeneo hayo mpaka kulifikisha kwenye Soko la Morogoro linafika shilingi 8000 na ndiyo hiyo tunasema mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo tunaizungumzia ni hii ambayo inaanzia unapovuka Mto Kilombero inakwenda moja kwa moja mpaka Mahenge na tawi lingine linaelekea kuanzia Lupilo mpaka Kilosa Mpepo, Londo kwa watani zangu kule Namtumbo. Barabara hii ni muhimu sana hasa kuanzia Lupilo mpaka Kilosa Mpepo kwa sababu ndiyo bonde kubwa sana linalozalisha Zao la Mpunga. Kama

barabara hii itaweza kupitika misimu yote miwili; masika na kiangazi, inaweza kusaidia kiasi kikubwa sana kutatua tatizo la uhaba wa chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie suala la kivuko. Tumeona jitihada za Serikali na naishukuru sana, sioni haja kwa nini wengine wanafikia hatua ya kusema Bajeti ya Wizara hii isipite wakati mahali ambapo Serikali ya CCM wamefanya vyema sana ni katika Wizara hii ya Ujenzi. Sasa hivi unaweza kutoka Mtwara kwa bajaji mpaka Kagera, ukiondoa eneo dogo tu hili la kilometa 30 pale.

Mheshimiwa Spika, sisi pale Mto Kilombero wakati daraja linajengwa bado tunasumbuliwa na kivuko. Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika Hotuba yake kwamba, atafanya ukarabati. Angalizo langu, kile kivuko kimeshachoka hata mkikikarabati kitaishia kama mwaka 1999, kututokomeza kama tulivyopoteza ndugu zetu 100. Nimeona hapa vilevile kuna jitihada za makusudi kabisa za Serikali kushirikiana na wabia wengine binafsi kuweza kutatua matatizo, mojawapo la kivuko tayari sisi tumeshaanza, tunaomba mkono wenu Serikali kupitia Ubalozi wa Finland na Kampuni ya Mitiki, wao wana nia njema ya kuweka kivuko cha kisasa pale. Wakati Serikali inajenga Daraja la Mto Kilombero, namwomba Mheshimiwa Waziri aharakishe mazungumzo hayo na mgao huu ili haraka iwezekavyo tuanze kupata huduma ya kivuko hicho wakati tunategemea daraja kubwa hilo la Kilombero likianza kujengwa na kumalizika. Nina imani kabla ya mwaka 2015 daraja hili litakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Spika, katika Mji Mdogo wa Malinyi, ambao hauna lami wala umeme, wana changamoto kubwa ya mafuriko. Ahsante na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Hiyo ya Malinyi utamwandikia Waziri, sasa namwita Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita na Mheshimiwa Katagira atajiandaa.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi, kwa kutayarisha Bajeti kisayansi na ambayo kwa kweli inatekelezeka. Iwapo watayatimiza haya, watakuwa wamefanya kazi nzuri sana. Aidha, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Magufuli, nilimwomba tufanye ziara kutembelea Barabara ya kutoka Dodoma mpaka Mayamaya, kilomita 19, alikubali na tukatembelea tukaona jumla ya kilomita 19 tayari zimekwishatengenezwa tuta; ninakushukuru na ninakuomba tuongozane tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi na Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Nkamia, tunaishukuru sana Serikali, kwa sababu ujenzi umeanza kufanyika katika maeneo mengi. Tuliomba barabara ya kutoka Bicha kwenda Kondoa ijengwe nayo kwa kiwango cha lami, imeshaanza kujengwa, tunashukuru sana. Barabara ya kutoka Babati mpaka Bonga, kilomita 19, nayo kuna kama kilomita 11 tayari zimekwishawekwa lami; tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara ya kutoka Mayamaya mpaka Bonga, kilomita 188, ilikuwa ni sehemu kubwa ambayo ilikuwa haina mpango wowote. Ninashukuru leo nimepata taarifa kwamba, barabara hii imekwishatengewa pesa za ndani na pia zimetengwa fedha kutoka mkopo wa *ADB* na *JICA*; ni hatua nzuri.

Tayari imeshagawanywa katika maeneo mawili, tunaomba mchakato wa kuwapata Makandarasi ufanyike na pesa itolewe kwa wakati ili kazi iweze kuanza na pesa za baadaye ziendelee kutolewa ili hawa Wakandarasi wasije wakafika mahali wakakamilisha kazi pesa ikawa bado wakadai fidia. Kutokana na Waziri Magufuli, naamini kazi itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nikichangia Wizara hii mwaka jana katika Mkutano wa Nne, Kikao cha 37, Tarehe 1 Agosti 2011, nilitoa hoja kwamba, Barabara ya kutoka Katesh, Wilaya ya Hanang', imechukuliwa na *TANROADS* mpaka kufikia mwisho wa Wilaya ya Hanang wakati Barabara hii inatoka Katesh mpaka Kondoa. Niliomba sehemu iliyobaki kutoka Mtiriangwi mpaka Kondoa nayo ichukuliwe na *TANROADS* ili mwendelezo huu wa kutoka Katesh mpaka Kondoa uendelee.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini kuona barabara hiyo moja katika Wilaya moja imechukuliwa na *TANROADS* lakini ilipofika mwisho wa Wilaya hiyo ikaachwa kwa Wilaya nyingine. Naomba hiki kipande kingine nacho kichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho hicho pia nilieleza kuwa, mwaka 2010 Rais aliahidi kwamba, barabara inayotoka Galapo mpaka Mtiriangwi mpaka Ntundwi nayo itachukuliwa na *TANROADS,* tunaomba ahadi ile ithaminiwe. Rais wetu aliahidi na kwa sababu aliahidi ni imani yangu kwamba, Serikali inachukua ahadi hizo na kwa vyovyote vile itatimiza ahadi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, mimi leo nina amani, nina faraja na ninaamini Wananchi wa Wilaya ya Kondoa nisikilizeni ndugu zangu, tumeahidiwa hapa Kondoa na Chemba kwamba, barabara ya kutoka Dodoma mpaka kufika Babati *Inshallah* ikifika mwaka 2015 itakuwa ya lami. Kwa maana hiyo, mtu anaweza kutoka na bajaji Dodoma mpaka Babati, Mungu atupe nini ndugu zangu. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mwezi wa Ramadhani umekaribia, naomba nichukue nafasi hii adhimu niwatakie Watanzania wote Mwezi huu Mtukufu uwe wa kheri, fanaka na amani.

Mheshimiwa Spika, leo singojei kugongewa kengele, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia, hatutampa nafasi ya kuongea kwa sababu umeshasema mambo yenu wote mazuri. Naomba nimwite Mheshimiwa Eustace Katagira, huyu ni Mwalimu wangu.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu na mimi nichangie katika hoja hii. Pia nakushukuru kwa kuendelea kunitambua na kunikumbuka kwamba mimi ni mwalimu wako, walimu huwa hatusahauliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ujenzi na Timu yake, kwa maandalizi mazuri ya bajeti ambayo inaleta matumaini. Niongelee barabara za maeneo yangu.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kyaka - Bugene, inajengwa kwa kiwango cha lami na ninaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kufanya hivyo. Barabara hii inaunganisha Uchumi wa Wilaya mbili; Wilaya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe ikiunganisha na sehemu nyingine za Dunia.

Mheshimiwa Spika, kazi pale inaendelea lakini mwaka huu ambao umeisha shughuli zilisimama kwa muda kwa sababu ya kukosa malipo. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa ijitahidi pale pasisimame, Mkandarasi alipwe ili kazi iendelee na iweze kukamilika ukifika muda unaostahili. Itakapokamilika Wananchi wa Wilaya ya Karagwe na Kyerwa watanufaika na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru uboreshaji wa Barabara za Mgakorongo - Kigalama kwenda Mrongo mpaka Uganda. Tuna mategemeo makubwa kwa mipango ambayo imewekwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuiboresha zaidi, naomba mipango

hiyo iendelee ili Wananchi wa Wilaya mbili za Kyerwa na Karagwe waweze kufaidika na mwendelezo huo wa barabara inayounganisha Tanzania na Nchi ya Uganda.

Mheshimiwa Spika, barabara muhimu sana ya Bugene – Mkwenda - Mrongo mpaka Nchi ya Uganda, sasa hivi ipo katika kiwango cha udongo, lakini naomba kueleza kwamba katika mikutano miwili Mheshimiwa Rais amewaahidi Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kwamba, barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Nilikuwa katika mkutano mkubwa pale Isingiro katika ziara ya kawaida ya Rais, lakini pia katika mkutano wa kampeni pale Nkwenda, aliahidi akasema kufuatia umuhimu wa barabara hii, Serikali tutaweza kuijenga kwa kiwango cha lami. Naomba sasa Serikali itimize ahadi hii ya Rais.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu barabara hii ni muhimu sana kwa Wilaya zote mbili za Kyerwa na Karagwe, kwa sababu kwanza inaunganisha Wilaya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe pamoja na nchi ya Uganda na kuna biashara kubwa sana katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna magari mengi sana ambayo yanatumia barabara hii, *high traffic density* na inabeba uchumi mkubwa. Uchumi wa kahawa, uchumi wa maharagwe na uchumi wa mazao mengine kwenda nchi jirani ya Uganda na kwenda katika maeneo ya Mkoa wa Kagera na maeneo mengine kama Kahama mpaka Dar es Salaam, kahawa yote inatoka huko inakuja mpaka Dar es

Salaam lakini barabara bado ni ya udongo na inaleta shida kubwa wakati wa msimu wa kahawa.

Mheshimiwa Spika, kubwa kabisa ni kwamba, barabara hii sasa hivi inaunganisha Makao ya Wilaya ya Koragwe na Makao Makuu ya Wilaya Mpya Kyerwa. Kwa hiyo, tunaomba sana Waziri aiangalie hii na aweze kutimiza ahadi ya Rais. Aangalie pia umuhimu wa barabara hii na aweze kuiweka katika orodha ya barabara ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Mlima wa Rwagunika *(Rwagunika Escapement),* hii *escapement* ipo kwenye Barabara ya Bugene - Nkwenda mpaka Mrongo kwenda Uganda.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yake ya kawaida, Mheshimiwa Rais alipitia katika *escapement* hiyo na alisikitika sana kuona ni kilima cha hatari sana, pale pale aliagiza akasema *escapement* hii ijengwe katika kiwango cha lami. Urefu wa *escapement* yenyewe hauzidi kilomita nne, lakini shida ni kwamba, *gradient* ya kilima ni kubwa, kona ni mbaya na baada ya agizo hilo katika bajeti hii ambayo imekwisha, Serikali ilijitahidi kutekeleza maelekezo ya Rais.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha ni kwamba, katika kilomita nne Serikali imejenga mita sabini na ninaposema mita sabini ninamaanisha kwamba, urefu wa barabara iliyojengwa hautimii hata urefu wa uwanja wa mpira. Watu wangu wanaona hii ni aibu

kabisa katika utekelezaji wa ahadi ya Rais, lakini pia katika utekelezaji wa mipango ya barabara.

Tunaomba katika bajeti hii katika mpango ambao utaendelea, Kilima cha Rwagunuka kiweze kutengewa fedha ya kutosha ili kujenga kilomita zote nne siyo kilomita thelathini, siyo kilomita arobaini, wala siyo kilomita hamsini, ni kilomita nne tu. Kwa hiyo, tunaomba pesa zitengwe, kilomita nne hizi zijengwe kwa kiwango cha lami, lakini pia ujenzi huu uweze kutekeleza matakwa ya yule ambaye aliagiza kwamba mradi huu utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, mawazo hasa ilikuwa ni kupunguza hali ya hatari kwa wananchi wanaopita pale na magari, baiskeli na pikipiki na kwa kufanya hivyo inatakiwa Mkandarasi anayefaa aweze kwanza kupunguza *gradient* ya mwinuko katika kilima kile. Zaidi ya hapo, kona zirudiwe kidogo ili zisiwe za hatari, ili wakati wa mvua barabara hiyo iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba hicho kilima kipo katika barabara ambayo inaunganisha Tanzania na nchi jirani ya Uganda na kwa hiyo magari makubwa, yenye mizigo yanapita na kupeleka biashara Uganda lakini pia kutoa biashara Uganda na kuleta katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba haya Waziri wa Ujenzi ayaangalie vizuri ili miradi yetu hii ya barabara iweze kutekelezwa. Itasaidia katika Wilaya hii ambayo ipo katika sehemu ambayo ni jirani sana na Nchi ya Uganda na Nchi ya Rwanda. Barabara hizi zitasaidia

pia wakati wowote ambapo zitahitajika hasa katika masuala ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, nirudie kusema kwamba, naunga mkono hoja nikiwa na mategemeo makubwa kwamba, Wananchi wa Wilaya Mpya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe watafarijika na mipango hii ambayo nimeiongelea ya ujenzi wa barabara ili waweze kusaidia kuleta maendeleo katika maeneo ya Wilaya hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa asubuhi hii nadhani tuhitimishe hapo, kwa sababu muda uliobakia hauwezi kutosha mtu mmoja kujadili. Tutakaporudi saa kumi na moja Wabunge wafuatao wajiandae:-

Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Silvestry Koka na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa. Wengine nitawataja ni vizuri mkafika mapema.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo tunalitaka, Wabunge pamoja na kwamba mnakuwa

na shughuli ni vizuri Ukumbi wa Bunge uonekane una watu, zaidi tunapoingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kama Kamati ya matumizi tutakuwa chini ya kiwango cha *quorum,* ipo siku hatutapitisha Bajeti na nisingependa kitu cha namna hiyo kitokee. Wakati wa Kamati ya Matumizi ni vyema muwaambie wafuasi wenu wafike hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Napenda kutoa shukrani kwanza, kwa Mungu wa Elia, Mungu anayepiga kwa kusema tenda neno, shika neno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani vile vile kwa familia yangu na watu wote wanaoniombea kila siku; mchana na usiku kusudi niweze kutekeleza na kutunza umuhimu wa kazi yangu. *(Makofi)*

Kabla sijasema yote, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, kwa Hotuba yake nzuri aliyoitoa mwisho wa mwezi kuhusu sakata la Madaktari. Vile vile napenda kuwapongeza

Wanakilombero wote na Chama cha Mapinduzi, Chama Dume, Dume la Mbegu Bora, ambao wamemletea Katibu mzuri, Katibu Mpya katika Wilaya yangu. Wameniletea DC Mpya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo haijengi barabara.

**MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA:** Sawa, natoa shukrani kwanza. Naishukuru Serikali kwa kutupatia daraja. Daraja la Kilombero lilikuwa kero kubwa sana kati ya Wananchi wa Jimbo la Ulanga na Jimbo la Kilombero. Kwa hiyo, namshukuru Waziri anayehusika, Bwana Magufuli, mtani wangu, kwa kunipata daraja wakati kama huu. *(Makofi)*

Sitakuwa na muungwana nisiposhukuru kwa sababu binadamu ukipewa kidogo unashukuru, usingoje kushukuru kikubwa tu. Pamoja na yote hayo, kuna Barabara ya Kidatu mpaka Ifakara, kama unaweza kukumbuka kama alivyozungumza ndugu yangu, mdogo wangu Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mbunge wa Ulanga kwamba, Ifakara na Ulanga hasa Ifakara, Jimbo la Kilombero limechaguliwa kuendesha kilimo cha *Southern Agriculture Growth of Tanzania (SAGCOT).* Sasa hawa watu wanakuja kuwekeza wengi na miundombinu ikiwa mibovu uwekezaji wao utakuwa hauna maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoka Ifikara kwenda Mlimba ambako Mgeta kuna *KPL* ambayo ni Kampuni kubwa sana, inalima mpunga na bahati nzuri Mheshimiwa Rais alitembelea mwaka huu akapata manung'uniko ya

wale Wazungu Wawekezaji kwamba, barabara ni mbaya. Sasa naona barabara hiyo haijapangiwa fungu lolote na wakati Mheshimiwa Rais aliweka ahadi kwamba, zitatengenezwa kilomita 100. Mkumbuke kwamba, yalitokea masika mwaka huu pale Mbingu hata magari ya msaada yalishindwa kupita. Naona mambo ya kutengeneza barabara ya kokoto kila mwaka Serikali inapoteza hela nyingi sana, kwa sababu kila mwaka ikifika masika lazima watengeneze barabara tena. Kwa hiyo, inaigharimu Serikali, bora zitafutwe fedha itengenezwe barabara ya lami.

Kutoka Mlimba kwenda Tanganyika Masagati barabara iko mpaka Taveta lakini kutoka Taveta kwenda Tanganyika Masagati kuna mazao mengi sana; kuna machungwa mengi, kuna mipira, kuna mashamba makubwa sana lakini hakuendeki, watu wanatupa machungwa yao, michungwa yao inauzwa kwa bei ndogo sana kwa sababu usafiri ni tabu. Cha kushangaza zaidi katika Jimbo hakuna barabara inayounganisha Kata ya Uchindile na Mlimba. Inabidi nikienda nitembee mpaka Tanganyika Masagati nirudi tena Ifakara nije Mikumi niende Iringa niingie tena Uchindile kwenye Jimbo langu. Hicho kitu kinanisikitisha sana. Naomba Bwana Magufuli, Waziri wetu, ashughulikie suala hilo, *TANROAD* waweze kutufungulia barabara pale kwa sababu Halmashauri haina kipato kikubwa.

Kuna barabara nyingine ya kutoka Chita na Mofu ni mbovu. Sasa naomba Mheshimiwa Magufuli, a-*consider* tena hicho kitu kwa sababu hali yetu ni mbaya sana katika usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sina mengi sana, mengi amezungumza ndugu yangu Mheshimiwa Hadji Mponda, shida zetu zote zinafanana kuhusu daraja na barabara. Sipendi kupoteza muda wa watu wengi sana, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. OMARI RASHID NUNDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, muweza, Mwenyezi Mungu wa haki, mwenye rehema kubwa, kwa kunipa afya na pia kwa kunijalia kuwa hapa leo kuchangia hoja ambayo inaendelea hapa. *(Makofi)*

Vile vile nawashukuru ndugu zangu wa Tanga kwa kunikabidhi Ubunge wao niufanyie kazi, pia kwa kuniamini kwa upendo na ushirikiano wanaonipa. Zaidi ya yote, kwa dua zao za dhati kwa Mwenyezi Mungu, anijalie niepukane na shari niwe na heri. Nawaahidi tena, kamwe sitatetereka kimaadili na utumishi wangu kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali na niisifu kwa kujenga barabara nyingi sana kwa muda mfupi, kwa kipindi hiki cha Awamu ya Nne. Baada ya kusema yote hayo na kujua kuwa barabara zimeenea nchi nzima na mimi nimeweza kuzitembelea na ni nzuri kinyume cha mategemeo yangu. Nirudie sasa kuziangalia barabara za Mkoa na Wilaya ya Tanga. Mji wa Tanga unaunganishwa na dunia na barabara tatu; kuna barabara inayokwenda Korogwe, inayokwenda Hororo na inayokwenda Pangani. Ukizikamilisha hizo

kuziweka lami itakuwa Mji wa Tanga una barabara zote zinazotoka Mji huo. Kwa bahati mbaya sana, Barabara ya Tanga hadi Korogwe ilijengwa na Dumes kwenye miaka ya 1954 na kilomita 24 za barabara hiyo ndizo ambazo ziko katika Wilaya ya Tanga. Tangu mwaka 1954 mpaka juzi mwaka 2009, barabara za lami zinazotoka Mji wa Tanga kwenda nje zilibaki hizo kilomita 24 peke yake. Hii ya Hororo na ya Pangani zimekuwa ni hadithi. Barabara mbili hizi zina faida na tija kubwa sana siyo kwa Tanga bali kwa nchi nzima. Sina muda wa kuzielezea faida zote; kuna faida za kiuchumi, za kijamii, za kitalii za kiulizi na kadhalika na ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru tena Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuliona hilo na kuanza kuzishughulikia barabara mbili hizo. Mwaka 2005 aliahidi Barabara ya Tanga kwenda Pangani itawekwa lami. Ilikuwa ni ahadi sasa hivi ipo kwenye Ilani. Mwaka 2009 Barabara ya Hororo ilianza kujengwa kwa lami kwa msaada wa Amerika, sasa hivi imekaribia kumalizika. Nilipoambiwa Barabara ya Hororo itajengwa kwa lami, wakazi wanaoishi sehemu ambayo barabara ingepita, ambapo siyo *road reserve,* walijitolea kubomoa nyumba zao kabla hata barabara yenyewe haijaanza kujengwa. Kilichotokea baadaye ni kuwa wale ambao hawakubomoa nyumba walilipwa. Hawa ambao walibomoa nyumba kwa hiari yao mpaka leo malipo yao bado pamoja na kuwa Mheshimiwa Rais alipofika kule mwezi Mei mwaka 2010 katika kuzindua barabara hiyo aliwaahidi kuwa fedha hizo zitalipwa.

Nimeangalia katika Kitabu cha Makisio ya Wizara nimeona kumetengwa milioni 12, ninavyojua watu hao ni wengi, ni zaidi ya 30, kuna wakati walitaharuki mpaka wakaandika barua ambazo siyo nzuri kwa Mheshimiwa Waziri; na mimi nikawakanya hata kwenye mikutano ya hadhara kuwa wasifanye hivyo na wamwombe radhi. Sasa leo najisikia kama sikufanya kitu sawa sawa; shilingi milioni 12 kufidia watu ambao walijitolea kuvunja nyumba zao, watu zaidi ya 30, sijui kama hiyo ni sawa sawa. Ninaomba Wizara itupe ufafanuzi kuhusu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Barabara ya Pangani; Barabara ya Pangani inaziungaisha Wilaya tatu. Barabara hii ina urefu wa maili 32 tu, sawa sawa na kilomita 51, inaunganisha Wilaya ya Tanga, Wilaya Muheza na Wilaya ya Pangani na ndiyo barabara pekee ambayo inaunganisha Pangani na Duniani kote kwingine. Vinginevyo, inabidi uvuke Mto Luvu au Mto Pangani uelekee Bagamoyo. Barabara hii siyo nzuri, mvua ikinyesha haipitiki kuna milima ya Kinare na Gongolo, lakini kwa miaka yote hiyo pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Rais, miaka mitano (2005 – 2010) ilipita hakuna ambacho kimefanyika. Mwaka jana tuliahidiwa kuwa upembuzi yakinifu ulikuwa unafanywa kwa barabara hiyo ya Tanga mpaka Pangani tu. Leo hii ninapoangalia *Vote* katika kitabu cha nne Vote 98 sioni ikitajwa. Mheshimiwa Waziri alisema kuwa bado anaendelea kufanya upembezi yakinifu kuunganisha na Bagamoyo na ametenga shilingi 2,055,000,000 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nirejee kusema kuwa, Tanga imedorora na siyo kwa hizi barabara, huu ni mfano mdogo tu. Ningeomba sana Serikali iliangalie hilo kwa sababu wananchi wa Tanga ni wavumilivu, ni wenye upendo mkubwa sana na ni wakarimu sana. Ukarimu una kikomo, watafika mahali watakuwa hawaelewi kile kinachoendelea.

Barabara za Tanga zote ni km 906 na kati hizo barabara km 124 zaidi ya 100 ziko *TANROAD* na kati ya hizo ni kilomita 40 tu ndizo ambazo zina lami. Hizo ni pamoja na barabara nyingine ambazo zimejengwa kwa lami na Jiji ambazo ni kilomita 84 na zile za vumbi zote hali zao siyo nzuri. Ninapoangalia katika kasma hii na kuangalia fedha zilizotengwa kwa ku-*rehabilitate* barabara, ningependa pia nipate ufafanuzi kati ya hizo ni ngapi ambazo zitatumika kwa barabara hizi za Tanga. Wilaya ya Tanga imesambaa sana, ina vijiji ambavyo viko mbali, vijiji ambavyo ni vizuri kwa rasilimali walizonazo kwa maendeleo ya aina mbalimbali. Kwa mfano, Kijiji cha Pande ambacho kina udongo wa mfinyanzi kwa siku nyingi, ambavyo tungetegemea leo hii ungekuwa umeendelezwa mpaka kupata sahani za kauri kutoka kule. Hata ukitengeneza mitungi kule inavunjika kabla hujafika sokoni Tanga. Barabara ni mbaya, ni barabara ambayo *TANROAD* kupitia Wizara wangeifikiria kama ingewezekana ikaondoka kwenye Halmashauri ikarudi *TANROAD*. Kuna Kijiji cha Mapojoni ambacho kina umbali takriban sawa sawa na huo wa Pande na hicho ni Kijiji kizuri sana kwa mambo ya uchumi, lakini pia barabara zake hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa nitilie msisitizo kuwa Tanga na Pangani zinahitaji kuungana na sehemu nyingine za Dunia. Pangani ni Mji wa Wilaya, Pangani haina barabara ya lami, Tanga ni Mji wa Mkoa. Tunashukuru Barabara ya Hororo sasa inamalizika, lakini zile kero za fidia za wananchi tunaomba zitafutiwe utatuzi. Barabara ya Pangani iangaliwe kama Barabara ya Tanga – Pangani badala ya kuunganishwa na barabara nyingine na mikakati thabiti ifanyike ili barabara hii nayo ipate kiwango cha lami, Mji wa Pangani ufunguke.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja nitakapopata utatuzi wa matatizo hayo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujaendelea, naomba niwatambue sijui ndiyo wenyewe; wanafunzi 90 kutoka Shule ya Msingi Nzasa iliyoko Wilaya ya Temeke wasimame kama wapo. Ahsante, karibuni sana na poleni kwa safari ndefu, tunasikitika asubuhi hatukuwatambulisha hatukuwa na orodha.

Tuna wanafunzi wengine 100 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Mgulani Temeke; kama wapo wasimame. Ahsanteni sana, tumefurahi mmekuja. Nadhani mtajifunza mambo mengi kuhusu Shughuli za Bunge.

Kuna wanafunzi 64 kutoka Shule ya Msingi Iboni ya Kondoa na wao kama wapo wasimame na walimu wao. Ahsanteni sana, tunategemea mtajifunza mambo mengi sana hapa.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwepo hapa leo. Pili, nakupa wewe pole kwa msiba uliokukuta.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimetumwa na wapiga kura wangu, nimtolee salamu Mheshimiwa Waziri Magufuli. Salamu zenyewe zinakuja kwa jinsi hii; wanamshukuru kwa fedha za mwaka 2011/2012, lakini salamu hizo zina swali kwamba kwanza; fedha zinachelewa; pili, Daraja la Mto Magara ambayo ni Barabara ya Mbuyu ya Jerumani kwenda Mbulu, Serikali ilipanga milioni 600 tangu mwaka 2010 mpaka leo hizo fedha hazionekani na kipindi cha mvua watu hawa wanakwama kutumia barabara hiyo. Pia Serikali iliwapangia fedha za kuweka *concrete surface* katika mlima wa barabara hiyo, lakini mpaka sasa ni kilomita 1.07 tu ndiyo iliyotengenezwa. Wanakushukuru kwa barabara zingine zilizotengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina barabara zaidi ya kilomita 85,000 na Serikali inatumia fedha nyingi lakini sehemu kubwa ni barabara za udongo. Tunatumia fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya *repairs,* baadaye barabara hizo mvua ikinyesha zinaondoka. Ninaishauri Serikali kwamba, umefika wakati sasa tutafute njia ya kuwa na *permanent roads* ili fedha nyingi zitumike maana tunamwaga fedha barabarani mvua ikija inazoa.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitajikita katika maeneo kama matatu; Barabara za Wilaya, za Mkoa na muda ukiruhusu Barabara Kuu na

matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara na mwisho kabisa msongamano *(congestion)* ya Barabara za Dar es Salaam. Katika Barabara za Wilaya, fedha ambazo zinatoka *Road Fund Board,* wananchi wanashukuru sana sehemu nyingi, lakini fedha hizo zinachelewa hasa kutoka TAMISEMI; jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni usimamizi wa wananchi kupata *value of money*. Wakandarasi wengi wanatumia udongo badala ya moramu, kwa hiyo badala ya kupanda daraja, zinateremka kimatumizi daraja. Mimi siyo *engineer* lakini ninafahamu kwamba, kuna *specification* za barabara kwamba, Barabara ya Daraja la A inatunzwa ili ibakie A, lakini sisi tunavyotumia sasa hivi, tunatumia barabara ya Daraja la A kwenda B na B kwenda C, ina maana barabara nchi hii sasa zitakwisha. Kwa hiyo, ushauri wangu hapa ni kwamba, ili *value of money* ipatikane basi usimamizi wa wakandarasi hasa wale walioko Wilayani wakati wakijenga wawe wanafuatilia, wasitoe *certificates* mwisho tu.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingi inachelewa, Miradi ya tangu mwaka 2007 mpaka leo haijaisha; kwa hiyo, gharama yake inapanda na hii nitaitolea mfano wa barabara nitakayoitamka baadaye. Pili, nataka kuishauri Serikali kuhusu barabara inayotoka Arusha kwenda Namanga, barabara hiyo inayotumika kwa utalii na kwa kusafirisha mizigo. Mkandarasi yule anatakiwa asimamie kwa ukaribu kwa sababu uzoefu umeonesha kwamba, baada ya kukabidhi barabara hiyo kabla muda haujakwisha, barabara imeisha. Uzoefu umetokana na barabara ya Arusha - Singida au

Arusha – Makuyuni, sasa hivi imejaa mashimo mengi na hela zinazopangwa ni za *rehabilitation* badala ya kui-*reconstruct* upya.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni Barabara ya Dodoma - Babati, imezungumzwa leo asubuhi hapa. Barabara hii ni kama ya Mkoa wa Dodoma, ni Barabara Kuu, ni *International Road,* ni barabara ya kuanzia Cairo kwenda Cape Town kupitia Tanzania. Kwa hiyo, ni Barabara ya Taifa na nimeona kwenye Kitabu imepangiwa fedha kwa Kimkoa. Ushauri wetu ni kwamba, ile barabara imalizike kwa muda maalum ili iweze kutumika kwa biashara ya Wananchi wa Tanzania na Afrika ya Mashariki mpaka Cairo, kwa sababu siyo tu watu wa Babati na Dodoma, lakini ni *Centre* ya Tanzania, kwa hiyo, bajeti yake ikiongezwa ikimalizika mapema itasaidia uchumi wa nchi. Nimeona Randama ya Wizara ya Ujenzi, inaonesha barabara ambazo zimewekwa. Muhimu ni barabara ambazo zinaunganisha Mkoa na Mkoa au inaangalia sehemu ambazo ni za kiuchumi.

Hii barabara ina umuhimu mkubwa kiuchumi, bila kujali kwamba ni barabara ya sehemu moja. Kwenye Kitabu cha Maendeleo nimeona pesa iliyooneshwa ni shilingi bilioni 36, kwa hiyo, nitamwomba Waziri wakati wa kujumuisha, atuoneshe itamalizikaje na Mheshimiwa Mbunge wa Kondoa Kaskazini amesema itakuwa ya lami hivi karibuni. Mimi sielewi kama itakuwa ya lami kwa bilioni 36. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nizungumzie *Road Fund Board.* Katika pesa zote za Serikali ya Tanzania ambazo wananchi wana matumizi yake ni Mfuko huu. Kwa

sababu hizo pesa ni *ring faced.* Tunashauri Serikali pesa zingine kama zile *road licence* tunazolipa kwa magari, zitumike kwenye hizo barabara maana hatuelewi pesa hizo zinaenda wapi, kama inakatwa kwa ajili ya barabara kutumika, *road license* maana kibali cha kutumia barabara, basi iletwe huko ili Mfuko uongezeke kwa sababu pesa nimeziona mwaka huu, Mfuko umepungua pesa, kwa hiyo, lile pendekezo la kuongeza wigoni muhimu.

Mheshimiwa Spika, pili, fedha hizo za *Road Fund Board* zinatufikia Wilayani na kama zitatumika vizuri, zitumike kwa Miradi ambayo itakuwa inaisaidia Wilaya hata ikienda kwa *Zone* kwa sababu tunazozisambaza hivi sasa hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kengele ya kwanza imelia, labda nizungumzie juu ya msongamano wa magari Dar es Salaam. Nimesoma kwenye *forum* moja kwamba, wamependekeza tangu mwaka 2010 *solution* kama tisa hivi, lakini nilivyoona kama mbili, tatu, inaweza ikatumika. Ya kwanza, yale magari ya mizigo yasiruhusiwe kupita barabara moja pamoja na magari ya kawaida, kuwe na barabara yao pembeni. Ya pili, mabasi ya Dar es Salaam, mabasi makubwa kama ile IKARIUS ya zamani yarejeshwe ili watu wengi wapande hayo mabasi *friendly use* kwa sababu watu wengi wataacha kutumia magari yao. Tatu, barabara zile na *road shoulders* kwa ajili ya baisikeli tu-*promote bicycle transport* ili msongamano upungue. Nne, zile *satellite towns*, yaani Miji mingine inazungukia Dar es Salaam na huduma zipatikane pembeni hata Ofisi za Serikali ziwe pembeni ili kule Mjini kusiwe na msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia Jijini Dar es Salaam kuna makontena mengi ambayo yanaingia Mjini, haya nayo yanaharibu barabara...

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini pia nichukue fursa ya mwanzo kabisa nimrudishie sifa na shukrani Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya na uzima hata nikasimama leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, kwa maneno ya jumla kabisa napenda kuipongeza Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ujenzi na Taasisi zote zilizoko chini yake, kwa jitihada kubwa ambayo inaendelea kuzifanya katika kuboresha miundombinu. Wengi wanazungumzia barabara, lakini napenda tuungane sote kwa pamoja kujua kwamba, Wizara ya Ujenzi inajenga barabara lakini pia inajenga majengo na miundombinu mingine, lakini kwa kuwa naizungumzia Serikali kwa ujumla niseme kwamba, tukirejea vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tutakumbuka jinsi ambavyo Taifa letu lina jukumu kubwa sana la kuweza kuendeleza miundombinu yetu, barabara zikiwa ni mojawapo.

Mheshimiwa Spika, kwa leo nitaanza na eneo la Jimboni, nikiishukuru kwanza Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kupitisha au kupasisha barabara ambayo kwa muda mrefu sana tumekuwa tukifuatilia na kushauriana na Wizara kwamba ipandishwe daraja

kwa sababu inaunganisha Wilaya ya Tunduru na Wilaya ya Nachingwea. Kwa hiyo, ni Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi. Napenda kuwaarifu wapiga kura wote wa Jimbo la Tunduru Kaskazini hasa wale wa Kata ya Ngapa, Mindu na Kapanya na zilizo karibu kwamba barabara inayoanzia Mji Mwema kupitia Ngapa kwenda Nachingwea sasa ni Barabara ya Mkoa. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, nizungumzie kuhusiana na Barabara ya Namtumbo - Tunduru yenye *lots* tatu ambazo sitazitaja zote kwa sababu ya muda. Naishukuru Serikali, kwanza, kwa kufanya Mradi ule uweze kuchangia kufungua eneo la Kusini na hasa Mkoa wa Ruvuma na *Mtwara Corridor* kwa ujumla. Kweli kuna changamoto nyingi sana kwenye Mradi ule na hasa ni *performance* ya Mkandarasi kwamba inatakiwa kufanyiwa kazi kwa karibu. Naipongeza *TANROADS* kwa ujumla wake, Bodi ya Usajili ya Wahandisi, lakini pia Kamati ya Miundombinu ya Bunge, kwa kuja kufuatilia kwa karibu barabara ile na kuweza ku-*address* hata tatizo moja kubwa ambalo linahusiana na uwezo wa wataalamu katika Mradi ule.

Nakumbuka baada ya kuwasiliana nao wameshakuja mara kadhaa, kuja kushughulikia matatizo yanayohusiana na Mradi ule ikiwa ni pamoja na ku-*assess competences* za wataalamu wanaoshiriki kwenye Mradi ule hasa wahandisi na hatua zilichukuliwa. Wapo wahandisi huko walitoka India walirudishwa kwa sababu ya kutokuwa na sifa, lakini pia wafanyakazi wengine wa taaluma zingine ambao walikuwa hawana sifa kwa Sheria zingine za nchi,

wengi tu walirudishwa. Naipongeza sana Serikali kwa kutusaidia kufuatilia Mradi ule. *(Makofi)*

Pia, hata Baraza la Ushauri la Mkoa *(RCC),* mimi nikiwa ni Mjumbe, mara ya mwisho tuliweza kutoa tamko la kwamba sasa umefika wakati tunatakiwa kuifanya barabara ile au mradi ule uweze kufanyika vizuri. Tumevumilia sana, tukifikiri kwamba tuwape nafasi kwa sababu kwanza Mkandarasi huyu ni mgeni na ule ni Mradi wake wa kwanza. Kwa hiyo, tulidhani kwamba, angeweza kujirekebisha, lakini nataka niseme leo kwa niaba ya Wapiga Kura na Wananchi wa Jimbo la Tunduru Kaskazini na kwa niaba ya *Mtwara Corridor* yote, Mikoa yote ya Kusini, lakini pia kwa niaba ya Taifa kwamba, sasa Mkandarasi huyu umefika wakati tumechoka kumvumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwishasema kwenye Taarifa ya Kamati ya Miundombinu, tufuate taratibu za kimkataba, *Contract Management* ambayo itakuwa ni sahihi kabisa ya kuweza kusitisha mkataba huu baada ya kujiridhisha kwamba ni lazima kufanya hivyo basi zifanyike hatua ambazo ni za kitaalamu ili kuweza kuto-*risk* sasa kwamba tunaweza tukafika mahali tukaingia kwenye mgogoro ambao utafanya Mradi huu uweze kukwama zaidi. Lingine, nasema kwamba, yaliyotokea katika Mradi huu yawe ni fundisho kwa Mradi mwingine unaofuatia wa Tunduru - Mangaka kwenda mpaka Mtambaswala.

Mheshimiwa Spika, Mradi ambao tumeambiwa kwenye *speech* ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwamba katika mwaka ujao wa fedha, taratibu za

kumpata Mkandarasi zinafuata, ninaomba sana safari hii tusirudie makosa tukapata Mkandarasi wa aina kama ya *Progressive Heighleg JVC.*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, sasa nizungumzie juu ya suala la kujenga uwezo kama Watanzania na kama Taifa katika suala la kuendeleza na kujenga miundombinu yetu, barabara ikiwa ni mfano mmojawapo. Tuna changamoto kubwa, tuna matatizo ya mahitaji ya wataalamu, lakini pia tuna matatizo ya kukuza uwezo wa wataalamu ikiwemo pia kukuza uwezo wa Wakandarasi. Kwa bahati nzuri, Mpango wetu wa Miaka Miatano wa Maendeleo, umeliona tatizo hili na umeli-*address* vizuri sana, kinachotakiwa sasa ni kutekeleza yale ambayo yamo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwa haraka haraka tu, Tanzania inakusudia kufikia lengo la kuwa nchi ya uchumi wa kati *(the middle income country) by 2025* ambayo sasa tunategemea kui-*achieve* katika Mpango ya miaka mitano, mitano ya maendeleo hadi kufikia mwaka 2025. Sasa kule tumeshaambiwa kwamba, uwiano kwa asilimia kwa *working population*, yaani ukiwachukua wafanyakazi wote wa nchi hii, Tanzania ina uwiano wa *professionals* asilimia 0.7 wakati kama tunataka kuwa *a middle income country (MIC)* ni lazima twende kwenye asilimia 4.66 lakini pia kwa *technicians* na *associates* ambao ni *artisans* tunatakiwa kutoka kwenye asilimia 1.8 kwenda kwenye asilimia 4.73.

Mheshimiwa Spika, bado mpango pia umeeleza kwamba, tunatakiwa kuwa na Wahandisi na *Architects* na *related technicians* 88,000 kufikia mwaka 2015,

lengo ambalo ni kubwa sana, lakini tunaweza kulifikia kama tutajipanga. Je, tumejipangaje kwenda kufikia kule? *Speech* ya Waziri imeonesha kabisa kutokana na takwimu zilizopo Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili ya *Architect* kwamba bado tuko mbali sana kwenye lengo hili. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati atakaposimama, atueleze tumejipanga namna gani kwenda kufika kwenye malengo yale.

Mheshimiwa Spika, kufundisha wataalamu hawa kwa ngazi yote ya kuwafanya kwanza wapate sifa, lakini pia kuwajengea uwezo, kunahitaji fedha. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umeeleza kwamba, mojawapo ya maeneo ambayo tunaweza kujipanga vizuri ni kwenye *skills development levy,* ile ambayo imehuishwa iko kwenye Mpango wa Maendeleo inayosema sasa *skills development levy* haitakusanywa tu na zile Taasisi ambazo zina mwelekeo wa kiufundi hasa kwa kusisitiza zaidi kuwa ni *VETA.* Mpango huu ni wa waajiri wote na kila mmoja atatakiwa kuchanga asilimia tatu ya *pay roll* yake.

Mheshimiwa Spika, mimi suala langu haliko kwenye kukusanya fedha tu, liko kwenye matumizi ya fedha pia. Tulifanya kidogo marekebisho ya Sheria kwenye Bunge lililopita ambapo fedha za *skills development* zilielekezwa kwenye elimu ya juu na zingine zikiwa kwenye elimu ya chini, naweza kusema kwa maana ya *VETA,* lakini elimu ya kati kwa maana ya *technicians* au mafundi sanifu ikawa imeachwa bila kupewa fedha hizo. Naomba sana safari hii wakati tutakapokuwa tunawapa jukumu hili *Tanzania Employment Services Agency (TAESA),* ambayo ndiyo

wamepewa jukumu hili la kusimamia hizi *development levy* kwa utaratibu mpya basi tusisitize sana kujenga uwezo katika kada za kati, kwa sababu bila hivyo, utekelezaji wa miundombinu utakuwa wa matatizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tunashukuru, ahsante.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza, naomba nikupe pole kwa msiba wa mtu wako wa karibu uliokupata, lakini pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Masatu Wasira na Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, kwa kupoteza wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Serikali iniwie radhi kidogo kwa sababu katika hoja hii ya leo, siiungi mkono kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwenye bajeti ya mwaka jana Waziri Mheshimiwa Dkt. Magufuli, aliji-*commit* kwamba kwenye bajeti ya mwaka huu, angetenga pesa za kutosha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi. Jambo hili

hakulifanya. Hela zilizotengwa hapa ni milioni mia saba na zile za mwaka jana milioni mia tatu sabini na tano, ni kama bilioni moja  na milioni sabini na tano, wakati kazi yenyewe inahitaji karibu bilioni moja na milioni mia tano. Kwa sasa siungi mkono hoja mpaka pale atakaponihakikishia kwamba zinapatikana milioni mia nne ishirini na tano kwa ajili ya kufanya kazi hii. Sababu yangu kubwa ni kwamba, tunapata manung'uniko na kelele nyingi kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu mpendwa, wakati wa kampeni alipokuwa Jimboni kwangu Tandahimba na Jimbo la Mheshimiwa Mkuchika, Newala, aliwahakikishia Watanzania kwamba angehakikisha kabla hajatoka Mkandarasi anakuwa *site* kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Pia mwaka jana alipofanya ziara kwenye Mkoa huo, alipata malalamiko ya wananchi kwenye eneo hilo hilo la barabara kwamba mbona upembuzi yakinifu haujaanza na wala hatujui hatua za dhati za kuanza na ujenzi wa barabara hiyo.  Alisema bajeti hii ingetengewa hela za kutosha kabisa ili upembuzi yakinifu uishe na hivyo kuwe tu na suala la kutafuta pesa za ujenzi wa barabara. Jambo ambalo halipo hapa.

Mheshimiwa Spika, kama unakumbuka, yeye alinisahihisha kwamba Daraja lile la Mwiti pale, nilipokuwa nasahau sahau lile Daraja akasema Daraja la Mwiti nalijua, tunatenga pesa hapa lakini hazitoshi. Kwa hiyo, kwa mtaji huo inaniwia vigumu sana mimi kuunga mkono hoja hii kwa sababu tunalalamikiwa sana, tunapata manung'uniko sana kwenye eneo hili. Mimi nitaunga tu bajeti hii kama nitahakikishiwa milioni

425 zinatafutwa mahali barabara hiyo ianze upembuzi yakinifu ili tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu wakati mwingine analalamikiwa kwenye vitu vya namna hii; watendaji wake kutojali ahadi anazozitoa. Mimi nadhani tubadilike, Rais akisema ni maagizo, sasa inakuwaje amesema lakini nia ya dhati haifanywi kwa kwenda sambamba na kauli yake. Naomba mjirekebishe wale mnaohusika kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ninataka itambulike wazi kwamba, barabara hiyo ni ya uchumi kwa Mkoa wa Mtwara. Asilimia 60 ya korosho zote zinazozalishwa Mtwara zinapita kwenye barabara hiyo. Barabara hiyo inaiingizia Serikali gharama ya kutengeza kila mwaka pasipo sababu. Ikitengenezwa sasa, hii hela tunayoitafuta kila mwaka kuifanya ipitike wakati wote wa misimu itakuwa haipo, itakuwa imeshaisha. Kwa hiyo, mimi nadhani nia ya dhati hapa lazima iwepo ili barabara hii ijengwe.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuizungumzia Barabara ya Ndundu - Somaga, kilometa 60 zilianza kujengwa na Mkandarasi tangu Julai 2008, lakini mpaka leo tunapoongea ni kilometa 20 tu zimekamilika kwa lami na tunaambiwa itamalizika Oktoba mwaka huu. Mimi nadhani hapa lipo tatizo na tuelezwe wazi wazi tatizo ni nini? Mheshimiwa Fatma Mikidadi, alipokuwa anajibiwa swali lake hapa wiki mbili zilizopita, alielezwa Mkandarasi ameshapewa pesa za kutosha, karibu zaidi ya asilimia 70 ya pesa anazo; sasa kama

pesa amepewa za kutosha; tatizo ni nini? Kwa nini haimaliziki?

Mheshimiwa Spika, inalekea kuna jambo hapa linafichwafichwa, halina ukweli; ni vizuri tukaelezwa tatizo ni nini tutafute dawa ya kulimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wananung'unika wakipita pale, adha nyingi. Mimi nadhani tumalize hili jambo. Mheshimiwa Dokta Magufuli, aliliambia Taifa hili kwamba, anampa Mkandarasi yule situ 180, kwa hesabu zangu mimi ilikuwa miezi sita na kwa muda ule alioutoa ingekuwa Machi 2012. Leo tunapoongea hapa ni Julai 5, kama niko sawasawa, hakuna kinachoendelea pale cha kuleta matumaini kwamba, Oktoba barabara hiyo itamalizika; tufanye kila njia tupamalize pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimewahi kusema hapa kwamba, Kusini kule ndiyo ilikuwa Ngome ya Ukombozi wa Kusini mwa Afrika, mlituacha sana. Sasa yaishe, mambo si yameshaisha kule, tupeni nafasi tusogee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nina jambo lingine; ninakwazwa sana na usimamizi wa barabara unaofanywa na Wahandisi wetu wa kazi. Lipo tatizo limejitokeza, watu wanangoja Mkandarasi afanye, halafu wakati wa kukabidhi barabara ndiyo anaambiwa haipo kwenye *Standard* zinazotakiwa; hivi jamani Wahenga si walisema kwamba kinga ni bora kuliko tiba? Kwa nini usizuwie pale mapema; usimsimamie mapema ukamwambia unajenga nje ya

kiwango fanya kwa kiwango hiki. Kinachotokea, tunawaacha. Mifano ipo mingi tu, Mbwemkulu kuja hapa Nangulukulu. Zakhem pale, Mbagala Zakhem kwenda Mtoni Mtongani, tumeacha inajengwa *sub-standard,* tunaenda tena. Tunachukua muda mrefu bila kukamilisha zoezi hilo bila sababu. Mimi nadhani wasimamizi wetu wa barabara hizo wafanye kila jitihada kuwasimamia vizuri. Tusingoje kuharibikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tandahimba imezaliwa au asili yake ni Wilaya ya Newala. Ilimegwa kutoka Wilaya ya Newala na kwa utamaduni, mila na desturi tunafanana, *custom and usage* tunafanana sana. Serikali mnafanya jambo ambalo si sawasawa kwenye *Political Management.* Watu wanaofanana kwa kila kitu, ukijenga Newala lami kilometa tisa halafu Tandahimba unaiacha, unatafuta maneno kwa Mbunge wa Tandahimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuache hiyo. Tuwekeeni pale kilometa tano, tisa, barabara ya lami, wananchi wafaidi kama wanavyofaidi jirani zangu Newala. Sina nia mbaya, nia yangu hapa ni angalau mambo yawe yanafanana fanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Barabara ya Ulinzi kule sisi inatoka Mtwara, inapita Mtwara Vijijini, inaenda Newala – Tandahimba – Masasi mpaka Nanyumbu. Barabara hiyo inapita kandokando ya Mto Ruvuma, mahali ambapo ni *erable land* kabisa kwa ajili ya uzalishaji na mambo mengine ya kiuchumi, lakini na mawasiliano na jirani zetu wa Msumbiji na pia

kuimarisha ulinzi. Barabara hiyo imeachwa, yaani ni pori; tuiangalie hiyo barabara sasa, tuifufue ili iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa neema na fadhila zake nyingi. Nikushukuru na wewe pia Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa Hotuba yake nzuri, pia na Kitabu chake kizuri alichotugawia. Nataka nianze na Kitabu alichotugawia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Kitabu kwenye jalada, huku nyuma kuna jengo moja zuri sana la *TBA.* Makusudio ya kuanzishwa kwa *TBA,* moja ni kupunguza tatizo la uhaba wa nyumba za watumishi wa umma na kuwa na makazi. Nitapenda kufahamu, jengo hili ambalo ni mali ya *TBA,* limepunguza kwa kiasi gani tatizo la nyumba kwa watumishi wanaostahiki kupata nyumba za umma, hususan pale Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu jengo hili limejengwa la biashara, *TBA* imeacha makusudio yake ya kusimamia kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi ama kwa kuwauzia ili wawe na makazi baada ya kustaafu au wale ambao wana stahiki za kupata

nyumba wapate makazi. Wameingia kujenga nyumba za biashara sasa na kuingia ubia na kufanya biashara kama lilivyo Shirika la Nyumba, *National Housing.* Lazima tufike mahali tujue ni nini majukumu ya *TBA* na ni nini majukumu ya *National Housing.* Vinginevyo, kutakuwa na ushindani usio wa lazima kuwepo na Shirika likajitoa katika majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha linaondoa tatizo la nyumba kwa watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo la *TBA,* lakini pia *TBA* wana mpango wa kujenga nyumba na hususan niizungumzie Mikoa hii Mipya, ambayo ni Katavi, Simiyu, Geita na Njombe. Mahitaji yao ya kupewa viwanja, yako tayari yamepokelewa na viwanja vipo, tunawahakikishia tutawapa. *TBA* wanakuja kujenga nyumba za aina gani; na je ni kwa ajili ya kuja kufanya biashara; makazi au za kuuza? Tunataka tupate ufafanuzi, maana nimeona wameomba viwanja vingi na tupo tayari kuwapa hivyo viwanja wanavyovihitaji, lakini tuhakikishe kwamba, tatizo la nyumba kwa wafanyakazi wanaokuja kufanya kazi katika Mikoa hii Mipya, lisiwepo. Tutafurahi kama kazi hiyo itaanza mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu barabara. Tatizo kubwa ambalo tunalo ni kutokana na miradi ya barabara mingi ambayo inajengwa ama kwa kiwango cha chini, kwa maana ya kusuasua, haiendi kwa kasi iliyokusudiwa kutokana na tatizo kubwa la fedha. Mpaka Mei, jumla ya takriban shilingi milioni 152, Wizara ya Ujenzi imekuwa ikidaiwa na wakandarasi mbalimbali. Ninaamini kabisa fedha

itakayotolewa, itakayoidhinishwa katika bajeti hii, sehemu yake itakwenda kulipa madeni hayo. Wakati huo huo kazi zinaendelea kufanywa na madeni yataendelea kuwepo kwa kazi zilizofanyika. Kuna mkakati gani wa makusudi wa kumaliza kadhia hii ya madeni ili tuweze kwenda vizuri kutokana na fedha tunayoidhinisha katika bajeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa ambalo lipo ni mahusiano kati ya Wizara ya Ujenzi na Hazina. Hazina imekuwa ni tatizo kubwa sana na ni kikwazo kikubwa sana; mpaka washikane mashati ndiyo wanatoa fedha. Fedha imeshaidhinishwa na Bunge, hatuoni sababu yoyote ile, kwa nini Hazina imekuwa ikichelewesha kupeleka fedha siyo kwenye Wizara ya Ujenzi tu, takriban katika maeneo yote ambayo Bunge tayari limeshaidhinisha! Lazima tuwe na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba, fedha ambayo imeidhinishwa na Bunge, inakwenda katika miradi iliyokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie matengenezo ya muda mrefu. Mradi wa matengenezo ya barabara ya muda mrefu *(PMMR),* kwa majaribio ulikuwa katika mikoa minne kama sikosei, Rukwa ikiwa ni mojawapo, Mwanza na Tanga. Mpango huu ulikuwa mzuri sana na kwa Rukwa, tulifanya kwa mafanikio makubwa sana. Nilikuwa na matarajio kwamba, Mpango huu labda ungekuwa umepanuliwa sasa, ukaenda katika sehemu kubwa sana ya nchi, badala ya mikoa minne ambayo ilikuwa imeanza. Huu ni mpango ambao kama tutajipanga vizuri, utatusaidia sana kupunguza

matengenezo ya barabara ya mara kwa mara. Tukiwa na mpango ambao utasimamiwa vizuri, tukapata fedha kwa wakati ili tuwe na wakandarasi katika barabara zetu kwa muda wote, kuhakikisha barabara zetu zinapitika ni mpango mzuri. Niiombe tu Wizara ya Ujenzi, iangalie ni namna gani inalisimamia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili tumetoa mapendekezo kwa sababu kumekuwepo maombi mengi ya kutaka kupandisha hadhi barabara katika maeneo yetu, Wilaya na Mikoa; ni vyema sasa Serikali kwa ujumla wake, kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ujenzi na Wizara nyinginezo zinazohusika, wakaangalia sasa umuhimu wa kuanzisha taasisi nyingine itakayoshughulikia barabara za Vijijini, yaani Mamlaka ya Kusimamia Barabara za Vijijini *(Tanzania Rural Roads Agency).* Itapunguza kelele hii ya kutaka kupandisha hadhi barabara. Tutakuwa na chombo ambacho kitakuwa na Wataalamu wenye ujuzi, vinginevyo, hii *TANROADS* nayo itaelemewa. Afadhali sasa tuigawe, tuanzishe Chombo kingine kitakachosimamia barabara za vijijini ili tuwe na uhakika wa kuwa na barabara nzuri, zenye kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara ya Kizi – Stalike – Mpanda. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba, angalau ameitaja katika Hotuba yake barabara hii na fedha zilizotengwa siyo nyingi. Ukiangalia barabara yenyewe ni ya kilometa 95, kuna bilioni tatu. Najua siyo mwanzo mbaya; ni katika hatua za awali za ujenzi wa barabara ya lami ya kutoka Kizi – Stalike – Mpanda. Nitapenda tu kwa sababu katika

Hotuba imeonekana kwamba, ujenzi umeanza, Mheshimiwa Waziri sasa awahakikishie Watu wa Mpanda kwamba lini ujenzi huo utaanza rasmi. Kadhalika, tulikuwa tumetoa maoni katika Hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani, yale maeneo ambayo mpaka hivi sasa hayajapata Wakandarasi, kutoka katika Barabara ya Itigi kwenda Tabora, baada ya mpaka wa Singida, hakuna Mkandarasi pale mpaka Nyahua na baada ya Urambo, hakuna Mkandarasi mpaka Ilunde. Haya maeneo ni muhimu sana mkaangalia uwezekano sasa wa kutafuta kila njia yakajengwa ili barabara hii ikamilike kwa wakati mmoja. Kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmesaidia sana kufungua Ukanda wa Magharibi uweze kupitika kwa urahisi na kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Daraja la Mto Malagarasi. Nilibahatika kutembelea pale nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Mradi ule unakwenda vizuri na Wakorea wanafanya kazi nzuri sana, tunastahili kuwapongeza. Tatizo kubwa ni *commitment* ya Serikali yetu. Serikali yetu, inaweza ikawa ni sababu ya kuufanya ule mradi usikamilike kwa wakati. Niiombe basi iangalie kila namna itakavyoweza wasikwamishe juhudi na jitihada zinazofanywa na wenzetu wanaotusaidia katika maendeleo, waone kwamba na sisi kweli tunastahili kusaidiwa. Unapobebwa, basi jishike. Wenzetu wametubeba, wamechangia asilimia 80, sisi tunatakiwa kuchangia asilimia 20 tu, lakini hata hizo bado tunasuasua, tumeshindwa kukamilisha. Naiomba Serikali, barabara hii ya kwenda Kigoma ikamilike.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza, kukushukuru. Vile vile kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka hai hadi siku ya leo. *(Makofi)*

Nimesimama hapa niweze kuchangia yale ambayo ninadhani yanaweza kusaidia Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, Jimbo la Kwela na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba, barabara ni kama mshipa wa damu, ukitaka watu waendelee ni lazima uhakikishe wanapata barabara. Ukiwanyima watu barabara ni sawasawa na kuwafunika kwenye chungu, hawana namna nyingine ya kuweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie barabara ya kutoka Kibaoni kwenda Muze, Muze – Mtowisa, Mtowisa – Ilemba, Ilemba – Kiyamatundu, Kiyamatundu unakwenda Kamsamba. Barabara hii ni muhimu sana, inaambaa ambaa katika Ukanda wa Mlima Lyamba – lya – Mfipa na upande huu Ziwa Rukwa. Barabara hii imekaa katika eneo la Bonde la Ufa. Sisi sote ni lazima tukubali, sehemu inayoitwa Bonde la Ufa ni sehemu ambayo ina sifa zote kwa kilimo cha aina zote; iwe mazao, matunda, inakubali karibu kila zao.

Mheshimiwa Spika, lakini barabara hii kwa miaka mingi ilikuwa imekufa kabisa. Ninashukuru kwa sasa,

walau unafuu upo, lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ambavyo aliweza kuweka msukumo wa kutosha juu ya barabara hii. Kwa sababu yeye mwenyewe ni shahidi, kuna siku alipita barabara hii, alikuwa akitokea kwenye mazizi ya wafugaji, ikamlazimu kutafuta ni namna gani aweze kuikomboa hii barabara. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii pamoja na jitihada za Serikali zinazofanyika, kulingana na changamoto zilizopo, maana imekaribia mlima, kwa hiyo, kunakuwa na maporomoko ya maji ambayo, yanasababisha barabara hii isiweze kuimarika zaidi kama tutaendelea kuitengeneza kwa kutumia udongo. Ni vyema sasa Serikali ijipange kuona ni namna gani barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha lami kwa maana ya kuunganisha Kibaoni mpaka Kiyamatundu, Kiyamatundu unaingia Mbozi unatokea Mloo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifungua hii barabara, tutakuwa tumefungua uchumi mkubwa wa wananchi wa eneo lile, hata Mkoa wa Rukwa na Mbeya. Kwa sababu wananchi wengi wa Mbeya, wanategemea na wanakuja kulima karibu na eneo hili kwa sababu ni eneo lenye rutuba nyingi sana. Ninawashukuru wametupa hata mwamko wa kuweza kulitumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara hiyo, ipo changamoto kubwa ya kukosekana kwa Daraja la Mto Momba. Hiki ni kilio kikubwa. Ninasikitika ni mara nyingi

jambo hili tumelisema, jinsi wananchi wanavyohangaika. Mheshimiwa Waziri, nimemwandikia barua mara kadhaa, nimemwona mara kadhaa; umuhimu wa lile daraja na jinsi wananchi wanavyohangaika, hakuna daraja, kilikuwepo kivuko kilichotengenezwa na Wamisionari, ambapo mwananchi akitaka kuvuka ni lazima atoe hela. Juzi tu imetokea hatari, karibu kihatarishe maisha ya wananchi kilipokatika. Sasa ukiiuliza Serikali wanasema limefanyiwa upembuzi yakinifu; upembuzi yakinifu karibu miaka mitatu sasa! Nataka Mheshimiwa Waziri, wakati anatoa majumuisho, aeleze daraja hili litatengenezwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo kwenye daraja hili, tunalizungumzia Wabunge wawili; analizungumzia Mheshimiwa Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi na mimi Mbunge wa Kwela. Yeye akibanwa na wananchi, anatema ipeni Serikali CHADEMA mwone kama daraja halitatengenezwa. Mimi nikienda, najitahidi kutafuta *propaganda* kwamba, upembuzi yakinifu unaendelea kufanyika. Sasa majibu yamefikia mwisho, naomba Waziri, atambue hilo kwamba, majibu sasa yamefikia mwisho. Inatakiwa Serikali, itengeneze ili kuweza kumpiku mwenzangu anayetaka CHADEMA ichukue Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nilitaka nizungumzie tatizo lililopo la barabara za Jimbo langu la Kwela, Jimbo ambalo lina Jiografia za aina mbili tofauti; Ukanda wa Juu na Ukanda wa Chini. Ukanda wa Chini, unakumbwa na milima. Barabara hiyo inahitaji hela nyingi ambazo Halmashauri haiwezi kutengeneza. Kwa

hiyo, Halmashauri mara kadhaa imekuwa ikishindwa, inaandika maombi maalum kwamba, Serikali, itusaidie. Hivi karibuni, tuliweza kuiomba Wizara iichukue, lakini imeshindikana. Sasa tunaiomba Serikali, ione umuhimu wa kuetengeneza barabara hizo. Barabara ya Kalambanzite – Ilemba, inahitaji fedha nyingi, Barabara ya Miangalua – Chombe, inahitaji fedha nyingi. Bila kutengeneza barabara hiyo, hakutakuwa hata na maana ya barabara hii ya lami kwa sababu utakuwa umewatenga Wananchi wa Ukanda ule. Ili wananchi wafaidike na barabara hii ya lami ambayo tunaitengeneza, lazima uhakikishe kumekuwa na matoleo ya barabara yanayoingiliana, Ukanda wa juu na Ukanda wa Chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, alione hilo. Bahati nzuri majuzi tu, nimemwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kwamba, tunashukuru mlitupatia milioni 400, ambayo imetengeneza sehemu ndogo. Sasa mmeachia pale, badala ya kumalizia ile milioni 800 iliyobakia ile barabara itengenezwe, mmeachia pale. Maana mnataka hata ile milioni 400 mliyotoa, ionekane haijafanyika kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba leo hii wakati Waziri atakuwa anatoa majumuisho, aniambie, anataka hata zile Shilingi milioni 400 zipotee na wananchi waendelee kuteseka au ataongezea hela nyingine ili kukamilisha ile barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nililotaka kuzungumzia, ni lile ambalo amelizungumzia ndugu yangu Mheshimiwa Arfi, kwamba mkataba wa kutengeneza barabara kwa kupitia mradi wa *PMMR* umeleta mafanikio makubwa sana na mimi kwa barabara ile ya Tende - Muze kwa kweli imeleta mafanikio makubwa sana; japokuwa zipo taarifa kwamba karibuni ule mkataba utakwisha, tungeomba Serikali ifanye kila linalowezekana Mkataba ule uendelee ili kuimarisha ile barabara. Au vinginevyo, basi Serikali ifikirie kuiweka lami, maana ni kilomita 28 tu ukitoka pale Tende kwenda Muze ni kilomita 28 kama unatengeneza barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Namanyele; ni kidogo tu, unachepuka lami kilomita 28 utakuwa umeshakomboa wananchi wa Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kuendelea kusema mengi, lakini nirudie kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa kweli ni hodari, mchapa kazi na anatupa heshima kubwa katika nchi hii, heshima kubwa mno kwa jinsi anavyosimamia Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, hata wananchi wanakupongeza sana. Hongera sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, nami nichangie hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi. Awali ya yote, naomba niwape pole wote waliofikwa na msiba ndani ya Bunge

hili. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote mia kwa mia. Kwa nini naunga mkono? Naunga mkono kwa sababu zifuatazo: Kwanza, nashukuru sana Serikali kwa kumaliza ujenzi wa barabara ya kutoka Masasi hadi Mangaka kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu hawa waliopita Mikoa ya Kusini hivi majuzi, walipita kwenye barabara hiyo hiyo, lakini mwisho wake wakaleta kashfa, wametukejeli hapa kwamba tuna mawazo mgando, sijui barabara hii hawakuiona, sijui walivaa miwani za mbao, sielewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamepita kwenye barabara hii ya lami kutoka Masasi mpaka Mangaka, sasa wanakuja kusema Serikali ya CCM hakuna inachofanya. Tufanye nini zaidi ya haya mambo yanayofanyika? Lakini vilevile naunga mkono kwa sababu sasa Serikali imeshatenga pesa, mfadhili yupo *African Development Bank* pamoja na Serikali ya Tanzania kuanza ujenzi wa barabara ya kutoka Mtambaswala mpaka Mangaka. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Mtambaswala, Lukula, Chungu, Nanyumbu, Chipuputa, mpaka Mangaka, kaeni mkao wa kula, barabara ya lami inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naunga mkono hoja hii kwa sababu Serikali hii ya Tanzania pamoja na *African Development Bank*, pesa zimepatikana na wameahidi

kujenga barabara ya kutoka Mangaka mpaka Tunduru. Mungu atupe gunia la Chawa?

**MBUNGE FULANI:** Nashangaa!

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Haya ndiyo maendeleo tunayoyataka na ndugu zangu Wilaya ya Nanyumbu wapiga kura wangu neema imetufikia, tutakuwa na mtandao mkubwa wa barabara za lami ndani ya muda mfupi Wilayani Nanyumbu. Hongera sana Wizara ya Ujenzi, kwa kweli mmetuona kwa jicho la huruma kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nina machache ya kuzungumza ambayo ni changamoto Wilayani Nanyumbu, la kwanza, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi wakati wa kampeni ya ujenzi wa barabara ya kutoka Nagomba mpaka Nanyumbu, tayari kuna majumba yameshawekewa alama ya ‘X’, hii inaonyesha kwamba tayari mambo yako jikoni yanaiva. Hivyo, naiomba Serikali iharakishe ujenzi wa barabara hii pengine katika mwaka ujao wa fedha ili mtandao wa barabara za lami Wilayani Nanyumbu uzidi kuongezeka na kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Vilevile wananchi hawa waliopo kwenye barabara hizi kutoka Mtambaswala, Mangaka, mpaka pale mpakani Mwalumesule ambao wamewekewa alama za ‘X’ na ile barabara ya Nangomba mpaka Nanyumbu ambao wamewekewa alama za ‘X’ naomba sana Serikali ifanye haraka iwezekanavyo

kuwalipa wenye majumba haya fidia ili waweze kutafuta maeneo mengine ya kujenga nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, daraja la mto Lukwamba, kama kuna kero inanisumbua Jimboni kwangu, ni Ujenzi wa Barabara juu ya Mto Lukwamba, ambayo ipo kwenye Kata ya Napacho, kwenye Kijiji cha Mpombe. Kila mwaka wa fedha barabara hii inatengewa pesa kidogo, lakini hata hizo kidogo huwa hazipatikani, na mwaka huu wa fedha 2012/2013 daraja hili limetengewa fedha Shilingi milioni 190. Naomba sana Mheshimiwa Waziri usiuweke Ubunge wangu rehani. Kila ninapokwenda Mpombe, kitu cha kwanza naulizwa, daraja hili litajengwa lini? Kweli ukienda pale utawaonea huruma wakati wa masika; wanakatika kabisa, hawaendi Wilayani, hawaendi Zahanati pale Mburusa, wanakaa tu wanatumia madawa ya kienyeji badala ya kwenda hospitali.

Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, tena sana, najua wewe ni msikivu, wananchi hawa wa Mpombe wajengee hili daraja haraka iwezekanavyo katika mwaka wa fedha huu ujao. Najua Shilingi milioni 190 haiwezi kumaliza daraja, lakini hata ukionyesha dhamira ile kwamba kuna kitu kinaendelea pale, nadhani wananchi hawa wa Mpombe wataishukuru Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kuna daraja la Mto Lukwika pale kati ya Mpwahiya na Chimika. Mto huu ni mkubwa sana, Halmashauri ilijaribu pale mradi wa *TASAF* naona hakuna kilichoendelea. Naomba sana, tena sana, daraja hili najua ni la Halmashauri, lakini

naona hawawezi kulimudu. Kama Serikali inaweza kulichukua hili daraja, mimi ningeshukuru sana, wananchi wangu wa pale Mpwahiya, na Chimika na maeneo mengine ya Kata ya Napacho wanaweza kupita kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Njwayo alizungumzia kuhusu barabara ya Ulinzi. Naomba nichangie kidogo kwa kweli kwamba barabara hii imesahaulika. Imesahaulika kwa sababu labda urafiki wetu na Msumbiji ndiyo unaofanya hasa barabara hii isahaulike. Lakini huwezi kujua kuna siku pengine mambo yanaweza kubadilika, tukahitaji hii barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imesahaulika hasa kutoka Marumba mpaka Wanika, kupitia pale Nambunda, kuna mito mingi haina daraja. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri angalau upite siku moja uangalie uone ni kitu gani ambacho mimi nazungumzia. Lakini vilevile kuna daraja juu ya Mto Mbangala kutoka Lipupu kwenda Mtawatawa, kuna daraja juu ya Mto Mbangala kutoka Maratani, Mehiru mpaka Chitowe na kuna daraja vilevile linatakiwa kutoka kwenye Mto Miesi kati ya Ngalole na Mbunju. Lakini vilevile tuna shida ya daraja juu ya Mto Mbangala ambao kutoka Mbangala Mbuyuni kwenda Nantona, maeneo haya kwa kweli wakati ya masika hayapitiki. Kuna matatizo makubwa sana, mito inajaa na wananchi wanakuwa wamekamatwa kabisa, hawawezi kwenda upande wowote kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Kwa kumalizia, naomba nirudie tena kusema kwamba nashukuru sana, naunga mkono hoja hii. Lakini naomba hizi barabara kutoka Mtambaswala kwenda Tunduru, basi wananchi wa Nanyumbu tuipokee kwa mikono miwili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukupa pole kwa kufiwa. La pili, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hii Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa sababu Waziri wa Ujenzi wakati anasoma ripoti yake, kwa kweli mimi imenifurahisha kuona kwamba katika Taifa letu la Tanzania sasa hivi na sisi tunaweza tukasimama tukasema sehemu ambayo tunafanya vizuri ni Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, nakupongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Pia mwaka 2011 nimeuliza swali langu hapa la barabara ya kutoka Nyololo, kwenda Kibao na ya Mtwango mpaka Mgololo, na nilitoa sababu za msingi kwmaba ile barabara ni ya muhimu sana. Bahati nzuri wakati napitia kitabu cha Waziri hapa, nimeona ile barabara wameiweka kwenye *plan* kwamba mwaka huu itafanyiwa *feasibility study* pamoja na *details design*. Lakini kuna mambo hayajanifurahisha sana, sijui umepata ushauri kwa wataalam! Kwa sababu sijui ni *typing error* au ni kitu gani! Nimeona pale imeandikwa kwamba itafanyiwa *feasibility study* kwenye kilomita kumi. Sasa mimi nikawa najiuliza, hizi kilomita kumi ni za wapi? Kwa sababu zile barabara hazina kilomita kumi, ina kilomita 94.

Sasa Mheshimiwa Waziri hizi details inabidi labda afanye marekebisho kidogo. Kufuatana na taarifa sahihi ni kwamba, ile barabara ya kutoka Nyololo kwenda Igohole, kwenda Kibao, Mtwango mpaka Mgololo ina kilomita 94.

Kwa hiyo, fedha iliyotengwa hapa, nimekuta ni fedha kidogo sana. Imetengwa kama Shilingi milioni 65. Sasa sidhani kama kwa Shilingi milioni 65 zitatosha kufanya *feasibility study* pamoja na *detail design.* Sidhani kama ni hivyo! Lakini nadhani wataalam wapo na kama wametoa *data* ambazo siyo sahihi na *engineer* wa *TANROADS* Iringa mimi namfahamu, itabidi nimwulize kwa sababu yeye kwenye *RCC* tulipitisha. Sasa hii *detail* siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninachompongeza Mheshimiwa Waziri ni kwamba ameshaingiza kwenye kiwango cha lami, hilo ni suala la msingi sana kwamba hata wananchi wa Mfindi sasa hivi wanasikia, na sisi hiki kitabu tunakitunza na tutafanya *follow up* na ukiangalia kwamba barabara nyingi hapa zinasomwa, umejitahidi katika Tanzania Mikoa mingi sana wanakusifia kwamba umefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *presentation* ya Mheshimiwa Waziri ni *presentation* moja ambayo nimeiona kwake ambayo ni ya kitaalam kidogo. Amefanya *presentation* pamoja na kuonyesha kwenye *TV,* tunaona kwamba kule amefanya hivi, kule amejenga madaraja yanaonekana, kwa hiyo, ni *evidence*

ambayo mtu anaweza akaiona. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Sasa hizo *evidence* tulizoziona kwa wenzetu, mwakani nataka nione Mufindi. Nataka nione Mufindi ile barabara na sisi utaonyesha *evidence* kwamba barabara ya Nyololo kwenda mpaka Mgololo iko vile. Tusipoiona kwa kweli ndugu yangu Waziri nadhani tunaweza tukakupa mpaka uwe unaishia huku, usikanyage kwetu na mimi sipendi niseme hivyo kwa sababu nakuamini katika utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri, Naibu Waziri anapita kila siku kule, anakufahamu vizuri, kwa hiyo, atakupa *information* sahihi. Mimi sipendi *information* ambazo siyo sahihi, na wewe ni mtu wa *information* sahihi, nimeshakuona kwa sababu *evidence* zako ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kule kwangu kuna barabara zile za Mkoa ambazo zinasimamiwa na *TANROADS.* Naweza nikasema *TANROADS* Iringa wanazipitia zile barabara, kwa mfano kuna barabara ya kutoka Mbaramaziwa mpaka kwa Twanga, ile barabara inatengenezwa na *TANROAD*. Lakini utengenezaji wake ule, mimi bado sijaufurahia kwa sababu sisi kijiografia Jimbo la Mufindi Kusini, jiografia yake ni kwamba hali ya hewa ni ya mvua mvua. Kwa hiyo, sasa ukianza kuweka kifusi cha udongo, hapa hujafanya ukarabati. Kwa sababu kule inabidi uweke kokoto, ukiweka udongo, unakaa miezi mitatu mitatu, babarara imeshaharibika tena. Sasa utakuwa umefanya kazi bure, unaingia gharama kubwa, lakini

matengenezo yake hayakidhi haja, kwa sababu ya hali ya hewa ya unyenyevu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri napendekeza kwamba masuala ya udongo kule achana nayo, utakuwa unapoteza gharama. Weka kokoto. Ukiweka kokoto utakuwa unafanya ukarabati sahihi. Kwa hiyo, nimeona nikwambie kabisa kwa sababu kuna mfano wa barabara hii ya kutoka Nyololo mpaka Igowole, mpaka sasa hivi imeharika, haipitiki kabisa na bahati nzuri sasa nadhani kule kuna watu wanaanza kufanya matengenezo, lakini yale matengenezo usiweke tena udongo, utakuwa umefanya kazi bure. Sisi mvua ni kila wakati inanyesha kule.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna barabara moja ya kutoka Kasanga mpaka Mtambula, na yenyewe hivyo hivyo usiweke udongo, uweke kokoto. Ukiweka kokoto unaweza ukafanya ukarabati wa mwaka mmoja ukakaa hata miaka mitano. Kwa sababu ukishaweka kokoto itakuwa inapitika, lakini ukiweka udongo, maana yake kila baada ya miezi sita tutakuwa tunalalamika tunasema barabara imeharibika. Hilo nimeona la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nimeliona, ni zile sheria za barabara. Zile sheria za barabara bado zina matatizo kwetu, matatizo ni kwamba, mtu anaruhusiwa kujenga mita 22.5 au mita 30 na katika sheria inasema kwamba kama barabara imemfuata mtu, anaweza akalipwa na kama mtu ameifuata barabara, hawezi kulipwa. Sasa wananchi wengi sana, hususan kwenye Jimbo langu, bado

hawajaelewa vizuri. Sasa nilikuwa napendekeza, kwanini Wizara yako isiende baada ya kuja hapa, sisi Wabunge tunasomewa hiyo sheria; kwanini usifanye kuwafundisha wale wanavijiji upite kwenye ile barabara ambayo inapita, mtoe elimu kwa wananchi, mfanye mikutano, mwaelekeze ili mnapofanya kazi kusiwe na mgongano, mtu aelewe kwamba analipwa au halipwi? Halafu kuna suala lingine linalojitokeza, kwa mfano, uliweka 'X'. Kule kuna waungwana, watu ambao ni waungwana ni waelewa, walitoa nyumba zao wenyewe. Sasa wale waliotoa wenyewe, unasema huwalipi. Sasa kigezo hapo watu hawaelewi. Sasa wewe mtu amekiri sheria yako, na akafanya kwa vitendo; badala ya kumpa na *bonus* umwongezee kwa kukiri, sasa wewe unasema humlipi kabisa. Sasa hapa pataleta matatizo. Mimi nilikuwa nafikiria hiyo sheria hebu iangalie vizuri Mheshimiwa Waziri inawezekana kwa hiyo sheria, inabidi yule aliyeitii umpe *bonus,* yaani umlipe na *bonus* juu kwa sababu ametii sheria. Lakini ukisema unamlipa yule anayeleta kiburi, halafu unabomoa ndiyo unasema unamlipa, tena mimi naona hapo, sheria hebu iangalie vizuri Mheshimiwa Waziri, wale wanaoitii na wenyewe waweze kulipwa. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo naliona, kwa mfano, kutoka Mtwango kwenda mpaka Mgololo kule, sisi tuna kilimo kikubwa sana cha umwagiliaji. Bahati mbaya hata kwenye vitabu vya Wizara ya Kilimo sijaona wanataja umwagiliaji kule bonde la Mgololo, nadhani ni vizuri sana Mawaziri muwe mnatembelea sehemu.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna mradi mkubwa sana wa umwagiliaji kule ambao hii barabara ya lami ikienda kule Mgololo itakuwa ni msaada mkubwa sana kwa Taifa hili kwa sababu kilimo cha umwagiliaji bila barabara huwezi ukafanya kitu. Hilo nimeona ni suala la msingi nikwambie. Vilevile barabara za kule, magari makubwa yanapita kwa sababu tuna viwanda vingi sana, vile viwanda sidhani kama Mheshimiwa Waziri ulishapita kule ukaviona, kwa sababu nimeona barabara nyingi sana umejenga, lakini ukijenga sehemu nyingine naona hata kiwanda hakuna. Sasa kwanini usiwe unajenga huko kwenye viwanda ambako kunaongeza uchumi, kuna watu wengine wanafuga ng'ombe tu, wamepewa barabara ya lami, lakini sisi tuna viwanda vizito, hakuna barabara ya lami? *(Makofi)*

Kwa mfano, kule kwetu ukiangalia kuna kiwanda cha Chai...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Ni kiwanda kikubwa sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, maana yake…

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Kigola. Sasa namwita Mheshimiwa Desderius John Mipata na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya ajiandae na Mheshimiwa Max pia ajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami nitangulize kumshukuru Mwenyezi Mungu na wana Jimbo la Nkasi Kusini kwa kunichagua. Naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo tumekuwa tukitekeleza barabara hii ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga. *Speed* kwa kweli inaridhisha na kazi inaonekana. Tungeomba kipande kile cha kutoka Sumbawanga kwenda Kanazi kwenda Kibaoni kwa kweli hela ziongezeke. Nimeona katika bajeti hii tumetengewa Shilingi bilioni 6.4. Mradi huu ni mkubwa, ulitengemewa kwisha mwaka 2013, lakini sasa kama itakuwa inatengwa hela kidogo kidogo namna hii, itakuwa hasara kwa Taifa vilevile, kwa sababu wenzetu watakaa muda mrefu, watengenezaji wale na watatutoza pesa nyingi. Nashauri nalo hili, *speed* iongezeke na pengine hela ziongezewe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini iko barabara ya kwenda Kasanga nayo inakwenda vizuri, isiishie Kasanga tu, tungefikiri ifike Nakasesha hiyo barabara ya lami, ingetusaidia sana kutuunganisha Mkoani.

Mheshimiwa Spika, tunapokuja Namanyele, ukiishia Namanyele ukaenda Mpanda, bado hujasaidia sana ukanda ule. Ukituunganisha Kirando,

ukagusa tu Ziwa Tanganyika, pale jirani na Kirando kuna bandari nzuri inajengwa Kipili na tunafanya biashara na nchi zote za kule kwa maana ya *Congo DRC*, Rwanda na Burundi kupitia Kirando. Kwa hiyo, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza pia wazo ambalo limejitokeza hapa kwamba, tunaanza tena kujenga barabara kutoka Kizi kuelekea Mpanda na kwingineko. Hili wazo ni zuri sana na litatufungua vizuri mno. Lakini nigeshauri jambo lingine. Tunapozungumzia barabara hizi za Taifa, barabara zetu za Mkoa ni za muhimu. Barabara hii ambayo nimeitaja ya kutoka Namanyele kwenda Kirando iko chini ya ule mradi wa *PMMR* na utekelezaji ni mzuri sana, lakini muda umekwisha. Sasa kama hatuwezi kupata *replacement* nzuri ya kufanya hiyo kazi, itatusumbua.

Mtandao mwingine wa barabara katika Mkoa, nashukuru kusema kwamba vijana wetu wa Mkoa wanafanya vizuri, barabara zinapitika vizuri, lakini tatizo liko kwenye barabara za Halmashauri. Nina barabara mbili; Barabara ya Kitosi - Wampembe kilomita 67, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaifahamu vizuri sana, amewahi kupita kule na wanakusalimia wanasema uliwaahidi kwamba utawatembelea. Wangependa ukawatembelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini iko barabara nyingine ya Kana - Kala kilomita 67. Barabara hizi ziliikwishaishinda Halmashauri kwa asilimia 100 na Mkoa ulishakubali kimsingi kabisa kwamba, haziwezekani na zinakwenda kwenye maporomoko ya Ziwa Tanganyika. Huko Ziwa

Tanganyika maeneo yale hayana mawasiliano ya simu, hayana miundombinu ya afya, na pia matukio ya ujambazi yameshamiri kule. Kwa hiyo, matatizo ni makubwa.

Kuna kijiji kimoja kinaitwa Kijiji cha Msamba, wamevamizwa zaidi ya mara tatu kwa mwaka huu. Kuna kijiji changu kingine kiko pale Kala, wamevamiwa zaidi ya mara nne katika mwaka huu. Hakuna *access* ya barabara wala mawasiliano. Kwa hiyo, barabara hizi mtusaidie. Halmashauri kimsingi imeshindwa.

Nimeshughulika mimi kama Mbunge wao kwa kuiandikia Wizara barua, kwa kuandika maswali, na nimejibiwa vizuri tu kwamba nenda uishawishi Halmashauri yako itume maombi maalum. Tumetuma maombi maalum na mwezi wa Tatu niliandamana na Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mbunge mwenzangu tukakwama, tukalala njiani siku mbili. Nikaja Bungeni hapa nikalia, nikasema; kwa hiyo, ndugu zangu nataka niseme tu kwamba, hatuna namna nyingine yoyote ya kuhudumia barabara zile, kama neema haitoki hapo kwako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri, tumeona unafanya kazi vizuri sehemu zote, sasa eneo hili ndiyo maana nikasema ndiyo *the most remote area* katika Tanzania. Ni eneo ambalo limeachwa na kila kitu. Hakuna barabara, hakuna mawasiliano ya simu, magonjwa ndiyo yametapakaa, watoto *under the age of five* wanakufa wengi, akina mama wajawazito wanakufa wengi kwa sababu hakuna vituo vya afya. Kwa hiyo, ukiwasaidia barabara hiyo, utakuwa umetusaidia.

Mheshimiwa Spika, japo ziko barabara nyingi hapa katika Wilaya ya Nkasi na Jimbo langu, lakini kama kweli tuna huruma na wanyonge ambao hawana msaada kwa sasa na nasema tuwa-*promote* watu kwa kuwapa barabara hata moja kati ya zile nilizozitaja ili kufungua eneo zima la Ziwa Tanganyika, tungeweza kuwasaidia kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado nina changamoto nyingine. Katika barabara zetu za Mkoa, iko barabara ambayo inaambaa kutoka Nkundi - Kate Makao Makuu ya Jimbo, lakini pia inaunga Namanyele. Barabara ile ni ndefu na fedha kidogo inayotengwa haitusaidii sana. Ingeongezewa jitihada kwa kweli ingeweza kupitika vizuri kwa sababu inaunganisha maeneo ambayo yanashamiri sana kwa kilimo. Ukisikia Rukwa tumezalisha mahindi ni katika maeneo haya. Sasa hivi tunasema tutakuwa na ziada, tumezalisha zaidi ya tani Sh. 200,000/=. Tutazipeleka wapi, barabara haipo? Kwa hiyo, kasi ya utengenezaji wa barabara ungeweza kutusaidia.

Kadhalika, iko barabara ambayo inasimamiwa na Mkoa kutoka Lyazumbi kwenda Kabwe. Barabara hii bado siyo nzuri sana, ingeongezewa. Imepewa fedha chache sidhani kama itaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo narudia, barabara yangu ya Kitosi – Wampembe na Nkana – Kala ndiyo inashikilia Ubunge wangu, ndiyo inashikilia Chama cha Mapinduzi na wanamsalimia sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wanaomba

awatembelee, kwa sababu aliwahidi kwamba atawatembelea. Naomba hilo. Nimelishughulikia kwa kiwango cha upeo wa Ubunge wangu kwa sababu nimeandika barua, nimemwona Mkurugenzi wa barabara nchini. Nilieleza hapa juzi kwamba, nimekwenda TAMISEMI, sasa uwezo wangu kama Mbunge umekwisha, labda nitumie ngazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kutumia Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Magufuli najua ni msikivu na mchapa kazi na kusema kweli Mungu atakuandalia mambo makubwa zaidi. Unafanya vizuri katika nchi hii. Unatuinua, unatufanyia vizuri, lazima tukusifu, japo ile barabara yangu haijatekelezwa, lakini lazima nikuunge mkono. Nitaiunga mkono bajeti yako kwa sababu najua nikisema utafanya. Kila Mtanzania akipita anaona kazi zako zinapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, wamesema ombeni bila kuchoka. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Nichukue nafasi hii kuwasalimia Waheshimiwa Wabunge. Bahati mbaya sikuwepo, nilikuwa nauguliwa na mume wangu. Nashukuru kwa maombi yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nichukue fursa hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha

kuwa hai mpaka leo na kuwepo hapa, mimi pamoja na Wapiga kura wangu wa Morogoro Kusini Mashariki. Napenda kuwaambia kwamba sasa nimeripoti. Walikuwa wananiombea sana niweze kumwuguza mume wangu vizuri apate nafuu nije Bungeni niwatetee. Namshukuru Mungu kwamba nimekuja leo, ndiyo siku Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anawasilisha bajeti yake, kwa sababu Morogoro Vijijini wamekuwa ni masikini wa kutupwa kwa sababu hakuna miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwanza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake kwa bajeti nzuri. Naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuonyesha juhudi kubwa ya kuhakikisha kwamba, Watanzania sasa tunaweza tukasalimiana kutoka Mtwara – Kilimanjaro – Mara - Bukoba na kuingia Uganda. Ni kazi kubwa ambayo imefanyika, ambaye hataki kutambua hilo, basi ningeomba akamwone daktari wa macho aweze kumpa miwani ili aone hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi, napenda kusema kwamba nimesikitishwa kidogo baada ya kuangalia majedwali kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kwamba, Morogoro Vijijini tuna barabara moja tu ambayo imeangaliwa, nayo ni barabara ya kutoka Bigwa – Kisaki.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini yanayojengwa kwenye eneo la

Mvuha. Lakini wakati wa mvua, hii barabara haipitiki. Kuna maeneo mengi sana ambayo ni makorofi, nilitarajia kwamba leo hii ningekuta kwamba kwenye hili jedwali tumewekewa na sisi mgao wa kujenga ile barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba Mheshimiwa Waziri ananisikia na ninaomba kabla sijaunga mkono hoja, atakapokuwa anahitimisha aniahidi kwamba, atakuja asafiri na mimi mpaka Kisaki halafu aone utajiri mkubwa uliopo Morogoro Vijijini. Sasa, kwa sababu tuko milimani, hakuna mtu anayetaka kutuangalia.

Mheshimiwa Spika, tuna Karafuu nyingi, Mdalasini mwingi, tuna iliki nyingi pia tunalima mazao mengi sana kule Morogoro Vijijini hasa ambayo ni mbegu za mafuta. Lakini wananchi wanakufa maskini kwa sababu walanguzi wanaokuja kule wananunua na inabidi waajiri wapagazi kubeba yale mazao wanayonunua. Kwa hiyo, wananunua kwa bei wanayoitaka wenyewe, ukikataa hawatanunua na hivyo utabaki nayo.

Mheshimiwa Spika, ukiugua ni shida, hasa kama *ambulance* moja ambayo inafika kule kwa shida sana imekufa. Kule Kisaki magari ya abiria yanatoka mara moja tu usiku kuja Morogoro Mjini na yanarudi usiku. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri naona ananisikia kwamba, kule kuna utajiri mkubwa. Kuna madini na Mbuga ya *Selous* inafika mpaka kwetu kule. Sioni kwanini mtu akitaka kwenda *Selous* kwa urahisi wakati wa mvua apitie *TAZARA* ambayo wakati mwingine haifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri alisikie ni kwamba, nashukuru ameiona barabara ya kutoka Ubena – Ngerengere tu, lakini Morogoro Vijijini inaanzia Ngerengere. Kuna barabara ya *TANROADS* kutoka Ngerengere kwenda Magogoni inavuka na kuelekea Kisaki kwenye daraja moja tu tena ambalo tumewekewa na Jeshi. Sasa ile barabara wakati wa mvua haipitiki. Ile barabara inaunganisha Morogoro Vijijini na barabara kuu bila kupitia milimani, kwa sababu magari makubwa yenye mizigo mikubwa hayawezi kupanda mlima Chamananyi pamoja na Mlima Ng'alo, inakuwa ni matatizo. Mlimani wakati mwingine mvua ikinyesha magari hayapiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri anisikie kuhusu hilo kwamba, ile barabara tunaihitaji itengenezwe, kuna maeneo korofi na kuna maeneo yanayohitaji madaraja.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie madaraja katika Wilaya ya Morogoro Vijijini. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameliona daraja la Mto Ruvu linalounganisha Kibangile na Msitu wa Kimbosa. Lakini Morogoro Vijijini siyo kwamba ni ile barabara tu, kuna maeneo mengine ambayo yana matunda kwa wingi, kuna shule hazina Walimu, kuna hospitali hazina wahudumu na kuna wakati mvua inapozidi na Mto Ruvu ukifurika, unaanzia kule kwetu. Sasa mkitukorofisha, tutaharibu mazingira, halafu Dar es Salaam mtakosa maji.

Mheshimiwa Spika, kuna daraja la Mto Ruvu linaloitwa daraja la Gizigizi. Hili daraja kila siku wananchi wamekuwa wakipata ahadi, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini haina uwezo wa kujenga lile daraja ili tuweze kuchochea maendeleo ya uchumi katika maeneo yale. Lile daraja limeshafanyiwa upembuzi na *BOQ* na linahitaji Shilingi milioni 189 tu.

Mheshimiwa Magufuli ninakuomba, lile daraja likijengwa wale wananchi wataacha kusema kwamba wako Tanganyika. Siku nyingine ukifika kule inabidi uvue nguo upite upande mmoja na wanaume wanapita upande mwingine uweze kuvuka mto kwa kushikwa mkono na mtu aliyevaa jiwe kusudi msisombwe na maji. Hivyo, Walimu hawaendi kwenye Shule kule, Wauguzi hawaendi pamoja na kwamba tumejenga *Dispensary* kule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba, pamoja na kwamba haiko kwenye *TANROADS* Serikali iangalie namna ya kusaidia wale wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine ambalo linaunganisha Makao Makuu ya Mnvuha na Ngerengere, ni eneo la Tononguo. Nasikitika kusema kwamba siyo kitambo sana kuna familia moja imetumbukia mle na mtumbwi wao mdogo mpaka watoto wawili wameliwa na Mamba. Ule Mto Ruvu ni mkubwa, Halmashauri ya Morogoro Vijijini haina uwezo wa kujenga daraja pale. Namwomba Mheshimiwa Magufuli awaangalie wale akina mama wanaotakiwa kuvuka pale kupeleka watoto kliniki na kwenda

kujifungulia katika *Dispensary* ya Tononguo, pamoja na watoto wanaovuka kwenda Sekondari ya Tononguo kwa sababu ni Kata moja ambayo imekatika katikati kutokana na ule mto.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni rahisi kujenga upande huu ambako huhitaji kuvuka na mtumbwi, kila Mhisani anayekuja anajenga upande mwingine wa mto ule. Kwa hiyo, wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki wamenituma wakiomba kwamba, Serikali iwaangalie kwa madaraja hayo mawili; daraja la Gizigizi linalounganisha Tarafa ya Mkuyuni ambako ndiko kuna Hospitali na Shule pamoja na Vijiji vitatu vya Kata ya Kinole, Lung'ala na Ludewa pamoja na Mbehoni.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kuomba kwamba, kuna barabara nyingine ambayo inakwenda kule milimani ambako wananchi wanalima Karafuu nyingi sana kuliko hata Zanzibar, lakini haiuziki. Hata mimi nina shamba kule, sivuni kwa sababu nikivuna nitamuuzia nani anayefika kule? Mimi mwenyewe siwezi kubeba kichwani. Kwa hiyo, naomba ile barabara ya kutoka Madamu – Kinole iongezewe sasa urefu kutoka pale Kinole - Tandai ifike mpaka Tegetero – Kibogwa ambako kuna Karafuu nyingi sana ambayo inaweza pia ikaongeza uchumi wa wananchi wa Morogoro pamoja na kuleta *foreign currency. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, nafikiri Mheshimiwa Waziri amenisikia, namkaribisha twende naye Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nijiunge na Wabunge wenzangu katika kuwapa pole wewe na Mheshimiwa Wasira.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kusema kwamba, naomba niipongeze Wizara ya Ujenzi. Katika kipindi cha miaka 10 kama tunavyofahamu wote, mbali ya kwamba tulikuwa na mporomoko wa uchumi wa Dunia, lakini Wizara hii katika kipindi cha miaka 10 kazi iliyofanya ni kubwa. Naomba niwapongeze wafanyazi wote wa Wizara hii kwa kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kusema mengi, lakini nilikuwa napenda kutoa ushauri. Cha kwanza kabisa, nafikiri Mheshimiwa Waziri atusaidie hapa, kwamba, kama *TANROADS* iko Mikoani, lakini nilikuwa nafikiri kwamba kingeundwa chombo ambacho kinashughulikia Vijiji. Kitu kama *TANROADS* Vijijini, kwa sababu kule Vijijini ndiko kwenye shida, licha ya kwamba ndiyo kwenye uzalishaji, shule zetu nyingi ziko kule, na sasa hivi tunahangaika na hizo Zahanati. Lakini ninachosema ni kwamba, *TANROADS* mpaka uifuate kwenye Mkoa, kule vijijini kidogo kuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya hatutoi elimu ya kutosha kwa viongozi wetu kwa sababu hapa kwenye hii mifuko ya barabara, kuna barabara za Serikali Kuu, barabara za Mikoa, barabara za *TANROADS* na kuna

barabara za Halmashauri. Sasa ule usimamizi watu wanapopeleka maombi ya kutengeneza barabara huenda wengine hawajui hata waombee wapi. Sasa nilikuwa nafikiri kwamba huu wigo wa *TANROADS* kidogo ungepanuka. Kama inawezekana ikawepo *TANROADS* Vijijini, tungeshukuru zaidi ambapo itakuwa chini ya Halmashauri na Waheshimiwa Madiwani wangeweza kutusaidia pale.

Mheshimiwa Spika, narudi kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala letu la Geita Mjini pale. Leo ni mwaka wa saba, nafikiri anajua mazingira yetu ya pale kwa sababu ya ule udongo mwekundu. Tuliomba toka mwaka 2005, tumeomba mwaka 2010 na sasa hivi tunarudia kuomba tena. Tungeomba suala hilo lirekebishwe kwa sababu pale ni kama vile tumezidiwa kidogo. Wakazi wa pale mjini peke yetu tuko zaidi ya 600,000, na ujue kwamba kwa sababu kuna uchimbaji mdogo na kuna migodi, ina maana pale matumizi yanakuwa ni makubwa mno. Sasa hizi *drainage systems* na hali halisi iliyopo pale wakati wa masika ni shida, na inapokuja kiangazi nayo kuna shida yake. Kwa hiyo, mimi ningeomba kwa niaba ya Wakazi wa Geita, nimkumbushie Mheshimiwa Waziri, ni kama kilomita nne au tano pale mjini. Naomba sasa atukumbuke.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi vilevile ningependa kumshukuru *Engineer* wa *TANROADS* Mkoa wa Mwanza. Wakati inajengwa barabara ya Chato – Usagara – Mwanza wale Wakandarasi walitoa makalvati ambayo ni ya *concretes*. Yale makalvati hayabebeki, bahati nzuri Halmashauri za Wilaya ya

Sengerema na Geita tumechanga mafuta lita 300. Msaada tunaoomba kwenu, sisi hatuna uwezo wa kuyanyanyua yale, hata tukienda watu 1,000 hatuwezi kuyabeba. Tunachoomba, tutafutiwe *Winch* au *Crane*.

Mheshimiwa Spika, dada yangu Mheshimiwa Nkya amezungumza; ukija kule Geita hasa Vijijini mito ile ni mikubwa sana, masika yote watoto hawaendi shule. Tumejenga Shule za Msingi, Sekondari, sasa inapofika masika, watoto wanakaa nyumbani kwa sababu ya madaraja. Sasa yale makalvati yaliyotolewa kwenye ile barabara ya Geita yenye urefu wa mita mbili au tatu ambayo yametengenezwa kwa *concrete* yanaweza kuokoa shule nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nina matatizo kuhusu mpaka wa Sengerema na Geita; panaitwa Idoselo pale Kwezera, kwenda hapa kwa dada yangu Jimbo la Busanda ni umbali wa kilomita 25. Pale ni jaruba tupu la mbuga za mpunga. Lakini ukiangalia pale watu wamejijengea madaraja ya kienyeji ya magogo, wanatoza nauli kupitisha magunia ya mpunga kwa baiskeli. Kwa hiyo, hata kama Waziri utataka kwenda pale, lazima tukubebe kwenye pikipiki kwa sababu hakuna barabara.

Sasa mimi nilikuwa naomba kwamba kwa sababu makalvati haya tumepewa kibali na *TANROADS* kwa maandishi, tupate msaada aidha kupitia *Nyanza Road Works* au kampuni yoyote ile, yaje yanyanyuliwe, yapelekwe kule tulikoyaombea. Sisi hatuna makubwa, lakini naomba sana yale makalvati yapo pale, yamelala kwenye barabara ya Geita – Mwanza,

hayana kazi yoyote, na sisi tuna matatizo makubwa na mito yetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa kupitia Meza yako, nilikuwa naomba tu nitoe tangazo dogo kwa Wanageita hasa wale Wananchi wachimbaji wadogo wadogo wa Magwangala, na wananchi wote wa Geita kwamba, Naibu Waziri wa Nishati na Madini atakuwa Geita Jumamosi, nawaomba wakutane Nyakabale wakazungumze matatizo yanayowakabili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kuokoa muda. Sasa nimwite Mheshimiwa John M. Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaomba kutumia kwanza dakika mbili hivi kusema mambo ambayo yanahusiana na barabara.

La kwanza, leo nitalala vizuri kwa sababu ya habari njema ambazo nimeziona hapa kwenye gazeti la *Daily News* kwamba Muhimbili inatoa maneno mazuri juu ya Madaktari, na Moi wanasema wagonjwa njooni tunawahitaji. Leo nitalala vizuri na Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

La pili ambalo nasema lipo nje, ambalo nategemea nitalisema ni Pamba. Nawaomba wanunuzi wote wa Pamba wafike Sh.1,000/=, la sivyo wakulima watapata hasara na hawatalima mwaka

unaokuja. Msimamo unabaki pale pale kwamba bila buku hakuna Pamba.

La tatu, Serikali ihakikishe kwamba Bodi ya Pamba haiweki tena vikwazo nani anunue. Hakuna uhusiano wa vikundi na leseni ya kununua Pamba. Aliye na pesa anunue Pamba sasa hivi.

**SPIKA:** Sikusikia. Mtu mwingine asiige, maana yake siyo utaratibu. Hilo la kwanza, sawa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, sasa narudi kwenye barabara.

La kwanza, mimi naona kama Watanzania na ninaweza kusema kwa uhakika kwamba nilipokuwa nagombea Urais mwaka 1995 na mwaka 2000 niliona nchi hii jinsi ilivyokuwa ngumu kufika mahali popote, lakini leo tunafika karibu kila mahali. Hii tusiipongeze tu Serikali, lakini tujipongeze wote, yaani vyama vyote ambavyotumekuwa hapa katika kujaribu kusukuma kuhakikisha kwamba tuna miradi ya kutosha ya ujenzi wa barabara na tusiondokane na *push* hii, bali tuendelee hivyo hivyo lakini bila kusahau umuhimu wa reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikurudi nyumbani kwenye Jimbo langu, nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa vile vidaraja viwili, yaani Bukingwaminze, imo nimeiona kwenye *program* na pia Gamaroha nimeiona kwenye *program*.

Mheshimiwa Spika, pia nimeona fedha ndogondogo kusema kweli ulivyokuwa unasoma

hotuba ni kama umetugawanya sisi wote kidogo kidogo. Ni pipi pipi pipi kila mahali. Sasa labda tufanye mkataba mmoja na Serikali kwamba kama hizi fedha zimegawanywa kidogo kidogo, zisipoonekana, sisi wote tutaonekana wadogo sana na Bunge hili. Kwa hiyo, ni vizuri tufanye mkataba, Bunge hili na Serikali na Waziri Mkuu yuko hapa anasikia, kwamba hizi fedha za barabara Shilingi trilioni moja ambazo tutaidhinisha kesho, ziwe *ring fenced,* zitoke, isiwe maneno tu kwamba tumeweka hapa hivi na vile na kadhalika. Hiyo kuwekaweka haitajenga barabara. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nimesikitika kusema kweli kwamba kabarabra ketu kadogo ka lami peke yake katika Mkoa mpya wa Simiyu kutoka Mwigumbi – Maswa - Bariadi inafika mpaka Ramadi tunapewa Shilingi bilioni tano. Shilingi bilioni tano utafanya nini nazo? Halafu Shilingi bilioni 1.5 utafanya nini na hizo pesa? Mradi huu, Mheshimiwa Rais alikuja kule, tukampa kura kibao, akatuambia tuna barabara moja safi sana inakuja na kadhalika, watu wameanza, yaani ni kama vile unamwonjesha mtu tu, anapoanza kupata utamu, ndiyo unasema sifanyi tena. *(Kicheko/Makofi)*

Hapa ndugu yangu najua tatizo tulilonalo ni kama tulivyosema kwamba, ni afadhali hizi *sector commited* tuwe tunazizungumza kwanza, halafu mwishoni ndiyo tunazungumza bajeti yote. Kwa sababu kama tungekuwa tumezungumza kwanza, mimi ningekuwa mmojawao ambaye nisingekubali kabisa kuwa mradi pekee wa lami katika Mkoa mpya wa Simiyu kupewa Shilingi bilioni tano, halafu kwingine unaona Shilingi

bilioni 26 na kadhalika. Hivi kweli kutakuwa na stakabadhi ngapi katika mwaka mzima? Ni stakabadhi tu za Shlingi bilioni tano au huu mradi utasimama tena kama vile ulivyokuwa umesimama kwa muda wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja ni kwamba kila wakati hii miradi ikisimama maana yake gharama inaongezeka. Sijui utafanya nini, lakini kwa hali halisi wale Wasukuma wanaokusikia kusema kweli hapa hatujapata haki ambayo tulikuwa tunategemea tungeweza kupata.

Nashukuru kuna vipesa vidogo ambavyo vimetolewa katika sehemu nyingine za ukarabati, lakini hii barabara ya kutoka Bariadi kupitia Gambasingu na kuendelea Ngwanunzi, Sibiti mpaka Singida, mimi naona katika mipango inayofuata tungeiwekea umuhimu sana kwa sababu ndiyo barabara pekee ambayo itahakikisha kwamba Pamba yetu inafika Dar es Salaam kwa bei nafuu na watu wataweza kupata fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutoka Bariadi uende Shinyanga halafu uende Nzega ndiyo uanze kwenda Dar es Salaam, kusema kweli ni safari ndefu sana. Kwa hiyo, hili sikwambii ufanye leo, lakini kwa kuwa umeshaweka Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya Sibiti, njia ya kuweka *value for money* au thamani ya pesa ni kuhakikisha kwamba sasa hii barabara ya Bariadi – Gambasingu - Mwanhunzi mpaka Singida inaimarishwa ili iweze kutoa thamani ambayo tunastahili.

Mambo mengine ambayo ningependa kuzungumzia ni kwamba, kwanza, *TANROAD,* mfuko wa barabara wamefanya kazi nzuri sana na matunda tumeyaona. Ukiangalia bajeti hii mahali ambapo kweli tunaweza kukimbilia na tuna uhakika ni mfuko wa barabara. Lakini bado kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ambayo mimi naiona, ni hiyo sehemu ya *BOQ*. Mimi nilipokuwa nasoma, niliona watu walikuwa wanasona *Accountancy*, kuna *Financial Accountancy, Cost Accountancy* na kadhalika. Hivi hatuwezi kweli kupata *Ma-cost Accountants* ambao wataangalia *BOQ* hizi? Maana *BOQ* zinatuumiza na zaidi katika barabara za vijijini mtu unasema unataka kujenga hapa unaletewa Shilingi milioni 30, ukiangalia chini vizuri unajenga kwa Shilingi milioni 10. Hii ni *area* ambayo mimi nafikiri ni changamoto kubwa ili uweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, uliposema kwamba umepunguza gharama, lakini sijui umepunguzaje. Umepunguza gharama kutoka Shilingi bilioni 1.8 na sasa umetuambia barabara zetu zinaweza kwenda kwa Shilingi milioni 700 na ushee. Hii mimi siwezi kusema kama inawezekana, lakini ningeshauri Kamati ya Miundombinu iangalie ukweli wa jambo hili ili tusije tukajikita, tunaonekana kweli tuna bajeti kubwa, kumbe tunajenga barabara ambazo zipo chini ya kiwango. Kama kweli tunaweza tukajenga barabara kwa Shilingi milioni 700 na ushee na ikawa ni barabara yenye ubora unaostahili, kwa kweli hii ni pongezi na ninakupa mkono wa heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo naiona baada ya kutembelea miradi mbalimbali kama Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee,* ni utegemezi wa nchi moja kama mjenzi. Unakuta karibu, (sitaki kutaja nchi), lakini unakuta Wakandarasi wengi wanatoka nchi moja na mimi sishangai kwa nini baadhi ya nchi kama *European Union* hatupi fedha, kwa sababu hawataki kutoa fedha zao ili pesa zile ziishie tu kwa nchi moja ambayo inasemekana kama vile inapendelewa na nchi yetu kuweza kupata miradi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna hatari kwamba hawa Wakandarasi wanaweza wakaja pamoja, kwa sababu wanatoka nchi moja wakafanya *cartel* kwa ajili ya nchi hii. Kwa hiyo, ni kwamba utegemezi wetu unatumaliza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kibona, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusema machache kuhusu mjadala uliopo mbele yetu siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, napenda na mimi niungane na wazungumzaji walioanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa jinsi alivyowasilisha bajeti yake siku ya leo. Kitabu cha leo katika vitabu nilivyowahi kuvisikia na kuvisoma tangu nimeingia hapa Bungeni, kwa kweli

hiki kimetia fora. Kwetu sisi nyumbani Ileje Mbeya tuna msemo mmoja ambao watu wa Ileje wataelewa, unasema: "Mumumo Jikwicha", yaani watu wa namna hii tunahitaji kuwaombea sana, watu kama akina Magufuli. Tukipata akina Magufuli wengi wengi katika nchi ya Tanzania, tutatoka hapa tulipo na kufika mahali ambapo ni pazuri. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wako wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa bila kupoteza muda, niende kwenye bajeti. Wilaya ya Ileje katika Mkoa wa Mbeya na Nyanda za juu Kusini inaongoza kwa matatizo ya miundombinu na umaskini. Wilaya ya Ileje haijui, yaani wananchi wanaokaa kule ni wazee wa zamani na vijana ambao hawajatoka nje ya Wilaya ya Ileje, hawajijui lami.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 nimeuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri: Ni lini barabara ya kutoka Mpemba kwenda Isongole itajengwa kwa kiwango cha lami? Wananchi wa Jimbo la Ileje walikuwa wakisikiliza kwenye Redio na kwenye *TV*. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba wametenga Shilingi milioni 100 kwa ajili ya upembuzi wa kina na baada ya kukamilika, hatua za kutafuta pesa kwa ajili ya kujenga ile barabara zingeanza. Lakini leo kwenye kitabu hiki naona barabara ya kutoka Mpemba kwenda Isongole imetengewa Shilingi milioni 93.55 kwa ajili ya yale yale aliyosema kipindi alipokuwa akinijibu upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri unisaidie mimi mwenyewe niliyepo hapa na wananchi

wa Jimbo la Ileje wanaonisikiliza na watakaokusikiliza; Ni lini sasa upembuzi yakinifu wa kina na *terms* nyingine utakamilika? Tafadhali nakuomba uweze kulieleza sawasawa wananchi wa Ileje wapate kuelewa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Wilaya ya Ileje ina matatizo ya barabara, mvua zinazonyesha Wilaya ya Ileje, inawezekana ni Wilaya inayoongoza kwa mvua kuliko mahali pengine nchini Tanzania. Mvua zinaanza mwezi Novemba, zinaisha mwezi Agosti. Mwezi Septemba kunakuwa na jua, mwezi Oktoba kunakuwa na jua na mwezi Novemba mvua zinaanza tena. Halmashauri ya Wilaya ya Ileje haiwezi kutengeneza baadhi ya barabara ambazo ninaomba Mheshimiwa Waziri uweze kuziandika, na kwa kweli unisaidie na uwasaidie wapiga kura wa Jimbo la Ileje, ziingie katika mpango wa kuwa barabara za Mkoa.

Barabara hizo ni kutoka Ibaba, Katengele mpaka Isoko ambapo pana Hospitali Teule ya Wilaya. Wagonjwa kutoka katika Kata mbalimbali zipatazo saba wote wanapaswa kwenda kutibiwa katika hospitali ile. Miundombinu na mvua zinanyesha kwa wingi, utelezi, pikipiki zinashindwa kupita. Acha magari, pikipiki haziwezi kupita! Naomba barabara hizo ziweze kuchukuliwa, tumeshaziombea katika *RCC* Mkoani Mbeya, tafadhali na chonde chonde wasaidie wananchi wale maskini wanaopata taabu kupita katika barabara zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni barabara inayoweza kuwaunganisha wananchi wa Kata ya Ngulilokatika Wilaya ya Ileje kuunganisha kwenda

Wilaya ya Mbeya Vijijini ambapo huduma zao nyingi karibu zote 100% wanapata kutoka Mbalizi na Mbeya Mjini. Wananchi wale wako kisiwani. Tena nakuomba Mheshimiwa Waziri, siku moja utembelee Mbeya hususan Wilaya ya Ileje ili uweze kuyaona haya ninayoyasema. Wakati mwingine ni vizuri kuona kuliko kusikia.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara moja ambayo mwaka jana nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, anaonaje kwamba barabara hii iingie kwenye mpango wa kuwa kiwango cha lami? Mheshimiwa Waziri alisema: "Mheshimiwa Mbunge Kibona, haitawezekana kwa sababu tunaanza kwanza hizi zilizopo, na tukikamilisha, tunahamia nyingine."

Sasa ninachokuomba Mheshimiwa Waziri, barabara inayotoka Kasumulo - Kyela inakwenda mpaka hapa ambapo tayari imewekwa katika mpango wa kuwekwa lami pale Isongole. Ile barabara imejengwa miaka ya 1968, 1969, 1970 mpaka mwaka 1971 wakati ule Rais wa Malawi Kamuzu Banda wa Muyaya ambaye sasa ni Marehamu alipokuwa akichokoza, kwamba Mkoa wa Mbeya ni sehemu ya Malawi. Barabara ile ilijengwa na Wanajeshi, teknolojia ya wakati ule na sasa hivi ni tofauti. Barabara ni nyembamba, wakati ule zilikuwa zikipita gari aina ya *Land Rover 109.* Lakini sasa hivi maisha yamebadilika, tunahitaji mabasi, *Fuso* zimetengenezwa, watu wanahitaji kufika kule kusomba mbao na vitu vingine. Ninaomba barabara kutoka Kasumulo ipitiwe upya kwa sababu kuna milima ya ajabu ambayo gari haziwezi kupanda.

Ninaamini kwa teknolojia ya sasa hivi, kona zilizopo kule zitapunguzwa na kuwa chache. Nitakushukuru sana na ninakuamini, nimekuombea, nimesema hata lugha ya nyumbani kwamba *momumo jikwicha*, yaani kwamba watu wazuri kama hawa huwa hawadumu duniani, na ninyi ni mashahidi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tufunge wale wa Makanisani waombe kwa ajili ya Mheshimiwa Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa ajili ya nafasi hii, namkaribisha Mheshimiwa Wairi Ileje ajionee hali ilivyo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mama zako Wasabato wako hapa siku zote hizi, nadhani wanasikia, haya maombi watafanya. Ahsante sana, lakini tuiombee na Serikali yote.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa anayefuata ni Mheshimiwa Mkosamali na atafuatiwa na Mheshimiwa Koka.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie machache kwenye Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, huwa nafurahi sana ninapomwona Mheshimiwa Magufuli anapofukuza Wakandarasi ambao wanashindwa kuendelea na barabara vizuri. Nami nitakuletea Wakandarasi ambao wananiharibia barabara kule Kibondo ili uendelee kuwafukuza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini siungi mkono hoja hii kwa sababu ya fedha kidogo ambazo tumekuwa tunatengewa watu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, watu wa Kigoma tumekuwa tunadanganywa toka bajeti ya mwaka 2010/2011. Tuliambiwa mwaka 2010/2011 kwamba barabara ya Nyakanazi –Kibondo - Kasulu mpaka Kidahwe ilitengewa Shilingi bilioni sita ambazo hazikutoka. Mwaka 2011/2012 tulitengewa Shilingi bilioni 2.3, fedha hizo hazikutoka. Haya ni maagizo ya Wabunge wote wa Kigoma, hakuna cha CCM, *NCCR – MAGEUZI* wala CHADEMA. Barabara hii tunaihitaji Wabunge wote wa Kigoma. Sasa mwaka huu bajeti hii imetenga Shilingi bilioni 3.5, barabara ya kilometa 310. Hivi mnatujua sisi watu wa Kigoma au mnatusikia? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ndiyo ambayo magari yote yanayotoka Kigoma yanapita pale. Barabara hii inatuunganisha na nchi za Congo, Burundi, Rwanda, Mikoa ya Mwanza, Kagera na kadhalika, yote inaunganishwa na barabara hii. Lakini nimesikitika kweli nilipokuta Shilingi bilioni tatu. Hivi hamtaki Kigoma iunganishwe na Mikoa mingine? Mimi sina tatizo, tumeona barabara zinazokwenda Songea kutoka Masasi, safi sana, barabara za Rukwa vizuri, kwa sababu Mikoa hii ilikuwa imetengwa muda mrefu. Lakini sisi Kigoma, kwa nini mnatufanyia mambo ya namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara nyingine ya Kigoma – Kidahwe - Uvinza mpaka Tabora,

imetengewa fedha kidogo pia. Fedha hizi hazitoshi kwenye barabara ile. Ukiwa Kasulu, kuna barabara iliyounganisha Kasulu; ukiwa Jimboni kwangu Kibondo kuna barabara inayokwenda Burundi. Ukijenga ile barabara ni kilomita 30 tu ufike Burundi. Kwa historia, wote walikuwa wakitoka Kagera, Bukoba wanapita ile barabara Mabamba wanalala pale, ndiyo wanakwenda Burundi. Hamjatenga fedha za barabara zile. Kigoma hakuna barabara ambazo mmetutengea, hakuna fedha. Shilingi bilioni tatu siyo fedha ya kujenga kilomita zote hizi ninazozungumza hapa. Hizi ni fedha za kilomita tatu mpaka nne mkoa mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli watu wa Kigoma watakasirika mno! Hii imetuumiza sana na tumekasirika na tumeumia sana! Hatukutegemea kama mambo ya namna hii yataendelea! Lakini kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais pale Kibondo Mjini kilomita moja na nusu; hata kilomita moja na nusu ya Rais pale Kibondo Mjini mmeshindwa! Kwa nini? Hivi mmeona Mbunge wa Kilimanjaro anaongea hata mmoja leo? Nenda hata kwenye orodha pale, hayupo hata mmoja!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali, zungumzia habari zako, kwa sababu mimi nina orodha hapa.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Lazima tueleze ili watu waweze kuona mambo ya namna hii, namna gani yanavyotuumiza watu wa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye mambo mengine ya Kitaifa. *TBA* inapaswa kuongezewa nguvu,

inapashwa kupewa nguvu hizi nyumba ambazo zinajengwa kwenye Halmashauri zetu, hazina viwango. Hizi shule ambazo zinajengwa kila siku, shule wiki mbili, mpeni Magufuli afanye kazi *TBA* ijenge nyumba! Ofisi za *TBA* Mikoani ziwe na nguvu, zijenge nyumba. Acheni kuwapa Halmashauri, mnawapa wakandarasi wanachakachua kila siku. Tumekuwa tunashauri *(DART)* Mpango wa Mabasi yaendayo Kasi Dar es Salaam, leteni Wizara ya Ujenzi. Mnapeleka TAMISEMI, hawawezi kufanya ile kazi. Wameanza kufanya toka mwaka 2002, mpaka leo mwaka 2012 zaidi ya miaka 10; fedha wanazo, foleni zinazidi Dar es Salaam. Wekeni hii, toeni kule, leteni Wizara ya Ujenzi watu wachape kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilimweleza hata Mheshimiwa Mwanri, tumekwenda kukagua pale *DART* Wizara ya Katiba na Sheria, tukawaambia, mbona michoro mingi hapa? Mheshimiwa Magufuli tunaomba vikao vya Bodi ya Barabara visiitishwe tukiwa Bungeni. Vikao vinaitishwa tukiwa Bungeni, hatujui kinachoendelea kwenye Halmashauri zetu kwenye barabara za *TANROADS*. Lakini pia uwaambie kule kwangu Kigoma - Kibondo ile barabara ya kutoka Kibondo kwenye Mabamba hawachongi mita 32 kama Sheria ya Barabara inavyosema ya mwaka 2007. Uwaambie wafuate sheria.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kushauri kwamba tumekuwa tunaomba kuhusu *Rural Road Agency* na hii mngeweza kuangalia namna ya kuiunganisha na *TBA* ili wafanye shughuli za ujenzi wa nyumba vijijini, lakini na ujenzi wa barabara za vijijini. Wabunge wote hapa

wanalalamika, tunatoa fedha kwa ajili ya kujenga barabara za vijijini watu hawazifanyii matengenezo, fedha zipo, kazi hazifanyiki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Siungi mkono hoja kwa sababu tumetengwa kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibaha Mjini, niungane mkono na wenzangu kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa hotuba nzuri na *presentation* nzuri. Naomba wote tumpongeze Waziri kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kibaha ni Mji mdogo, lakini unaokua kwa kasi na naamini kwamba sasa Dar es Salaam inapata mahali pa kupumulia. Tunazo barabara mbalimbali ambazo zilikuwa ni za lami, lakini cha kusikitisha na kinachonipa huzuni kubwa ni jinsi barabara hizi zimeachwa bila ya kupatiwa matengenezo na sasa zinakwenda kuwa barabara za udongo kabisa. Mfano mzuri ni barabara ya Kwa Mathias kupitia Shirika la Kiteknolojia la Jeshi la Nyumbu hadi Msangani ambapo tuna Makao Makuu ya Jeshi la Ardhi, yaani kwa *Kimombo Land Force Headquarters.*

Mheshimiwa Spika, namkumbuka kwa umahiri wa Mheshimiwa Waziri, wakati akifungua barabara mbalimbali zinazokwenda katika Vikosi vya Jeshi, mfano Makao Makuu ya Jeshi la Anga kule Lugalo, alisema wazi kwamba atajenga barabara zote zinazokwenda Vikosi vya Jeshi katika kiwango cha lami.

Barabara hii ya Kwa Mathias mpaka Msangani ilikuwa ya lami na nilichokiomba hapa hata katika bajeti iliyopita ni kuwa na mpango wa kuhakikisha angalau ile lami inarudishwa.

Hali kadhalika katika Mji wa Kibaha, tunazo takribani kilomita 18 za barabara ya zamani ambazo zilikuwa ni lami. Toka barabara mpya imejengwa, barabara hii imetelekezwa na inaharibika kuwa ya udongo mtupu, barabara ambayo ina mchango mkubwa wa uchumi kwa wananchi ambao wanafanya biashara kando kando ya barabara hii. Lakini sio hivyo tu, ni barabara ambayo itasaidia sana kuondoa msongamano katika barabara kubwa ya Morogoro. Kwa maana leo hii mtu anayetaka kwenda kilomita moja kutoka eneo la Kibaha Mjini hadi lingine, bado analazimika kuingia barabara kubwa kwa ajili ya ubovu wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, wote tumeshuhudia wakati wa ajali, magari yote huhamia katika barabara hii. Ninakumbuka bajeti ya mwaka 2011 wakati wa mshahara wa Waziri, Mheshimiwa Waziri aliahidi kuwa na mpango kabambe wa kushughulikia barabara hizi. Nasikitika katika bajeti hii sijaona. Namwomba Waziri alichukue hili na alifanyie kazi ili tuweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Spika, tunayo barabara ya Kongowe inayopitia Yombo hadi Bagamoyo. Barabara hii imefungwa tu eti kwa kisingizio kwamba inapita kwenye msitu. Hili ni jambo la kushangaza kwa sababu tunazo barabara nyingi zinazopita katika misitu

mikubwa na hata katika mbuga za wanyama na bado magari yanapita na shughuli za kiuchumi zinafanyika. Namwomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na Wizara husika ili barabara hii iweze kufunguka na shughuli za kiuchumi kati ya Kibaha kupitia Kongowe na Bagamoyo ziweze kuendelea sawasawa.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kibaha ambao ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani toka mwaka 1979 hadi leo haujapata barabara za lami. Zilizokuwepo ni kidogo na sasa mpango uliopo na unaoendelea ni kujenga barabara ya lami ya kilomita 1.1 tu kwa muda wa miaka yote hii. Ninakumbuka kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kilomita 10 ambayo tulikubaliana inaanza na kilomita tano, lakini katika bajeti ya mwaka huu, sijaona mwendelezo ili kuweza kufikia zile kilomita tano ambazo tulipata kama ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nimwombe Mheshimiwa Waziri asaidie kuhakikisha kwamba ahadi hii inatekelezeka, kwani Halmashauri za Miji yetu ni ndogo ni changa na kamwe hazina uwezo wa kufanya miradi mikubwa kama hii.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara una changamoto kubwa na ni hakika ni wa gharama kubwa. Jambo kubwa sasa ni kutumia hii rasilimali kidogo tuliyonayo kuhakikisha tunaendelea kuwa na barabara zinazojengwa chache, lakini zenye viwango ambavyo baadaye hatutahangaika tena kuona kwamba hatukufanya vyema. Tumekuwa tunatumia fedha nyingi sana kulipa fidia wakati tuna miradi hii ya barabara na imesababishwa na kutokuwa na *master plan* ya barabara kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa kazi aliyoifanya angalau ya kuweka mipaka katika barabara kubwa nchi nzima. Lakini bado ningeisihi Wizara ifanye kazi ya ziada kutambua barabara zote na kuziwekea kuwa na *master plan* kwa maana ya michoro ili kila anayeendeleza katika eneo lolote, hata kama anajenga nyumba yake ya tope na miti, anajua wazi kwamba hapa siku moja barabara kubwa inapita, atageuzia mlango pale na thamani ya lile eneo na ardhi yake litakuwa kubwa na wawekezaji hawatakuwa na mashaka katika kuendeleza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na barabara zinazoendelea kujengwa vizuri, lakini bado tunazo changamoto. Namwomba Waziri mhusika ajiulize: Kwa nini tunapotembea nchi za wenzetu, michoro na mipango ya barabara inakuwa ni mizuri sana? Kwa mfano, tumekuwa tukilalamika hapa kwamba hata tukisafiri wananchi, wengi hawana mahali pa kujisaidia, hawana mahali pa kupumzika baada ya safari ndefu, hata kama dereva anachoka. Katika hii miji yetu midogo midogo, hakuna huduma za kuridhisha. Sasa kwa nini tunapoweka mipango ya barabara, hatuweki sehemu za mapumziko, yaani *rest arrears* kama tunavyoona katika nchi mbalimbali zilizoendelea zinazojenga barabara? Nina imani hili suala, hata la rasilimali fedha peke yake, kwa sababu kama tutakuwa na mchoro mzuri katika hizi *highways* na tuka-*identify* maeneo, tukaweka na michoro, tukasema hapa ni mahali pa kupumzika kati ya Dar es Salaam pengine na Morogoro au kati ya Morogoro pengine na Dodoma na tukaweka michoro mizuri, basi

tunaweza tukatumia *Private Partnership* wakaendeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, endapo Waziri atajibu hoja zangu. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya watu wa Jimbo la Kilolo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ambayo imewasilishwa leo hii asubuhi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja, siyo kwamba Wizara hii imefanya jambo lolote kubwa katika Wilaya yangu, lakini naunga mkono kwa matumaini. Kwa sababu ukiona mwenzako ananyolewa na wewe uanze kuloweka nywele. Kwa hiyo, naishi kwa matumaini nikitegemea kwamba kuna siku itafika na siyo mbali Kilolo nayo itaangaliwa kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, nina mambo matatu ya kutaka kuchangia. La kwanza kabisa, ni bughudha ambayo wananchi katika Jimbo langu wameipata katika ujenzi wa barabara ambako hifadhi ya barabara imewafuata wananchi na kuwekewa alama. Wananchi wamekuwa wakilalamika sana wakitaka wapate ufafanuzi na hasa wale ambao walikuwa nje tayari, lakini hifadhi ya barabara ikawafuata. Watu hao tayari wameshapata hofu, hawafanyi maendeleo yoyote, wanasubiri waambiwe ni lini mipango yote itakamilika? Kuna watu wamepewa barua kwamba muda utakapofika, basi watapewa fidia ya eneo na

mali. Lakini muda huo haufahamiki. Kwa hiyo, nao wanaishi katika matumaini, kwani hawajui ni lini jambo hili litatokea.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wangu, nafikiri kwamba ingekuwa busara kwa Serikali pale ambapo tayari imeamua, imechukua na inajua hifadhi ya barabara, imewafuata wananchi, basi wapewe kilicho chao ili wakati huu gharama za ujenzi na kadhalika waweze kuanza kuondoka watafute nafasi nyingine wajenge kwa bei nafuu. Kwa sababu kama watakuja kulipwa pengine miaka 15 ijayo maana yake ile fedha atakayokuwa amelipwa itakuwa haiwezi kufidia na kumwezesha huyu mtu aweze kujenga nyumba. Wasiwasi huo mkubwa uko kuanzia Ruaha Mbuyuni, Mtandika, Mahenge, Ilula, Itunda, Mazombe, Mbigili ndipo unaingia Iringa Mjini na ni watu wengi sana wamekuwa na wasiwasi mkubwa wa namna hiyo. Tunaomba Wizara au Serikali ifikirie namna gani inaweza kulimaliza tatizo hili kwa hawa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, ningependa kuzungumzia juu ya tatizo la msongamano wa magari Dar es Salaam. Tatizo la msongamano wa magari Dar es Salaam watu wengi wamelizungumza. Lakini kwa bahati mbaya hakuna mtu anayekuja na takwimu kwamba hasara yake hasa ni nini. Baada ya Serikali kuuza nyumba kwa watu binafsi, wale Maafisa wengine walioajiriwa wanakaa sehemu mbali sana. Unaweza kumkuta Afisa anakaa Bunju, dereva wake anakaa Ukonga, mwendo wa kwenda kumchukua yule Afisa, arudi hapa katikati Mjini, yaani Ofisini ni kilomita 50 *oneway,* atarudi kilomita 50. Atamrudisha

jioni kilomita 50, atarudi yeye dereva kilomita 50, jumla ni kilomita 200 kwa gari moja. Lakini kwa kutokana na msongamano ule vilevile magari yanakwenda pole pole sana, lita moja ya dizeli ama ya petroli inaweza kusukuma gari kwa kilomita tano, ambazo ni kwa 200 kwa siku. Ukizidisha mara Sh. 2,000/= unapata Sh. 80,000/=, kwa siku.

Mheshimiwa Spika, sasa siyo gari moja, ukichukua angalau magari 100 ya Serikali yanafanya hivyo, acha yale ya Mashirika, zinatumika zaidi ya Shilingi milioni 12 kwa siku na hii ni *very conservative figure*. Nafikiri hili jambo ambalo linazungumzwa kwa ajili ya kuboresha usafiri Dar es Salaam lipewe kipaumbe zaidi kwa sababu Serikali inapoteza fedha nyingi sana kuliko watu wanavyoona.

Mheshimiwa Spika, lingine ni barabara zetu kufunguka. Barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia inapita katika maeneo ambayo kwa kweli ni ya hatari. Ukitoka Dar es Salaam pale Ruvu limejengwa daraja la kudumu, lakini kilichotengenezwa na mwanadamu kinaweza kubomoka. Lakini kuna hali mbaya zaidi sehemu ya mlima wa Kitonga katika Wilaya ya Kilolo ambapo mwaka huu magari yalisimama. Lakini kila siku tunatazama kitu kimoja bila kuangalia njia mbadala. Ruvu leo ikikatika pale ambayo ndiyo inasafirisha kila kitu kutoka Dar es Salaam kwenda Afrika Kusini au nchi za Afrika Kusini zinazosafirisha kupeleka Dar es Salaam, Ruvu ikikatika, tutasimama na hakuna *alternative way. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kitonga ikikatika leo hii, hakuna njia ya kufika Dar es Salaam. Lazima tutafute njia nyingine. Aidha, magari yapite kuja Dodoma Kilomita 251 yafike hapa Dodoma kutoka Iringa halafu baada ya hapo yasafiri kwenda Dar es Salaam kitu ambacho ni gharama sana. Inaonekana kwamba hatujiweki *strategically* katika kupanga mipango yetu katika maeneo ambayo tunaona tuna udhaifu.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilolo kuna nafasi kubwa sana. Ukitoka Iringa Mjini ukitengeneza ile barabara ambayo ni ya *TANROAD,* inakwenda Kilolo - Kidabaga - Idete - Itonya - Muhanga telemka Mungita unapita *Udizungwa National Park*, utatokea Kilombero, na unafika Mikumi ambayo ni kilomita 120 tu. Ningeshauri sana Serikali iangalie *alternatives* ambazo zinaweza zikatusaidia wakati wa dharura, kwa sababu vinginevyo, kuna siku barabara inakatika na kila mmoja anasema sijui tupite njia ipi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kufikiria, tuanze kuona mbali leo, siyo tungojee mpaka jambo linatokea ndiyo tuseme sasa tuanze kuhangaika kufanya namna hii. *We must be strategic in our thinking and in our planning* na nina hakika Wizara hii ambayo mimi nasema kwa kwetu Kilolo bado hatujanufaika sana, lakini tunaishi kwa matumaini tukijua kwamba hizo ndiyo njia mojawapo ambayo linaweza kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya milima ya Udzungwa ni sehemu ya utalii, tunafungua fursa. Kuna aina mbalimbali za utalii, kuna hata wanyama ambao

sehemu nyingine duniani hawapatikani. Kuna vyura wenye pembe tatu, duniani hawapo; ila wapo Kilolo tu; kuna milima na mapango ambayo kwa kweli ni sehemu ya vivutio. Lakini sasa hivi wanajenga zaidi Kilombero kwa sababu wenzetu kule wamepanua barabara wakati upande wa Mkoa wa Iringa haujapanuliwa ambao ungeweza kuwa na fursa nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na afya njema ili na mimi niweze kutoa mchango katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo anaifanya kazi yake kwa umahiri mkubwa. Ni jambo ambalo halifichiki kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji katika Wizara husika wamefanya kazi kubwa na ni karibia kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama hapa na wananchi kwa ujumla wameiona kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru pia Serikali kwa sababu ninaona upanuzi wa barabara ya Ukonga kuelekea Chanika bado inaendelea kupanuliwa vizuri, lakini pia nishukuru kwa sababu kwenye bajeti ziko barabara mbili ambazo nazo zimetengewa fedha ikiwepo barabara hii ambayo inapanuliwa ya Ukonga kuelekea Msongola mpaka Mvuti. Lakini pia tumepata

barabara nyingine ya changarawe ambayo inatoka Gongolamboto *Kiltex* inakwenda kutokezea Kata ya Pugu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, katika Jimbo la Ukonga, asilimia 98 ya barabara ni barabara za changarawe. Lakini sehemu ya Ukonga ni sehemu kubwa ambayo ina kama kilomita za mraba zaidi ya 150. Barabara hizi huwa zinatengenezwa kwa nguvu ya Manispaa ya Wilaya ya Ilala. Lakini kwa sababu ni changarawe, zinatengenezwa na baada tu ya mvua kunyesha barabara hizi zinakuwa kama vile hazijatengenezwa, kwa hiyo, nakiri kwamba Serikali inapoteza fedha nyingi sana kurudia barabara hizo mara kwa mara. Nadhani hata Serikali inajua ni fedha kiasi gani zimepotea kwa sababu ya mvua iliyonyesha mwishoni mwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi nchini zimeachwa ili zitengenezwe na Manispaa, lakini Manispaa zetu nyingi hazina uwezo wa kutengeneza barabara hasa kwa kiwango cha lami. Nilikuwa naomba sasa Serikali ifike mahali ianze kuangalia tena vile vipengele ambavyo vinaruhusu barabara kupandishwa hadhi ili barabara nyingi ziweze kuchukuliwa na *TANROAD*.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayofanya Jiji la Dar es Salaam liwe na msongamano mkubwa ni barabara mbovu za pembezoni tulizonazo. Naomba sana kwamba sasa ifike mahali tuangalie upya vile vipengele. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, chonde chonde, kama nilivyosema barabara nyingi ni

za changarawe na kwa sababu nilishaomba barabara mbili zikapandishwa hadhi, na nikushukuru sana ulinijibu hata barua yangu, barabara zile mbili nikimaanisha barabara ya Banana kwenda Kitunda, Kivule na kwenda Msongola barabara ile inatengenezwa na *TANROAD*.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwamba mwaka 2011 waliweza kutengeneza nusu Kilomita angalau. Lakini kwa mwaka huu ile barabara haijatengewa fedha. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri utakapotuletea mrejesho, naomba sana hii barabara nayo uipangie angalau kiasi kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini iko barabara nyingine ambayo mliikubali pia kuipandisha daraja. Barabara ambayo inatoka Nzasa inakwenda mpaka Kisarawe. Ile barabara imekuwa ni mbovu sana kwa sababu ya malori ya mchanga yanapita kule na kwa kweli kwa wakati wa mvua hii barabara haipitiki. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba sana ile barabara nayo kwa sababu umeikubali uitengee kiasi cha fedha ili mwaka huu wa fedha nayo kidogo tuweze kuanza kutengeneza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi yangu hayo ya barabara hizo mbili, naomba sana barabara hizi za changarawe ambazo zinatengenezwa na *TANROAD,* angalau zisimamiwe ili ziweze kuwekwa ile changarawe nzuri. Barabara zinazowekwa changarawe, nyingi huwa haiwekwi ile changarawe nzuri, na ndiyo sababu unakuta kwamba upepo ukija

barabara nayo inaharibika; mvua zikija barabara zinaharibika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sana barabara zangu hizo mbili ziweze kupata fedha, lakini ninajua kabisa Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi na nimwombe sana aangalie kwa jicho lingine kwa makini zaidi barabara za Mkoa wa Dar es Salaam ili tuweze kupunguza ule msongamano wa magari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii muhimu sana. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya, kukumbuka kwa mara ya kwanza baraba ya Mwalimu Nyerere. Miaka 12 nimekuwa napiga kelele hapa, barabara inayotoka Makutano kupita Butiama, Ikizu inakwenda Nata mpaka Serengeti. La ajabu ni kwamba ile barabara tuliyoahidiwa nyuma huko itapita Serengeti, watu wa Kenya wamefanya mbinu chafu kuhakikisha barabara hii haijengwi na badala yake wanahakikisha kwa kasi sana ile barabara ya kutoka Sirari kwenda Mwanza ndiyo unaona ujenzi unaendelea pale. Lakini barabara ya mbugani haijengwi, na Serikali imenyamaza.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata kauli ya Serikali kuhusu hii barabara ya Serengeti: Ni nini mme-

*surrender*, tumebwaga silaha chini na kusalimu amri za watu wa Kenya kutuzuia tusiende Serengeti?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mara, barabara hiyo ni muhimu sana kupeleka mazao yetu Serengeti. Babara hiyo sasa imekatwa na kwamba inatoka Makutano kwenda Nata halafu inapiga chenga, lakini hatujui imefikia wapi. Ningependa kupata kauli ya Serikali kuhusu hatma ya barabara hii. Lakini pia inaonekana pia kuna ujanja ujanja fulani unafanyika hapa. Kuna barabara za Mikoa mingine zinajengwa haraka kweli, nyingine zinachomekwa tu. Kwa mfano, ile ya Kilosa haiko kwenye Ilani, iliwekwa tu, Kilosa – Dumila hapo hapo imekwenda imepatiwa fedha inajengwa. Lakini barabara ya Nyerere leo miaka 40, fedha zimetengwa eti ni Shilingi bilioni tatu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sitaunga mkono hoja bajeti hii kwa sababu tu barabara ya Nyerere imesahauliwa. Sitakubali Shilingi bilioni tatu zinaweza kujenga kilometa 80. Mwaka 2011 nilisema ningetoa Shilingi, nikabembelezwa sana na Ndugu yangu Waziri, tutafanya, hela itakuja, lakini hakuna. Ukiona ukurasa wa 122 nitanukuu: "Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya Shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano - Nata - Mugumu kilometa 80. Shilingi bilioni tatu ni sawa sawa na Dola za Kimarekani 200,000. Sasa nini nitawaambia watu wa Mara kuhusu hii barabara tangu wakati wa uhuru tunaizungumza?

Mheshimiwa Spika, wakati huo Mwalimu alisema, msijenge barabara kutoka Makutano kutoka kwake tu, maana itakuwa inaishia pale. Alitaka ijengwe iende mpaka Serengeti na mpaka wakati anafariki alikuwa anafuatilia hiyo barabara. Nataka kujua na narudia kauli ya Serikali kuhusu ndoto ya Mwalimu, tuache leo ama la? Nataka kujua hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna barabara nyingine mbili kubwa, sioni zinasemewa nini. Miaka mitatu iliyopita, ndugu yangu Mheshimiwa Magufuli alikuwa pale Mgango; barabara ya kutoka Msoma kupitia Mgango kwenda Busekela, alisema itajengwa kwa kiwango cha lami na wakaongea na watu Wizarani anasema tuhakikishe inafanya nini. Mheshimiwa Rais alikuja Busekela, pia akawaambia wananchi wa Busekela barabara hiyo nimemwachia Waziri atajenga. Kwenye Ilani ya Chama barabara hii imo, lakini sioni chochote kinachofanywa kuhusu hii barabara ya muhimu sana kutoka Musoma kwenda Majita kupitia Mugano na Suguti.

Mheshimiwa Spika, niwaambieje wananchi wale? Nikienda kule wananiuliza, Mheshimiwa Mkono, Rais aliahidi, mbona chochote hakiendelei? Nataka kujua hawa watu waende wapi? Mazao yote Ziwani yanaishia pale, hawaruhusiwi kwenda Serengeti, wayapeleke wapi? Uganda ni mbali, kuna Zina, barabara ya Mugango ama Majita kwenda Mwanza ni mbali, hawa wananchi wangu wafanyeje kama miundombinu hakuna? Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ya tatu ambayo ni ya muhimu ni kutoka Kirumi kupitia Kaigata kwenda Serengeti, hiyo barabara ni ya muhimu sana na kila wakati madaraja yanavunjika, lakini sioni Serikali inafanya nini kuhusu hizo barabara. Ukiona kiasi cha fedha kinachotakikana kutengwa, unaweza kuchukua *local component* na *foreign component*. Mimi sioni kweli fedha zitapatikana za kujenga hata hiyo nusu wanayosema kwa huu mradi mkubwa wa Nata mpaka Loliondo. Mimi siamini! Lakini njia pekee kama Kenya wanasema hatutajenga, basi mtuambie kwamba Tanzania pia tuna-*surrender* Watanzania wajue, badala ya kila mwaka mnatuambia itajengwa, lakini haijengwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi mwingine ni *Airport;* Mara haina uwanja wowote, barabara hakuna, lakini ukianza kuangalia: Je, ile *Airport* ya Musoma haiwezi kukidhi mahitaji ya mazao yetu tukitaka ku-*export* nje? Sioni chochote kinachozungumzwa juu ya Uwanja wa Ndege tuliahidiwa huko nyuma. Sioni chochote! Nataka kujua hatima ya uwanja huo. Upande wa Tarime, upande wa Serengeti tulikuwa tumebuni mpango wa kujenga uwanja mwingine wa ndege mkubwa pale, lakini kwa makadirio haya, naona ni kimya. Wajita wanasema: *"Njibile ya jibi, jibi, jibi."* Hakuna kinachoendelea. Nataka kujua hivi Mara ni sehemu ya Tanzania, ama hapana? Kwanini miradi hakuna? Nimekuwa Mbunge miaka 12, sijaona mradi wowote mkubwa wa maana unaofanywa Mkoa wa Mara. Sioni! Kuna nini huko? Tunakosea nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nasema siungi mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia haumtoshi mchangiaji hata mmoja, kwa hiyo napenda kesho nitangaze wale watakaokuwepo. Kama nilivyosema, tumefunga orodha ya waombaji kuchangia. Kesho tutaanza na Mheshimiwa Modestus Kilufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mchungaji Msigwa, Mheshimiwa Muhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Rajab Mbarouk wajiandae. Hawa wanatosha kwa kazi ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyofanya leo. Mmefanya kazi nzuri sana, tumetumia muda wetu kila dakika, toka asubuhi pamoja na kusoma hotuba zote zile tumekuwa na wachangajia zaidi ya 30, kwa sababu ya matumizi ya muda. Hii habari ya mwongozo, mwongozo huwa tunamaliza wakati. Halafu wengine wanasema Spika ajibu, sasa na mimi nijibu nipoteze wakati? Kwa sababu hata kama nina majibu, mwongozo aliyepewa Mheshimiwa Chambiri na Mheshimiwa Machali hapa ukisoma alivyosema Mheshimiwa Chambiri na alivyosema Mheshimiwa Machali tofauti. Sasa kusoma hapa naona tena napoteza muda, maana nina *page.*

Hata hivyo, katika *Hansard* yetu Mheshimiwa Chambiri alisema kwamba alisafiri na kijana wa miaka ishirini na ngapi kutoka Minjingu kwenda Babati na humo njiani alikuwa anasema hakuna lililofanyika katika miaka yote 50. Walipofika Babati akasema hivi mbona kutoka Minjingu mpaka Babati tumetumia dakika 45 kinyume na saa nne tulizokuwa tunatumia zamani? Nalo hilo hulioni? Halafu akasema tatizo la watu waliochaguliwa humu ndani kati ya miaka 21 mpaka 24 walioweza sana, ni 30; akasema hawa hawajui tulikotoka.

Sasa Mheshimiwa Machali akaja anasema mwongozo, atoe maneno hayo afute. Sasa afute nini? Kwani siyo kweli kwamba wapo Wabunge wa miaka 21, 23 sana sana 30, hawajui kweli uhuru ulipotokea? Sasa mwongozo wa namna hii hauna mantiki kabisa. Tunapotaka mwongozo, suala alilosema Mbunge kilichopita ni sahihi au siyo sahihi? Ndiyo inavyokuwa.

Sasa mimi huwa napenda sana tujifunze hilo ili tutumie muda wetu vizuri, wale wanaopenda kutusikiliza kule, ukisema mwongozo waweze kwa kweli kuona hili ni jambo zuri. Tukifanya hivyo, Bunge letu litapata heshima inayostahili.

Kuna Wabunge wengine walianza vizuri kwelikweli mpaka mimi nikasema tuna-*assets* hapa. Sasa hivi wameharibikiwa, sijui kitu gani? Halafu siri moja nyingine, acha kumtaja mtu kwa jina. Kanuni ya 64 (d) inasema, usimzungumze mtu. Ukizungumza mtu, atakujibu. Lakini ukizungumza *issues,* sasa inawezakana

kweli amefanya hilo, lakini *issues can happen anywhere*. Sasa haya ni mambo madogo ambayo tunapaswa kuyafuata kwa sababu ukimtaja mtu umem-*provoke,* lazima atajibu. Lakini wanaotusikiliza hawatuelewi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndugu zangu tunatafuta hela kidogo tuweze kufanya *review* na katika *review* yetu tutafanya marudio ya Kanuni zetu, tutakuwa tunaelezana kwa kusema kwa mfano, siku ile fulani alifanya hivi, haikuwa sahihi, alipaswa afanye hivi. Tutakwenda *to that degree*. Siku hiyo tutakuwa ndani, hatutakuwa hapa, kwa sababu tutaelezana kwamba siku fulani mtu alifanya hivi, lakini haikuwa sahihi, alipaswa afanye hivi kusudi tuweze kwenda na wakati na Kanuni zetu. Ndiyo wengine wanasema Spika hajibu hoja. Siwezi kujibu wakati mwingine kwanza naona napoteza muda wa watu kwa sababu vitu vingine vilikuwa havina msingi. Kwa hiyo, kitu kisichokuwa na msingi tena na mimi naendelea kupoteza muda, na mimi naingia kwenye ulimbo wa kupoteza muda na mimi hilo siko tayari.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana tumefanya kazi nzuri leo, mmejadili mambo ya kwenu, Waziri ameyapata. Tutamaliza kipindi cha asubuhi maswali kesho, najua kwenye Kamati ya Matumizi mtakwenda mbali sana. Kwa hiyo, lazima nitoe muda kama utatosha itakuwa vizuri.

Kwa leo nawashukuruni sana, muwe na jioni njema. Naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 6 Julai, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*